# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TANO

### Kikao cha Tatu – Tarehe 3 Novemba, 2016

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tutaanza na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri ni Viongozi wa Umma kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995. Kuna taarifa kwamba siku ya Jumanne tarehe 25 mwezi wa 10 saa 2.00 usiku kiliitishwa Kikao cha Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambapo wewe ulikuwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao hicho ambacho kilihudhuriwa pia na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, pamoja na mambo mengine Muswada ambao unategemea kuletwa Bungeni kesho wa mambo ya Habari pamoja na Mpango wa Taifa ambao tunaendelea kuujadili, ulijadiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine yote, kikao kile kiliamua kutoa zawadi kwa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wakiwemo Mawaziri. Kiasi cha shilingi milioni 10 kwa kila Mbunge wa Chama

cha Mapinduzi wakiwemo Mawaziri zimetolewa kwa viongozi ambao wanabanwa na Sheria ya Maadili ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mgao huo wa shilingi milioni 10 ambao umeendelea kutolewa katika Ofisi za Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi ukiratibiwa na Naibu Katibu wa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambaye vile vile ni Mbunge. Waziri Mkuu, taarifa hizi ni za kweli? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, maswali kwa Waziri Mkuu ni maswali yanayohusu sera. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tukumbushane tu vizuri; Mheshimiwa Mbowe, naomba swali lako liwe linahusu sera. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Suala la *corruption* na maadili ya viongozi siyo sera? *(Kicheko)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikilizeni. Masuala ya rushwa na maadili ya viongozi ni sehemu ya sera. Kama Bunge hili linataka kuaminishwa kwamba masuala haya siyo ya sera, masuala ambayo yapo *so serious* kwa Taifa, hamtaki Waziri Mkuu atoe maelezo kwa sababu Naibu Spika wewe unajaribu kulinda jambo hili kwamba siyo suala la sera. Kama siyo sera, jambo hili ni nini?

**MBUNGE FULANI:** Waziri Mkuu ajibu swali.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Waziri Mkuu tunaomba utujibu swali tafadhali.
Mheshimiwa Naibu Spika mwache Waziri Mkuu ajibu swali. Hili ni swali la kisera. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, Waziri Mkuu nitamruhusu…

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mimi nitamruhusu kujibu maswali yanayohusu sera, kama ambavyo nitamzuia mtu mwingine yeyote. Kwa hiyo, hata wewe, ndio maana nimekupa nafasi tena ili uulize swali linalohusu sera, ndivyo kanuni zetu zinavyosema. Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. DEO K. SANGA:** Taarifa!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena. Suala la *corruption* katika Taifa hili ni suala la kisera na nimelizungumza. Sera zinazaa sheria, naomba tuelewane. Sera zinazaa sheria; na sheria hizi ninazozizungumza hapa, *The Prevention and Combating of Corruption Act,* 2007 na Sheria ya

Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995 ni matunda ya sera. Kwa hiyo, hili swali naliuliza ni la kisera. *(Makofi)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**MHE. DEO K. SANGA:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga naomba ukae. Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijasema tuhuma hizi ni za kweli, ila nimeuliza Waziri Mkuu atujibu ni za kweli ama siyo za kweli? Sasa unalinda nini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, nadhani kwa hapa sasa tulipofika, kama wewe unaona hilo swali ni la sera, kanuni hizi ndizo zinazoniongoza mimi… *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Swali ni rahisi kabisa, angemwacha ajibu. *(Kicheko/Makofi/Kelele)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa maana hiyo, nitaendelea na maswali mengine. Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali kwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa Serikali ina mifumo, sheria, miongozo na taratibu ya upelekaji wa fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu mara tu baada ya bajeti ya Serikali kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa sheria hizi na miongozo hii haifuatwi na kupelekea Halmashauri zetu kupelekewa robo tu ya fedha au nusu tu ya fedha zikiwemo Halmashauri zangu za Mkoa wa Tabora ambazo zote saba hazijawahi kupata fedha kamili. Hii inaleta taharuki kubwa ndani ya Halmashauri zetu. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu unatoa kauli gani kuhusu ucheleweshwaji wa fedha za bajeti kwenda kwenye Halmashauri zetu kwa wakati muafaka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya kelele nyingi ambazo zipo, Mheshimiwa Mbunge wakati anauliza swali kulikuwa na kelele nyingi naomba nimsihi arudie tena ili niweze kujibu kwa usahihi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Munde Tambwe Abdallah, swali kwa Waziri Mkuu.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hili swali halikusikika, nami nafurahi ili nilirudie vizuri. Kwa kuwa Serikali ina mifumo, ina sheria, ina miongozo na taratibu zake za upelekaji fedha za bajeti kwenye Halmashauri zetu mara tu baada ya bajeti ya Serikali kupelekwa; na ni wazi fedha hizi hazipelekwi kwa wakati; fedha hizi zinapelekwa robo tu ya fedha za bajeti ndani ya Halmashauri au nusu yake tu: Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa kauli gani kuhusu ucheleweshwaji wa fedha hizi za maendeleo katika Halmashauri zetu ikiwemo Halmashauri zangu zote za Mkoa wa Tabora? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijaanza kujibu swali, uridhie kuwakumbusha Watanzania kwamba leo hii Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatimiza siku ya 365 kwa maana ya mwaka mmoja. Naamini Watanzania wote tumeona utendaji wake na hasa mwelekeo wake wa kuiongoza Serikali hii kwa mafanikio. Jukumu letu ni kumwombea Mheshimiwa Rais aweze kuendelea vizuri na kuiongoza nchi yetu na wananchi wote tuungane pamoja kila mmoja kwa dhehebu lake kuiombea Serikali hii iweze kupata mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze kujibu swali la Mheshimiwa Munde kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu baada ya bajeti inawajibika kutekeleza maamuzi ya Bunge letu hasa katika kupeleka fedha za bajeti zilizopangwa. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote mnajua kwamba baada ya Bunge kuridhia na kutoa mamlaka ya matumizi ya fedha, Serikali hii tulianza na majukumu muhimu; moja, ilikuwa kwanza kujiridhisha kuwepo kwa mifumo sahihi ya makusanyo ya mapato na matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili kwa upya wake tulianza kupeleka watumishi watakaosimamia shughuli za usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na matumizi yake kwenye Halmashauri zote nchini. Kazi kubwa ya tatu ilikuwa ni kuratibu na kutathmini miradi yote iliyokuwa imeanza halafu ilikuwa

haijaendelezwa na ile miradi mipya ili tuweze kutambua pamoja na thamani zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa tumejiridhisha sasa tumeanza kupeleka fedha kwenye Halmashauri zote nchini. Kwa mujibu wa kumbukumbu kutoka Hazina ambazo wakati wote tunapewa taarifa; ofisini kwangu pia napewa taarifa; kufikia mwezi Oktoba tumeshapeleka zaidi ya shilingi bilioni 177 za miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri zetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge watabaini wiki hizi tatu tumeanza kuona kwenye magazeti yetu mengi matangazo mengi ya zabuni kutoka kwenye Halmashauri mbalimbali. Hii ina maana kwamba tayari miradi ile ambayo ilikuwepo na ile ambayo inaendelea na mipya imeshaanza kutengewa fedha na kuanza kutangazwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba sasa Serikali itaendelea na upelekaji wa fedha kwenye Halmashauri kwa ajili ya shughuli zetu za maendeleo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado msisitizo umebaki pale pale kwamba Halmashauri ziendelee kukusanya mapato ya ndani ili kuongezea bajeti kwa fedha za Serikali ambazo tunazipeleka na tumesisitiza ukusanyaji huo uwe ni wa mfumo wa kielektroniki ili kudhibiti mapato ambayo tunayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumeendelea kusisitiza matumizi sahihi ya fedha ambazo tunazipeleka kwenye Halmashauri kwamba fedha hizi ni lazima zitumike kadiri ilivyokusudiwa kwa miradi iliyoandaliwa kwenye Halmashauri zenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, sisi wenyewe ni Wajumbe wa Baraza letu la Madiwani kwenye Halmashauri zetu; niendelee kuwasihi kusimamia na kufuatilia matumizi ya fedha tunazopeleka kwenye Halmashauri ili ziweze kutekeleza miradi ile kikamilifu. Serikali itaendelea kutuma fedha kwenye Halmashauri zetu kadri miradi ile ilivyoweza kuratibiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi binafsi na Watanzania wote wana imani na Rais Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Waziri Mkuu wetu na tuna imani haya yote aliyoyasema hapa kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano yatatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuulize swali dogo tu la nyongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Atakuwa tayari sasa kuzifuatilia Halmashauri zote ziwe zinapokea pesa kwa kutumia mashine za kielektroniki? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pamoja na maelekezo yake yote, tumeendelea kuwaagiza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na watendaji wa Halmashauri wakiwemo Wakurugenzi kuhakikisha kwamba moja ya majukumu yao waliyonayo ni kuhakikisha na kujiridhisha kwamba kila eneo la makusanyo, vifaa vya kielektroniki vinatumika na kwa hiyo, wajibu wangu ni kusimamia kuona kwamba matumizi ya vifaa hivi yanafanyika na yanaendelea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, swali kwa Waziri Mkuu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nampongeza kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa swali zuri ambalo wewe mwenyewe Naibu Spika, umesaidia kuiua CCM humu ndani. Watu wataamini hizo hela mmekula, bora ungeacha ajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nitatumia maneno ambayo watawala wanapenda kuyasikia kwamba Serikali hii haijafilisika kabisa na Serikali hii ina mikakati mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika Ubunge wangu wa muda mfupi huu, ile Sheria ya Mfuko wa Jimbo ndiyo sheria ambayo nimeona imekaa vizuri kweli kweli kwa sababu ni fedha ambazo Mbunge anapewa kwa taarifa tu zinaingia kwenye Halmashauri halafu Kamati yake inakaa, miradi inaibuliwa halafu wanapanga inaenda kwa wananchi moja kwa moja, Mbunge hagusi hata shilingi mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali haijafilisika, tangu bajeti ya Serikali yenu hii ya Awamu ya Tano imepitishwa, Waheshimiwa Wabunge hawajapewa fedha hii ya Mfuko wa Jimbo. Sasa naomba unieleze, kama Serikali haijafilisika, Waheshimiwa Wabunge wameahidi miradi mbalimbali katika maeneo yao ya kiuongozi na wananchi wakawa wanasubiri miradi ile, Waheshimiwa Wabunge wanaonekana waongo kwa sababu fedha hazijaenda na Wabunge hawawezi kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini kauli yako juu ya hili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimwambie kwamba Serikali hii haijafilisika. Mfuko wa Jimbo wa Mbunge ni miongoni mwa fedha zilizoandaliwa kwa bajeti ambayo tuliipitisha mwezi Julai, lakini Mfuko huu unapelekwa mara moja kwa mwaka kwenye Majimbo yetu. Nawe ni shahidi kwamba toka tumemaliza Bunge sasa tuna miezi mitatu. Bado tuna miezi kama saba ili kuweza kuhakikisha kwamba fedha yote tuliyokubaliana hapa inaenda kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo yana kipaumbele chake, yapo yale ambayo yanaweza kutekelezwa ndani ya mwaka mzima, lakini nataka nikukumbushe kwamba mfumo wa fedha zetu ni *cash budget,* tunakusanya halafu pia tunapeleka kwenye miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe Mheshimiwa Mbunge faraja kwamba suala la Mfuko wa Jimbo bado unatambulika na fedha tutazipeleka kwenye Majimbo na Waheshimiwa Wabunge wote tutawajulisha tumepeleka kiasi gani ili sheria zile ziendelee kutumika na Mheshimiwa Mbunge kama Mwenyekiti wa Mfuko wa Jimbo utaendelea kuratibu mipango yako ya Jimbo lako na fedha ambayo tutaipeleka. Kwa hiyo, endelea kuwa mtulivu, fedha tutazipeleka na tutawajulisha Wabunge wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza niseme tu kwamba majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yamenishtua; amesema fedha inatolewa mara moja kwa mwaka na wengine wanasema ni mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nijue, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Ukonga; niliposoma sheria inasema unapogawanya zile fedha inabidi kuangalia *population* na mazingira ya Jimbo. Kwa mfano, Jimbo la Ukonga na Jimbo la Segerea, mwenzangu anapokea shilingi milioni 33, mimi napokea shilingi milioni 16. Ni kama mara mbili yangu, lakini wananchi wa Segerea ni karibu 600,000; mimi watu wa Jimbo langu tumezidiana kama watu 50,000 hivi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu upo tayari kusimamia Serikali yako ili kuangalia hali halisi ya majimbo yetu yalivyo. Mtu mwenye mazingira magumu ya Jimbo lake apate fedha nyingi zaidi kwa sababu hata mahitaji ya miundombinu ni mingi zaidi kuliko Majimbo mengine? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumejitokeza matatizo kidogo kwenye Halmashauri zenye Jimbo zaidi ya moja na hasa Majimbo yale ambayo yameanzishwa kipindi hiki cha karibuni. Jukumu la Serikali kupitia Wizara husika ni kuendelea kufanya sensa kabla hatujaanza kuzipeleka fedha ya kutambua idadi ya wananchi walioko kwenye Jimbo husika baada ya kuwa Halmashauri yote kuwa ina Majimbo zaidi ya moja; tuweze kujua kila Jimbo lina wananchi wangapi ili sasa tunapopeleka fedha, tupeleke tukiwa tuna maelekezo hasa kwenye Halmashauri zenye Majimbo zaidi ya moja, kwamba kila Jimbo sasa lipate mgao kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mwita niseme, tatizo lililoko Ukonga na eneo la Segerea litakwisha kwa sababu kazi hiyo inafanyika ndani ya Wizara kabla hatujaanza kupelekka fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kama Jimbo lako lina idadi kubwa ndilo ambalo litapata fedha nyingi kulinganisha na Jimbo lingine ambalo lina idadi ndogo ya wananchi ili sasa kila Mbunge kwenye eneo lake aweze kupanga mipango ya maendeleo kwa fedha ambayo imekuja inayolingana na idadi ya wakazi kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali kwa Waziri Mkuu.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakuna Serikali yoyote duniani ambayo haitozi kodi. Ni lazima tulipe kodi ili tupate madawa, watoto wasome, tupate maji na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu sana, wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kunyanyaswa na baadhi ya Maafisa wa Kodi na wengine wakikadiriwa kodi isiyostahili na mbaya zaidi kuna wazabuni ambao wanaidai Serikali yetu. Je, nini kauli ya Serikali kwa jambo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabati, Mbunge wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba nimepata malalamiko na baadhi ya wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali. Mimi nimekuwepo kwenye ziara ya kawaida Mkoani Mbeya na kwenye kikao changu na wafanyabiashara, wamewahi kueleza matatizo yanayowapata chini ya chombo chetu cha *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wao niliwahakikishia, naomba nirudie tena kwamba Serikali hii inaheshimu na kuwathamini wafanyabiashara wote, wawekezaji wote na wadau wote walipa kodi ndani ya nchi hii, kwa sababu maendeleo yetu katika nchi yataletwa na sekta ya wafanyabiashara na wawekezaji wakiwa ndio walipa kodi wakubwa, wazuri nchini na uchumi wetu unategemea sana kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo ndani ya chombo chetu cha *TRA*, tumeendelea kufanya vikao nao, kuwasisitiza na kuwataka wafuate kanuni na taratibu za ukusanyaji wa kodi na kuwasisitiza watumie lugha zenye busara pale wanapotakiwa kwenda kuonana na mfanyabiashara kuzungumzia jambo lolote au kukusanya kodi wanapofika kwenye duka lake au sehemu yake ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka niwasihi wafanyabiashara, popote ambako unadhani hutajendewa haki na mtumishi wa *TRA; TRA* yetu inacho chombo cha nidhamu na maadili cha *TRA* ambacho kinapokea malalamiko mbalimbali dhidi ya watumishi ambao hawafuati kanuni na hawana maadili katika kutekeleza jukumu lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mfanyabiashara yeyote, mwekezaji yeyote, mlipa kodi yeyote ambaye pia atakuwa na malalamiko yoyote yale, bado anayo nafasi ya kwenda kwenye chombo chochote cha usalama kutoa taarifa ya jambo ambalo limemkwaza ili pia tuweze kutafuta dawa sahihi ya baadhi ya watumishi ambao hawafanyi kazi yao vizuri kwenye chombo chetu cha *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuwahakikishia wafanyabiashara, wawekezaji na walipa kodi wote, Serikali hii itaendelea kuwapa ushirikiano wa dhati. Serikali hii ambayo sasa tunahitaji kupanua Sekta za Biashara itaendelea kuwaunga mkono kwenye jitihada zenu za kibiashara ili tuweze kupata mafanikio ya maendeleo na kuinua uchumi wetu katika Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali kwa Waziri Mkuu.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nina swali moja kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu napata ufahamu kulikuwa na sera katika nchi yetu ya wataalam, wafanyakazi wale wa nje, zamani walikuwa wanaitwa ma-*TX*. Wafanyakazi wa nje, kulikuwa na sera kwamba wanafanya kazi kwa kupata kibali kutoka uhamiaji cha miaka miwili, wakitegemewa kwamba kipindi hicho wana-*recruit* Mtanzania kwenye kampuni au kwenye kiwanda hicho na baada ya miaka miwili tunatarajia kwamba yule *TX* atakuwa ameshamhitimisha

yule kijana au yule mfanyakazi atakuwa amehitimu na kibali chake kitakoma. Kama huo ujuzi utakuwa bado unahitajika, yaani hapana mtu aliyehitimu, ataongezewa tena miaka miwili kutimiza miaka minne. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hiyo sera bado ipo? Kama ipo, bado inatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba, sera ile bado ipo na Serikali tunaisimamia. Msingi wa jambo hili wa kuwapa muda mfupi hawa watalaam wenye ufundi maalum nchini kwetu katika sekta za kazi, ilikuwa ni kujenga wigo mpana kwa Watanzania kupata ajira na kuweza kusimamia maeneo haya ambayo yanahitaji pia utalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya hili kutoa nafasi kwa watumishi wa nchi za nje kuja nchini Tanzania kufanya kazi ambazo hapa ndani tunakosa utalaam; ndiyo tunapofuata utaratibu huo. Tunawapa miaka miwili ya kwanza, tukiamini kwamba Watanzania waambata watakuwa wameshajifunza utalaam ule na baada ya miaka miwili wanaweza kuondoka. Pale ambapo inaonekana kuna uhitaji zaidi, sheria inawaruhusu kuwaongezea miaka miwili ili tuendelee, lakini mwisho tunaweza kumwongezea mwaka mmoja na kufanya miaka mitano ya mwisho. Baada ya hapo, tunaamini Watanzania watakuwa wameshaweza kupata ile taaluma na kusimamia sekta za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka niwahakikishie, mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunafungua milango ya ajira kwenye sekta zote ikiwemo na utaalam, tutaendelea kuusimamia utaratibu huu wa kupokea watalaam kutoka nje wenye utalaam ambao nchini kwetu haupo ili kutoa nafasi kwa Watanzania kujifunza na baada ya miaka miwili tutataka wale wa kutoka nje warudi nchini kwao ili nafasi zile ziendelee kushikiliwa na Watanzania. Tutaendelea kusimamia Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Waziri Mkuu kuonesha kwamba hiyo sera bado ipo. Kwa uzoefu wangu, utekelezaji wa sera hiyo haupo. Nina mifano, nchi za jirani anapokuja mwekezaji kuwekeza katika nchi hiyo huwa anaruhusiwa kuja na watu watano tu kutoka nchini kwake, tofauti na ilivyo hapa nchini kwetu. Wawekezaji wa kwetu hawana hiyo sera; hawana *limit* ya kuweka wafanyakazi kutoka nchini kwao. Ndiyo hiyo inayosababisha sasa hivi viwanda vingi vinaendeshwa na wageni wakati sisi wenyewe Watanzania tunapoteza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi huo ninao kwa sababu nimefanya kazi kwenye sekta ya watu binafsi siyo chini ya miaka 30 mpaka naingia hapa Bungeni. Tumeshaona wafanyakazi wengi wako zaidi ya miaka 20 wafanyakazi wa nchi za nje. Ukiwauliza vibali vyao havieleweki na wengine kama wanakuja Wakaguzi, wanafungiwa kwenye ma-*godown,* huo ushahidi ninao.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, nipe kauli yako, ni lini Serikali yetu itaweza kufuatilia hili suala ili kuzalisha ajira kwa watu wetu? Lini itaweka sheria kwa wawekezaji kwamba wanahitajika walete wafanyakazi wangapi kutoka kwenye nchi wanazotoka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba jambo hili tunalisimamia tena kwa ukaribu zaidi. Sera aliyoitaja ya nchi za nje ndiyo sera yetu nchini kwamba mwekezaji yeyote anayekuja kuwekeza nchini iwe ni kiwanda au sekta ambayo inahitaji utalaam, tumeruhusu watumishi watano, ndio ambao wanaruhusiwa kuingia kufanya kazi nchini. Sekta zote ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania, tumeweka utaratibu na tunasimamia kwamba sekta zote hizo zitafanya kazi na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna eneo ambalo linalalamikiwa, basi Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane, kwa sababu sekta ya kazi iko ofisi kwangu. Nina Naibu Waziri anayeshughulikia ajira na kazi na nina Katibu Mkuu. Kwa hiyo, ni rahisi pia kufuatilia maeneo hayo ili tuone kwamba tunafungua nafasi hizo kwa Watanzania badala ya kuwa tunajaza raia kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali hii haizuii mashirika ya nje au wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza nchini, lakini lazima wanapofika Tanzania wataendelea kufuata sheria na sisi Serikali tutasimamia sheria hiyo kuwa inatumika ili kufungua nafasi kwa Watanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mwulizaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Oran Njeza; swali kwa Waziri Mkuu.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wakati tunaelekea kwenye msimu mwingine wa kilimo na mvua zimeshaanza kunyesha kwenye maeneo mengi ya nchi yetu likiwemo Jimbo langu la Mbeya Vijijini, lakini pembejeo za ruzuku za kilimo bado hazijawafikia walengwa. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa hizo pembejeo za ruzuku zinawafikia wakulima kwa muda muafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njeka, samahani…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**WAZIRI MKUU:** Njenga!

**MBUNGE FULANI:** Njeza.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:- *(Makofi/ kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya kilimo imeweka utarabu wa kusambaza pembejeo kwenye maeneo yetu kote nchini, pembejeo za mbegu na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeamua msimu huu wa kilimo, kuanzia mwaka huu, kutumia taasisi inaitwa *Tanzania Fertilizer Cooperation Company* ili kupeleka mbolea, lakini pia mashirika mengine kusambaza pembejeo za aina nyingine. Mashirika haya tayari yameshakaa na Wizara ya Kilimo kwa pamoja ili kuweza kuratibu vizuri usambazaji wa pembejeo mpaka kwenye ngazi za vijiji na kuweza kuwafikia wakulima kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwezi uliopita tumeshatoa fedha kwa ajili ya kununua pembejeo na tumekabidhi taasisi zote ambazo nimezitaja ambazo pia zenyewe zinaweza kupata Mawakala kwenye ngazi ya Wilaya kule ili kuwafikishia wananchi kwenye ngazi ya vijiji na msimu huu wa kilimo utakapoanza, wakulima waweze kupata hizo pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote ambao kweli tumejikita kwenye kilimo kwamba, Serikali itaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati na hasa wakati huu ambao mvua zimeshaanza kunyesha katika baadhi ya maeneo, kabla ya mazao husika kulimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kusimamia na tutaendelea kutoa fedha zaidi ili tuweze kupeleka mbolea, mbegu za mazao ambayo yako kwenye orodha ya pembejeo kama ambavyo tumekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua ambazo Serikali imechukua kuhakikisha kuwa wakulima wetu wanapata pembejeo za ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda niulize swali dogo tu la nyongeza. Pamoja na hizo pembejeo za ruzuku, Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi tuliahadi kupunguza bei za pembejeo kwa msimu huu. Je, Serikali imechukua hatua gani au mkakati gani kuhakikisha kuwa kwa msimu huu pembejeo zote zinakuwa na nafuu kwa wakulima wetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli azma yetu Serikali ni kuhakikisha kwamba mkulima anapata pembejeo kwa gharama nafuu, lakini pia kwa wakati ili aweze kulima mazao mengi zaidi ili pia tuondokane na shida ya chakula nchini, lakini pia aweze kuuza mazao hayo pale ambako wanahitaji kuuza kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kifedha ndani ya familia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumesema kwamba Serikali inatoa pembejeo kwa asilimia 25 ya mahitaji ya pembejeo na asilimia zilizobaki mkulima mwenyewe huwa anaweza kuendelea kuongeza ili kuweza kupata pembejeo; hii ni gharama nafuu, lakini tutaendelea kuangalia unafuu zaidi ili kumwezesha mkulima kupata pembejeo kwa gharama nafuu aweze kulima kilimo chenye tija kwa gharama nafuu vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue jambo lako na tuendelee kuingia kwenye Serikali tuone utaratibu wa kuweza kupunguza gharama hizi ili wakulima wetu waweze kulipa fedha kidogo zaidi kuliko ilivyokuwa awali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante, muda wetu umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, majina yalikuwa kama 11 hivi, lakini hayajaweza kufikiwa yote kwa sababu Kanuni zetu zinasema, Waziri Mkuu ataulizwa maswali kwa muda wa nusu saa. Kwa hiyo, nusu saa yetu imekwisha.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante kwa majibu ya maswali. Sasa tunaendelea, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, sasa aulize swali lake.

Na. 31

**Majibu ya Serikali Kupingana na Ahadi ya Mheshimiwa Rais**

**MHE. AHMED A. SALUM** aliuliza:-

Majibu ya Serikali ya Swali Na.1 la tarehe 6 Septemba, 2016 yanapingana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli aliyoitoa wakati akiwa kwenye kampeni katika Jimbo la Solwa:-

(a) Je, kwa nini Serikali inapingana na ahadi ya Mheshimiwa Rais?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ahadi zote za Mheshimiwa Rais unafanyika kupitia mpango wa bajeti iliyotengwa kila mwaka. Hivyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali haipingani na agizo la Mheshimiwa Rais na kwamba Hospitali hiyo itajengwa kama agizo lilivyotolewa. Serikali itaendelea kuweka kipaumbele na kutenga bajeti kuhakikisha ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika jibu la msingi la Swali Na.1 la tarehe 9 Septemba, 2016, azma ya Serikali ni kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa Hospitali ile, ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa shilingi milioni 40 kutokana na ukomo wa bajeti kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais ndani ya kipindi hiki cha utekelezaji wa Ilani, ambapo tunatarajia kuongeza nguvu ya kibajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, swali la nyongeza.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye matumaini kwa wananchi wa Jimbo la Solwa na hasa Hospitali yetu ya Wilaya katika Kata hii ya Salamagazi, Makao Makuu ya Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali hii imechukua muda mrefu, sasa imefika miaka karibu sita na nguvu ya Halmashauri yetu ilifika mahali ikawa haiwezekani kuikamilisha; na kwa kuwa tumeomba fedha hizi kwa muda mrefu; na kwa kuwa Serikali sasa imeahidi kulikamilisha: Je, fedha tunazozihitaji tunaweza tukazipata zote katika bajeti hii inayokuja ya 2017/2018? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri, Jafo mdogo wangu, namwamini, naiamini Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, yeye mwenyewe na Serikali yake yote kwa ujumla, anaweza akawa tayari kuja kutembelea hospitali hii akajionea hatua na nguvu ya Halmashauri yetu tuliyoiweka na kwa nini tunaomba fedha hizo ili Hospitali yetu ya Wilaya iweze kukamilika na kutoa huduma kwa wananchi wetu wa Jimbo la Solwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Ahmed kwa sababu amekuwa akizungumzia sana hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme wazi kwamba nami nilifika katika Mkoa wa Shinyanga, nimebaini changamoto zinazoukabili mkoa huu, hasa ukiangalia kwanza pale tuna Hospitali ya Mkoa, lakini ukiangalia katika eneo hili la Shinyanga Vijijini hakuna hospitali ambayo itaweza ku-*accommodate* idadi kubwa sana ya watu. Kwa hiyo, kinachotokea ni kwamba, wagonjwa wengi sana wanakwenda pale katika hospitali ile. Kwa hiyo, ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika mpango huu wa bajeti ya mwaka huu wa fedha tutahakikisha kwamba, zile shughuli za awali za kuhakikisha kwamba hospitali inasimama, tutajikita nazo hizo. Naomba nimtoe hofu kabisa, tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo. Leo hii asubuhi nilikuwa nafanya mawasiliano na Mkurugenzi kule Shinyanga Vijijini kuona jinsi gani wanajipanga na kuwapa agizo na sisi huku Serikali Kuu tuweke nguvu ya pamoja ili wananchi wa eneo hili waweze kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kiujumla ni kwamba Serikali itajitahidi kwa kadri iwezekanavyo; na katika mchakato wa bajeti nami nitatoa kipaumbele sana kwa sababu nimefika eneo lile, nimebaini changamoto na Mheshimiwa Mbunge muda mrefu alikuwa analipigia kelele eneo hili, lakini kwa bahati nzuri ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo wananchi wana imani kubwa katika hilo na kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameahidi, lazima litekelezwe. Ni jukumu letu sisi Serikali kuhakikisha tunafanya, tusimwangushe Mheshimiwa Rais, ahadi ile iweze kutekelezeka na wananchi wapate huduma ya afya iliyo bora. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saumu Sakala.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la kuuliza.

Katika Kijiji cha Ushongo kilichopo Wilaya ya Pangani, wakazi wake wamejitahidi kujenga jengo la zahanati kadri ya walivyoweza hadi kufikia kiwango cha lenta, lakini kulikuwa na ahadi kuwa Serikali itamalizia jengo hilo pamoja na kuleta huduma muhimu ikiwemo wahudumu pamoja na dawa, mpaka sasa Serikali bado haijatimiza ahadi hiyo ikiwa ni takriban miaka mitatu sasa. Sasa Serikali itatimiza lini ahadi yake hiyo, hasa ukizingatia kijiji hicho hakina huduma ya usafiri wa umma? Wanatumia boda boda na gari za kukodi. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia wazazi… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sakala, umeshasema unashukuru.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba hilo jibu lisiwe tu la hicho kijiji, ujibu kwa ujumla kwa sababu maeneo mengi majengo yamejengwa lakini hayajamaliziwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tumesikia suala hili, ndiyo maana hapa katikati tulizungumza kwamba tunafanya tathmini ya maeneo yote kwa majengo ambayo yamejengwa hayajakamilika na katika upande wa zahanati, tuna takribani zahanati 1,358 ambazo ukiangalia tuna bajeti siyo chini ya shilingi bilioni 78 kuweza kumaliza shughuli hizi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kwamba tulifanya *assessment* ile ili tuweze kujua nini tunatakiwa tukipange katika mpango wa bajeti tuweze kuondoa haya maboma na kujali juhudi kubwa zilizofanywa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Saumu na Waheshimiwa Wabunge wote, katika suala zima la magofu ambayo hayajakamilika yale ya zahanati na vituo vya afya sambamba na hospitali zetu za wilaya, tunaweka mpango mkakati kabambe ambapo tutawaomba Waheshimiwa Wabunge katika mchakato wa bajeti mtuunge mkono ilimradi tuweze kuondoa hivi viporo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini tukifanikiwa hata kwa asilimia 60 kwa hivyo viporo ambavyo vipo *site* huko, tutakuwa tumewezesha kwa kiwango kikubwa kuwapatia wananchi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania afya bora na miundombinu ya ujenzi wa zahanati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Agizo la Kutowasumbua Wafanyabiashara Wadogo Wadogo "Wamachinga"**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akiwa Mwanza alipiga marufuku na kuziagiza mamlaka zinazohusika kuacha kuwasumbua wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Wamachinga:-

Je, Serikali inatekeleza agizo hilo kwa kiwango gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki ya agizo la Mheshimiwa Rais akiwa Mwanza ilikuwa ni kutowahamisha wafanyabiashara wadogo katika maeneo walipo endapo hakuna maeneo mbadala yaliyotengwa kwa ajili ya biashara zao. Mikoa na Halmashauri zimeendelea kutimiza malengo ya kuweka

mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wadogo kwa kutenga maeneo rasmi ya kufanyia biashara na kuboresha yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyotengwa rasmi kwa wafanyabiashara wadogo katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara ni Likonde, Mbae na Mjimwema. Vilevile, Halmashauri inaboresha Soko la Skoya ambalo halitumiki kwa muda mrefu kutokana na kujaa maji wakati wa mvua. Kazi zinazofanyika ni kurekebisha mitaro ya kupitisha maji ili eneo hilo liweze kutumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuzikumbusha Halmashauri zote nchini kutenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo kutokana na umuhimu wao katika kukuza kipato na ajira. Aidha, wafanyabiashara wadogo wanatakiwa kuzingatia sheria na kuhakikisha wanaendesha biashara katika maeneo yaliyotengwa rasmi ili kuepuka usumbufu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nachuma, swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Nimesikitishwa sana na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri pale alivyoeleza kwamba Manispaa ya Mtwara Mikindani imetenga maeneo kama vile Likonde, Mbae na Mjimwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe maeneo haya ni Tarafa mbili tofauti; na siku ya tarehe 21 mwezi wa Nane, Serikali iliweza kubomoa vibanda vidogo vidogo ambavyo vimejengwa katika Kata ya Jangwani, Tarafa ya Mikindani ambapo ni kilometa takribani 10 kwa maeneo aliyoyataja ambapo kuna akinamama wafanyabiashara wadogo wadogo wanauza samaki kihalali kabisa katika maeneo yale. Cha ajabu wale samaki wao wamevunjwavunjwa na kumwagwa. Akinamama wale walikopa pesa kutoka katika mabenki na taasisi mbalimbali za kifedha na mpaka hivi sasa ninavyozungumza hawana uwezo wa kulipa mikopo ambayo wamekopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari hivi sasa afuatane na Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini ambaye anazungumza, aje kuangalia mazingira yale ambayo wale akinamama wamebomolewa maeneo yao ya kuuza samaki ambapo ni mbali takriban kilometa 10 kutoka eneo ambalo amelitaja yeye?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu. Muda wetu unakimbia halafu wengi mnataka kuuliza maswali ya nyongeza, tafadhali muulize maswali ya nyongeza kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maftaha yuko pale *site;* na hapa nimesema majibu ya msingi ya Serikali ni kwamba lazima Halmashauri zitenge maeneo. Hata hivyo, tumezielekeza Halmashauri kwamba, maeneo watakayotenga lazima waangalie kile kitu kinaitwa *accessibility,* yaani ni jinsi gani yatafikika? Ndiyo maana Halmashauri mbalimbali tumezielekeza kwamba ziwasiliane na *SUMATRA* katika maeneo hayo kwamba kuwe na uwezekano hata wa daladala ziweze kufika kwa sababu maeneo mengine unakuta watu wanashindwa kwenda kwa sababu daladala hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba, jana nilipokuwa nikijibu hapa maswali mbalimbali nikasema Mkoa wa Mtwara ni mkoa wangu wa kipaumbele, ni mkoa wa kwanza. Naomba niseme kwamba nimekubali ombi lake, tutakwenda *site,* lengo kubwa ni kuwasaidia hawa Watanzania wadogo wanaotaka kujikomboa katika suala la uchumi. Kwa hiyo, hilo, aondoe shaka ndugu yangu, mimi nitafika *site,* tutakwenda pamoja katika hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kutokana na sababu ya msingi kwamba tatizo la Machinga, yaani wafanyabiashara ndogo ndogo pengine linaweza kuwa endelevu, hasa kwenye Halmashauri zenye miji mikubwa ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Mwanza ambayo ipo Jimbo la Nyamagana, napenda tu kuiuliza Serikali kwamba, pamoja na utaratibu huu mzuri ambao inaelekeza, Halmashauri zetu zimekuwa na changamoto kubwa ya kifedha. Je, Serikali sasa iko tayari kupitia Wizara ya TAMISEMI kuzisaidia Halmashauri kwa namna moja au nyingine kuweza kuboresha maeneo haya na yawe rafiki kwa hawa wafanyabiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mabula kwamba siku zote Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) iko tayari. Ndiyo maana katika nyakati tofauti

tumekuwa tukitoa maelekezo mbalimbali, lakini siyo maelekezo ya maneno peke yake, mpaka ya kiutaalam. Ndiyo maana kuna Halmashauri mbalimbali hivi sasa, wengine wapo katika suala zima la uwekezaji kupitia asasi mbalimbali lakini wanaleta madokezo mbalimbali na miradi yao pale Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), lengo ni kwamba tunayapima, yale ambayo yanaonekana kabisa kama jambo hili litasaidia Halmashauri lakini bila kukwaza Halmashauri hiyo kutokuingia katika mgogoro, tumekuwa tukizisaidia Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Stanslaus kwamba ofisi yetu sisi itashirikiana na Halmashauri zote. Tunajua kwamba zikipata uchumi wa kutosha zitaweza kujiendesha, zitapata *own source* ya kutosha, akinamama na vijana watapata mikopo, uchumi utabadilika. Kwa hiyo, sisi tupo tayari muda wote kuhakikisha Halmashauri zinafanya kazi zake vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafo, nataka niongezee kwenye swali lililoulizwa na Mheshimiwa Mabula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inatambua ukuaji wa miji hii mikubwa na ongezeko la watu wengi wanaokimbilia mijini kwa ajili ya kutafuta riziki, ikiwemo na shughuli hizi zinazofanywa na wafanyabiashara wadogo wadogo. Hata hivyo, Serikali ina programu inayoendelea sasa ya miji mikubwa ya kimkakati ikiwemo na Mwanza ambapo tunatumia kiasi cha karibu shilingi bilioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupanga vipaumbele hivyo, Halmashauri walihusishwa na walibainisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wajitahidi sana katika kuhakikisha kwamba watakapowapangia wafanyabiashara wadogo maeneo ya kufanyia biashara, basi wahakikishe kwamba mabasi madogo madogo yanayoweza kupeleka watu yanaweza kufika katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ni kweli kwamba wamachinga au wafanyabiashara wadogo wadogo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu kwa sababu ni wengi na wanafanya shughuli ambazo zinasaidia uchumi wetu. Hata hivyo, niwasihi na niwaombe wajitahidi kufanya biashara katika maeneo yaliyopangwa. Kufanya biashara kwenye kila eneo ikiwemo barabarani na kuziba barabara ili watumiaji wengine wasitumie barabara,

inaathiri shughuli nyingine za kiuchumi na kwa hiyo faida yao inakuwa haionekani kwa sababu inazuia shughuli nyingine za watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, busara hii wakiwa nayo, pia busara hiyo hiyo ya wajibu wa Serikali kwa maana ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri zao kuwapangia maeneo mbadala yanayofikika na yanayofaa kwa biashara zao, jukumu hilo ni muhimu sana kufanywa na Serikali za maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, swali la nyongeza. Kwa kifupi tafadhali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** nakushukuru sana dada yangu Mheshimiwa Naibu Spika na Mbunge wa Viti Maalum Kinondoni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Wamachinga siyo eneo, ni mazingira ya biashara. Nimekuwa nalisema hili mara zote. Ndiyo maana tulikuwa wakati ule tukisafiri kwenda China, Beijing, mimi kazi ya kwanza naangalia mazingira ya Wamachinga, wapo hawapo? Unakuta wapo. Ukienda *New York* unaangalia Wamachinga; wapo? Unakuta wapo. Kinachotakiwa ni mazingira ya kibiashara. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Uliza swali tafadhali! *(Kelele)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Hebu tulieni ninyi! *(Kelele)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa msingewapa shilingi milioni kumi kumi hawa, zinaharibu Bunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba tusikilizane. Mheshimiwa, uliza swali, una sekunde kumi. Uliza swali!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Msingewapa shilingi milioni kumi kumi hawa, walikuwa wanakwenda vizuri, mmewapa shilingi milioni kumi wanaharibu Bunge sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, uliza swali. *(Kelele)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mambo gani haya, eeh! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie basi tusikilize swali ili tumpe pia nafasi Waziri aweze kusikia. Kwa hiyo, tutulie.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *Yah!* Halafu *you are shouting, why are you shouting?*

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Mbilinyi, usijibizane na Waheshimiwa Wabunge, uliza swali. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Tunajenga nchi hapa!

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Wamachinga siyo eneo, kisayansi tu, mmejenga pale *Machinga Complex* imeshindikana. Wameshindwa kutoka Mchikichini tu kwenda pale *Machinga Complex. (Kelele)*

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Mbilinyi, muda wetu unakimbia. Uliza swali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Aaah! *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba ukae kidogo. Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, mimi ni Mbunge wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, sio Mbunge wa Viti Maalum. Kwa hiyo, lazima kumbukumbu zikae sawasawa. *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Viti Maalum Kinondoni! *(Kelele)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbilinyi, kwamba tatizo la wafanyabiashara wadogo wadogo wanaojulikana…*(Kelele)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi hicho unachofanya sasa ni fujo. Nimempa nafasi Mheshimiwa Waziri ya kuongea kama nilivyokuwa nimekupa wewe. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwelewa Mheshimiwa Mbilinyi kwamba Wamachinga tatizo lao siyo kuwajengea, ila tatizo lao ni mazingira yanayofaa kwa biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nataka nikubaliane naye kabisa kwa sababu Wamachinga hata ukiwajengea sehemu nzuri namna gani, kwa sababu wateja wa Wamachinga wanajulikana. Kama wateja wale hawafiki, ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niziombe Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini, Mheshimiwa Rais amesema wasibugudhiwe hawa; maana yake nini? Watafutiwe maeneo yanayofaa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge; yanayofaa kwa shughuli zao. Kwa hiyo, naweza kusema nimeelewa swali la Mheshimiwa Mbunge na kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafahamu wajibu wao na zilikwishaelekezwa na Mheshimiwa Rais alikwishasema kwamba watengewe maeneo yanayofaa kwa shughuli zao. *(Makofi)*

Na. 33

**Tatizo la Maji Safi na Salama Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya Wilaya sita zenye Majimbo tisa ya uchaguzi, unakabiliwa na tatizo kubwa la maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji safi na salama katika Mkoa wa Ruvuma?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa utekelezaji wa miradi ya maji vijijini ulioanza mwaka wa fedha 2006/2007, Mkoa wa Ruvuma ulipangiwa vijiji 80. Kati ya vijiji hivyo, vijiji 76 vilipata vyanzo vya maji na Vijiji vinne vya Mchoteka, Nakapanya, Mtina na Muhuwesi katika Halmashauri ya Tunduru vilikosa vyanzo. Miradi ya maji katika vijiji 43 imekamilika na miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Mkoa wa Ruvuma umetengewa jumla ya shilingi bilioni 13.17 kwa ajili ya miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na mipango ya kuboresha huduma ya maji katika Miji ya Songea, Mbinga, Namtumbo na Tunduru ya Mkoa wa Ruvuma. Kwa Mji wa Songea, Serikali imekamilisha mradi wa ukarabati wa chanzo cha maji cha Mto Ruhila Darajani kwa gharama ya shilingi

bilioni 2.6 ambapo umeongeza kiasi cha maji lita milioni sita kwa siku. Mradi huo umekamilika mwezi Februari, 2016 na sasa upo kwenye majaribio. Kukamilika kwa mradi huo kumewanufaisha wakazi 164,162 wa Manispaa ya Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mpango wa muda mrefu Serikali imekamilisha usanifu wa kina na uandaaji makabrasha ya zabuni kwa ajili ya uboreshaji huduma ya maji katika Miji ya Tunduru, Namtumbo na Mbinga. Utekelezaji wa miradi hiyo utagharimu Dola za Marekani milioni 7.3 kwa Mji wa Tunduru, Dola milioni 12.08 kwa Mji wa Namtumbo na Dola milioni 11.86 kwa Mji wa Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuuliza Waziri wa Maji, kumekuwa na miradi ya *World Bank* ambayo ilianza mwaka 2013 na miradi hii baadhi yake huwa inatolewa ripoti kwamba tayari imekamilika ilhali maji hayatoki katika maeneo hayo. Napenda kuainisha maeneo ambayo maji hayatoki ikiwa ni pamoja na kumwomba Waziri mwenye dhamana akubaliane nami baada ya Bunge hili twende pamoja kwenye maeneo hayo ili akajionee yeye mwenyewe adha ambayo wanaipata wanawake kuhusiana na miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ni yafuatayo: Litola na Kumbara ni baadhi tu ya maeneo katika Wilaya ya Namtumbo; Wilaya ya Mbinga kuna mradi wa Mkako na Litoha; Wilaya ya Tunduru kuna Nanembo na Lukumbule; lakini pia katika Manispaa ya Songea kupitia SOWASA Kata ya Ruvuma, Subira, Luwiko, Bombambili, Msamala na Matalawe ni maeneo ambayo maji hayapatikani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningependa baada ya Bunge hili tuweze kuongozana akaone mwenyewe kwa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi ngoja tuelewane vizuri, swali lako la nyongeza la kwanza ni kwamba unataka kujua kama Waziri yuko tayari kuongozana na wewe ama swali ni lipi sasa hapo? Halafu swali la pili usilipe maelezo mwanzo tafadhali nenda moja kwa moja kwenye swali. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Nahitaji Waziri niongozane na yeye akaone mwenyewe. *(Makofi)*

Swali la pili, katika Kituo cha Afya cha Lipalamba hakuna maji kabisa na wananchi sasa wameshaanza kujichangisha kwa ajili ya kuchimba mitaro kwa ajili ya kutandika mipira ya mabomba. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutoa fedha kwa ajili ya kununua *roll* mita 30 kwa ajili ya kutandika pamoja na vifaa vyake vya kuungia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ameomba kama niko tayari kuongoza naye kwenda kuona maendeleo ya utoaji wa huduma ya maji katika Mkoa wa Ruvuma. Nakubali ombi lake, nitafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili na katika jibu la msingi, tumesema kweli katika vijiji 80 vipo vijiji ambavyo bado miradi haijakamilika na kwamba iko katika hatua mbalimbali. Sasa kuwa na jibu ambalo ni mahususi kujua kijiji gani tumesema imekamilika na maji hayatoki, hii inabidi tuifanyie *verification*. Haya majibu yanayoletwa inawezekana yakawa sio sahihi, lakini naomba sana Waheshimiwa Wabunge katika vikao vya Halmashauri za Wilaya taarifa hizi za maendeleo ya huduma za maji katika maeneo yale huwa zinatolewa kila robo mwaka, naomba sana tuwe tunahudhuria vikao vile ili tuweze kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kama kuna tatizo la msingi la kisera ambalo Waziri inabidi nijue, naomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kuwasiliana ili tuweze kuona namna gani tutamaliza matatizo ya maji kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Rais alipotembelea Mji wa Makambako aliwaahidi Wanamakambako kwamba atatoa fedha kwa ajili ya kutatua tatizo la Mji wa Makambako kupatiwa maji; naishukuru Serikali kwamba na kwenye bajeti zilitengwa fedha za kutoka India: Mheshimiwa Waziri anawaambia nini Wanamakambako kuhusu fedha ambazo zimetengwa kutoka Serikali ya India kutatua tatizo la Mji wa Makambako kupata maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa kampeni aliahidi kwamba tutaboresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Makambako. Tayari Serikali ya Tanzania pamoja na Serikali ya India imeweza kupata fedha za

kuchangia uboreshaji wa huduma za maji katika Mji wa Makambako. Taratibu za kupata Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu wa kina ili kuweza kujua ni maeneo yapi na usambazaji wake ukafanyika zinaendelea kufanyika na hatua hizo zitakapokuwa tayari, tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Mlundikano wa Mahabusu Gereza la Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Askari Magereza katika Mji wa Tarime wamekuwa wakilalamika kuwepo kwa mlundikano wa mahabusu ndani ya Gereza la Mji wa Tarime. Hii inatokana na mlundikano wa kesi ndani ya Mahakama ya Wilaya kwa kigezo cha upelelezi kutokamilika:-

(a) Je, kwa nini kesi zenye vigezo vya dhamana watuhumiwa wasipewe dhamana ili kupunguza mlundikano wa mahabusu na gharama kwa Serikali?

(b) Je, nini mkakati mahususi wa Serikali katika kuhakikisha Jeshi la Polisi linamaliza upelelezi kwa wakati ili kuweza kupunguza mlundikano?

(c) Je, ni hatua gani zinachukuliwa kwa Askari Polisi ambao wanawababmbikia kesi wananchi na kupoteza nguvu kazi za Taifa kwa kuwafanya wananchi waishi Gerezani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi nchini, chini ya Kifungu 64 cha Sheria na Mwenendo wa Makosa ya Jinai limepewa mamlaka ya kutoa dhamana kwa baadhi ya makosa kabla washtakiwa kufikishwa Mahakamani. Mara nyingi mahabusu wanaendelea kukaa magerezani licha ya makosa yao kuwa ya dhamana kwa kushindwa kukamilisha masharti chini ya Kifungu 148(5),

(6) na (7) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 na masharti mengine yanayotolewa na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya upelelezi ya muda mfupi na muda mrefu nje na ndani ya nchi ili kuwajengea weledi wapelelezi na kufanya upelelezi kufanyika na kukamilika kwa wakati. Aidha, Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa na Wilaya wanaendelea kuboresha mifumo ya usimamizi wa upelelezi na kukagua mafaili mara kwa mara ili kujionea mwenendo wa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa siyo kweli kwamba Askari Polisi hukumbatia kesi za wananchi. Uhaba wa vitendea kazi vya uchunguzi ambavyo hupatikana Makao Makuu tu, vile ambavyo ni vya kisayansi kuchelewa kupatikana kwa majibu ya uchunguzi wa kisayansi kutoka vyombo vingine, ni baadhi ya sababu ambazo zinafanya baadhi ya upelelezi kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, iwapo kuna malalamiko dhidi ya Polisi, uchunguzi hufanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 103 ya Kanuni za Kudumu za Polisi na Askari akipatikana kwa makusudi akawa na hatia, hatua za kinidhamu na kisheria huchukuliwa dhidi yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kiukweli majibu ya Mheshimiwa Waziri yapo kiujumla zaidi na inasikitisha kwa sababu tunapokuwa tunatoa maswali yetu tunatarajia mwende sehemu husika kujua uhalisia wa sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mahabusu waliopo Gereza la Tarime, zaidi ya asilimia 65 ni kesi au makosa ambayo yanatakiwa yapewe dhamana; na kwa kuwa kesi nyingi ni kesi za kisiasa za kubambikwa na nyingine ni kesi za watoto chini ya miaka 15; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alikuja Tarime na hakupata muda wa kuingia Gerezani, ningependa sasa leo mtuambie ni lini Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Katiba na Sheria, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mkurugenzi wa Mashtaka watakuja Tarime kuangalia hali halisi ya mahabusu walioko Gereza la Tarime ili waweze kuondoa zile kesi ambazo jana Mheshimiwa Waziri alikiri kwamba nyingine ni za *juice,* ili Watanzania warudi uraiani na wafanye kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa kuna msongamano mkubwa sana kwenye Gereza la Tarime, *capacity* yake ilikuwa ni watu 260 wakiwa wamezidi sana. Sasa hivi ni zaidi ya watu 600; na kwa kuwa ukitokea mlipuko wa magonjwa tutapoteza Watanzania wengi waliopo kwenye lile

Gereza; na kwa kuwa gereza lile linahudumia Wilaya ya Rorya na Tarime: ni lini sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi mtajenga gereza katika Wilaya ya Rorya, mtajenga Mahakama ya Wilaya kule Rorya ili wale Watanzania wa Rorya waweze kushtakiwa kule na kuhudhuria kesi zao kule ili kuondoa msongamano ambao upo katika Gereza la Tarime? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwape pole timu yangu ya Magereza *(Tanzania Prisons)* kwa kushindwa jana kwa figisu za Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda zilipocheza na Ndanda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mwanasheria Mkuu na Wizara ya Katiba na Sheria tutalifanyia kazi jambo hilo; huo ni wajibu wetu na tumekuwa tukifanya hivyo. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameshafika Mkoa wa Geita, ameshafika Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Kagera na anakuwa na Ofisi ya *DPP* na anakuwa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. Nikubaliane nalo, hilo tutafanya, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba wale ambao kwa kweli wanaweza wakapata namna ya kwenda nje waende nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitofautiane na Mheshimiwa Mbunge kwenye takwimu, anasema asilimia 75 ya kesi ni za Wanasiasa. Natofautiana naye kwa sababu amesema asilimia 75 ni za wanasiasa na wakati ule ule ni za watoto. Huwezi ukawa na asilimia 75 ya wanasiasa na watoto. Kwa hiyo, kwenye hilo siyo kweli na kama kuna *issue specific* ya kesi ya mtu mmoja mmoja, Waheshimiwa Wabunge ninyi ni Viongozi, tusaidiane kupeana taarifa ili tuweze kufanya *intervention* inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujenga gereza Rorya hata Mheshimiwa Mbunge wa Rorya amelisema mara nyingi na ameongelea matatizo wanayopata wananchi wake. Ni kweli wanapata shida kwa sababu mashahidi wanatakiwa kutoka Rorya na ni gharama hata kwa Serikali kuwatoa watu Wilaya nyingine kwenda kutoa ushahidi katika Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo tumelipokea na kama Serikali tunachukua hatua kwa Wilaya zote mpya ambazo zimeanzishwa, ambazo bado hazina huduma hizo za Mahakama pamoja na Magereza, kuhakikisha kwamba tunawapunguzia usumbufu wananchi na sheria iweze kuchukua mkondo wake kwa wakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Masaba, swali la nyongeza.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya Tarime Mjini yanafanana kabisa na Gereza la Bariadi Mjini, msongamano wa wafungwa. Naomba niulize kuwa Mheshimiwa Waziri alifika katika Gereza la Bariadi Mjini, hali halisi aliiona jinsi ambavyo wamesongamana hawa watu na Gereza hili linatumika kwa Wilaya zote tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inajenga Gereza ambalo lina hadhi ya Kimkoa? Kwa sababu kesi nyingine zinasababishwa na Jeshi la Polisi kuwabambikizia watu kesi, wakiwemo Madiwani wa Wilaya ya Itilima, Wenyeviti wa Vijiji, Kiongozi Naibu Katibu Mkuu CHADEMA ambaye alishikiliwa takriban siku 12 bila sababu za msingi akiwa na vijana…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi nadhani umeshauliza swali lako. Sasa ukae Mheshimiwa Waziri akujibu. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea pendekezo ama ombi la Serikali kuangalia upya mazingira ya Gereza la Bariadi, nami nilifika, kuna mambo ya kufanyia kazi pale na sisi kama Wizara tume-*earmark* kwamba kuna jambo la kufanyika ukianzia na nafasi yenyewe ya Gereza, lakini pia na ngome/kuta kwa ajili ya Gereza. Kwa hiyo, hilo tumelipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, sisi ni viongozi. Mimi nimetembelea Magereza, nimeongea na wafungwa na mahabusu. Wale watu ukifika katika mikoa yote nilikotembelea ni mmoja tu ambaye nilipomwuliza kama umefanya kosa ama hukufanya akasema nimefanya. Wengine wote ukiwasikiliza, kama una fursa ya kuwatoa, unaweza ukawatoa dakika hiyo hiyo, wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimekuja kupeleleza baada ya hapo, napeleleza mmoja mmoja; ukipeleleza mmoja mmoja utakuta makosa aliyofanya ni ya kupindukia. Kwa maana hiyo, tunapokuwa tunasemea kwa ujumla wake kwamba Polisi wanabambika kesi, nadhani tuwaamini kwamba wale ni Watanzania ambao wanafanya kazi kwa kiapo. Kama kuna jambo la mtu mmoja mmoja, hayo ndiyo kama viongozi tuyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie kule Magerezani, chukueni muda Waheshimiwa Wabunge; ninyi ni viongozi, nendeni mkawasikilize. Ukiwasikiliza wote unaweza ukadhania Gereza hilo limeshika malaika, lakini ukifuatilia undani wake utaona mambo mabaya waliyoyafanya katika familia nyingine ambayo wanastahili kwa kweli kuwa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, muda wetu umekimbia, Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Khadija Nassir Ali Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Upatikanaji wa *Gauze* na *Drip* Toka Nje**

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI** aliuliza:-

Tanzania tunalima pamba kwa wingi lakini bado tunaagiza *Gauze* toka Uganda ambao hawana zao la pamba, lakini pia tunaagiza *Drip* toka nje ya nchi wakati tuna maji ya kutosha ya kuweza kutengeneza *Drip* hizo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia malighafi hizo ili kuzalisha *Gauze* na *Drip* hapa nchini na kuacha kuagiza bidhaa hizo toka nje?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Khadija alivyotoa mfano wa *gauze* na *Intravenous Fluid* zinazotundikwa wagonjwa na kujulikana kama *drip* tumekuwa tukiagiza bidhaa toka nje ya nchi ambazo kimsingi zinaweza kutengenezwa kirahisi hapa nchini. Ukirejea mkakati unganishi wa maendeleo ya viwanda *IIDS* na Mpango wa Pili wa Miaka Mitano, lengo lake hasa ni kuondoa upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mashirika ya *MSD*, *TIRDO, NHIF, TIB, TFDA* wamepewa jukumu la kuandaa mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Madawa ya Binadamu na Vifaa Tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa bidhaa inayolengwa ni ya *IV Fluids* na *gauze* zitokanazo na pamba. Chini ya uhamasishaji wa Wizara yangu na Kituo cha Uwekezaji *(TIC),* wawekezaji wamejitokeza kuwekeza katika Sekta ya Madawa ya Binadamu na Vifaa Tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako nitaje baadhi ya makampuni ambayo yamejitokeza. *JSN solution* watakaojenga kiwanda cha *IV Fluid*, China *Dalian International group* watakaojenga kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba, *Zinga Pharmaceutical* watakaotengeneza madawa mbalimbali ya binadam; *Boryung Pharmaceutical* kutoka Korea ambao watatengeneza *Penicilin* na *Antibiotics* za namna hiyo; *Agakhan Foundation Network* watakaoanzisha

viwanda vya madawa mbalimbali na *Hainan Hualon* ambao watazalisha madawa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kuwa katika hiki kipindi kifupi, tutaweza kuwa na sekta ya madawa ya binadamu ambayo pamoja na kuzalisha madawa na vifaa tiba itatoa ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Khadija Ali, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Ikizingatiwa azma ya kujenga Tanzania ya viwanda, ni lini Serikali itajenga viwanda hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa nini Serikali isiwekeze kwenye kujenga viwanda vidogo vya *drip* kwenye hospitali za Rufaa za Mikoa nchini ili ku-*supply drip* kwenye hospitali husika kama ilivyokuwa zamani badala ya kuagiza *drip* hizo nje ya nchi jambo ambalo ni aibu kwa Taifa letu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunajenga viwanda na niwatoe wasiwasi Wabunge wenzangu kuna kampuni mbili za *media* zimekubali kunisaidia kujibu maswali ya Wabunge kuanzia kesho. Wataonesha vipindi vyote, kiwanda hiki Mwijage naonyesha, hiki kinajengwa hiki kinajengwa. Hata hivyo, kwenye swali langu la msingi nimeorodhesha makampuni ambayo nimehamasisha, nimepiga *sound,* wakaja kuomba kuwekeza. Kwa hiyo kazi yangu ndiyo hiyo, nimeeleza viwanda vyote hivi wamekuja kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa nini hospitali ndogo zisitengeneze *drip*. Nimshukuru Mheshimiwa Khadija, hospitali za kwetu nchini ukienda Tabora, Kagondo, Bugando wanatengeneza *drip*. Nitumie fursa hii kama kuna hospitali yoyote ambayo inataka kwenda kupata ile mitambo ya kutengeneza *drip* iwasiliane na Wizara ya Afya tuna utaratibu maalum. Viwanda vya kutengeneza *drip* siyo pesa za ajabu, ndiyo vile viwanda wanavyosema Mwijage anatembea navyo mfukoni, kweli ninavyo. *(Makofi/Vicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumepata changamoto ya muda, kwa hiyo mniwie radhi inabidi tuendelee, maswali ya nyongeza yataulizwa na wale wenye maswali, kwa sababu muda wetu umebaki kidogo. Mheshimiwa

Godbless Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Na. 36

**Umuhimu wa Kiwanda cha *General Tyre* Kuanza Uzalishaji**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y MHE. GODBLESS J. LEMA)** aliuliza:-

Mahitaji ya tairi za magari katika Mkoa wa Arusha na Tanzania kwa ujumla ni makubwa. Mpango wa Serikali kufufua kiwanda cha tairi cha *General Tyre* unaonekana kwenda taratibu:-

(a) Je, ni lini Serikali itatambua umuhimu wa kiwanda hicho kuanza uzalishaji mapema;

(b) Wapo baadhi ya waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho bado hawajalipwa mafao tangu kiwanda kifungwe: Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahakikisha wafanyakazi hao wanalipwa stahili zao?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua na kuthamini uwepo wa kiwanda cha kutengeneza matairi nchini. Ili kutimiza azma hiyo, Wizara yangu kama tulivyoelekeza katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017 tumeanza jukumu hilo kwa kubaini mambo ya msingi tunayopaswa kuzingatia katika kujenga kiwanda cha matairi ambacho imara na shindani. Baada ya taarifa ya kitaalam *(Roadmap)* ambayo itakamilika wakati wowote, kwa kushirikisha ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwepo Kamati ya Bunge inayosimamia Viwanda, Biashara na Mazingira, uamuzi juu ya uwekezaji utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kiwanda cha matairi ili kutekeleza dhima ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kiwanda hiki kitatoa ajira, kitazalisha bidhaa bora, salama na imara na kwa kuzalisha tairi nyingi tutaokoa fedha za kigeni zinazotumika sana kuagiza matairi kutoka nje ya nchi. Pia uwepo wa kiwanda hicho ni kichocheo kwa soko la malighafi ya mpira ambalo tuna fursa ya kuzalisha kwa wingi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, mtupe muda tusimamie kikamilifu utekelezaji wa jukumu hili muhimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, umuhimu wa kiwanda hiki cha matairi unajulikana na uwepo wa kiwanda hiki kufufuliwa katika Mkoa wa Arusha utaongeza ajira, lakini katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 60, mpaka tunapoongea imetolewa shilingi bilioni mbili tu. Je, kwa Serikali hii ambayo imefilisika kuna dhamira ya kweli kufufua kiwanda hiki?

Swali la pili; kuna wafanyakazi ambao bado wanakidai kiwanda hiki na madai yao wameshayafikisha Hazina, lakini mpaka leo hawajalipwa. Je, ni lini sasa madai haya ya wafanyakazi yatalipwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na lile gumu la madai ya wafanyakazi. Mheshimiwa Mbunge naomba nakala ya madai iliyopelekwa kwa *Treasury Registrar*, nipewe nakala hiyo, mimi nitafuatilia. Naomba Mheshimiwa Mbunge anifuatilie mimi na mimi nimfuatilie *Treasury Registrar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza juu ya dhamira ya kweli, Serikali hii ina dhamira ya kweli na nitumie fursa hii, kwamba Tanzania kuna soko la matairi siyo habari mpya, kwamba sisi ni sehemu ya Afrika Mashariki, *it is not the news*, kwamba sisi tuko *SADC* siyo tatizo, tumeelekezwa katika Ilani ya Chama chetu na Mpango wa Pili wa Miaka Mitano *General Tyre* ifufuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kama kuna mtu yeyote ana mwekezaji, anataka kujenga kiwanda mimi nitahakikisha nitajenga kiwanda, Mheshimiwa Rajab Adadi na Mheshimiwa Stephen Ngonyani (Majimarefu) wamekuwa wakinifuatilia, fursa ipo, sisi kazi yetu ni kuweka mazingira wezeshi, kupiga *sound* ili kusudi wawekezaji waje wawekeze, Serikali haitajenga kiwanda inatengeneza mazingira wezeshi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Sasa tunaelekea Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Flatei Gregory Maasay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 37

**Hospitali ya KKKT Haydom kuwa Hospitali ya Kanda**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Hospitali ya KKKT Hydom ilipanda hadhi kuwa Hospitali ya Mkoa muda mrefu, sasa inahudumia Mikoa ya Manyara, Shinyanga, Singida, Arusha na Simiyu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi ili iwe Hospitali ya Kanda kuiwezesha kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Hospitali ya KKKT Haydom ilipandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa ngazi ya Mkoa mwaka 2010. Aidha, hospitali hii haikupandishwa hadhi ili iwe Hospitali ya Mkoa. Mkoa wa Manyara una Hospitali yake ya Rufaa ya Mkoa. Madhumuni ya kuipandisha hadhi Hospitali hiyo yalikuwa ni kuifanya itoe huduma za ngazi ya rufaa ya Mkoa ikisaidiana na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara. Ili hospitali iwe ya rufaa ngazi ya Kanda, ni lazima iwe na miundombinu bora tofauti na iliyopo sasa, pamoja na watumishi waliopata mafunzo yanayohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Kaskazini tayari kuna hospitali zinazotoa huduma za kibingwa kama *KCMC* ila kwa vigezo vingine Hospitali hii imeshakaguliwa na imeonekana ina upungufu kadhaa, pale utakapokamilika itatoa huduma hizo. Aidha, hosptiali ya KKKT Hyadom toka awali ilikuwa inahudumia wananchi wa mikoa iliyotajwa. Hali hii inachangiwa na sehemu ya kijiografia iliyopo hospitali hiyo kwani inafikika kirahisi na wananchi wa mikoa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri amefika katika hospitali ya Hydom, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba hospitali hii imepandishwa hadhi miaka sita toka 2010 hadi leo ya kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na haijapata hata siku moja ile haki ya kibajeti

ya hospitali ya Mkoa. Je, sasa ni lini hospitali hii itatengewa bajeti ili ifanane na hospitali zote za Rufaa za Mikoa ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa kwenye majibu ya msingi amesema hospitali hii ina tatizo la miundombinu na watumishi. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuijengea uwezo na kuipatia watumishi ili hospitali ya Haydom iweze kutoa huduma kwa sababu na yeye amekiri kwamba inafikika na maeneo ya jirani na mikoa hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Flatei Massay kwa ufuatiliaji anaoufanya kiasi kwamba amenilazimisha kufika kwenye hospitali hii katika ziara zangu mara mbili toka nimeteuliwa katika nafasi hii. Katika mara zote nimefika na kutatua changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiikabili hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, pamoja na kwamba hospitali hii ingependa iwe Hospitali ya Rufaa ya Kanda bado haijakidhi vigezo. Pili, kuteuliwa kuwa hospitali ya ngazi ya Kanda hakuifanyi hospitali kudai haki ya kupewa fedha kibajeti wakati haimilikiwi na Serikali. Serikali inashirikiana na mashirika ya hiyari kama KKKT kutoa huduma kwa wananchi kwa kuwawezesha kupata michango ya *health basket fund* pamoja na watumishi ambao wanapelekwa *by secondment* na Serikali kwenye hospitali husika. Kwa sasa, Mkoa wa Manyara una hospitali yake ya rufaa ya mkoa na Serikali inaijengea uwezo hospitali hii ili iweze kutoa huduma ambazo zinaendana na hadhi ya hospitali ya rufaa ya mkoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munira Mustafa Khatibu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 38

### Kuanzisha Vituo Maalum vya Watoto Wanaozaliwa Kabla ya Muda

**MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vituo maalum vya kulelea watoto wanaozaliwa kabla ya wakati kuliko ilivyo sasa ambapo huchanganywa na watoto wenye matatizo mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munira Mustafa Khatibu, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba wa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya wakati wanayo mahitaji maalum ukilinganisha na watoto wengine. Matatizo yanayoambatana na kuzaliwa kabla ya wakati au uzito pungufu yaani chini ya kilo 2.5 yanachangia kwa asilimia ishirini na tano ya vifo vya watoto wachanga nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwamba Serikali wameshindwa kuweka sehemu yao ila imeonekana kuwa ni msaada kuwafanya waweze kupona na kukua katika uhalisia na mazingira bora kama watapewa huduma na wazazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilianzisha huduma ya matunzo ya mtoto mchanga aliyezaliwa kabla ya wakati kwa kumbeba kifuani ngozi-kwa-ngozi yaani *Kangaroo method* na huduma hii ilianzishwa katika hospitali zote za mikoa na baadhi ya hospitali za wilaya na hivi sasa tuna vituo vipatavyo sabini vinavyota huduma hii muhimu hapa nchini. Wizara inaendelea na kazi hii ya kuanzisha vituo hivi kwa kasi zaidi na tunategemea kuanzisha vituo vingine zaidi katika hospitali za wilaya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kwa ufadhili wa fedha za *RMNCH Trust Fund*, Wizara imenunua vifaa mbalimbali ili kurahisisha uanzishaji wa huduma hii. Vifaa hivyo ni pamoja na vitanda maalum vya kutolea huduma hii, vikombe vidogo vya kulishia watoto hawa ambao mara nyingi hushindwa kunyonya ipasavyo, vipima joto maalum *(low reading thermometers),* mizani ya kupima uzito na watoto wachanga na mablanketi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munira, swali la nyongeza.

**MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri ambayo amenijibu, lakini napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Je, ni utaratibu gani uliotumika kugawa hivi vifaa katika hospitali zetu za wilaya na mikoa kwa sababu vifaa hivi ndani ya hospitali zetu za wilaya na mikoa havionekani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, ni utaratibu gani unaotumika kuwapa elimu akinamama wajawazito kuweza kuwalea watoto hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI, WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza *Kangaroo Mother Care* haihitaji vifaa vyovyote vile, kwa sababu ni huduma ambayo inatolewa na aidha mzazi mama, baba, ama mtoa huduma yeyote yule ambaye atakuwa amechaguliwa na familia kutoa huduma hiyo. Huduma hii inahusisha kumchukua mtoto kumweka kifuani ngozi kwa ngozi na mzazi huyo, mara nyingi inakuwa ni mama. Kwa maana hiyo, hakuna vifaa vinavyohitajika pale zaidi ya mashuka na mablanketi ambayo yanagawanywa kwenye hospitali zote nchini kwa utaratibu wa kawaida wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa kupitia Wizara ya Afya ina *encourage* zaidi kutoa huduma kwa kutumia njia hii ya *Kangaroo Mother Care* na ndiyo maana hatuwekezi sana kwenye kujenga vituo maalum pembeni kwa ajili ya kuwatenga watoto na wazazi wao, kwa sababu imeonekana wakikaa na wazazi wao wanajengwa afya zao kisaikolojia zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Barabara ya Mkiwa-Rungwa-Makongorosi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Barabara ya Mkiwa – Rungwa - Makongorosi ni ya udongo na nyakati za mvua barabara hiyo inaharibika sana kiasi cha kutopitika kabisa:-

Je, Serikali ina Mpango gani wa kuitengeneza barabara hiyo kwa lami ili kuwaondelea kero wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi hususan wa Kata za Mwamagembe, Rungwa na Kijiji cha Kitanula.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mkiwa - Rungwa - Makongorosi ni sehemu ya barabara kuu ya kutoka Mbeya – Chunya – Makongorosi - Rungwa - Itigi hadi Mkiwa yenye urefu wa kilomita 413. Kati ya hizo kilometa 219 zimo katika mtandao wa barabara Mkoa wa Singida na sehemu kubwa ikiwa katika Jimbo la Manyoni Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mbeya hadi Chunya kilometa 72 umekamilika. Barabara ya Mkiwa - Rungwa hadi Makongorosi ni ya changarawe na hupitika kipindi chote cha mwaka isipokuwa sehemu korofi katika maeneo ya Kintanula na Mwamalugu katika Mkoa wa Singida ambazo husumbua wakati wa kipindi cha mvua nyingi kutokana na hali ya kijiografia na udongo unaoteleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Nchini *TANROADS* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami barabara hiyo. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 5.848 kwa ajili ya kuanza sehemu ya barabara sehemu ya Mkiwa – Itigi - Noranga ambazo ni kilometa 57. Tumetenga shilingi bilioni 8.848 kwa ajili ya kuanza ujenzi sehemu ya Chunya - Makongorosi ambayo ni kilometa 43. Aidha, zabuni kwa ajili ya kazi hizi zinatarajiwa kuitishwa mwezi huu Novemba, 2016.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa katika barabara hii korofi kipindi chake cha kuharibika sasa kimekaribia, kipindi cha mvua ambacho katika maeneo ya Lulanga, Itagata, Ukimbu, Mitundu, Kiombo, Mwamaluku, Mwamagembe, Kintanula hadi Rungwa udongo huo aliousema ni mbaya na ukarabati uliofanyika kipindi cha nyuma ulikuwa haukidhi kiwango. Je, sasa Serikali iko tayari kufanya marekebisho ya kutosha katika kipindi hiki kabla mvua hazijaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika ujenzi wa kipande hiki cha kilometa 57 ambacho Meshimiwa Naibu Waziri amekisemea hapa, watakapoanza wanatarajia ni muda gani utachukua kukamilika? Maana yake wananchi wanahamu kubwa ya kuona barabara ya lami katika kipande hiki nikiwemo mimi Mbunge wao.

Mhesshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya Bunge hili nitakuwa na safari ya kuipitia barabara hii. Nitamjulisha Mheshimiwa Mbunge tarehe kamili nitakapokuwa katika eneo lake ili tusaidiane kutambua kwa karibu zaidi na kwa macho siyo kuandikiwa tu, hatimaye tuhakikishe tunaposimamia hatua za marekebisho ambazo Mheshimiwa Mbunge anazihitaji tuweze kuzisimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini tutakamilisha, nimwombe Mheshimiwa Mbunge ajue dhamira ya Serikali hii ya kuikamilisha hii barabara, aone kama ambavyo tumejibu katika swali la msingi maeneo ambayo tayari tumeyakamilisha na tupo katika kuendelea kukamilisha maeneo yaliyobaki. Naomba atuamini, kusema ni lini huwa naogopa sana kwa kazi hizi za ujenzi ambazo zina *process,* lazima upate hela na hatimaye ujihakikishie kipande gani kinakamilika kwa wakati gani. Naomba aniwie radhi kwamba hiyo kazi ya kusema lini hasa siyo rahisi sana. Kikubwa tuna dhamira ya dhati na tutakamilisha kujenga hii barabara kama ambavyo kwenye Ilani imeeleza. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu, lakini hizi fedha zilizotengwa hapa zimeandikwa kwamba mnaanza ujenzi. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba pengine hawa *TANROADS* bajeti ijayo hizi barabara ulizozitaja hazitasahaulika kama ambavyo zimeahidiwa kwenye Ilani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi.

Na. 40

**Daraja la Kigamboni na Jina la Baba wa Taifa.**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Hivi karibuni tumeshuhudia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua Daraja la Kisasa la Kigamboni ambalo limepewa jina la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ambaye hakuwahi kuishi Kigamboni;

Kwa nini daraja hili halikupewa jina na Rais Mstaafu wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu wa Muungano, Mheshimiwa Aboud Jumbe ambaye ana historia kubwa katika Mji huo kwa kuishi karibu miaka 32.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kigamboni una historia ndefu kwa viongozi mbalimbail wa Taifa letu wakiwemo Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Hayati Rashid Mfaume Kawawa na Hayati Aboud Jumbe na wengine wengi. Daraja la Kigamboni lilipewa jina la daraja la Nyerere kwa heshima ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kutokana na mchango wake mkubwa kwa maendaeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba wazo la ujenzi wa daraja la Kigamboni lilianza wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza ambapo katika mipango ya maendeleo ya miaka 60, Serikali chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ilianza mikakati ya ujenzi wa madaraja makubwa matano ya Kigamboni, Rufiji, Malagarasi, Kirumi na Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna barabara, madaraja na miundombinu mbalimbali ya umma iliyopo na inayoendelea kujengwa. Mheshimiwa Mbunge anaweza kupeleka mapendekezo katika mamlaka zinazohusika ili moja ya barabara, daraja au miundombinu iliyopo au itakayojengwa iweze kuitwa kwa jina la Aboud Jumbe kadri itakayoonekana inafaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku Ayoub, swali la nyongeza.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa kutokana na mchango mkubwa wa maendeleo wa Taifa wa Baba Hayati Mwalimu Nyerere ni mkubwa nikiri hivyo, lakini nataka kuweka *Hansard* sawa. Rais Marehemu Aboud Jumbe ni Rais aliyefungua demokrasia mwanzo Zanzibar ikiwemo Baraza la Wawakilishi la Katiba ya Zanzibar. Lakini kumbukumbu nyingi zinaonyesha Baba Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anazo ikiwemo Ukumbi wa Mkutano wa Kimataifa, Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa kuitwa jina lake, Mfuko wa Taasisi ya Fedha, kuna barabara hata Zanzibar zipo zinaitwa Baba Nyerere. Leo kweli tunamtendea haki Hayati Aboud Jumbe Mwinyi mtu aliyeishi karibu miaka 32 na kila mmoja Mtanzania anajua aliishi kule Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuteleza siyo kuanguka, kutokuwa na meno siyo uzee, je, Serikali imesema ipo tayari kuchukua mapendekezo yangu na kubadilisha jina hilo? Hilo la kwanza.

Pili, je, kwa nini Serikali haikutafakari mapema na badala yake Serikali inasubiri mapendekezo kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge. Lini Serikali ya Jamhuri ya Muungano itawaenzi viongozi wetu kwa kuweka historia katika kumbukumbu ili vizazi vijavyo vikaja kuwa na historia hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku naona umeuliza maswali matatu hapo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano jibu maswali mawili tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ambaye hatambui michango ya viongozi wetu wa Kitaifa wote, nimwombe tu, bahati nzuri yeye ni Mbunge wa Baraza la Wawakilishi na nina hakika anafahamu kwamba tuna *forum* kati ya Serikali hizi mbili, tuombe tuzitumie zile *forum* kama kuna kitu anadhani kina tatizo, tuweze kukijadili na kukirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana kama kuna daraja lingine, kama kuna barabara nyingine, tafadhali wewe tuambie ili tuweze kuangalia uwezekano wa kutumia hilo jina kwa hilo eneo ambalo hata ninyi watu wa Baraza la Wawakilishi mtaridhika nalo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara na Waheshimiwa wote mliosimama naomba mkae. Waheshimiwa Wabunge kila wakati tunakumbushana anayekuwa anaendesha kikao cha Bunge akiwa amesimama haruhusiwi mtu mwingine kusimama, unasimama mimi nikiwa nimekaa, tunakumbushana kila wakati jambo hili, tuzingatie Kanuni tafadhali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naleta kwenu matangazo yaliyopo mezani kabla hatujaendelea, tunayo matangazo ya wageni waliotufikia asubuhi hii.

Wapo wageni waliopo jukwaa la Spika, ambao ni wageni watano wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Ruangwa Mkoani Lindi, wakiongozwa na Ndugu Kasambe Hokororo ambaye ni Katibu wake Jimboni. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 10 wa Mheshimiwa John Peter Kadutu ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Ulyankulu Mkoani Tabora wakiongozwa na Ndugu Ahmed Kombo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ambaye ni Mwalimu na mdau wa mambo ya elimu kutoka Maswa Mkoani Simiyu na huyu ni Ndugu Grace Ball. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Mary Nagu ambao ni Umoja wa Mama Ntilie kutoka Mkoani Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Mwanahamisi Mwandoro ambaye ni Mwenyekiti wao, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni marafiki zake kutoka Mkoani Dar es Salaam, Ndugu Madonna Pemba na Ndugu Consolata Richard. Karibuni. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni mpiga kura wake anayesoma Chuo Kikuu cha Dodoma, anayeitwa ndugu Onesfoa John. Karibu. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambaye ni mtoto wake kutoka Liwale Mkoani Lindi na huyu ni Ndugu Hamisi Z. Kuchauka. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 13 kutoka Shirikisho la Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu kutoka Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nililetewa tangazo hapa kwamba wapo wageni waliotoka Kondoa sijui wapo wapi hawajaletwa humu, wageni kutoka Kondoa wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge, labda niwaombe mwongeze makofi, hawa ni *best performers* wanaotoka kwenye hilo Jimbo la Mheshimiwa Ashatu Kijaji, karibuni sana binti zetu na mwendelee kujibidiisha katika masomo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ambaye anasema alisahau simu yake aina ya *Samsung S5* ndani ya Ukumbi wa Bunge, aliyeokota au kuiona anaomba amrudishie tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya nikumbushie tu ili baadaye itakapotokea tusije tukajisikia vibaya.

Mheshimiwa Spika katika Bunge lililopita alikuwa ametoa maelekezo kuhusu kutambulishwa wageni ndani ya Bunge, jambo hili leo wametangazwa wote kwa majina yao kwa sababu bado linafanyiwa kazi, lakini litakapokamilika, tutaachana na huu utaratibu wa kutangaza wageni kwa majina yao. Kwa hiyo, tutaacha hilo zoezi la kutangaza wageni, tutawatambua tu uwepo wao katika Bunge. Kwa sasa hivi kwa kuwa bado linafanyiwa kazi, ndiyo maana bado tunasoma, lakini tutakapoacha lisije likaleta tatizo kwa Waheshimiwa Wabunge na pia kwa wageni wetu. Tunaendelea.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7) ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wanaifahamu sihitaji kuisoma kwa sababu ya muda, juu ya jambo ambalo linakuwa limetokea hapo kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa maswali na majibu kwa Waziri Mkuu leo asubuhi Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni aliuliza suala zito sana linalohusu fedha zilizotolewa kwa Wabungae wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hilo ambalo liliulizwa kwa Waziri Mkuu wewe ulilitolea mwongozo papo hapo kwamba suala lile siyo la kisera, isipokuwa ulikuwa unataka suala la kisera. Wakati Kiongozi wa Upinzani akiendelea kusema hapa mbele yako alijaribu kukuainishia sheria alikuonyesha za rushwa kwa sababu fedha hizo zilikuwa zinaambatana na rushwa juu ya Muswada wa Habari ambao unakwenda kuanza siku ya kesho.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walipiga kelele za kuzomea)*

**MBUNGE FULANI:** Hatujapewa hiyo hela sisi.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala hilo…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Tutasikilizana tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde endelea.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala hilo lililoletwa ndani ya Bunge ni suala zito sana na Kiongozi wa Upinzani Bungeni na halikupatiwa majibu sahihi wakati linaulizwa. je, ni kwa nini sasa, pamoja na kwamba umesema kwamba suala hilo siyo la kisera lakini kwa sababu limehusu tuhuma nzito na linachafua mhimili wa Bunge na Wabunge, ni kwa nini sasa isiundwe Tume huru ya Kimahakama ya Kibunge ili suala hilo lifanyiwe uchunguzi ndani ya Bunge lako Tukufu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako juu ya jambo hilo ambalo limetokea hapo asubuhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimeshasema unione na mimi hapa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia naomba utulie kidogo, Mheshimiwa Waitara hii nyumba jamani inaendeshwa kwa taratibu, akionwa mwenzio usione kana kwamba wewe unaonewa, wewe kama nimekuona nitakupa nafasi, kama sikukupa nafasi pia Kanuni zinaniruhusu. Sasa nimemruhusu Mheshimiwa Silinde ameongea na ni wa upande wako sasa wewe ukitaka kufanya vurugu humu ndani tutakuwa hatuendi Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niombe mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kwa sababu ya muda naomba nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, leo asubuhi wakati wa maswali ya papo kwa papo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha CHADEMA ndugu yangu, rafiki yangu Freeman Mbowe aliuliza swali kwamba Wabunge wa CCM tumepewa rushwa na Mheshimiwa Rais ya shilingi milioni 10 kila Mbunge, mimi pia ni mmoja kati ya Wabunge wa CCM kwa bahati mbaya sana sikuziona na wala sijapewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu Chama chochote cha siasa kina taratibu zake, Wabunge wa CCM kila mwezi tunakatwa fedha, Wabunge wa CHADEMA wanakatwa fedha, Wabunge wa *CUF* wanakatwa fedha, vivyo hivyo kwa wale wengine wawili kupitia vyama vyao. Kila chama kinapata

ruzuku na ruzuku hii anayeikagua ni *CAG,* hata kama hizo fedha kweli zingetolewa ambaye alikuwa na mamlaka ya kuhoji ni *CAG* ili kujua matumizi yake na sio Kiongozi wa Chama cha Siasa ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiongozi wa Chama cha Siasa ambaye ni Mbunge kuja ndani ya Bunge na kumtuhumu Mheshimiwa Rais kwamba ametupa rushwa Wabunge wa CCM. Bahati nzuri hata Mheshimiwa Silinde wakati anaomba mwongozo hapa amesisitiza juu ya jambo hili, naomba mwongozo wako, hivi sisi Wabunge wa CCM tukienda kuhoji michango ya 1.7 *million* wanaochanga Wabunge wa CHADEMA kwa ajili ya Chama chao, naomba mwongozo hapa ndani ya Bunge, kwamba hizo fedha wanazochanga kila mwezi Wabunge wa CHADEMA kukichangia Chama chao watoe maelezo hapa ndani ya Bunge zinatumikaje siyo rushwa, hilo litakuwa halali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, una haraka ya nini tulia wewe hayakuhusu mhh!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia naomba usijibizane na Wabunge, wewe ongea na mimi.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mara nyingi huwa sipigizani kelele na watu. Mwisho je, Mbunge mwenzangu pale rafiki yangu Mheshimiwa Mbowe anaweza kuthibitisha ndani ya Bunge hili kwamba kweli Wabunge wa CCM tulipewa milioni 10 kila mmoja na kama hawezi kuthibitisha ni hatua gani atachukuliwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Lipumba wa *CUF* akaja hapa akaanza kuhoji matumizi ya fedha ya CCM, akaja hapa eeeh! Kweli tutakwenda? Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Lipumba sio *CUF*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo na Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Nkamia ambayo kwa sehemu kubwa inashabihiana kwa sababu inaongelea jambo moja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu tulizojiwekea wenyewe na Kanuni hizi zinatoa fursa kwa Mbunge yeyote ambaye jambo likiwa limetokea Bungeni kuomba mwongozo wa Kiti kama hilo jambo linaruhusiwa ama la! Sasa nianze na mwongozo wa Mheshimiwa David Ernest Silinde ambaye ameomba mwongozo kwa kuzuiwa kujibiwa kwa swali lililokuwa limeulizwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kuhusu swali lake alilokuwa ameliuliza. Kwa sababu wote tulikuwepo

sina haja ya kurudia, lakini katika hayo machache nirudie aliyoyarudia Mheshimiwa David Ernest Silinde wakati akiomba mwongozo kwamba rushwa imetolewa kwa ajili ya Muswada wa Habari.

Waheshimiwa Wabunge, lazima sisi kama sehemu ya Viongozi tuwe makini na taarifa na maneno tunayoyatumia. Ukisema rushwa wote tunajua wazi viko vyombo mahsusi kwa ajili ya kushughulika na masuala ya rushwa. Kwa hivyo, Bunge hili haliwezi kujiweka mahali ambapo linaweza sasa kuanza kusikiliza tuhuma ama kesi za rushwa. Kwa hivyo, kama kuna tuhuma ama kesi za rushwa nitoe tu ushauri kwamba ziende huko, lakini kwa kuwa nimeombwa mwongozo nilizuia jambo hili kujibiwa kwa kuwa Bunge wala Waziri Mkuu hawana mamlaka kuongelea mambo ya rushwa ambayo kuna chombo mahsusi cha kushughulika nayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge lisingeweza kuanza kujibizana mambo ambayo ni tuhuma na ambazo ni lazima zipitie vyombo mahsusi zikathibitishwe huko, ndiyo Bunge hili ambalo ni maalum lifanye kazi hiyo. Haliwezi kuwa linafanya kazi kwa mambo ambayo hatuyajui wala hatuna namna ya kuthibitisha kama Bunge zima, lakini mtu binafsi ama chombo fulani anaweza kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu ni huo kwamba nililikataa hilo jambo kwa kuwa linahusu mambo ambayo Bunge halina mamlaka nayo.

Mwongozo mwingine ulioombwa ni wa Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia ameeleza mambo mengi akieleza hapo hapo kwenye fedha ambazo zinadhaniwa ama zinasadikiwa kwamba, Wabunge wa CCM wamelipwa ameeleza mambo kadhaa lakini amesema je, Mheshimiwa Mbowe ana uwezo wa kuthibitisha jambo hilo!

Waheshimiwa Wabunge, maelezo niliyotoka kutoa kwa mwongozo alioomba Mheshimiwa Silinde, mimi kama niliyekalia Kiti leo sitamtaka athibitishe kwa sababu jambo hilo nililizuia tangu asubuhi kutoa majibu, kwa hiyo hatathibitisha jambo lolote na mimi sitamtaka athibitishe lakini kama kuna ushahidi basi upelekwe kwenye vyombo vinavyohusika Bunge litashughulika nao wakati huo. Kwa sababu wote tunajua anayefanya mambo hayo yote ni nani na kama kuna sababu sisi wote kama Viongozi wa Umma kama kuna mtu atakuwa amevunja taratibu na sheria zinazotuhusu ambavyo Mheshimiwa Mbowe alitukumbusha, basi tutaendelea na taratibu hizo ili wote sasa tutoke madarakani kwa sababu tutakuwa tumevunja hiyo sheria, lakini ni mpaka chombo kinachohusika kifanye kazi yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa tunaendelea. Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa sasa tunaendelea, Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali Pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Tunaendelea na uchangiaji wa Mpango kwa mujibu wa Kanuni ya 94. Nimepata majina kadhaa hapa kutoka vyama mbalimbali kwa hivyo, nitakuwa nikiita kwa kadri yalivyo hapa mbele. Tutaanza na wachangiaji kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tutaanza na Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Molel.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Mpango huu muhimu wa leo. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kuwashukuru Wabunge wenzangu wa CHADEMA kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu na nawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisaidiana hapa Bungeni na nimepata taarifa kuna karatasi zinatembea hapa upande mwingine wa kumchangia mpiga kura wangu Mzee Wassira na mimi Mbunge wake naombeni pia nishiriki kumchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba niende kuzungumzia Mpango…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya samahani kidogo, muda uliotolewa kulingana na idadi ambayo nimeletewa kutoka upande wa CHADEMA mnagawana dakika, kwa hiyo utakuwa na dakika saba na nusu ndiyo kwa *list* niliyonayo hapa, karibu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tunapopanga mipango kama Taifa lazima tupange maeneo yanayogusa watu wengi na katika Taifa letu maeneo yanayogusa watu wengi ni sekta ya kilimo, takribani asilimia 80 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miaka mitatu mfululizo tumekuwa tukipanga trilioni 2.7 kwenda katika sekta ya kilimo, lakini zikatengwa bilioni 371, zilizotoka milioni 250 sawa na asilimia tisa, sasa kama tunapanga kutoka trilioni 2.7 kwenye sekta inayoajiri watu wengi tunatoa asilimia tisa tuna dhamira ya dhati ya kumkomboa Mtanzania! Haya ndiyo mambo ya msingi Wabunge wenzangu tujiulize na hasa sisi tunaotoka Majimbo ya Vijijini ambayo yanaitwa Mjini leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipanga hapa huko kwenye sekta ya kilimo tufikie asilimia 10 hatukufika, tukapunguza asilimia sita hatukufika, ikawa asilimia 3.2, leo kwenye sekta ya kilimo iko asilimia 2.3, tunaenda mbele tunarudi nyuma. Tuna mpango kweli wa kuhakikisha hii sekta inaondoa umaskini katika Taifa letu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitatu mfululizo asilimia tisa kwenye sekta inayowaajiri watu wengi, halafu tukija kuongea hapa watu tunapiga bla bla! *Please* Mheshimiwa Mpango naomba apange na atekeleze kama kazi yake ni kupanga ajifunze na kutekeleza ili haya mambo yaende katika hii sekta nyeti, Watanzania wanufaike nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeangalia katika mipango mbalimbali, Serikali kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hapa naongea kama Waziri Kivuli, inadaiwa trilioni saba, kwenye hii mipango sijaona mkilipa. Trilioni sita ziko *PSPF,* Mfuko ambao hali ni hohehahe, tukisema Serikali mtachangia kwenda kufilisi Mfuko huu, mtajibu nini? Miongoni mwa fedha hizo ni fedha za mikopo takribani miaka 10 hamjalipa, lakini hamna mpango wa kulipa. Serikali inadaiwa mbele, inadaiwa nyuma, inadaiwa kushoto, inadaiwa kulia, lini sasa haya mambo yatakwisha? Hakuna humu katika mpango, jamani hii Mifuko tunatambua kuna mambo ya msingi ambayo inachangia, lakini tunahitaji hii Mifuko isaidie wanachama wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inadaiwa trilioni sita katika Mfuko mmoja ambao tumeambiwa unakaribia kufilisika, huna mpango wa kuonesha unaanza kulipa lini na ni deni la muda mrefu, tunajua deni lingine mlilirithi kwa watu ambao walikuwa hawajaanza kuchangia. Sasa haya mambo lazima tuoneshe kuna mikakati dhahiri ya kulipa, ndiyo kwanza mnapanga kukopa tena, tena ndani trilioni 6.8 wakati tunajua mkiendelea kukopa ndani mzunguko wa fedha unakuwa finyu. Hali ya umaskini ni kubwa wananchi ni hohehahe, uchumi umeshuka, huko kitaa hali ngumu, Wabunge hali ngumu, kila mtu kapauka tu, pesa hakuna. Haya lazima tuyaseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili naomba nimwambie ukweli, duniani kote kama Waziri wa Fedha hakuwa *stable* nchi inayumba, hatuhitaji Taifa letu liyumbe. Tunaomba mipango inayopangwa

itekelezwe kwa maslahi ya Taifa letu, ni jambo la msingi sana. Leo hii tunazungumzia masuala ya viwanda lakini ukiangalia huku hakuna *connection* yoyote kati ya sekta ya kilimo, sekta ya viwanda pamoja na Wizara ya Elimu na Wizara ya Mafunzo na Ufundi, hivi vitu vinakwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwaambia kwenye bajeti tulijua basi leo mngeleta katika Mpango, hakuna. Tukitoka mnasema, tukibaki tukiwashauri mnasema, mnataka nini sasa? Chukueni basi hata haya mazuri maana unajiuliza haya hatukuwepo uchumi umekua! Mikutano ya hadhara mmezuia uchumi umekua! Mmetufukuza Bungeni uchumi umekua! Kwenye mipango mmeshindwa kupanga sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge, kama Taifa tunaomba tuweke maslahi ya Taifa mbele tusijiwekee sisi kulinda nafsi zetu wenyewe, tumshauri Mheshimiwa Rais vizuri. Hali ya uchumi haiko vizuri, bandarini kumekauka kila sehemu kumekauka. Tuliongea katika *briefing* hapa, leo hii Bunge ni aibu ukiangalia kule majani ile *green* yote imekauka sasa hivi shida kila kona, wananchi wana njaa, Wabunge wana njaa, kila sehemu kuna njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwambia Mheshimiwa Mpango apange na kutekeleza, huko kwenye Halmashauri ndiyo kabisa, yeye asipopanga vizuri, asipotekeleza Wizara zingine na zenyewe hali yake ni ngumu. Kwenye Halmashauri zetu mpaka leo fedha hazijafika, kwangu pale Bunda Mjini kwa sababu nimeamua kuongoza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, malizia sekunde chache muda wako umekwisha.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunda Mjini hata *photocopy* tu wanakuja kutoa kwenye ofisi ya Mbunge kwa sababu nimeamua kuongoza. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Molel, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. AMINA S. MOLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu ili nami niweze kuchangia mawili matatu katika kuishauri Serikali yangu. Vilevile nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza zaidi katika kutoa ushauri na ushauri wangu utakwenda hasa kwa kuzingatia Wizara mbili ili kuweza kuishauri Serikali yangu katika mpango huu kwamba tunapoandaa mpango huu wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 ni mambo gani ya msingi ambayo yanahitaji kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 45 naomba kunukuu kwamba, hapa Waziri anasisitiza Maafisa Masuuli wanapaswa kujumuisha masuala mtambuka katika mipango na bajeti ya mwaka 2017/2018 na kwamba, ili kufanikisha lengo hili kila Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinasisitizwa kutenga fedha za kutekeleza vipaumbele kwenye masuala mtambuka. Vipaumbele hivyo ni pamoja na masuala ya kijinsia, vilevile masuala ya watu wenye ulemavu katika kuangalia hasa suala zima la ajira, afya, elimu na ujenzi wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Naomba nijikite katika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu au mwongozo huu wa bajeti umeeleza tu *in general* kwa sababu haujaweza kufafanua na kusisitiza masuala hayo kwamba yatatekelezwa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tunapozungumzia huduma muhimu za kijamii na hivi sasa katika Serikali yetu tunatoa elimu bure, lakini suala la kijinsia hasa kwa watoto wa kike na katika bajeti iliyopita, halikupewa kipaumbele kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba mahitaji muhimu kwa watoto wa shule hasa wasichana yamezingatiwa kwa kiasi gani. Mfano, tunafahamu kabisa watoto wa kike na hasa watoto wa kike wa vijijini na hata wale wa mijini tunafahamu kwamba, kwa mwezi wanakosa kuhudhuria masomo kwa siku nne, tano mpaka saba na hii ni kutokana na siku zao zile ambazo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali na najua Mheshimiwa Waziri ni baba na baba ana watoto na watoto hao wapo watoto wa kike wa kwake, lakini pia jamii yote kwa ujumla hao watoto wa kike tunawaangalia vipi! Mfano, katika vyoo, vyoo hivi vya shule na hasa maeneo mengi unakuta kwamba shule nyingi zina matundu matano mpaka saba na katika Sera ya Elimu inasema kwamba, matundu ya vyoo vya shule kila choo idadi ni 20 kwa 25, ishirini kwa watoto wa kike na ishirini kwa wavulana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watoto wa kike wana mahitaji muhimu mfano, tunazungumzia huduma za maji, mtoto huyu wa kike akiwa katika siku zake anahitaji pia maji, je, tumejipanga vipi katika bajeti zetu kuhakikisha kwamba maji yanakuwepo ili watoto hawa wa kike waweze kujisitiri vizuri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, katika bajeti yetu pia tumejipanga vipi na je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kupunguza kodi au kuondoa kodi kabisa katika suala zima la pedi ili hawa watoto wa kike waweze kupata pedi na hata ikibidi Serikali ilibebe hili kuhakikisha kwamba, wanagawa pedi kwa watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huduma za afya tunajua kabisa na tumesikia mengi tu na tumeona maeneo mengi hata ya Vijijini vituo vingine vya afya akinamama wanajifungulia kwenye nyumba za nyasi *(full suit)*. Je, bajeti hii imeangalia vipi mchanganuo wake kuweka vipaumbele katika kujenga vituo vya afya na zahanati ambazo wanawake wamaeneo yote ya vijijini watajifungua salama na kuondoa tatizo la vifo kwa mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii tunasema kwamba, kama wanawake haya ndiyo masuala muhimu ya kuzingatiwa na tunafahamu kabisa katika Wizara hii tunaye mwanamke na huyu mwanamke tunatarajia kabisa kwamba yeye ndiye atakuwa jicho la wanawake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabila la Warangi wana msemo unasema kwamba, *mwana wa mukiva amanyire michungiro,* kwa maana kwamba mtoto wa maskini hata awe na shida vipi anajua jinsi gani ya kuhimili ile shida. Kwa maana kwamba kama ni khanga imechanika huku nyuma ataishona mbele ataiunga atajifunga na maisha yatakwenda mbele. Kwa maana hiyo, natumia msemo huu kwa kusema kwamba, Naibu Waziri katika Wizara hii yeye ndiyo jicho la kuangalia Wanawake wa Tanzania kwa sababu amebeba dhamana yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekitiki, katika suala la watu wenye ulemavu. Tumetaja tu ujumla ajira, elimu, afya lakini, je, tumejiandaa vipi kuhakikisha kwamba bajeti kadhaa itakwenda katika kununua vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu? Bajeti kadhaa itakwenda katika kuhakikisha kwamba miundombinu inakuwa rafiki ili watoto wote waweze kupata elimu na hasa watoto wa vijijini ambao miundombinu siyo rafiki. Je, Bajeti hii tumejipanga vipi kuhakikisha kwamba tunaorodhesha idadi kamili ambayo itatimiza mahitaji ya watoto wenye ulemavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la ajira. Sheria na Wizara pia na yenyewe kama Wizara ya Fedha bado ina jukumu hilo. Je, tunawekaje mipango yetu katika kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu na wenye sifa wanapata ajira, vilevile mitaji kwa ajili ya kuwawezesha ili waweze kujiajiri. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kama baba, lakini kama Waziri mwenye dhamana katika Wizara hii kuhakikisha kwamba haya mambo katika hii bajeti ijayo ili kusiwepo na maswali haya tuone kwamba tumejipanga vipi ili

katika kila kipengele kimoja kijitosheleze katika kusaidia mahitaji hayo ya makundi haya niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema; siku zote katika maisha unapokuwa mwongo basi ni vema pia ukawa na kumbukumbu. Tumesikia michango mingi sana ya Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba nikumbushe tu mambo yaliyojiri kwa kasi sana mwaka jana, tuliambiwa kwamba: "Nawashangaa sana wanaochoma moto vibaka kwa kumuacha Lowassa akitanua mitaani."

Mwingine akasema kwamba; "CCM wamempatia Fisadi fomu ya kugombea Urais ni hatari sana." Swali langu, je, kati ya CCM na wao ni nani hatari katika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wanasema kwamba "nina ushahidi wa kutosha kuhusiana na wizi na ufisadi wa Lowassa na Rostam Aziz." Leo hii ni nani ambao walimbeba na kumtangaza nchi nzima kumsafisha na wakati huo huko nyuma walisema kwamba ni fisadi? Ndiyo maana nikasema kwamba ukiwa mwongo uwe pia na kumbukumbu ya yale maneno unayosema. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa kuchangia. Naomba moja kwa moja niende kwenye hoja. Kwanza naanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutimiza wajibu wake kwa kuivunja Bodi ya Korosho na sasa hivi tunaona wakulima na wananchi wa Mtwara wakiwa wanafurahi kwa sababu korosho yetu imefikia kuuzwa kwa sh. 3,800. Hata hivyo, Mheshimiwa Mpango pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo sijaona vema katika mpango wenu juu ya maendelezo au mwendelezo wa viwanda tulivyonavyo Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema toka mwanzo kwamba Mtwara hatuhitaji viwanda vipya kabisa, tunahitaji tu maboresho kwenye viwanda vyetu vya korosho na tunataka kufanya sasa tathmini ya vile viwanda kwa sababu majengo tulikuwa nayo, lakini yaliuzwa kwa watu ambao hawajulikani au wanajulikana kwa bei chee kabisa na wanawatumia kufanyia shughuli nyingine hasa zaidi wamegeuza kuwa maghala badala ya kufanya sehemu za kuzalisha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa tathmini ifanyike, mpitie pamoja na mikataba waliyouzia maghala yale ikiwezekana sasa mle ndani viwekwe viwanda vidogovidogo na wazalishaji waendelee kubangua korosho zao kama

ambavyo inafanyika kwenye kiwanda kwa Mheshimiwa Nape katika Jimbo la Mtama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakumbuka miaka ya 80, Tanzania ilikopa shilingi bilioni 20 kutoka kwa Wajapan pamoja na Serikali ya Italia, sasa tunataka hizi pesa kweli zilete manufaa kwa wananchi. Pamoja na manufaa ya wananchi wanayoyapata kutoka kwenye korosho, sasa hivi pamekuwa kidogo na ucheleweshaji wa malipo. Tunaomba na hili Waziri wa Kilimo alifuatilie tuone hawa wananchi wanalipwa kwa wakati kwa sababu sasa hivi ni mnada wa tatu kufanyika lakini bado wananchi hawajapata posho zao kwa uhakika na hawajui watamalizia lini kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Waziri wa Kilimo pamoja na mazuri yote yanayofanyika, kuna hii karatasi ipo hapa mbele yangu. Kuna Kampuni moja inaitwa *HAMAS* iko kule Mtwara, hawa watu wali-*supply sulphur* kwa ajili ya wakulima wa korosho mwaka jana na mwaka juzi, matokeo yake waliishia kufikishana Mahakamani na kampuni hii ililipwa shilingi milioni 953.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naileta kwenu kwa sababu sisi wananchi wa Mtwara tusingependa Kampuni hii tena ikapewa tenda ya ku-*supply sulphur* kwa sababu wanaleta ujanja ujanja na mwishoni wanapeleka Mahakamani wanaishia kulipwa pesa ambayo hawajaifanyia kazi. Nitaomba nafasi na Waziri Mkuu ikiwezekana tulijadili jambo hili kwa kina kwa sababu kuna taarifa za kutosha, achilia mbali hii karatasi niliyoshika hapa mbele yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri cha Mpango kwenye ukurasa wa 22, tumeongelea pale ndani kwamba kuna samaki wanaoingizwa nchini wanaagizwa kutoka nje. Tungependa sasa kufahamu kwa nini viwanda vyetu au maziwa yetu yasitumike watu wale wakawezeshwa wakaanza kuzalisha samaki hapa nchini baada ya kuamua wao kuvua na tunaleta sisi samaki kutoka nje. Kwa hiyo, kwa vyovyote lazima sasa tuamue tuwawezeshe watu wetu wao wajitosheleze kwanza soko la ndani, kama tuna soko la kutosha kabisa la ndani kwa nini sasa tuanze kuagiza samaki kutoka nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 34 inaonesha pale ndani kuna tafiti mbalimbali zimefanyika za masuala ya kilimo. Mimi bado nirudi tena kwa wakulima wa korosho, niseme kuna tafiti nyingi kweli zimefanyika na Serikali imewekeza pesa nyingi sana pale ndani ikiwemo utafiti wa mabibo ambao unaonyesha una asilimia mara tano zaidi kutoa *vitamin 'C'* tofauti ilivyokuwa tunda la chungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka sasa zile tafiti zianze kufanyiwa kazi, tusiendelee tu kukaa na mavitabu tukaanza tena kuwekeza kwenye pesa kwa ajili ya tafiti, twende tukawasaidie wale wakulima wa korosho kwa sababu kwa kufanya hizi tafiti vile viwanda vikianza kutengeneza basi kutaongeza mapato kwa wakulima wa korosho kwa sababu, sasa hivi hata bibo tunatamani lianze kununuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa badala ya kuendeleza kufanya taafiti mbalimbali, tafiti ambazo tayari zilishafanyika kutoka kwenye korosho, basi zitekelezwe ili kuwaongezea wakulima kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 38, tunakuta pale ndani Mheshimiwa Waziri wanasema tunataka kuwa-*encourage investors* waje kuwekeza nchini kwenye masuala ya viwanda. Naomba niongelee kwa masikitiko sana Kiwanda cha Dangote. Dangote walipokuja kuweka kiwanda Mtwara walisema kwamba watapewa umeme wa kutumia gesi ili waweze kuzalisha kwa gharama nafuu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshukuru kidogo bei ya *cement* imeshuka katika maeneo yetu imefikia shilingi 11,000, Mwekezaji huyu ana matatizo makubwa sana, mpaka sasa hivi hajapelekewa gesi pale kiwandani, amelazimishwa akanunue makaa ya mawe kutoka Mchuchuma na utafiti unaonesha kwamba gharama za kutoa makaa wa mawe Mchuchuma zimeongezeka kwa asilimia 20 zaidi tofauti na ambavyo angeweza kuleta makaa ya mawe au ambavyo alikuwa analeta kutoka South Africa. Kwa hiyo, tumsaidie yule Mwekezaji aendelee kuzalisha *cement* katika eneo lile ili simenti iweze kushuka, tuachane sasa na biashara ya zamani ya biashara ya matope wananchi watumie tofali za *cement* kujenga nyumba bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba sasa hivi bandari ya Mtwara ndiyo iwe bandari kuu itakayotumika kusafirisha mazao yetu ikiwemo pamoja na korosho. Tulipata pale taarifa wakati fulani kwamba Dangote na tunafahamu Dangote wanaleta *cement* Dar es Salaam kwa kutumia barabara. Barabara ile tumelalamikia kwa miaka 54 iliyopita ni miaka mitatu, minne iliyopita ndiyo barabara ya Mtwara imejengwa, sasa badala ya kusafirisha *cement* ya Dangote kwa kutumia bandari ya Mtwara bado *cement* inakuja Dar es Salaam kwa kutumia barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile ikiharibika Serikali hii haitaweza tena kujenga barabara, tunaomba tafadhali utaratibu ufanyike *cement* ya Dangote isafirishwe kwa kutumia Bandari ya Mtwara na siyo kupeleka kwa barabara, barabara itumike kwa matumizi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu hizi kampuni zinazosafirisha *cement* ni Kampuni za wakubwa wanasingizia kuna kipande fulani cha barabara panaitwa Mikindani kwamba tuta lile litaharibika, kuharibu tuta dogo la kilometa 10 ni nafuu zaidi kuliko kuharibu barabara nzima ya kilometa 300 hadi 400 kufika Dar es Salaam, mtaturudisha kule tulikotutoa siku za mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa hivi katika maeneo mengi ya Kusini kuna uchimbaji wa madini unafanyika katika maeneo madogo madogo (*small scale)*. Tunataka kupata taarifa sahihi kule kunakochimbwa madini ni nini kinapatikana, madini gani yapo tuwaeleze wananchi wa Mtwara ili waweze sasa wao kuangalia nafasi ya kutumia fursa walizonazo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani walikuwa wanasema Mikoa ya Kusini iko nyuma hasa zaidi Mtwara na Lindi, sasa hivi fursa tunazo za kutosha, tunachoomba tu sasa kutengenezewa mazingira wezeshi tuweze kufanya shughuli zetu wenyewe za kujizalishia kipato badala ya kila kitu tulichonacho ninyi mnataka kukiondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuona sababu za msingi za kutengeneza ule mtambo wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi badala ule mtambo ungetengenezwa kule kwetu, ungeweza kutoa ajira kwa vijana wetu, kidogo tunachokipata mkiache tukitumie baadaye kinachobaki mkipeleke kwa wengine nao wakakitumie. Tulikuwa nyuma kwa muda mrefu sana, tunaomba sasa *resources* zilizoko Mtwara zitumike kwa ajili ya maendeleo ya watu wa Mtwara na kwa Taifa zima kwa ujumla ili vijana wetu waweze kupata ajira ya kutosha katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee bado katika lile jambo ambalo tulisema pale awali. Mtwara pia tunategemea sana uvuvi. Tuna eneo kubwa ambalo linaweza kufanyika shughuli za uvuvi. Tuiombe Serikali sasa iamue wazi kutuwekea hata kiwanda sasa cha uvuvi. Kama nilivyosema majengo ya kuweka hivi vitu tunayo lakini watu waliyageuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda aamue sasa mara moja aka-*review* mikataba iliyowapa watu uendeshaji wa maghala kule Mtwara badala ya kufanya viwanda na wanaendelea kuhifadhia mazao wakijipatia pesa kwa sababu si kitu ambacho walikubaliana. Tunataka sasa viwanda vile vianze uzalishaji wa korosho ili kuongeza tija kwenye mazao ya korosho na wakulima waweze kupata kipato cha kutosha pamoja na kuongeza mzunguko wa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipatia, nitakapopata tena wakati nitatoa maelezo zaidi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee nilikuwa nimetaja kwamba atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi badala yake atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, halafu Mheshimiwa Lusinde ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya ufinyu wa muda na kwa sababu nilipata nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, naomba Mama Ruth Mollel aweze kuchangia kwa niaba yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ambayo nimepewa kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo ilitolewa kabla. Katika mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano ni Tanzania ya viwanda, nimepitia katika Mpango huo ambao umewasilishwa na nasikitika kusema kwamba, katika Mpango wote ambao umewasilishwa pamoja na umuhimu wa kukuza viwanda, sijaona ni kwa namna gani rasilimali watu imepangwa kusudi kusaidia kuendesha viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu mwaka jana katika ule Mpango kulikuwa na suala la kupeleka wanafunzi 159 wa *petroleum and gas* kwenda kusoma, lakini sioni katika mpango wa mwaka huu ni kwa jinsi gani tumefikia wapi na wale 159 kwamba wanatosha au tunahitaji ku-*train* watumishi wengine kwa ajili ya *petroleum and gas.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mwaka jana Serikali iliahidi kwamba itajenga vyuo vinne vya ufundi katika mikoa mbalimbali lakini katika mpango wa mwaka huu Serikali haijaainisha kama bado tunaendelea na hivyo vyuo vinne vya ufundi, imekuja na mawazo mapya ya kutengeneza karakana, sijui miundombinu. Je, vile vyuo vinne ambavyo Serikali iliahidi itavijenga, imefikia wapi? Ingependeza zaidi kama tungeweza tukapata *status* ya yale ambayo yalisemwa mwaka jana tuweze kufuatilia kama kweli yanatekelezwa au la! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya elimu ya juu. Kama nilivyosema juzi, hii taasisi ya mikopo ilianzishwa ili kupanua udahili si kupanua udahili tu na kusaidia wanafunzi ambao ni wahitaji, lakini tumeona mwaka jana, kwa bajeti ya juzi hakuna pesa iliyotolewa ya kutosha na kwa mpango huu ambao umewasilishwa inasemekana kwamba udahili utaongezwa na tuta-*train* watu wengi, kama ikiwa mpaka sasa hivi bajeti inayotoka hata haikidhi wale wanafunzi waliokuwepo, je, ni kweli Serikali itakuwa na hiyo pesa ya kuingiza kwenye mzunguko mwaka kesho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ningependa Waziri anisaidie kujibu, kuna hii hoja ambayo imeshajitokeza kwamba kuna wanafunzi ambao wanaendelea wananyimwa mikopo, mimi nauliza busara ya kawaida tu inasema kwamba hawa wameshaingia kwenye mkataba na *Loans Board* na wamesaini mikataba ya jinsi ya kurudisha hiyo hela na leo Serikali inasitisha kuwapa mikopo hawa wanafunzi wanaoendelea, ni kwamba Serikali imekiuka utaratibu wake wenyewe wa kuwapa wanafunzi hawa mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, busara ya kawaida ingekuwa kuendelea kuwapa hawa wanaoendelea, halafu mipango mipya au uhuishaji au utaratibu mpya ungeanza na hawa ambao ni wapya, ndiyo utaratibu tunaofuata. Ningependa kupata ufafanuzi kuhusu hawa wanafunzi wanaoendelea ambao walikuwa wanapewa mikopo na sasa inasitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, ni suala la Watumishi wa Umma. Naomba ku-*declare* kwanza *interest* kwamba nilikuwa Katibu Mkuu Utumishi. Nasikitishwa kwa jinsi ambavyo watumishi wamekuwa wanatumbuliwa *left and right*. Utakuta Mawaziri wanatumbua japokuwa tangu majuzi kidogo wametulia, *Ma-RC* wanatumbua, *DC* anatumua, *DED* anatumbua, wakati tunajua kabisa Mamlaka ya nidhamu ni watu gani ambao Rais amewakasimu. Hii inapelekea watumishi kukosa imani, kukosa amani na kukosa ubunifu na matokeo yake Utumishi wa Umma ambao ndiyo injini ya maendeleo utashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Makada wengi ambao hawakuwepo katika Utumishi wa Umma kabisa wamewekwa kwenye maeneo ya utendaji ambayo inakwenda ku-*compromise* uadilifu na uimara wa Utumishi wa Umma. Utumishi wa Umma duniani kote unaishi zaidi ya Wanasiasa. Wanasiasa malengo yao ni miaka mitano tu. Utumishi wa umma ambao ni legelege hautaweza kutekeleza huu Mpango ambao unaletwa. Kwa hiyo, hili jambo ni lazima liangaliwe kwa ukaribu sana ili kusudi Watumishi wa Umma wapate imani na waweze kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Local Government Reforms,* Serikali Kuu imekasimu madaraka kwa *Local Government* na kati ya maeneo ambayo ilikuwa imekasimu ni *property tax* au kodi ya majengo, tumeona Awamu hii ya Tano imeanza tena kurudisha *collection* ya *property tax* kwa *TRA*. *TRA* walishashindwa siku nyingi na ndiyo maana ilihamishiwa *Local Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo gani ambacho Serikali imetumia kuhamisha tena *property tax* kutoka Serikali za Mitaa kuja *TRA* wakati walikwishashindwa na tunajua kwamba Serikali Kuu imekasimu madaraka kwa *Local Government*. Inawezekanaje umpe mtu madaraka, umpe na rasilimali watu, lakini ukamnyima rasilimali fedha ya kuifanyia kazi, wakati *Local*

*Government* ndiyo ina mashule, *Local Government* ndiyo ina hospitali, *Local Government* ndiyo ina barabara, watafanyaje hizi kazi ikiwa *resources* Serikali Kuu imewanyang'anya? Hili ni janga la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mikubwa ambayo imezungumziwa. Makaa ya mawe - Liganga, Mchuchuma, reli ya kati, *general tyre,* hizi *story* za siku nyingi tangu nikiwa Katibu Mkuu, nimestaafu miaka mitano sasa bado hadithi ni ile ile.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel naomba umalizie.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bado hadithi ni ile ile. Tunataka Mheshimiwa Mpango aje atueleze ni namna gani hili jambo litatekelezwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Joseph Mbilinyi naona amerudi, Mheshimiwa Sakaya itabidi usubiri kidogo. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Lusinde ajiandae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza naomba niwapongeze Wabunge wenzetu wa upande wa pili ambao walioneka kwamba wamesimama na kutetea hizi hoja zilizopita siku mbili kama Mheshimiwa Hussein Bashe na wengine, nawaomba waendelee hivyo na kesho kwenye Muswada wa Sheria ya Habari kwa sababu nao ni *disaster* kwa Taifa. Kwa hiyo, nawashukuru sana na tuendelee kuwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wamarekani wanasema uchumi ni mahesabu *(arithmetic's)* hautaki maneno maneno, mara uchumi umekua kwa 7.9%, mara 7.2%, uchumi ni *arithmetic's* (mahesabu). Humu ndani katika *retreat* ya kwanza kabisa nilisema, *I was scared of the future, now this is the future I was scared about* ambayo wote tunaijadili. Nilikuwa mtu wa kwanza kuongelea *in detail* matatizo ya bandari yaliyotokana na *Single Custom Territory.* Nikafanya *consultation* mpaka na Waziri Mkuu maana alikuwepo, lakini mpaka sasa hivi hakuna kilichotoa majibu zaidi ya kusema hata meli moja ikija bandarini haina tatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niendelee kusisitiza kwamba we *should take jets* kwa sababu lazima tuwe na *international interactions.* Nashukuru Mkulu ameanza kutoka, juzi alikuwa Nairobi, nafikiri ataongeza *mileage* kwenye ndege. Kwa sababu hata Wabunge wanaposhindwa kusafiri kwenda kwenye vyombo ambavyo ni vya makubaliano ya Kimataifa, hatuwezi kwenda *SADC,*

*PAP,* tunasikia hata Spika ananyimwa kibali cha kusafiri, sasa hii nchi tukijifungia ndani humu tutapata vipi maarifa, tutabadilishana vipi mawazo na wenzetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Marekani ambao wana kila kitu bado Obama anasafiri anakuja mpaka Kenya na Tanzania kwa sababu *international interactions* zinakuwa ni kwa maslahi mapana. Watu hawawezi kuwa wanakuja kwetu tu, Wabunge wanakuja kwetu, *delegation* zinakuja kwetu na sasa hivi naona Rais anapokea *delegation* nyingi nyingi lakini sisi hatutoki, wataacha kuja watasema hawa tunawatembelea wao hawatutembelei, acha wajifungie humo humo ndani watajijua wenyewe, sasa hii itakuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize, hatuwezi kuwa na mipango bila sera. Nataka Waziri wa Fedha aniambie leo ni nini sera yetu kuhusu misaada kutoka nje? Maana tunasikia kauli nyingi za majigambo, tuna wa-*criticize* Wamarekani, Wazungu kwamba wenyewe hawajafanya hiki na kile, hatuhitaji misaada tuko tayari kujitegemea, lakini *eventually* tunaishia kuomba msaada Morocco ambao ni *third world* wenzetu! Morocco ni dunia ya tatu wenzetu tunaomba msaada sijui watujengee uwanja na vitu gani sijui. Labda pengine tukiangalia ngozi nyeupe tunajua kila mtu mweupe ni Mzungu na ana hela, lakini Morocco ni *third world* ndugu zangu na wao wanahitaji misaada kama sisi, wale ilitakiwa tuongee mambo yao mengine tu kwa sababu yule bwana ni rafiki mzuri sana wa *Puff Daddy* wa Marekani na hata picha zimeonesha *lifestyle* yake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema uchumi unakua uchumi unakua kwa nani? Biashara zinakufa, Mpango inabidi ubadilishe jina kwa sababu *you have to live your name,* kama wewe ni Mpango basi uwe na mipango. Mimi Sugu hata ukiangalia nikikomaa na kitu nakomaa nacho kama sugu, *Iam living my name*. Kwa hiyo, unatakiwa Mheshimiwa Mpango uishi kwa jina lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuulize, fedha hamna, hivi ni yeye Mpango alimshauri Rais kwamba wachapishe noti mpya kwamba watu wanaficha fedha? Watu wakificha fedha hawawezi kuficha fedha hizi ambazo zinashuka thamani kila siku, wakificha fedha wataficha dola na kadhalika. Tatizo linalotokea ni kwamba wamekusanya fedha zote za Serikali kutoka kwenye mabenki wamepeleka *BoT* wakati wao hawazungushi fedha wanakaa tu. Rudisheni zile fedha *CRDB, NMB, NBC* wale ndiyo wanaofanya biashara waendelee kukopesha, watu waendelee kufanya biashara na kutanua mambo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 14 wanasema misingi ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa 2017/2018, halafu namba nne wanasema,

katika mikakati inayotarajiwa kuweka bajeti ni kusubiri bei za mafuta katika soko la dunia zinavyoendelea kuimarika. Sisi hatuchimbi mafuta, bei ya mafuta inaposhuka ni faida kwetu. Juzi nilikuwa naangalia Waziri wa Fedha wa India anasema uchumi wa India una-*boom*, *construction* zinaendelea, viwanda vinajengwa, tunachukua *advantage* ya kushuka kwa soko la mafuta kwa sababu sisi hatuchimbi mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watasema mafuta tunayo yatapatikana leo? Hiyo gesi imeshaanza kuchimbwa lakini bado hatuoni hata manufaa yake, mpaka leo ukienda Mtwara watu wanachoma vitumbua, watu wamechoka wanategemea korosho wakati gesi ipo na ndiyo maana hata Mheshimiwa Mwambe amechoka kugombea gesi, humsikii anasema gesi, yeye anazungumzia korosho tu. Hata watu wa Mtwara ukiwaambia gesi wanakwambia ninayo tumboni, wanaleta utani, *they joke about it* kwa sababu *they don't believe about it. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi leo hatuwezi kusema kwamba eti bajeti yetu itatengemaa kutegemea kuimarika kwa bei ya mafuta duniani. Kuimarika kwa bei ya mafuta duniani ni *disaster* kwetu. Faida kwetu sisi tena msimu huu ambao tunasema tunataka kujenga viwanda ni kukomaa kipindi hiki kuanzisha hivyo viwanda kwa sababu nishati ya mafuta bei iko chini na hamna namna nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema mipango, tutapeleka milioni 50 kila kijiji, za nini? Hii ni *mentality* ya rushwa wakati wa uchaguzi! Ndiyo maana *story* zinaendelea, milioni 50 kila kijiji, milioni 10 Wabunge, sijui milioni ngapi za nini, tena mnasema mtapeleka *cash* wafanyie nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri angalau wangesema kila kijiji kije na *proposal* kulingana na mazingira yake, kwa bajeti ya milioni 50 mtafanya nini? Mfano kijijini unasema sisi tunataka tuimarishe kilimo, tuna vijana hapa wanasoma mambo ya ugani kwenye vyuo vya kilimo, fedha hizi zikija sisi tutanunua maksai na plau. Kijana akirudi kutoka masomoni badala ya kulia anatafuta kazi tunamkabidhi plau halafu yule ng'ombe wa maksai anakuwa ni wa kijiji, unampa eneo anaendelea kulima pale *organic food* halafu ninyi mnatafuta soko la kuuza hizi *organic food* nje ya nchi kwa sababu zina soko sana kuliko hivi vyakula vya mbolea. Nyie mmeng'ang'ana na viwanda wakati mtaji hamna! Ooh sijui *General tyre* itarudi, Mbeya ZZK, nimechoka hata kuiulizia mpaka leo imebaki kuwa ghala tu la pombe ndugu zangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasimama hapa mnasema tumenunua ndege *(Bombadier),* nataka niulize ni nani aliyepanga nauli za ndege hii kwa sababu *highlight* ya nauli wametoa. Sasa hizo *Bombardier highlight* ya nauli eti kwenda Mwanza Sh.160,000, kwenda Mbeya Sh. 305,000, kuja Dodoma Sh.3 00,000, hivi

Mwanza na Dodoma mbali wapi au mnataka kumfurahisha ngosha? Tena huyu anatakiwa kutumbuliwa! Huwezi kusema nauli ya kwenda Mwanza ni Sh.160,000 ambako ni kilometa elfu moja na zaidi halafu kwenda Mbeya ambako ni kilometa 800 unasema Sh. 300,000…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa Mbilinyi muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kwa kumalizia...

**MWENYEKITI:** Yaani malizia sentensi uliyokuwa unasema siyo umalizie na *point* nyingine. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Ni inayounganika, nimetoka kuongea na Waziri Mkuu pale, sasa hivi kuna *disaster diaspora.* Serikali mmetoa tamko kwamba watu wote wa *diaspora* wenye *passport* za nje ambao wamejenga nyumba hapa zinataifishwa. Hii kauli imetolewa na Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi *and this is very bad* na nimeongea na Waziri Mkuu, lakini naongea hapa….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Dakika moja Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Sasa huwezi tena kuendelea kuongea.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Naomba dakika moja Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Uzuri umetupa taarifa umeshamwambia Waziri Mkuu, kwa hiyo atashughulika nayo. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Watu wanataka kujinyonga huko.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa. Mheshimiwa Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutuzawadia uhai na kwa huruma yake tuko salama na tuko ndani ya Bunge hili kwa sababu ya kujadili Mpango wa Maendeleo wa Serikali 2016/2017 na 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, nataka nichukue fursa hii ndugu zangu kwa unyenyekevu mkubwa sana kutoa pole kwa wananchi

wenzangu watatu watafiti kutoka Chuo cha Seliani waliouawa katika Kijiji cha Iringa-Mvumi, katika Wilaya ya Chamwino, nawapa pole sana familia. Vilevile nitoe pole sana kwa wananchi kadhaa wa Kijiji cha Mvumi *Mission* pamoja na Kata ya Manda na Kijiji chenyewe cha Iringa-Mvumi kwa familia ya Tatu ambaye naye pia aliuawa wiki moja kabla ya wale watafiti kukumbwa na kadhia hiyo. Naomba Mungu azipumzishe roho za marehemu wote mahali pema peponi, lakini niitake Serikali kuchukua hatua madhubuti kuwatafuta watu waliokimbia ambao kwa kweli kwa kiasi kikubwa wanatajwa kuhusika na mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, nina mambo machache ya kuzungumza. Jambo la kwanza, naomba niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri. Ndugu zangu nataka nirudie tena maneno ambayo nimekuwa nikiyasema mara nyingi kwamba katika kazi rahisi duniani, hakuna kazi rahisi kuliko kupinga, kupinga jambo lolote ni kufanya kazi rahisi sana. Maana mtu anajenga nyumba kwa gharama kubwa wewe unatumia dakika mbili tu kumwambia nyumba yako mbovu. Kwa hiyo, unaweza kuona namna ambavyo kupinga ni kazi rahisi sana na inayoweza kufanywa na mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, maneno mengi mazuri ameyaandika katika kitabu chake, mojawapo ni kukua kwa uchumi ambapo sasa hivi umekua kwa 5.7% na unategemewa kukua kwa 5.9%. Tatizo tulilo nalo Dkt. Mpango ni namna gani tunahusianisha kati ya ukuaji wa uchumi kwenye vitabu na hali halisi kwa wananchi wenyewe. Hapa ndiyo inatakiwa sasa mtusaidie ku-*link* kwa sababu tunavyoelewa ni kwamba uchumi unapokua ni lazima uguse baadhi ya wananchi au pengine wananchi wengi zaidi hasa wanaoishi maeneo ya vijijini. Huko bado tuna matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia viwanda vidogo vidogo, nashauri Serikali tujikite zaidi kwenye viwanda ambavyo vitainua kilimo. Tujikite kwenye viwanda vya mazao yanayolimwa na wananchi. Kwa mfano, kwa Mkoa wa Dodoma ukianzisha kiwanda kwa ajili ya kuinua zao la zabibu utakuwa umetusaidia zaidi kuliko tukiwa tunazungumza ukuaji wa uchumi wa *point* za kwenye karatasi ambao hauakisi wananchi wenyewe wanainukaje kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niyaseme haya maana imeonekana kwamba Wabunge wa CCM tuna uoga wa kumshauri Rais, lakini leo nataka nitamke kwenye Bunge hili, Rais anafanya kazi nzuri sana na aendelee kuifanya. Bahati nzuri tumekuwa na Rais kama Mbunge mwenzetu kwa miaka 20, anatujua Wabunge, anaijua nchi, anajua namna ambavyo tuna tabia za kuzusha, hawezi kubabaishwa na maneno yanayotoka humu. Katika nchi yetu

kwa miaka mingi sana tumekuwa na malalamiko kwamba Serikali yetu inalindana, mtu anaharibu hapa anahamishiwa hapa, mtu anaharibu hapa anapelekwa hapa, tunataka mabadiliko, amekuja Rais wa mabadiliko, ukiharibu unakwenda kupumzika nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu nataka niwaambie wala hakuna mtu anayetisha wala hakuna mtu anayeshindwa kumshauri. Ila nataka niwapongeze sana, mimi mara chache sana huwa nawapongeza Wabunge wa Upinzani lakini safari hii nataka niwapongeze, nawapongeza kwa sababu wamejitoa mhanga. Wanaposimama kusema Serikali imefilisika msifikiri wanaisema Serikali, hapana, wana sehemu wanayolenga kwa sababu ili ujue kwamba huyu mtu amefilisika kuna vielelezo. Cha kwanza, lazima ashindwe kulipa madeni, mtu akishindwa kulipa madeni ujue amefilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wabunge wa Upinzani acheni uoga, badala ya kusema Serikali imefilisika, Serikali inayolipa mishahara, Serikali inayowalipa nyie, Serikali inayosomesha watoto bure, tamkeni wazi kwamba Mbowe umefilisika maana umeshindwa kulipa madeni. Tamkeni wazi, hakuna sababu ya kuzungukazunguka unapiga kona ooh mimi nitakamatwa, sasa unatuambia sisi tuje tukuwekee dhamana, ukikamatwa ni kwa makosa yako. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ameteua Wakuu wa Mikoa wengi wazuri, lakini wachache nitawataja hapa, wa kwanza Mrisho Gambo, nampongeza sana. Wa pili Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rugimbana Jordan nampongeza sana. Wa tatu, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, nampongeza sana Mongella anafanya kazi nzuri. Rais anawajua watu wake, anapowapanga anajua kabisa nani anaweza kufanya kazi wapi. *Big up* sana Dkt. Magufuli, endelea kufanya kazi ukiamini kwamba nyuma yako wako watu wanaokuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie msamiati mgumu sana. Ni bora mtu ufe mawazo yako yabaki hai kuliko mtu uwe hai halafu mawazo yako yawe yamekufa, ujue wewe umepotea kabisa. Hatuwezi kuogopa kuchukua hatua. Leo hii tunasimama ndani ya Bunge hili tunasema utumishi ni uti wa mgongo, kwenye utumishi haitakiwi kuingiza siasa inakuwaje mtu aliyefikia *level* ya kuwa mtu mkubwa mpaka Katibu Mkuu leo Mbunge wa CHADEMA, alianza lini? Lazima alianza akiwa huko huko katika Utumishi, ndiyo maana lazima tufukue kila sehemu kuangalia tunao watumishi au tunao watu wanaopiga porojo za siasa badala ya kufanya kazi, lazima tusimamie nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mtu anafikiria kwamba eti tutakuwa na Taifa ambalo halina mabadiliko, haiwezekani! Tumeyaomba sana

mabadiliko, tumelala tunasisitiza kwamba tunataka mtu atakayekuja kubadilisha. Kama kuna mfanyakazi anaenda kazini akiwa hana hakika kwamba ajira yake ipo, sawasawa, yeye akachape kazi. Kazi peke yake ndiyo itasababisha ajira yako iendelee kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusidanganyane hapa. Tunasimama hapa na kuanza kusema ooh kwenye kikao cha chama cha Wabunge wa CCM wamepewa hela, aaah, wamepewa hela na nani? Mbona ninyi mnachangishwa kila siku hapa? Wabunge wanachangishwa kila siku milioni moja moja, wengine wanakuja wanalia wanasema Lusinde angalia meseji hii tunatakiwa tutoe milioni moja moja kwa ajili ya kesi, mbona sisi hatuyasemi yenu? Sisi tupewe pesa na nani? Wabunge wote tulipewa fursa ya kwenda kukopa, kila Mbunge kakopa, wengine wamekopa 200, wengine 300, leo hii uje upewe milioni 10 ili iweje, ni kutudhalilisha tu.

Msichukue fursa hiyo kutudhalilisha, Wabunge wa nchi hii wote wa Upinzani, wa CCM tulipewa fursa, tumekopa hela nyingi, hakuna Mbunge wa kuhongwa milioni 10 wala wa kupewa milioni moja. Ndiyo maana nyie mnachukua hela zenu kukichangia chama chenu, hakuna mtu anayewazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana wakati huu ambapo tunazungumzia mpango, baada ya kuwa nimeshawapa dawa kidogo, ni vyema tukajikita kwenye sekta binafsi. Serikali imeambiwa uti wa mgongo ni sekta binafsi. Rais amekwenda kufungua kiwanda kuna watu wanapiga kelele tena, mnaenda kwa Bakhresa, katika sekta binafsi kuna mtu mjasiriamali jamani katika nchi hii anayemfikia Bakhresa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bakhresa akimuita au akimuomba Rais kwenda kufungua kiwanda chake, uharamu wake uko wapi? Au Bakhresa kuacha kuwachangia wapinzani ndiyo imekuwa nongwa? Maana nashangaa unaanza kumlaumu eti kwa nini Rais kaenda kufungua kiwanda cha Bakhresa kampa na ardhi, kuna vivutio vya kuwafanya wawekezaji wa ndani nao waweze kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mpango kelele anazozisikia uchumi wa ndani una *booster* yake. *Booster* yake ni kuwalipa wadeni wa ndani, ukiweza kuwalipa wadeni wa ndani hela itaonekana mtaani na hizo kelele zitapungua. Mnapokumbuka madeni ya nje ni sawa, lakini kumbukeni na madeni ya ndani. Kuna wazabuni mbalimbali waliofanya kazi kwenye Serikali, hawa wakipata pesa mzunguko wa pesa ndani ya nchi nao utaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawashauri Serikali muangalie pande zote. Mnaposomesha bure tunaona, mnaponunua ndege tunaona,

tunajua yatasemwa mengi lakini endeleeni kufanya kazi kwa sababu hata Mungu angeleta majadiliano na wananchi hicho kikao kisingekwisha. Ndiyo maana ukaona akakaa mbali akaamrisha kama ni mvua, mvua, kama jua, jua. Mwambie Rais tunamuunga mkono, kazi anayofanya ni njema, tumepata Rais wa kunyooka, akinyooka na jambo linaenda kama alivyopanga na ndicho tunachokitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanalalamika hapa ooh Rais anafanya kazi yeye mwenyewe. Halafu mimi nashangaa hawa jamaa wanasema halafu wanajijibu wenyewe. Wananikumbusha Sauli kwenye Biblia alipokutana na kibano cha Mungu Sauli alisema, ni nani wewe Bwana? Yaani aliuliza swali halafu akajibu kwamba huyu ni Bwana, ndiyo hawa! Huku unasema Rais anafanya kazi zote, huku tena unabadilika unasema Rais anawatisha watumishi. Mtu anayewafanyia kazi zote atawatishaje sasa wakati kazi zote anafanya yeye mwenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Rais ananyooshe hii nchi na tuna uhakika Magufuli nchi hii atainyoosha kutoka pale ilipokuwa imeishia kwenda mbele zaidi. Nawaambia moja ya vitu ambavyo nataka Watanzania watusaidie 2020 nchi zetu za ulimwengu wa tatu hizi kuwahi kila kitu nalo ni tatizo, hata kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi tuliwahi ndiyo maana mnaona hoja zenyewe…..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde naomba umalize muda wako umekwisha.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Nimalize? Sasa unaingiaje Bungeni kujadili kaptura ya Mfalme wa Morocco hiyo ina uhusiano gani na matatizo ya wananchi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Kiteto Koshuma ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye mapendekezo ya mpango ambayo yako mbele yetu. Kwa sababu mengi yamezungumzwa na wengi sitazungumza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba pato la wastani la kila Mtanzania kwa mwaka 2015 ilikuwa ni

Sh.1,918,928. Nimekuwa najiuliza kwamba takwimu kama hizi zimechukuliwa kutoka katika maeneo gani? Kwa sababu kwa sisi ambao tunaishi na wananchi wetu vijijini wale ambao hawana uwezo wa kupata hata laki kwa mwezi, hawana uwezo wa kupata milo miwili ya uhakika kwa siku, unaambiwa kwamba kila Mtanzania ana uwezo wa kupata milioni moja na laki tisa, nadhani ni lazima Serikali inapochukua takwimu ichukue takwimu vijijini ambapo asilimia 80 ya watu wanaishi kule. Wakichukua takwimu za mjini hawawezi kupata hali halisi ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea hali ni mbaya kwelikweli, ni matatizo matupu, ukiambiwa kwamba kila mtu ana milioni moja na laki tisa, unapata mashaka makubwa sana. Kwa hiyo, naomba kwenye takwimu nyingi za Serikali chukueni maeneo ambapo *percent* kubwa ya Watanzania inaishi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la ongezeko la watu na nimekuwa nashangaa Serikali imekaa kimya sana kutokana na ongezeko kubwa la watu Tanzania. Ukiangalia kwenye sensa mwaka 2012 tulikuwa watu milioni 45 japokuwa wengine hawakuhesabiwa. Kwa takwimu za Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake 2016 tuko watu milioni 50.1, *prediction* 2025 tutakuwa watu milioni 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, spidi ya ongezeko la watu haiendani na spidi ya Serikali kutoa huduma muhimu, ni jambo ambalo liko wazi, haiendani kabisa. Ndiyo maana unaona leo wanafunzi wanagoma, mikopo haitoshi, huduma za afya hazitolewi kwa uhakika, elimu bado ni matatizo, Serikali inaogopa nini kuanza kuweka mikakati ya udhibiti wa ongezeko la watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa nchi nyingine, China walivyoweka kwamba mwisho watoto wawili kuna *factor* waliziangalia na maeneo mbalimbali wanaweka idadi kwamba angalau mtu awe na watoto watatu mpaka wanne ili kuweza kutoa huduma. Haifai na haileti tija watu wazaliwe mshindwe kutoa huduma, ni kama sehemu ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzazi ukiwa na watoto kumi huwezi kuwapa elimu nzuri, huwezi kuwavalisha vizuri, huwezi kuwapa huduma nzuri, unawatesa. *Simple applied* kwa Tanzania kuendelea kuona idadi ya watu inaongezeka kwa spidi kubwa lakini Serikali hatuzungumzi chochote ni kuendelea kuwafanya watu wateseke bila sababu. Watu tuwe na watoto ambao tunaweza kuwahudumia vizuri angalau kila mwananchi apate huduma anazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye suala la kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu litekelezwe kikamilifu kwenye bajeti ijayo. Nikianza na mpango wa elimu, Serikali kweli imeanza na mpango

wa kutoa elimu bure, tunatembea kwenye shule zetu bado fedha inayotolewa kwa *retention* haitoshi, changamoto ni lukuki katika shule zote. Kila unapokwenda ni kilio, Walimu wanalia wanafunzi wanalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumetengeneza madawati, madawati maeneo mengi yako kwenye maturubai, yamewekwa *shade* kwa kutumia majani hakuna madarasa ya kutosha, lakini pia hakuna miundombinu ya nyumba za Walimu, hakuna vyoo, ukienda kwenye shule zetu bado changamoto ni nyingi sana. Kwa hiyo, kwenye bajeti ijayo lazima Mheshimiwa Waziri aje na mpango mkakati wa kuongeza miundombinu ya madarasa, nyumba za Walimu kwenye shule zetu za *primary* na *secondary*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la kujenga vyuo vya elimu ya mafunzo, kwa spidi ambayo tunaongezeka nayo na kwa sasa hivi Serikali ambapo inasema *division one* na *two* ndio inaenda vyuo vikuu wengine wanaenda vyuo vya kawaida, vyuo vya mafunzo, wanafunzi wengi wanabaki vijijini, tunaulizwa maswali hatuna majibu. Tunaomba mpango ujao Mheshimiwa Waziri aje na mpango maalum kuhakikisha tunajenga vyuo vya *VETA* kwenye Wilaya zetu na atueleze ni vingapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye mpango huu hapa amesema mpango ni kumalizia chuo kinachojengwa Mahenge, haitoshi! Tunataka Wilaya zote ambazo hazina vyuo vya ufundi ni lazima vipate vyuo hivyo. Hii iende sambamba na kuweka karakana zinazoeleweka na miundombinu yote ili wanafunzi wetu wapate angalau stadi za kazi waweze kujitegemea kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la afya. Njia pekee ya kuondoa vifo vya akinamama na watoto, wazee na makundi mengine Tanzania ni kusogeza huduma karibu na walipo. Tulikubaliana na Serikali karibu miaka kumi sasa kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata mpaka sasa hivi mpango huo bado unakwenda taratibu. Kwa hiyo, kwenye mpango ujao Mheshimiwa Waziri tunataka atuambie zahanati ngapi zitajengwa, za kutekelezwa siyo za kwenye vitabu, ngapi zitajengwa Tanzania nzima? Ni vituo vya afya vingapi vitajengwa kwenye kata zipi, zianishwe na zitekelezwe kwenye mpango ujao ionekane. Pia kuhakikisha kwamba tunapata watumishi wa kutosha na huduma zote muhimu zipatikane na vifaa tiba na dawa ziwepo za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la maji. Watu wanaongezeka changamoto ya maji inaongezeka kila siku. Tunaomba kwenye mpango ujao lazima Waziri atuambie namna gani ya kuondoa changamoto za maji kuendana na ongezeko la watu. Tusingependa mwakani tuanze kushika hotuba ya mwaka huu na ya mwaka kesho hatutaki kama ambavyo Serikali zilizopita. Tunataka tujue yaliyopangwa kwenye bajeti ya mwaka huu yawe yamepita ya

mwakani tuwe na mipango mipya inayotekelezeka, tunaomba sana hilo. Kwa hiyo, lazima mipango mikakati ya maji ya kutekelezeka iweze kuletwa ndani ya Bunge, ianishe wazi na ikatekelezwe siyo kuja kubaki kwenye vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya elimu ya juu. Nimeangalia hotuba ya Waziri anasema kwa mwakani wanategemea kutoa ruzuku kwa wanafunzi kama 124,243 hata wanaoomba mwaka huu ni wengi zaidi ya hao. Inawezekana Serikali haifanyi tathmini ya kutosha kuanzia sekondari, vyuoni kujua idadi ya wanafunzi wanaohitaji kupata ruzuku kwa ajili ya elimu. Tumekubaliana kwamba kila Mtanzania awe maskini awe tajiri, mtoto wa maskini asome wa tajiri asome. Kama wengi hatuwapatii mikopo wanapataje uwezo wa kusoma mpaka kufika vyuo vikuu na hao ni Marais watarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe wanafanya tathmini ya kutosha mwakani wawe na uhakika kwamba watoto kadhaa wanakwenda kupata mikopo na wapate mikopo yao kwa ukamilifu. Mtoto wa maskini unampa asilimia 10 au 20 haimsaidii kitu, anaishi maisha magumu kweli shuleni, wanaishi kwa kula mihogo na magimbi. Tunaomba itengwe fedha ya kutosha kuendana na mahitaji ya watoto maskini ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hakuna mikakati mizuri ya kusimamia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya malizia sentensi unayosema.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hakuna mikakati mizuri ya kukusanya marejesho ya fedha za mikopo. Mimi nilisoma kwa kutumia mkopo wa Serikali, nimelipa miaka mitano iliyopita na nimekamilisha, juzi mwezi Agosti napata barua nadaiwa. Hii ikanipa picha kabisa kwamba hakuna mikakati ya kufuatilia mikopo, kama mtu amelipa miaka mitano iliyopita leo unampa barua anadaiwa, *it seems* kwamba hafuatilii mikopo inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sakaya. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Leah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Kiteto Koshuma, Mheshimiwa Hassan Elias Masala ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia mpango wa bajeti kwa

mwaka 2017/2018. Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mpango mzuri aliotuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia, naomba niunge mkono mpango huu ila naomba nishauri katika maeneo yafuatayo na Mheshimiwa Waziri aweze kuzingatia ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchangia kuhusu madeni ya ndani na nitajikita zaidi katika madeni ya Halmashauri. Halmashauri zetu zinakabiliwa na madeni makubwa ambayo yanaleta ugumu katika utendaji wa kazi. Napenda ku-*declare interest* nilikuwa mtumishi katika Serikali za Mitaa pia ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Madeni haya yamegawanyika katika sehemu mbalimbali naomba niyataje, madeni ya wazabuni, ya watumishi na ya mradi kwa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zinapata ugumu katika ulipaji wa madeni haya kutokana na baadhi ya Halmashauri vyanzo vyao vya mapato ni vidogo. Kwa hiyo, kutegemea Halmashauri ziweze kulipa madeni haya mambo mengi yatakwama kwa sababu wazabuni wamekopa mikopo, watumishi wanahitaji malipo yao na miradi kwa miradi inadaiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni haya nayazungumzia kwa sababu nina hoja za msingi, yamesababishwa na upelekaji kidogo wa fedha ambapo Serikali ilikuwa inatekeleza majukumu mengine muhimu ya kitaifa. Sababu nyingine ni Halmashauri zilitekeleza maagizo mbalimbali mengine ya Serikali ambayo ni muhimu na tumeona matokeo yake ikiwepo ujenzi wa maabara. Kwa hiyo, Halmashauri zimeachwa na madeni makubwa. Mheshimiwa Waziri naomba katika mpango wako uweke mpango pia wa kuzisaidia Halmashauri kulipa madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili naunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuhamisha ukusanyaji wa kodi ya majengo kukusanywa na *TRA*. Ninazo sababu za msingi. Kwanza, baadhi ya Halmashauri zilikuwa hazina takwimu za majengo yanayopaswa kukusanywa kodi ya majengo, hazikuwa na makadirio yanayoeleweka ya kukusanya mapato hayo zilikuwa zikikadiria mapato kidogo. Hata yale mapato kidogo yaliyokuwa yakikadiriwa ukusanyaji wake ulikuwa ni hafifu sana. Hivyo tu niishauri Serikali mfumo wa Taifa wa kukusanya mapato ya Serikali za Mitaa uzifikie Halmashauri kwa wakati na fedha hizo zikipatikana basi zirejeshwe haraka Halmashauri ili waweze kutekeleza shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa namna inavyokusanya mapato kikamilifu na imekuwa ikivuka malengo. Hata hivyo,

ukusanyaji huu wa mapato kikamilifu hauwezi kupunguza umaskini walionao wananchi wetu. Serikali inapaswa iwekeze kikamilifu katika sekta zinazogusa maisha ya wananchi moja kwa moja zikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee upande wa kilimo cha pamba. Sekta ya pamba bado inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinapelekea wakulima kuanza kujiondoa kuzalisha zao hilo. Baadhi ya changamoto ni ukosekanaji na uhafifu wa pembejeo wanazopewa wakulima. Wakulima wamekuwa wakipewa pembejeo hafifu kwa mfano mwaka jana dawa za kuua wadudu hazikufanikiwa, ziliwafanya wale wadudu wasinzie. Kwa mwaka huu dawa ziko kidogo, ziko kama kopo 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iweke mpango wa kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wingi kwa sababu wananchi wamepata pia mwamko wa kulima kutokana na bei ya pamba iliyotolewa mwaka jana ambayo Mheshimiwa Rais aliisimamia na wakulima wakapata angalau bei iliyoweza kuwanufaisha kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kukabiliwa na tatizo la mbegu. Ipo mbegu ya UK91 ambayo imeingia sokoni kwa muda mrefu na kupoteza ubora wake. Mbegu hii imekuwa ikipandwa na wakulima wakati mwingine imekuwa haioti na kusababisha umaskini kwa wakulima wetu. Nashauri Serikali iweke mpango kwa mwaka 2017/2018 wa kuidhinisha mbegu mpya ya pamba ili iweze kuinua uchumi wa wananchi hasa Kanda ya Magharibi, zao la pamba linategemewa katika uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea afya. Wakati tukichangia bajeti ya mwaka 2016/2017, yalitoka matamko ya Serikali kwamba Serikali inajipanga kufanya tathmini ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya. Kwa hiyo, natumaini safari hii mpango mzuri utakuwepo na bajeti ya kutosha itawekwa ili kuweza kukamilisha ujenzi wa zahanati na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna ufadhili ambao unatolewa kwa kitengo cha afya kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli ambazo siyo za *construction*. Tumeona wafadhili wakitoa fedha za *result based financing.* Naomba vigezo vinavyotumika vipitiwe upya kwa sababu ili hospitali ya wilaya au kituo cha afya kiweze kufuzu kupata fedha hizi inatakiwa zifikie nyota tano. Vituo hivi vya afya au zahanati zinawezaje kufuzu kupata hizo nyota tano ili ziweze kupata fedha hizo kwa sababu ukiangalia changamoto nyingi zinasababishwa na Serikali. Kwa hiyo, inakuwa viko nje ya uwezo wa Halmashauri. Naomba yafanyike upya mapitio ya vigezo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mheshimiwa Deo Ngalawa ajiandae.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili pia niweze kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu. Pia naendelea kumshukuru Mungu kwa sababu ameendelea kunipigania na kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoanza kuchangia Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2017/2018 nitapenda sana niwapitishe katika kitabu hiki kwa kutumia *pages*. Kwanza kabisa, naomba tuangalie ukurasa wa pili wa Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa, kifungu cha 1.4 kinazungumzia utaratibu wa kuandaa Mapendekezo ya Mpango. Katika utaratibu wa kuandaa Mapendekezo ya Mpango umeangalia mambo mbalimbali ikiwemo hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati anafungua Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anafungua Bunge hili la Kumi na Moja wote tulimsikiliza kwa makini. Mheshimiwa Rais aliongea vizuri sana na hotuba yake ilikuwa inalenga katika kuwakomboa wananchi wa Tanzania. Mheshimiwa Rais aliongea mambo mengi sana na moja ya jambo ambalo alisisitiza ni viwanda. Mheshimiwa Rais alisisitiza kwamba anataka Tanzania iwe ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimepitia mpango huu vizuri sana, ukiangalia viwanda vimeongelewa kwa kuguswaguswa, nasikitika sana kusema hilo. Kwa maana kwamba mpango haujajikita katika kusema waziwazi kwamba ni viwanda gani ambavyo sasa vinaenda kuangaliwa na mpango huu. Hivyo basi, napata wasiwasi kama kweli sisi tuko tayari kufuata ushauri ambao Mheshimiwa Rais alikuwa akiuongea? Aliongea katika kampeni zake, aliongea katika kulifungua Bunge hili na mpaka sasa bado Mheshimiwa Rais anaendelea kuongea na kusisitiza kuhusiana na suala zima la viwanda, napata wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kwamba anapotuletea mpango mwezi Mei nadhani baada ya kuchukua mapendekezo yetu Waheshimiwa Wabunge, namsihi sana katika mpango wake atuelezee ni viwanda gani hasa ambavyo anaenda kuviweka katika mpango wake. Vivyo hivyo atakapokuja kutenga bajeti atenge bajeti ambayo kweli ita-*reflect* kwamba sasa Tanzania inaenda kuwa Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la maji. Hatutaweza kuwa na viwanda nchini Tanzania na hatutaweza kamwe kufikia malengo ya Mheshimiwa Rais ambayo ni malengo mazuri sana kama haitakuwa Tanzania ambayo wananchi wa kawaida, mwananchi aliyeko kijijini anaweza akapata maji wakati wowote atakapoyahitaji. Nasema hivi kwa sababu gani? Maji ni kiungo kikubwa sana kwani yanaweza yakasaidia katika kilimo. Ukiangalia sasa hivi naweza nikasema nchi hii inaelekea kwenye jangwa kwa sababu hakuna maji kabisa. Nchi imekuwa na ukame na hata watu wa Idara ya Hali ya Hewa pia wametabiri kwamba sasa hivi hakutakuwa na mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Mwanza kuna kilimo cha pamba na mazao mengine mbalimbali lakini wananchi wanashindwa kulima kwa sababu ya ukosefu wa maji. Hata hivyo, ukiangalia katika mpango huu, kama ninavyosema na nitarudia kusema maji yanatajwa tu kwamba maji, maji yanafanya nini? Tuna mikakati gani kwamba maji sasa yanaenda kupatikana Tanzania? Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango atakapoleta mpango atuletee mpango mkakati kwamba anaenda kufanya nini ili kuhakikisha kwamba Tanzania inaenda kuwa na maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kuna suala pia la *irrigation scheme,* nimeliona limetajwa humu katika mpango lakini halioneshi dhamira kwamba kweli tunataka kufanya *irrigation scheme* hapa nchini Tanzania ili kuwezesha kilimo ambacho ndicho kitakachotupeleka kwenye viwanda. Kwa sababu tutakapoanzisha viwanda tunatarajia kuwa na *raw materials,* tunaenda kupata wapi hizi *raw materials* kama hatutaweza kuimarisha kilimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena niongelee suala kubwa sana ambalo Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, ameliongelea wakati wa kampeni zake. Wakati wa kampeni zake akifanya ufunguzi pale Jangwani aliongea kwa ari kubwa sana na alikuwa anamaanisha. Najua anamaanisha kwa sababu niliona jinsi alivyoongea. Hakuna mtu aliyemtuma kuongea, alijituma mwenyewe kwa sababu anao uchungu na anayo nia ya kuwasaidia Watanzania ili waondokane na umaskini. Mheshimiwa Rais alisema kwamba atahakikisha Serikali yake inatoa milioni 50 katika kila kijiji, hii ni katika kuwawezesha Watanzania kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitisha bajeti hapa niliongea kwa uchungu sana kuhusiana na suala la milioni 50. Nashukuru kwamba Serikali ilisikiliza na ikaongeza pesa kidogo hadi kufikia kutenga bajeti ya shilingi bilioni 49. Hata hivyo wakati nikichangia katika bajeti iliyopita nilisema kwamba shilingi bilioni 49 ambazo zimetengwa bado hazitoshi. Tuna vijiji 13,000 hizi hela ambazo zimetengwa bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, natambua juhudi za Serikali, natambua juhudi ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anazifanya kuhusiana na suala la kutimiza ahadi ya Rais ya milioni 50, ili kuweza kuwakomboa Watanzania kutokana na umaskini, namwomba na ninamsihi sana katika mpango wake ajaribu kuelezea ni vijiji vingapi ambavyo vitaweza kupata hii shilingi milioni 50. Atuoneshe na atuelezee wazi kwa sababu tunapata kigugumizi tunapozunguka kwenye Majimbo yetu, wananchi wameandaa vikundi mbalimbali wamevi-*register,* wako kamili wanasubiri milioni 50 ya Mheshimiwa Rais, lakini sasa kama hatutataja kwenye mpango wananchi tutawaambia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapoleta mpango uwe umejumuisha ni vijiji vingapi, vitapata shilingi ngapi, ni mkoa gani kwa Tanzania nzima? Hivyo vijiji avitaje ili tuweze kufahamu kwamba sasa mimi Mkoa wangu wa Mwanza vijiji kadhaa vitapata na Mkoa wa Tanga vijiji kadhaa vitapata. Naomba sana kuishauri Serikali kuhusu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea suala la afya. Juzi nilisimama hapa kwa uchungu mkubwa sana na nikasema kuhusiana na suala la dawa. Kumekuwa na upungufu wa dawa na hata Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu alikiri kuwepo kwa upungufu wa dawa. Tumekuwa tukiilaumu Wizara ya Afya ambapo sasa hivi naomba kabisa niombe radhi kwa Wizara ya Afya kwa sababu naamini kabisa nimewakosea kuwaonea nilitakiwa nimlaumu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa sababu yeye ndiye ambaye anahusika na suala zima la kutenga fedha kwa ajili ya dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango atakapoleta Mpango katika Bunge hili, atuoneshe wazi kwamba sasa ni fedha kiasi gani au ni mikakati gani aliyonayo ya kuhakikisha dawa zinapatikana Tanzania nzima ili akinamama wasiteseke. Akinamama ambao wanateseka ni wajawazito wanakwenda kwenye hospitali wanaishia kupimwa ujauzito tu basi, kuangalia vipimo kwamba mimba imefikia katika hatua gani lakini dawa hakuna! Inapotokea anapata tatizo lolote mama huyu anaandikiwa dawa anaambiwa nenda kanunue kwenye *pharmacy,* pesa hana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunayo nia ya kuwasaidia Watanzania namsihi sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu nadhani bado upo, dakika 15?

**MBUNGE FULANI:** Umekwisha.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiteto Koshuma. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Hassan Elias Masala ajiandae Mheshimiwa Deo Ngalawa ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga na tutamalizia na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani kwako kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu naomba nijielekeze katika maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza ambalo ningependa kuligusia kwa umuhimu wake ambalo hili linaunganisha maeneo yote ni eneo la elimu. Nimepitia vizuri mpango, naomba nitoe pongezi kwa yale ambayo tayari yameshafanyika ndani ya kipindi hiki lakini bado kuna maeneo ambayo nilifikiri kuna umuhimu wa kuelekeza nguvu na kuona namna gani tunaweza kuweka maboresho zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni uboreshaji wa miundombinu. Tayari tumeona utekelezaji wa upatikanaji wa elimu bure katika shule zetu za msingi pamoja na sekondari, lakini bado kuna tatizo kubwa za vyumba vya madarasa katika shule zetu lakini pia kumekuwa na matatizo makubwa katika upatikanaji wa nyumba za Walimu. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika mpango huu ambao tunaujadili sasa eneo hili ni lazima lioneshwe wazi ni kwa kiasi gani tunakwenda kuboresha miundombinu hii ili kuunga mkono kile ambacho tayari kimeshafanyika katika eneo hili la kutoa elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sera yetu ya kuboresha viwanda wataalam watapatikana kupitia elimu, lakini bado kuna umuhimu wa kuangalia namna gani tutahusianisha maendeleo yetu pamoja na elimu ambayo tunaitoa kwa vijana wetu katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie upande wa elimu ni suala zima la mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Kumekuwa na mkanganyiko mkubwa ambapo sisi kama Wabunge lazima tuishauri vizuri Serikali yetu ili iweze kuendelea kutoa mikopo kwa vigezo vile ambavyo vilishakuwa vinatumika. Yako marekebisho, upo upungufu

tulishazungumza hapa mwaka jana lakini kuna umuhimu sasa wa hiki ambacho kinafanyika sasa hivi kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Serikali kwa ujumla lazima ifanye jitihada za makusudi kuingilia kati ili kuhakikisha watoto wa wakulima ambao leo hii wanafukuzwa vyuoni bila sababu za msingi wanapata mikopo ili waweze kupata elimu, ambapo hawa ndiyo tutakwenda kuwatumia baadaye katika viwanda ambavyo tunasema tunataka kwenda kuviboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili naomba pia nimshauri Mheshimiwa Waziri, hebu wachukue jitihada za makusudi kuiangalia Bodi ya Mikopo. Sasa hivi wamekuja na vigezo ambavyo vitakwenda kuwabana watoto wetu kwa kiasi kikubwa sana. Wametengeneza fomu ambazo kimsingi ukiangalia kwa undani vigezo ambavyo wanakwenda kuviweka bado haviendi kumsaidia mtoto wa mkulima ambaye kwa kweli sehemu pekee ya kukimbilia ni katika Serikali ili waweze kupata mikopo ambayo itaenda kusaidia kuzalisha wasomi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka nichangie ni la kilimo. Naomba niungane au nitoe salamu kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Nachingwea na Kusini kwa ujumla. Kwa muda mrefu tulikuwa tunajadili kero ambazo tumekuwanazo kwenye zao la korosho sasa hivi korosho imekuwa na uchumi mkubwa sana. Serikali imeondoa tozo tano ambazo sisi tulizijadili hapa katika mpango huu mwaka jana. Katika hili Mheshimiwa Waziri naomba tuwapongeze sana kwa kusikiliza kilio chetu, tumeweza kuondoa kodi. Leo hii tunavyozungumza mkulima anapima korosho yake kilo moja shilingi elfu tatu mpaka elfu tatu na mia nane, hili ni jambo zito, ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu naomba tuharakishe katika suala zima la malipo kwa wakulima wetu mara baada ya kuwa minada imeshafanyika. Leo hii nazungumza kwenye Wilaya yangu ni zaidi ya siku nane mnada umeshafanyika bado wakulima wanaendelea kupata shida malipo yao hawajapata. Hii itaenda kusababisha chomachoma kuendelea kuwadhulumu wakulima kitu ambacho Serikali tayari ilishapiga hatua katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie katika eneo hili la korosho au katika eneo la kilimo ni suala zima linalohusiana na utendaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Serikali inapoteza mapato mengi sana katika eneo hili. Ukiondoa korosho ambayo leo kwetu imekuwa ni uchumi mkubwa bado tuna mazao kama ya ufuta, mbaazi ambayo mwaka jana na mwaka huu tumeuza kwa bei ya chini sana na hii ni kwa sababu Bodi ya Mazao Mchanganyiko haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapoteza kodi hapa, Halmashauri zetu zinapoteza kodi, lakini wakulima wetu pia wanapoteza fedha nyingi ambayo tulifikiri ingeweza kuwasaidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anapokwenda kujumuisha, anapokwenda kushauriana na wenziwe tunaomba katika eneo hili tusaidiane na watu wa Wizara ya Kilimo ili tuhakikishe Bodi ya Mazao Mchanganyiko inafanya kazi ili tuweze kukusanya kodi zaidi ambayo itasaidia katika eneo hili la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la upatikanaji wa pembejeo. Pembejeo bado hazipatikani kwa wakati. Hapa tunavyozungumza sasa hivi msimu wa kilimo umeanza lakini mpaka sasa hivi bado pembejeo kwa wakulima wetu hazina uelekeo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri, hatuwezi kujadili kuwa na viwanda kama hatuwezi kujadili namna ya kuwa na kilimo bora. Kilimo bora tutakipata kwa kuwapelekea wakulima pembejeo kwa wakati na vitendea kazi vingine ambavyo vitawasaidia. Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu tuishauri Serikali ili iweze kuboresha katika eneo hili ambalo kimsingi litakwenda kuwasaidia wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika kilimo ni suala zima la kufufua na kuchukua viwanda ambavyo tayari vilishachukuliwa na wawekezaji. Ndani ya Wilaya yangu ya Nachingwea tuna viwanda viwili, kimoja cha korosho lakini tunacho kiwanda kimoja cha kukamua mafuta. Naomba nimshukuru kwa upekee Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara katika haya maeneo, Serikali haina sababu ya kupoteza muda ichukue hivi viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale majengo sasa hivi yanatumika kwa matumizi ambayo hayakukusudiwa, vipuri vinaendelea kung'olewa katika vile viwanda. Leo hii tunahitaji kuwa na *processing industries* kwa hizi korosho tunazozalisha. Tungefurahi kuona Serikali yetu kwa hii sera ya kuwa na viwanda inaenda kuchukua hivi viwanda ili tuweze sisi wenyewe kuandaa korosho zetu, ufuta wetu kwa bei nafuu ambayo tunafikiri itakwenda kuleta tija kwa mkulima badala ya sasa hivi kuuza korosho na ufuta kwenda nje ya mipaka yetu kufanyiwa *processing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima linalohusu nishati. Hatuwezi kuwa na viwanda, hatuwezi kufanya lolote kama nishati ya umeme bado ni tatizo. Mikoa yetu mingi bado umeme wa uhakika hatuna. Kwa hiyo, naomba Waziri atakapokwenda kuhitimisha na kupitia mpango wake lazima aseme tatizo la umeme katika Majimbo yetu na Wilaya zetu linakwenda kupatiwa ufumbuzi kwa namna gani? Hili ni lazima lionekane katika mpango badala ya kuwa katika ujumla wake kama ambavyo imeonesha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii, naomba nikushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masala. Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Ngalawa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga na tutamalizia na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nijaribu kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Moja kwa moja nijikite juu ya suala la Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Liganga na Mchuchuma ni suala ambalo hata tafiti zake zimefanyika toka mwaka 1929. Serikali imekuwa ikilizungumzia suala hili kwa miaka chungu nzima, lakini tulijaribu kupata faraja hasa sisi watu wa Ludewa pale tulipoambiwa kwamba miradi hii inaanza. Ikumbukwe katika Bunge lako Tukufu niliuliza swali tarehe 19/4 juu ya fidia kwa wale ambao wamepisha hii miradi kufanyika. Tulijibiwa kwamba Juni ndugu zetu wale wa Ludewa wangeweza kulipwa fidia yao na vilevile Bunge liliambiwa mradi ule ungeweza kuanza Machi, 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Ludewa waliaminishwa na sasa wanapiga kelele sana juu ya hili. Nipende tu kutoa taarifa katika Bunge lako kwamba hawa watu wanajiandaa kuja Dodoma kujua hatma yao. Vinginevyo waruhusiwe yale maeneo waliyopisha kwa sababu ni maeneo ya kilimo na ndiyo wanayoyategemea waendelee na kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango Mheshimiwa Waziri anazungumzia sana hili suala la Liganga na Mchuchuma, lakini jinsi ninavyoiona ni kwamba, hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa. Mpango unazungumza hapa kwamba mradi wa umeme wa *megawatt* 600 unaendelea, sasa najiuliza unaendelea wapi? Mimi sijaona kitu chochote kinachoendelea pale Mchuchuma. Hakuna kitu kama hicho! Labda Mheshimiwa Waziri aje atueleze na alithibitishie Taifa kwamba nini kinachoendelea kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa juu ya *Power Purchase Agreement* ndiyo inayosumbua, lakini mpaka sasa hatujui *fate* yake na mradi utaanza lini? Je, *coordination* ipoje kati ya Wizara na Wizara na kati ya Waziri na Waziri? Huyu anasema fidia italipwa Juni, sasa hivi tokea Juni ni miezi minne imeshapita hakuna fidia na wala hakuna tamko la Serikali linalosema kitu chochote juu ya fidia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapotuaminisha kwenye Bunge sisi tunaenda kuwaambia wananchi Serikali imesema moja, mbili, tatu, nne; sasa leo hii nikienda kule mimi ndiyo ninayeonekana mwongo! Sasa suala la mimi

kuonekana mwongo haiwezekani, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje na tamko ili tulichukue na kulipeleka kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nijikite kwenye miundombinu. Leo hii tunasubiri suala la *standard gauge* kwa reli ya kati, tunaowategemea kuja kufanya hii kazi ni Wachina. Leo hii kitu kidogo kabisa cha Liganga na Mchuchuma tunakaa tukiyumbishana kwa suala la *Power Purchase Agreement*. Ninachofahamu mkataba huu siyo wa jana wala sio wa juzi, lazima kuwepo na *continuity,* walipoishia wenzetu sisi tuendelee. Kama pana tatizo basi tujue kwamba hili ni tatizo la msingi na tupeane maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tukiwafuatilia Mawaziri wetu hawana majibu na tunarushiana mpira. Ukienda kwa Waziri wa Madini anazungumza hivi, ukienda kwa Waziri wa Viwanda anazungumza hivi, ukienda kwa Waziri wa Fedha anazungumza hivi, inafika wakati tunakata tamaa juu ya suala hili. Waziri alikuja Mchuchuma Januari na alikuwa anazungumzia hili, sasa haya mazungumzo yanachukua muda gani, lazima tuwe na *time frame!* Ifike mahali tuseme itakapofika tarehe hii basi hii kazi iwe imekwisha, hapo tutakuwa tunaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya miundombinu. Kule kwetu Ludewa tumepakana na nchi ya Malawi, kuna eneo la kilometa zinazokadiriwa kuwa 200, eneo hilo halina miundombinu ya barabara hata moja na hilo ni eneo la mpakani. Nakumbuka juzi juzi hapa wenzetu walikuwa wana-*demand* lile ziwa na pakawa na kitu kama mgogoro. Sasa najiuliza, eneo la mpakani lenye urefu wa kilometa 200 halina miundombinu ya barabara, halina mawasiliano ya simu, hakuna umeme, je, likitokea la kutokea *defense* yetu ipoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kulieleza Bunge lako, wananchi kule wameamua kuchukua hatua kulima barabara kwa mikono. Tumeshalima kilometa 40 kwa jembe la mikono na sururu. Sasa kutokana na umuhimu wa eneo hilo kiulinzi na kiusalama na kiutalii Mheshimiwa Waziri aliweke kwenye mpango. Ziwa letu lina matatizo makubwa. Hivi ninavyozungumza wiki iliyopita watu watatu wamefariki kwa sababu ya usafiri na huwa linachafuka halitoi taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuchukua fursa hii kuomba Serikali iwasaidie wale watu ambao wameamua bila kulipwa kulima barabara kwa kutumia mikono yao. Eneo la Ziwa Nyasa, eneo kubwa ni eneo la Ludewa kuliko Kyela, Mbinga na Nyasa. Kwa hiyo ni lazima hawa watu tuwape kipaumbele. Tuna vijiji vinavyokadiriwa 20 hakuna mawasiliano ya simu kabisa yaani ukishazama huko umeshazama, taarifa zako huwezi kuzipata. Kwa hiyo,

ifike kipindi watu hawa tuwaonee huruma na Serikali itu-*support* kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la elimu, mpaka sasa Ludewa ina *deficit* ya Walimu 521 lakini tunapangiwa Walimu 40. Tumejaribu kulipeleka kwenye Idara na Wizara husika watusaidie. Sasa Mheshimiwa Mpango aliweke kwenye mpango wake kwamba Ludewa tuna uhaba wa Walimu na hata ukiangalia *performance* imeshuka sana kwa sababu hiyo. Kuna shule kama nane (8) hivi zina Walimu wawili au watatu, *maximum* ni Walimu wanne na tuna shule za misingi 108. Kwa hiyo, hivi vitu ni lazima tuviweke kwenye mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la afya, kweli Ilani ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia vituo vya afya kila kata na pia inazungumzia zahanati kila kijiji. Labda tuzungumze sasa hapa wajibu wetu sisi kama Wabunge ni nini? Wabunge ni wahamasishaji wa maendeleo na vilevile tuna wajibu wa kukusanya nguvu na ku-*mobilize* watu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Ngalawa. Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga tutamalizia na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango huu unaoendelea. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na timu yake yote kwa kutuletea huu mpango mapema zaidi ili tuweze kuufanyia kazi, uboreshwe na baadaye tuweze ku-*achieve* yale ambayo tunatarajia kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza sana Mheshimiwa wetu Rais wa Awamu hii ya Tano kwa nia njema kabisa ya kutaka kuleta maendeleo ya nchi hii hasa ukiangalia kwamba anataka keki ya Taifa igawanywe kuanzia kwa mwenye kipato cha chini mpaka mwenye kipato cha juu. Kwa hiyo, jitihada nyingi sana anazifanya na tukizingatia kwamba yeye ndiyo mara yake ya kwanza kushika uongozi ni lazima kutatokea changamoto za hapa na pale. Kwa mfano, anapambana na ufisadi, rushwa, wafanyakazi hewa, matumizi mabaya ya Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea sasa hivi kwa mtazamo wangu, watu wanalaumu wanaona kwamba *it is a government failure*, kwangu mimi sioni kwamba Serikali imeshindwa, ni muda mchache, hapa tupo kwenye *transitional period*, kwamba kuna *reforms* nyingi zinafanyika ili tuweze ku-*achieve* haya ambayo Mheshimiwa Rais wetu anayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *change* ya aina yoyote huwa kuna *early adapters, slow adapters* na *late adapters* kwamba wapo wale wanaokubali mabadiliko haraka sana na wapo ambao tayari wanampongeza Mheshimiwa Rais, hawa ni wale wanyonge ambao haki zao hazitolewi. Hata hivyo, wapo wale ambao wanakubali taratibu tunawaita *slow adapters,* hawa wanaangalia kwanza mazingira wajiweke sawa, lakini kuna wale *late* ambapo yeye anasubiri kwanza mambo yafanikiwe ndiyo aende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kinachotokea kutokana na *change,* wale wanaolaumu inawezekana ni katika kundi la wale watu ambao ni mafisadi, wala rushwa ndio wanamkwamisha Mheshimiwa Rais wetu. Kwa hiyo, hawa kwa vyovyote hawawezi kukubali hizi *reforms* ambazo zimepangwa ili tuweze ku-*achieve* kwamba sasa keki ya Taifa wafaidi wananchi kuanzia wa kipato cha chini mpaka kipato cha juu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba sasa tumpe *support* kwa sababu kila utawala mpya lazima utakuwa na changamoto zake. Yeye ni mara yake ya kwanza. Tukianza hata kihistoria Mwalimu Nyerere wakati amepokea utawala kutoka kwa wakoloni alipambana sana kwenye ujamaa na wapo watu ambao walikuwa ving'ang'anizi ndiyo wakatuletea hata huu ujinga ujinga wa *structural adjustment* ambayo hailingani. Kwa hiyo, alipambana na watu wengine walikataa kwa sababu ya maslahi yao, tuliwaona kina Kambona walikimbilia nje, ndiyo hiyo hiyo ambayo inatokea sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija upande wa Mheshimiwa Mstaafu Rais Mwinyi, watu walimuita ruksa lakini kutokana na mazingira aliyoyakuta wakati ule, bidhaa hamna akafungulia. Kwa hiyo, ni kama vile tunavyosema kila zama na kitabu chake. Pia ukiangalia wakati wa Mheshimiwa Mkapa watu waliita ukata lakini mwaka wa kwanza aliyumba baadaye mambo yakaenda, vizuri sasa hivi tunamkumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija upande huu wa Mheshimiwa Rais wetu aliyestaafu juzi, Rais Kikwete, wengi wakasema labda mpole lakini alifanya mambo makubwa lakini mwanzoni alivyoanza watu wakaona haendi. Sasa na hii Awamu ya Tano, hizi *reforms* jamani nani anayetaka ufisadi uendelee au rushwa iendelee, wafanyakazi hewa, tunapoteza fedha bure, ndiyo hiki kinachofanyika. Kwa hiyo, tumpe *support* Mheshimiwa Rais wetu afanye kazi na

sisi Watanzania ndiyo tunaotakiwa tumuunge mkono badala ya kumbeza na kuibeza Serikali. Nafikiri hii siyo vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande sasa wa mpango, naomba nichangie kuhusu viwanda. Sera ya viwanda ni nzuri lakini tuangalie, je, Tanzania sasa hivi tunataka viwanda vya aina ngani? Kwa sababu sasa hivi tukumbuke tuko kwenye utandawazi, ni *free market*, tusije tukatengeneza kiwanda ambacho tunategemea labda soko la ndani tuko karibu milioni 50 labda *consumers* ni milioni 20, kwa hiyo soko la ndani halitoshelezi. Tufanye utafiti na soko la nje, siyo kwamba viwanda ili mradi viwanda. Nia ya viwanda ni kuajiri watu wengi mbali ya *production,* kwa hiyo, tuhakikishe tunaanzisha viwanda vile ambavyo vitawalenga hawa watu wetu wa chini waweze kupata ajira hasa vijana wetu wanaomaliza vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna hili suala la kodi na tozo nyingi. Niungane na wenzangu, jamani sasa wasi-*take advantage* ya Serikali kukusanya kodi, kufanya mauzauza huko kuiharibia Serikali na ndiyo kinachofanyika sasa hivi. Kwa hiyo, tunaomba sana Waziri aliangalie suala hili, zile kodi na tozo ambazo ni kero kwa wananchi ziondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukienda kwenye mabenki kwa mfano *CRDB,* jamani ukitaka *statement* ya karatasi moja ni Sh.11,000/= hivi kweli! Ile si ni ku-*print out* tu kwa nini wasitoze hela kidogo lakini sasa watu wanatengeneza *business.* Sasa hivi ukitumia ile mashine ya *CRDB* labda umeenda kununua kitu wanakata asilimia tano ya *value* ya kile kitu ulichonunua. Kama ni shilingi milioni tatu asilimia tano ya milioni tatu inakatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wizi kwa sababu wewe ni mteja wao lazima wakupe hizo fursa, wachukue hata elfu moja kama vile unavyochukua kwenye *ATM,* kwa hiyo hizi ni kero. Hata *parking fee* hizi za magari jamani kwa siku mtu akipaki Sh.1,000x30 ni Sh. 30,000, Sh. 30,000x12 ni Sh. 360,000 hiyo ni mbali na *tax* nyingine ambazo tunalipa. Kwa hiyo, kodi kama hizi ziangaliwe *either* zitolewe au zipunguzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni *emphasize* kwenye maendeleo vijijini, hii ni *area* yangu maendeleo vijijini. Huwezi ukawa na uchumi wa kati bila ya kuwa-*empower* hawa watu wa vijijini. Kwa hiyo, naomba miradi ya maendeleo ile iliyoachwa 2014/2015, 2015/2016 ipewe kipaumbele ili ile *continuity* ya kuleta maendeleo na ile *Tanzanian vision* iweze kuwa *achieved.* Tukiiruka ile tukaanza na hii mipya hatutaweza kufika kule, programu zetu zitakwama. Kwa hiyo, ni-*emphasis* tuangalie vitu ambavyo ni mahitaji ya msingi vijijini kama vile maji, elimu, barabara na masoko kwa ajili ya mazao yao. Tuki-*promote* hivi naamini kabisa huu uchumi wa viwanda na kipato cha kati utafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kitu kingine, tusi-*undermine human capital,* ili tuweze kupata maendeleo lazima tuwekeze kwenye *capacity building*. Kwa hiyo, hizi semina za ndani na nje ni lazima hawa washiriki kwa sababu kwa dunia hii ya utandawazi ya sasa hivi kuna *new technologies, new skills, new approaches concept* ili tuweze kuingia kwenye hili soko la dunia na sisi tuweze ku-*compete*. *Otherwise* tukiangalia tu miradi tukasahau kwenye *human capital* itakuwa ni shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli naipongeza Serikali, napongeza Mapendekezo ya huu Mpango ambao umeletwa ili tuyafanyie kazi, tuboreshe badala ya kubeza na kudharau, hapana, huu ni mwanzo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha azingatie haya maoni ambayo wachangiaji mbalimbali wanatoa, yale ambayo tunaona kweli yanafaa ili kuboresha huu mpango na hatimaye nchi yetu iweze kufikia maendeleo endelevu ifikapo 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

**MHE. KANGI A.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pia kunipa nafasi ya mwisho katika kuchangia hoja ya Mpango wa Maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi ni binadamu husahau, sisi ni binadamu ambao wakati mwingine hatuwezi tukaukubali ukweli hata kama ukweli utabaki kuwa ukweli. Niwakumbushe Wabunge wenzangu kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Bunge hili pamoja na mambo mengine aliliomba Bunge hili, alituomba Wabunge kwamba ameomba kazi ya kutumbua majipu tumsaidie ahakikishe anatumbua majipu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia aliliomba Bunge hili limsaidie pale anapoleta mipango yake ya Serikali tumsaidie ili mipango hiyo iweze kutekelezeka, tuweze kuijenga nchi yetu. Hata hivyo, Bunge hili sasa linapoteza mwelekeo, limepoteza kumbukumbu limebaki sasa ni Bunge la kumlaumu Rais, limebaki ni Bunge la kulialia. Bunge hili litakuwa halimtendei haki Mheshimiwa Rais wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Rais ana nia njema na Taifa, najua Mheshimiwa Rais kwa kauli mbiu ya hapa kazi tu inasababisha watu ambao walikuwa wanaishi kwa mazoea waweze kumlaumu na kumlilia

kwamba anaharibu nchi yao. Tunamtia moyo, tunamwunga mkono aendelee kushika na kukandamiza mahali ambapo amekandamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazoea ni ya ajabu sana, tulizoea kwa makundi, wako wafanyabiashara walizoea kukwepa kodi, leo wameshikwa pabaya wanaanza kulia kwamba sasa biashara imekufa. Watumishi tulizoea posho za hapa na pale, tulizoea kusafiri, sasa wameshikwa pabaya wanaanza kulialia. Wabunge tulizoea kwenye Kamati tunapata chai nzuri, tunakula andazi la inchi kumi na nane leo tunakula andazi la sentimita mbili, tumeshikwa pabaya tunaanza kulialia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge sasa tunaanza kulialia kwa sababu tumeshikwa pabaya na kuwaingiza wananchi wanyonge kwamba wao ndiyo wanaonewa kwamba wao ndiyo hawana fedha. Mambo mengine ni ya ajabu sana, mpaka unajiuliza huyu ndiye Mheshimiwa Mbowe? Mbowe naye leo anailaumu Serikali imefilisika! Hivi ni Mbowe huyu kweli ambaye analipiwa gari na Serikali, shangingi, mafuta yamejaa, kiyoyozi kiko masaa 24, anasema Serikali imefilisika? Huku ni kuwatumia wananchi vibaya, ni kutaka kuwachonganisha wananchi na Serikali yao na Rais wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa kwa bahati mbaya leo hayupo, Mheshimiwa Msigwa yeye kama Mchungaji nilitarajia atatumia taaluma yake kuwashauri wenziwe kwamba hata wakati ule kwenye Biblia wakati Musa anawachukua wana wa Israel kutoka Misri awapeleke kwenye nchi ya ahadi, nchi yenye maisha mazuri jangwani walipata shida, hawana maji, wanang'atwa na nyoka lakini hatimaye kwa kuwa walikuwa na Mungu, Musa aliwafikisha salama na wakaishi maisha mazuri. Mheshimiwa Msigwa awashauri wenzake kwamba katika safari hii kutakuwa na misukosuko ya hapa na pale, lakini Musa wetu Mheshimiwa Rais Magufuli anatupeleka nchi ya Kaanani twende kuishi maisha ya asali. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo pia machache ya kumshauri Rais wetu wa nchi hii. Rais wetu alituahidi kwamba sisi Watanzania ambapo yeye ni dereva na sisi ni abiria wake anatusafirisha kutoka mahali tulipopandia basi atupeleke kwenye nchi ya ahadi. Namshauri Mheshimiwa Rais barabarani yeye kama dereva kuna matuta lazima ajue matuta haya akiendesha vibaya yataleta ajali na Watanzania hatutafika mahali anapotupeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri pia anapoendesha gari kuna *zebra cross,* wanafunzi wana-*cross,* ng'ombe wanapita, aendeshe vizuri Watanzania atufikishe salama. Naomba nimshauri pia anapoona wameandika *speed* 50 na yeye aende *speed* 50 ili Watanzania atufikishe salama. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango nimeusoma, Mpango huu ni mzuri, yako maeneo ya kushauri. Tunayo dira yetu ya Taifa ya Maendeleo 2025, tunayo Ilani ya CCM, vitabu hivi viwili ndivyo vinavyomsaidia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango katika kuja na mapendekezo mazuri ambayo yanaenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya CCM. Mheshimiwa Waziri yako maeneo humu ambayo inabidi nimshauri, kwenye Ilani yetu kuna mambo ya kilimo, kwenye mambo ya kilimo mpango wake umeacha kabisa mazao ya biashara kama vile pamba, tumbaku, kahawa, katani na pamba pamoja na mazao mengine imeshuka sana. Nimpe mfano, mwaka 2012/2013, tulizalisha pamba tani 356,000 na 2016/2017 imeshuka mpaka tani 120,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Kama leo watoto wetu wa maskini wanakosa mikopo ya elimu ya juu…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila utaratibu)*

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Kimbilio lao ni kwa wazazi wao ambao wanalima pamba. Kama wazazi wao wanalima pamba na humu hajaweka mpango wa kusaidia zao la biashara la pamba, watoto wa maskini hawatasoma, watoto hawa watakuwa wa mitaani. Namshauri atakapoleta Februari rasimu yake isheheni masuala ya kilimo cha mazao ya biashara, masuala ya mbolea ili watoto wa maskini waweze kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani Mheshimiwa Waziri ameweka kanda maalum za kiuchumi. Kanda maalum za kiuchumi Mheshimiwa Mpango tuna Ziwa Viktoria katika nchi yetu, zawadi ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, maji ya Ziwa Viktoria yamebaki kunufaisha Sudan na Misri wakati sisi wa Mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Mara na Mwanza tunatakiwa tuwe na miradi mikubwa ya uzalishaji kwa sababu tuna maji na ardhi nzuri. Kwa hiyo, Ziwa Viktoria liwekwe kwenye kanda maalum za kiuchumi ili tuweze kuzalisha kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la elimu ya juu. Kwenye Ilani tulisema tutajenga Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere, Wilaya ya Butiama. Sasa kama mpaka leo Waziri analeta mpango hauoneshi kwamba tutajenga Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere Butiama na ujenzi wa chuo kikuu ni miundombinu mikubwa, chuo hicho kitajengwa lini Mheshimiwa Mpango? Namwomba kwenye rasimu yake aje na mpango wa kujenga Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere pale Butiama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwana CCM ambaye niliapa kabisa nitasema kweli daima. Ninyi Mawaziri wa Serikali yangu ya CCM na ninyi ni abiria kwenye basi analoendesha Rais wetu na ninyi mmekaa siti za mbele,

wakati mwingine abiria ndiyo humchochea dereva kwamba mnataka kufika mapema. Baadhi ya Mawaziri msimdanganye Rais, msimpotoshe Rais…

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Asije akatuletea matatizo kwa sababu Rais anatakiwa ashauriwe vizuri, Rais wetu siyo mchumi. Hivi kweli mtamshaurije Rais kwamba kupotea kwa pesa ni kwa sababu watu wameficha kwenye magodoro, haiwezekani!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. KANGI A.N. LUGOLA:** Pesa zimepotea kwa sababu Benki Kuu wamezichukua kutoka kwenye mabenki maana yake hazionekani. Pesa zimepotea, mshaurini ni kwa sababu madeni ya ndani hayalipwi, mumshauri vizuri. Itakuwaje mnamshauri Rais kununua ndege kwa *cash* wakati…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WABUNGE FULANI:** Mwache aendelee. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:** Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae!

Waheshimiwa Wabunge, nitasoma majina machache ambayo tutaanza nayo mchana. Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Omar Mgumba, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma. Hao ndiyo tutakaoanza nao mchana halafu tutaendelea na ratiba kwa namna hiyo.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja leo jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**
**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Kamati ya Mipango nilisoma majina kadhaa kwamba tungeanza nao mchana huu. Tutaanza na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Naomba nitoe mchango wangu mfupi hasa kuhusiana na suala zima la hali ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia taarifa ya tathmini ya *MDG* kwa nchi yetu kuanzia mwaka 2000 hadi 2015, taarifa inaonyesha kwamba uchumi wetu umekua kwa asilimia saba kwa kipindi cha miaka 15. Lakini taarifa hiyo inaonesha kwamba kama uchumi utakuwa mfululizo kwa asilimia saba kwa miaka 15 maana yake inategemewa suala la umaskini utapungua kwa kiwango cha asilimia 50. Lakini taarifa hiyo inaonyesha kwa Tanzania imepungua kwa asilimia kumi tu, kwamba bado tuna safari ndefu ya kufikia hicho kinachoitwa uchumi wa kati ambayo ni dira ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukisema suala la ukuaji wa uchumi lazima pia tuangalie sekta zingine ambazo zinaweza kuchochea suala zima la ukuaji wa uchumi, bado tuna safari ndefu. Ukiangalia kwenye sekta tu ya kilimo uchumi unakua kwa asilimia mbili tu na tunajua kabisa suala la kilimo ni tegemeo kwa Watanzania wengi, wanategemea ili kuondokana na umaskini.

Lakini sekta hiyo imekua kwa asilimia mbili tu kama ambavyo taarifa hiyo inaonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la ukuaji wa uchumi Serikali mkija hapa na *figures* na kujigamba mkisema kwa ujumla wake inakuwa kwa asilimia saba bila shaka mtakuwa mna wahadaa wananchi lakini kwa uhalisia ukienda kwenye sekta moja moja ambazo zinachochea uchumi huo bado tupo nyuma na tuna hali ngumu. kwa hiyo, ni vizuri sana mnaposema suala hili la uchumi muangalie uhalisia wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema pia suala la uchumi tukiangalia hali ilivyo sasa kuna mdororo mkubwa wa uchumi, hakuna mzunguko wa fedha, hakuna fedha katika hata bajeti tuliyopitisha ukiangalia sasa tunaingia kwenye *quarter* ya pili hata asilimia 26 ya utekelezaji wa bajeti bado hamjafikia na kama mmefikia ni hiyo asilimia 26 tu. Kwenye Serikali za Mitaa hakuna fedha, kwenye taasisi za umma hakuna fedha, Wizarani tumeona taarifa mbalimbali Wizara zikiwasilisha kwenye Kamati hakuna fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya, hakuna fedha, nini kipaumbele? Mna mpango gani wa kufikia hiyo bajeti ambayo tumeipitisha kwa shilingi trilioni 29 katika mwaka huu. Lakini mnafanya *projection* ya bajeti ya shilingi trilioni 33 kwenye bajeti ijayo. Napata mashaka sana kama hii tu ya sasa utekelezaji wake tunaingia kwenye *quarter* ya pili bado hali ni mbaya halafu unafanya *projection* ya shilingi trilioni 33 kwenye bajeti ijayo tafsiri yake ni kwamba mnajifurahisha ninyi kama Serikali kwa namba hizi kubwa kubwa, lakini mnawaongezea wananchi mzigo wa kuendelea kulipa kodi.

Kwa hiyo, unaona kabisa ni bajeti ambayo kwa kweli mwisho wa siku haitaweza kutekelezeka ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeeleza katika mpango huu kumekuwa na changamoto mbalimbali za kuweza kufikia mipango hiyo. Mojawapo mmesema ushiriki mdogo wa sekta binafsi lakini pia kuna suala la upatikanaji wa mitaji ya uwekezaji. Hivi hizi sekta binafsi kama hazijatengenezewa mazingira rafiki, kama hizi sekta binafsi hazijawa na imani na Serikali iliyopo madarakani kwa sababu tumeona wakati mwingine mna ndimi mbili mbili sekta binafsi ataogopa ku-*invest* hela zake kwasababu hajui Serikali kesho inatamka nini? Inafanya nini? Kesho inakuja na kodi gani? Kama msipoweka haya mazingira mazuri hakuna sekta binafsi atakayeweza kuja kuwekeza katika nchi hii kama ambavyo nyie wenyewe mmekiri hapa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado tunahitaji kuwepo na sera na mazingira rafiki ya kuweza kuhakikisha hizi sekta binafsi kwa kweli zinakuwa na wao ni sehemu ya uchumi wa nchi hii. Mmeeleza pia changamoto nyingine ni

upatikanaji wa mitaji ya uwekezaji, hili pia ni changamoto kweli kwa sababu kama sasa hivi mabenki hali ni mbaya, mabenki mengine yameshakua chini ya usimamizi wa *BOT*, mabenki hayana mzunguko wa fedha, fedha ambazo zilikuwa za Serikali kwenye *commercial banks* zote zimehamishiwa *BOT, obviously* hakuna uwekezaji unaweza kufanyika. Kwa hiyo, bado tuna changamoto kubwa sana ambayo kwa kweli itakuwa ni ngumu sana kuweza kufikia hicho kinachoitwa uchumi wa kati ambayo ni dira ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hali ilivyo sasa hivi, lakini wakati mwingine unajiuliza hivi kuna haja gani ya kujadili pia mpango au kujiwekea mpango wakati mpango wenyewe ukienda kwenye utekelezaji hauwezi kufanyiwa tathmini na kuona matokeo. Lakini kuna vitu vingine ambavyo vinaenda kutekelezwa ambayo hayapo kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ambao tunaumalizia 2016/2017 suala la kuhamia Dodoma halikuwepo lakini Rais amelitamka limetekelezeka, halikuwepo kwenye mpango na kuhama Dodoma sio kazi ndogo, inahitaji fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini angalau sasa hivi mmeiweka kwenye mpango unaokuja; sasa unaona wakati mwingine kama tunaendeshwa kwa matamko ya namna hii ambayo hayapo kwenye mipango maana yake unaenda kuharibu bajeti ambayo imepitishwa hapo. Kwa hiyo, pia wakati mwingine ni lazima haya ambayo mnayatamka ni lazima yaendane na bajeti ambayo tumeipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuulize Waziri wa Fedha na anisaidie majibu atakapohitimisha. *TRA* wamesema wanakusanya *1.3 trillion* kila mwezi, hiyo ni *projection*. Mishahara inayolipwa nchi hii ni shilingi bilioni 540, madeni ya ndani ama ya nje inalipwa shilingi bilioni 900, ukifanya hapo mahesabu ni kama *one point four trillion* na makusanyo ni *1.3 trillion* kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza hizo ndege zilizonunuliwa kwa fedha *cash* hii hela mliipata wapi? Wakati mnachokikusanya *TRA* kila mwezi ni *1.3 trillion*, ukilipa madeni, ukilipa mishahara ni *1.4 trillion*; fedha za kununua ndege kwa hela *cash* mmeipata wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri unijibu ama ni hizo fedha zilizopo *BOT* ambazo zimekusanywa na taasisi zikawekwa kule mkaenda mkazichukua mkanunua ndege *cash*? Naomba nipate majibu ya suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala lingine ni kuhusu suala zima la elimu. Wakati nimechangia kwenye bajeti ya elimu hapa mnajivunia leo suala la elimu bure, lakini elimu bure hii ni bure tu kwa sababu hawalipi kile ambacho kinatakiwa. Ukienda kwenye uhalisia wa shule zetu hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi mmesema mwanzoni wakati wa awamu ya JK mliagiza kujengwe maabara nchi nzima; wananchi wakajichanga, mkaita wadau mbalimbali wakachanga maabara ikajengwa, yamebaki majengo yameachwa. Mmeyaacha yale majengo hayana vifaa, maabara hayafanyi kazi ni majengo tu yaliyosimama mkahamia kwenye madawati mmetangaza madawati nchi nzima watu wametengeneza madawati mengine hayana *standard,* hayana *quality* inayotakiwa leo mnataka kukimbilia kujenga madarasa kwa mfumo ule ule wa kulipuka. Kule mmeshasahau maabara, madawati mengine hayana kiwango, leo mnakurupuka mnaenda kujenga…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso muda wako umeisha, nikigonga hiyo maana yake umalizie sentensi sasa naona unaendelea na hoja, malizia sentensi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema muache kukurupuka, mkianzisha jambo moja likamilike, liwe na manufaa, lianze kufanya kazi muende kwenye jambo lingine, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitasoma Wabunge wachache wataofuatana, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, watafuatiwa na Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani, Mheshimiwa David Ernest Silinde atafuata. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia katika hoja ambayo ipo katika Bunge lako Tukufu. Moja kwa moja ningependa kuanza na suala la himaya ya pamoja ya ushuru wa forodha *(single customs territory).* Hii *single customs territory*ilianza mwaka 2013 lakini utekelezaji wake katika nchi za Afrika Mashariki ulianza mwaka 2014, Kenya na Uganda walianza Januari lakini ilivyofika Julai Tanzania na Rwanda nazo zikaanza utekelezaji wake hadi hivi ninavyozungumza wenzetu wa Burundi bado hawajaanza kutekeleza hii dhana nzima ya *single customs territory.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nasema haya? Nayasema haya kwa sababu hili ni eneo mojawapo ambalo sisi kama Tanzania inawezekana ikawa tumepigwa goli kwa sababu hii mizigo ambayo inakwenda Kongo sisi tunapo-*charge* hapa katika Tanzania halafu wengine hawafanyi hivyo ndio hii sasa ambayo wenzetu wanatumia mwanya kupitisha bandari nyingine hizo ili kukwepa hii *single customs territory*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Serikali kwa ujumla kwamba kwa kuwa hii *single customs territory* imeanza kwa nchi za Afrika Mashariki na nchi ya Kongo walivyoona kwamba ina manufaa wakaomba wao wenyewe kwamba bidhaa zinazokwenda katika nchi yao zitozwe kodi katika maeneo yetu. Basi naiomba Serikali sasa iweze kuwaandikia Kongo ikiwezekana pia wawaombe na Mozambique nao waingie katika huu utaratibu ili kwamba bandari zote ziwe *fair*. Lakini kama sisi tutaendelea kutekeleza wakati Mombasa hawatekelezi kwa asilimia 100 na kule Beira hawamo kabisa katika mpango huu na kule *Walvis Bay* kule Namibia pia hawamo katika mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo la Serikali kwa kuwa limeamuliwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki basi warudi kule wakahakikishe kwamba mambo haya yanatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lina faida ambayo faida yenyewe imejificha sana sio rahisi kuonekana kwa jicho la karibu. Faida namba moja ni kwamba kabla ya utaratibu huu haujaanzishwa mizigo mingi ya kwenda Kongo ilikuwa inakuwa *dumped* katika nchi yetu, mizigo ambayo inatakiwa kwenda *transit* haiendi inabaki katika soko la ndani, matokeo yake ni kwamba nchi inakosa uwezo wa kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, pia wakati huo hata wasafirishaji waliokuwa wanapeleka mizigo Kongo unaweza ukakuta lori limefika Kongo, akaa zaidi ya mwezi mwenye mzigo hajalipa mwezi mwenye mzigo hajalipa kodi kwa hiyo anashindwa kushusha, unakuta unatumia muda mrefu nina ushahidi wa wazi kabisa mimi ni-*declare interest* nilikuwa ni mdau katika eneo hili, yapo malori ambayo yanaweza yakafanya *trip* mbili kwa mwaka huko nyuma, lakini baada ya hii *single customs territory* kuanza kila mtu anaondoka hapa na mzigo ambao umelipiwa kodi anashusha kwa wakati na anarudi na tumekuwa tunatengeneza mpaka *trip* nane kwa mwaka. Kwa hiyo, ni jambo zuri lakini lazima lifanyiwe utafiti vizuri tuhakikishe kwamba utekelezaji wake usiwe wa nchi moja bali uwe wa Jumuiya nzima ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo pia nizungumzie suala zima la mpango pamoja na dhana nzima ya kilimo, kwamba ni kweli kwamba huoni *connection* ya moja kwa moja kati ya kilimo na hii dhana nzima ya uanzishwaji wa viwanda. Kwa hiyo, ningependa kuwashauri Serikali kwamba sasa hebu ije na *comprehensive information* ya kuweza kufanya *integration* kati ya kilimo kitaungana vipi kwenda kwenye viwanda. Hivi viwanda ambavyo mjomba wangu Mheshimiwa Mwijage anavinadi lazima tupate tafsiri ni viwanda vya namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ninavyofahamu mimi kwa Tanzania yetu kwa sababu sisi ni wakulima basi viwanda hivi vinatakiwa viwe vingi vya maeneo yanayoendana na mazao ya kilimo ili tutengeneze wigo mpana wa kuwasaidia wananchi wetu. Hatutarajii kuwa na kiwanda pekee kitakacho ajiri watu 500 lakini tunataka tuwe na kiwanda ambacho kitaajiri watu 500 kwenye kiwanda wafanye kazi za kiwanda, lakini hawa *outgrowers* huku nje nao waweze kuwa *supported*, watu wawe *busy* kwenye mashamba na wawe na masoko ya uhakika kupitia hivi viwanda ambavyo tunakusudia kuvianzisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili ni lazima hata tafiti za kilimo zifanyike upya. Sasa hivi wakulima wetu wengi wanafanya kazi hizi za kilimo kwa mazoea, tunazungumzia tatizo kubwa la mabadiliko ya tabia nchi duniani. Hali ya hewa imebadilika, tunaona hata mvua zinachelewa sio kwa wakati kama ilivyokuwa zamani. Kwa hiyo, hii yote inategemea pia na watu wa tafiti nao waende mbali zaidi watafiti kwa hali ya hewa iliyopo sasa ni mazao gani tuyapande yanayoendana na hali ya hewa husika? Kwa hiyo, niishauri Serikali kwamba eneo hilo ni lazima walifanyie mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo mazao ya biashara, mkonge, kule kwetu Mkoa wa Tanga tunalima sana mkonge na takribani mashamba 56 yaliyopo nchini, mashamba 36 yapo Mkoa wa Tanga. Kwa hiyo, naomba eneo hili pia lipewe kipaumbele ili kuweza kukuza uchumi wa Mkoa wa Tanga na nchi kwa ujumla. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Subira Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, halafu Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni ya leo kuchangia mapendekezo ya mpango yaliyowasilishwa na Waziri wa Fedha.

Awali ya yote nampongeza Waziri wa Fedha, sisi kama Kamati ya Bajeti tulishirikiana nae vizuri katika kujadili mapendekezo haya. Na naenda moja kwa moja kwenye mchango wangu katika suala zima la kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi wake wa kutoa elimu bure, nikiwaona mamia ya wanafunzi walioongezeka kwenye shule za msingi, sekondari, waliokuwa wanapoteza fursa kutokana na ada na michango mbalimbali na nikiona utayari wa wazazi kuchangia huduma ambazo pengine Serikali haijachangia kwenye ule mchango wa kila mwezi kwa kweli nafarijika. Ndio maana baadhi ya maeneo

sisi tumejipanga tunafyatua matofali kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya shule, ujenzi wa madarasa mapya na ndio maana baadhi ya maeneo tumejipanga, tumetengeneza wenyewe madawati pamoja na Waheshimiwa Wabunge acha yale ya kupewa na Bunge. Lakini yapo maeneo tumechangia madawati, tumejenga nyumba za kuhifadhi hayo madawati. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye masuala ya kufungamanisha maendeleo ya viwanda na afya. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali pia kwa jitihada mbalimbali za uboreshaji wa afya husasan katika tukio la mkutano wa wafadhili wa Kimataifa juu ya afya ya mama na mtoto. Nampongeza sana Mheshimiwa Ummy pamoja na Wizara yake kwa kufanikishwa kufanikisha kupatikana kwa zaidi ya dola milioni 30 kwa ukarabati wa vituo vya afya mia moja. Ukarabati huo utahusu ujenzi wa *theatre,* maabara ya kuhifadhi damu, wodi ya wazazi, nyumba moja ya mtumishi. Ninaamini itakuwa ni ukombozi mkubwa na Serikali ya Awamu ya Tano itakuwa imeaanza vizuri. Kwa kuwa tuna vituo 489, vituo 113 ndiyo vyenye fursa hizo ukivijumlisha na vituo hivi mia moja vinabaki vituo 376. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali, natarajia mapendekezo ya mpango huu utakapokuja kuwa kamili na tutakapo kaa Kamati ya Mipango mwezi wa pili, nadhani watakuja na mapango utakaoainisha vituo vilivyosalia namna ya ukarabati na uboreshaji, lakini pia ujenzi wa zahanati mpya kwa ajili ya kupunguza vifo vya akina mama, wajawazito na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimewasilishwa taarifa mbalimbali; mpango nimeuchangia kwenye Kamati, taarifa zilizowasilishwa kuna taarifa ya Waziri, lakini kuna taarifa ya Waziri Kivuli. Naomba kwa kuwa taarifa zote ni za Bunge na zinajadiliwa na ninapojadili hapa, kambi nyingine huwa wakiona Wabunge wanachingia wanasema anataka Uwaziri. Najua Wizara ile imejaa, Mawaziri wapo wanatosha lakini nachangia ili kuweka sahihi kumbukumbu na kuuacha upotoshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo ukurasa wa 19, tumeambiwa tulipitisha bajeti hewa na katika ukurasa wa 19, katika maelezo ya Waziri Kivuli anaeleza kwamba, sisi tulipitisha shilingi trilioni 23 kama matumizi. Nataka nimfahamishe kwa kuwa Waziri wetu Kivuli ni mgeni katika Wizara hiyo, alikuwa anahudumu Wizara ya Ardhi, mambo bado hajayajua. Lakini nataka nimfahamishe kuna vitabu *Volume III,* aliruka fedha za maendeleo kwa Mikoa bilioni 4.3. Pia aliruka fedha za maendeleo kwa ajili ya Halmashauri trilioni 1.3 na trilioni nne, hakuna, hakuna! Kwa kuwa hotuba hii ilichapwa kwenye magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako endapo zinawasilishwa hotuba zenye nia ya kupotosha na watu waliondoka wenyewe

ndani ya Bunge. Napenda niwataarifu Watanzania hatukupitisha bajeti hewa na hili nimelisemea kwa sababu Mheshimiwa Waziri Kivuli huyu hawezi kuendana sawa na Dkt. Mpango wala Dkt. Ashatu na watendaji wa Wizara ya Fedha waliopoteza muda mwingi kuandaa makaburasha haya, kila kitu kiko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niweke *record* sawa na kwa kuwa iligusa pia Kamati; anapozunguza masuala ya bajeti wa kuwasilisha pia maoni ni Kamati. Sasa nashangaa mwenzetu, lakini ninaomba pia wakati mwingine upangaji wa Wizara ziangalie na taaluma pia, nilishangaa Mwanasheria kuwa Waziri wa Fedha, nilishangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mapendekezo ya mpango walifanya tathimini ya sekta ya fedha na hapa naomba nijielekeze ni kweli katika taarifa aliyowasilishwa Waziri kunaonyesha mikopo ya kibiashara na shughuli za uchumi kwa *quarter* iliyoanza Julai zimeshuka na sababu zinazopelekea ni kupungua kwa shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ikae na mabenki, ikae na sekta za fedha kwa sababu sekta hii inachangia kwenye ukuaji wa uchumi kwa mwaka ambao miezi sita imechangia zaidi ya asilimia 13 inawezekana kupungua kwa fedha katika mabenki hayo inasababishwa na shughuli mbalimbali au maendeleo ya teknolojia ya simu ambazo watu wengi wanatumia miamala ya fedha au masuala ya *microfinance*. Kwa kuwa inachangia ningeomba sana Serikali isikilizane na sekta hii ya fedha, lakini sekta ya fedha nayo iweke mazingira wezeshi itafute wateja katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, muda umeisha?

**MBUNGE FULANI:** Bado!

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho lilizungumzwa, ukiangalia umbile la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira, muda umekwisha.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Eeh! Ahsante! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani hilo lililobaki unaweza kupeleka mchango kwa maandishi.

Mheshimiwa Elias Kwandikwa; ajiandae Mheshimiwa Omary Mgumba, halafu Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia huu Mpango wa Maendeleo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa sababu ukiuangalia kwa ujumla mpango huu, nimeusoma vizuri na pia niseme kwamba nimechangia kwa maandishi kwa sababu ya muda. Mpango huu ni mzuri kwa sababu mpango huu ni muendelezo wa ule mpango wa miaka mitano. Kwa hiyo ukiusoma vizuri utaona kabisa kwamba uko mwendelezo mzuri, sasa kuna mambo kadhaa ya kufanya, ambayo nilikuwa napenda kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu umezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia umezingatia mpango wa maendeleo endelevu. Kwa hiyo, nilikuwa nataka ni- *appreciate* kwa kuona kwamba kwa kweli ukiangalia hali ya uchumi kwa ujumla kwa taarifa ilitolewa na *BOT* mwezi Agasti, utaona kabisa kwa *performance* ya bajeti ya Julai, maendeleo ni mazuri, kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende tu moja kwa moja kwenye ushauri, nilikuwa napenda nishauri mambo kadhaa, ambayo tumeyaona kama changamono na Waheshimiwa wengi wamechangia hapa. Ipo changamoto ya ukusanyaji kodi kwamba yako maeneo kama mpango unavyosema kwamba unakwenda kutazama sekta binafsi, lakini pia tumezungumza juu ya kuendeleza viwanda, lakini uko uhusiano mkubwa kati ya sekta binafsi na ukuaji wa viwanda na suala la ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Kwa hiyo kuna mambo ya kuyaangalia hapa ili sasa tuweze kusaidia sekta, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia maeneo haya ya kodi, kwa sababu ukweli lazima wafanyabiasha na sekta binafsi walipe kodi. Lakini kuna maeneo ambayo ni ya kuyatazama ili kuweza kufanya ile *tax compliance* iwe ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kuangalia kwa mfano, upenda wa *VAT* kwenye viwanda vyetu ambavyo vipo kwa mfano, viwanda ambavyo vinasindika mafuta, mashudu yale yamewekea *VAT,* utakuja kuona kwamba *VAT register* ni kama *agent* wa *TRA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokuwa na hii *VAT* kwenye uzalishaji wa kwanza utaona inavutia kuongeza bei na kwamba ule ushindani sasa wa bei unakuwa ni mgumu kwa *product* inayofanana na wenzetu nje ya nchi na hata kwa watumiaji wa bidhaa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulitazame hili suala la namna ambayo kodi itahamasisha ili ule ulipaji wa kodi, *compliance* iwe kubwa kwamba mtu alipe bila kushurutishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lipo nilitaka nishauri, kumekuwa na tatizo hili la mzunguko wa fedha. Sasa nilikuwa najaribu kufikiria kwamba tulikuja na sheria ya bajeti ili mwezi ule wa saba kuwe na kiasi cha kutosha cha fedha kuweza kuendesha bajeti zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kunahitajika kutazama hili suala la *cash flow management,* Wizara ilitazame ili tunapokuja kupitisha bajeti mwanzoni mwa mwezi wa saba kuwe na *flow* nzuri ya fedha kulingana na uhitaji katika maeneo mbalimbali, katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, sikuona tatizo sana kwa sababu kama bajeti ipo na fedha inayotolewa iko *within the budget,* hapa hakuna shida, ila lipo suala la kuangalia ile *flow* ya pesa inayokwenda kwa ajili ya matumizi, kwa hiyo, Wizara hapa iangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mzunguko wa fedha, hili linaonyesha kwenye sekta ya fedha, Wizara ilitazame kwa sababu kunapokuwa na mabadiliko ya hizi sheria za kodi zilivyokuja, lakini pia mabadiliko katika taasisi zetu za kifedha, watu wanapata hofu ya kupeleka fedha katika hizi taasisi za fedha. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba zile *deposit* kwenda kwenye mabenki zimepungua kiasi kwamba ule mzunguko umepungua. Kwa hiyo, sasa *BOT* iangalie namna yaku-*regulate* ule mzunguko wa fedha ili tuione inaleta *impact* kwenye mzunguko na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko uhusiano mzuri sana kati ya sekta binafsi na ukuaji wa viwanda, sasa uko umuhimu pia wa kuliangalia suala la kilimo. Kilimo chetu hakijapewa msukumo wa nguvu ili kuhakikisha kwamba sasa tunapata *raw material* za kutosha kuendesha viwanda vyetu. Ukija kuangalia kwenye zao la pamba, uzalishaji wa pamba umeshuka, katika msimu huu ununuzi wa pamba umefanyika kwa wiki mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utakuta sekta binafsi watu wana viwanda vyao vya kuchambua pamba vimesimama mtu ambaye alitakiwa kununua tani 60,000 katika msimu huu amenunua tani 14,000 utaona kabisa kwamba tuna *dead asset,* ziko *asset* za wafanyabiashara hazisaidii mchango katika uzalishaji. Kwa hiyo, Wizara itazame namna gani ya kuweza kusaidia haya maeneo ili tuwe na uwiano mzuri kati ya uzalishaji katika kilimo, uzalishaji katika viwanda vyetu ili tuweze kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Serikali ijaribu kuangalia kusaidia tuje tupate kiwanda ambacho kita-*support* hivi viwanda vidogo ambavyo vipo vinachambua pamba, tupate kiwanda kikubwa kwa ajli ya kutengeneza nguo ili pia sasa tuweze kuzalisha nguo za kutosha ili wananchi wa Tanzania waweze kupata nguo kwa bei ambayo inakuwa ni nafuu na kufanya kwamba hali ya uchumi iweze kuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka pia nimalizie kutoa ushauri kwamba tulipokuwa tumeanzisha mfumo wa usimamizi wa fedha tumekuja na hii *concept* ya *accrual basis,* sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwandikwa ahsante. Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma, Mheshimiwa Katani Katani ajiandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango uliopo mbele yetu. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kutendo cha kudhibiti matumizi hasa kwenye taasisi zake na mashirika ya umma. Kubwa kuliko lote hasa kitendo cha kuhamisha akaunti zote za taasisi hizi kuwa *BOT,* ni kitendo ambacho ni cha kizalendo sana na hili nalisema kwa kinaga ubaga na mifano ipo hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna baadhi ya wenzetu wanasema kwamba hali halisi ya maisha yamekuwa magumu kwa sababu ya kitendo hiki, siyo kweli. Siyo kweli kwa sababu hizi benki zilianzishwa, kazi yake ni kuhudumia wateja, kutoa mikopo kwa wafanyabiashara. Lakini hujuma zilizokuwa zinafanyika nitoe mfano mmoja tu wa taasisi moja kama ya bandari, yenyewe iliweka bilioni 440, kwenye *fixed account* kwenye mabenki mbali mbali kwa *rate* ya *3.5%,* bilioni 440. Halafu yenyewe tena ikaenda kukopa kwenye benki hizo hizo bilioni 100 kwa ajili ya miradi yake ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu hapa, baada ya Serikali kuona hujuma hizo, kupeleka hizo akaunti *BOT* anasema Serikali imenyonga wafanyabiashara, siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taasisi nyingine hizo hizo, hii mifuko yetu ya kijamii, inakusanya shilingi bilioni 38 kwa mwaka, shilingi bilioni 27 matumizi kwa sababu fedha zipo tu za kutumia, inachangia kwenye mfuko shilingi bilioni mbili tu kwa mwaka mzima, leo Serikali imeona hujuma hizo imepeleka hizi fedha zote zikapate udhibiti *BOT* mtu anasema wafanyabiashara wamenyongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kitendo hiki cha kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima na ovyo ambacho sasa tuiombe tu Serikali ifanye mfumo mzuri ambao kama hizi benki zipo ziende sasa zikakope

kule *BOT* kwa *rate* inayokubalika ya sokoni siyo ile ya kiwizi wizi ya 3.5 halafu fedha nyingine zinaenda kwa wajanja wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa sababu huu unasema ni wizi alafu hizo hizo benki zilikuwa zinaikopesha Serikali kwenye *treasure bill,* Serikali ikiwa na tatizo inakwenda kukopa kwenye benki zile zile kwa *rate* kubwa zaidi ya asilimia 15, 20. Kwa hiyo, niwaombe Serikali hapo msilegeze, msimamo ni huo huo ili kwamba tuwe na nidhamu katika matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili kuhusu makusanyo hasa kwenye *TRA*, nilikuwa naomba Waziri Mpango katika mapendekezo ya kuongeza *tax base,* kweli tumepata muhamasisho wa Rais na watu mbalimbali kwamba watu wajitolee kwenda kulipa kodi kwa hiyari, lakini kitendo cha Mtanzania, wengi wanahofia ukisema leo nataka kuanza kulipa kodi, *TRA* sasa hawaanzi pale, watakupa hizo kodi miaka kumi ijayo hata kulipika hazilipiki. Ni sawa sawa sasa wanakwenda kufilisi, matokeo yake watu wanaogopa na watu walipakodi wanaendelea kubaki walewale, ni kitu ambacho hakitaisaidia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu, kama kuna uwezekano toweni muda maalum kwamba watu wajitokeze kulipa kodi ili muongeze wigo wa *tax base,* lakini mkasamehe hayo makando kando ya nyuma ili watu waanze kulipa kuanzia hapo kwenda mbele. Tutaongeza wigo mpana wa kulipa kodi kuliko kung'ang'ania kusema mpitie makando kando hayo watu hawana risiti, hawana uthibitisho zaidi ya kuwafilisi, matokeo yao watafilisika, hamtakusanya tena hizo kodi uko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine sasa hivi kwenye makusanyo hayo ya kodi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili imegonga.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani na Mheshimiwa Kuchauka ajiandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika mwelekeo wa mpango huu wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala hili la mashirika ya umma, Mama Lulida alikuwa kazungumza hapa siku ya jana akieleza kwa masikitiko makubwa sana. Alikuwa amezungumza kwamba baadhi ya mashirika ambayo takribani tuko nayo Tanzania kwa kiasi kikubwa mashirika ya umma yanaendeshwa kihasara. Yapo mashirika mpaka hivi sasa ninavyozungumza, miradi na mali walizokuwa nazo takribani na madeni yote madeni waliyokuwa nayo inazidi mali walizokuwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mfano Shirika la Mbolea Tanzania *(TFC)*, wakati tunapitia mpango wao katika Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, unaweza ukashangaa sana kwamba deni walilokuwa nalo ni takribani shilingi bilioni 66. Lakini madeni, mali waliyokuwa nayo, mali nzima ukiuza majengo na kila kitu wana mali zenye thamani ya shilingi bilioni 23.8. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni jambo la ajabu sana kwamba haya mashirika yamefilisika, Serikali, Waziri wa Fedha na Mipango, sijaona wakati napitia taarifa yake hapa na mwelekeo wa mpango hajaeleza kinaga ubaga kwamba kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba anafufua mashirika haya ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeona hapa na Wabunge wengi wamezungumza kwa kiasi kikubwa sana kwamba Serikali imekuwa ikikopa kwenye mashirika haya, mashirika ya fedha na mashirika ya umma ya ndani ya nchi. Tuhakikishe kwamba tunaweka mikakati kabambe ili haya mashirika yaweze kufufuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uendeshaji wa haya mashirika, yanaendeshwa kinyume na taratibu za kimaadili. Kwa mfano, mwaka jana tuliweza kuzungumza katika mpango hapa kwamba yapo baadhi ya mashirika yanatumia madaraka yao vibaya. Kwa mfano, Shirika la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliweza kuingia mkataba na mwekezaji kotoka Botswana, mkataba ambao haunufaishi Serikali. Lakini jabo la ajabu tuliweza kuzungumza katika mpango tukaongea kwenye bajeti hapa, lakini kwenye mpango aliokuja nao Mheshimiwa Mpango hapa hakuna mwelekeo wowote kwamba kuna nini kitafanyika ili kuhakikisha ya kwamba haya mashirika ambayo yanawekeza kinyume na taratibu na sera za uwekezaji Tanzania na kwamba hayaingizi kipato katika Serikali yetu yanachukuliwa hatua stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ukisoma mkataba wa *Mlimani City* ambao Mbotswana aliingia kwa kiasi kikubwa yule jamaa anakusanya pesa nyingi sana. Lakini jambo la ajabu Serikali inakusanya asilimia 10 tu ya mapato yote na hakuna uhakiki wowote ambao unafanyika wa kuhakikisha kwamba kile anachokusanya kinafanyiwa mahesabu sawasawa ili ile asilimia 10 ama anapata zaidi ya ile asilimia 10 anayotoa Serikali ya Tanzania iweze kunufaika. Ni kwa sababu mipango yetu haioneshi namna gani

tunaweza kuweka mazingira ya kiuwekezaji ambayo hawa wawekezaji kutoka nje wanaweza kuliingizia Taifa hili pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala zima ambalo niliweza kuzungumza katika mpango uliopita, kwamba mashirika haya kwa mfano *PSPF,* wamekuwa wakiwekeza kwenye viwanja kwa kiasi kikubwa sana na wakati wananunua hivi viwanja wananunua *square meter* moja kwa pesa nyingi sana kinyume kabisa na bei halisi na halali katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, niliweza kueleza hapa, na leo naomba nilizungumze tena, Shirika la *PSPF* waliweza kununua kiwanja Mjini Mwanza *square meter* moja walinunua shilingi 250,000, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini ukija kule Mtwara pia, wamenunua *square meter* moja shilingi155,000, maeneo ambayo bei hiyo haijafika, ni kwa sababu mashirika haya yanawekeza kiufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana katika mpango huu tuhakikishe ya kwamba haya mashirika yanapitiwa upya na waweze kuja na mpango kabambe ambao utaweza kuinua uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia suala zima la *PPP* (sekta binafsi). Tumeweza kuzungumza kwa muda mrefu katika Bunge hili kwamba hawa wawekezaji kutoka nje ya nchi ndio ambao wanategemewa sana na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, ambao tunawategemea wajenge viwanda na vile viwanda viweze kutoa ajira. Lakini cha ajabu mazingira mpaka leo tunavyozungumza sio rafiki kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa wakati wa mpango uliopita na nikazungumza wakati wa bajeti pia, kwamba tunao wawekezaji wamejenga viwanda, kwa mfano mwekezaji huyu Aliko Dangote kule kiwanda cha saruji Mtwara, lakini mpaka leo huyu mwekezaji ananyimwa kupewa gesi ambayo anaweza kuitumia kama nishati ili sasa bei ya saruji iweze kushuka na saruji iweze kuzalishwa kwa wingi Tanzania na watu wengi waweze kujenga, ni jambo la ajabu sana. Tunaomba sana hawa wawekezaji wapewe gesi, mwekezaji huyu wa saruji apewe gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna mwekezaji wa mbolea ambayo ni kwa muda mrefu hivi sasa, tuliongea wakati wa mpango, wakati wa bajeti pia tulizungumza, ambaye anaomba apewe gesi aweze kujenga kiwanda cha mbolea Msangamkuu pale Mtwara Vijijini. Mpaka leo yule mwekezaji hajapewa hiyo gesi. Tunaomba Waziri Mpango atakapokuja kuhitimisha atupe maelezo kwamba mpango ukoje wa mwakani wa kuhakikisha kwamba hawa watu, hawa wawekezaji wanapewa hii gesi ili iweze kunufaisha katika sekta hii ya viwanda na kweli iweze kuinua uchumi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nizungumze suala zima la miundombinu ambalo tumezungumza kwa kiasi kikubwa sana, lakini sijaona mkazo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mpango hapa wakati anazungumza. Tulizungumza sana kwamba uchumi wowote hauwezi kuimarika popote duniani kama miundombinu ni hafifu. Tunayo miundombinu ya barabara ambayo imesimama hivi sasa na tuliweza kuzungumza, kwa mfano barabara kadhaa za hapa nchini kama ile barabara ya Ulinzi kule Mtwara ambayo sijaona kwenye mwelekeo wa mpango wapi imewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliweza kuzungumza pia reli ya kutoka Mtwara kuelekea Liganga na Mchuchuma ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza. Kwa hiyo, niombe sana kwamba kama kweli tunahitaji kufufua uchumi tuhakikishe kwamba tunajenga miundombinu imara ili kweli Watanzania waweze kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa sababu ya muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha. Mheshimiwa Katani Katani, ajitayarishe Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pia kwa kunipa fursa hii. Nitaanza na suala la utawala bora ambalo lipo kwenye mapendekezo ya mpango huu tunaozungumza. Wakati tunazungumza suala la utawala bora sisi Watanganyika ambao tumejipa mamlaka ya kuwa Tanganyika sasa kuwa Gereza la *Guantanamo Bay* kwa kuwachukua Wazanzibari na kuwaleta Tanganyika bado watu mkazungumza suala la utawala bora, hatuwezi kuiendesha nchi na tukawa na mipango mizuri kama kuna watu wanadhulumiwa, kuna watu wanaonewa, bado mkaendelea kuzungumza mipango hii. Na kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, hili nalo lazima uliangalie sana kwa sababu linakugusa pia, ulione kwamba ni jambo la msingi tunapozungumza suala la mipango, suala la utawala bora na wa sheria ni lazima lizingatiwe kwa namna yoyote ile, ndiyo tutakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati nasoma ukurasa wa 62, mmezungumzia suala la Benki ya Maendeleo ya Kilimo, niliona miaka ya nyuma Benki ya Maendeleo ya Kilimo ikiwa Dar es Salaam, wakulima wenyewe wanapatikana Tandahimba, sasa ni mambo ya ajabu na vichekesho kwa Taifa hili, mnazungumza benki ambayo iko Dar es Salaam, wakulima wa Rujewa kule Mbarali, wakulima wa korosho wa Tandahimba hakuna wanachonufaika na benki hiyo ambayo inayokaa Dar es Salaam, ni jambo la ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nina ushahidi wakati hata mmeleta trekta, watu wangu wa Tandahimba mpaka leo, wajanja wachache wameshachukua

matrekta, wenyewe wakulima wa Tandahimba hawajachukua. Sasa wakati mnazungumza suala hili la Benki ya Maendeleo ya Kilimo basi mhakikishe na watu wa Tandahimba, watu wa Rujewa kule vijijini wananufaika na jambo hili la Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mnazungumza mambo haya mmezungumza suala la barabara ambalo nimeliona, suala la barabara ile ya Masasi – Mtwara – Newala – Tandahimba, ukaizungumzia ile ya Masasi – Songea – Tunduru, bahati nzuri hii ya Masasi – Songea – Tunduru inakwenda vizuri sana. Lakini hii ya kwetu ya kutoka Mtwara – Tandahimba – Newala, pamoja na kwamba umepitisha bajeti na wananchi wakakubali kubomoa mabanda yao yaliyo barabarani, mpaka leo hakuna kinachoeleweka na tunaandaa sasa mpango wa mwaka unaofuata. Hili ni jambo la ajabu na linaweza likawaangusha Serikali ya CCM, sasa kama mnataka mipango iende, tutekeleze kwanza tuliyokubaliana halafu ndiyo mlete mipango ambayo inaweza ikawasaidia Watanzania hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezungumza suala la viwanda. Suala la viwanda, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikwambie tu kwamba Kusini, kwa maana ya Mtwara na Lindi tulikuwa na viwanda vya korosho vya kutosha, viwanda ambavyo mmeuza kwa bei chee, tena kwa njia za panya, zaidi ya viwanda vinane tulikuwa navyo, sasa kama mna dhamira ya dhati muone namna gani mnakwenda kuvichukua vile viwanda. Na hili linawezekana kwa Serikali yenu, kwa sababu ni Serikali tu ikiamua jambo inafanya, sasa tuone viwanda vile vya korosho kule mnavichukua ili watu wa Mtwara na Lindi waweze kunufaika na viwanda vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza hapa, suala la *single customer territory,* napata shida kwenye jambo hili, kama makusanyo ya ndani yametushinda, tunakuja kujibebesha mzigo wa kukusanya na pesa za watu wa Kongo, Zambia, hii ni akili ya wapi? Una mzigo wa magunia wa kilo 200 umeshindwa kuubeba mwenyewe unasema niongezee kilo 400, hili ni Taifa la ajabu sana. Nikuombe sana, mlikwenda kwenye jambo hili mkiwa mmeshirikiana na watu wa Kenya kwenye suala la *VAT* kwenye suala la utalii, Wakenya wakatukimbia, leo tumeingia mkenge kwenye jambo hili tayari bandari yetu inadorora ambayo inaleta zaidi ya asilimia 60 ya Pato la Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, wewe ni msomi mzuri na mara zote tukiwaambia muwe mnapokea ushauri, sio kila kinachozungumzwa na upinzani ni maneno ambayo tunaiudhi Serikali, sisi tunajua nchi hii ni ya Watanzania wote na tunazungumza kwa maslahi ya Taifa la Tanzania hatuzungumzi kwa maslahi ya Chama cha Mapinduzi, hatuzungumzi kwa maslahi ya Chadema, hatuzungumzi kwa maslahi ya *CUF*. Tunapotoa hoja za msingi za Kitanzania pokeeni hoja na mzifanyie kazi badala

ya kukaa hapa mnatuletea ngonjera, mnazungumza majungu, mnazungumza mipasho, tuzungumze kauli za Kitanzania, tuwakomboe Watanzania wachache ambao wanapata shida huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii jioni hii. Naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu nikiangalia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye huu mpango. Nimesoma vipaumbele vyote vilivyotajwa sijaona kipaumbele cha kilimo na sisi tunajitangaza kwamba tunataka kwenda kwenye Taifa la viwanda. Lakini kwenye miradi hii ambayo imetekelezwa, hakuna mradi hata mmoja wa kilimo uliotajwa hapa. Nikifika na kwenye miradi ambayo inatekelezwa nako vilevile sijapata mradi hata mmoja wa kilimo unaotekelezwa zaidi ya kuona kuna Kijiji cha Kilimo Morogoro. Sasa je, hilo shamba ni la mazao gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, ulaji wetu kama Watanzania sasa hivi umebadilika, sasa hivi tunakula sana kwenye mazao ya chakula (ngano) kuliko mazao ya mahindi au mchele kama tulivyozoea. Lakini kwenye mpango huu sijaona mahali popote ilipotajwa kuendeleza hili zao la ngano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mashamba ya ngano *NAFCO,* yale mashamba sijui yamepotelea wapi. Na hapa nataka ni-*declare interest,* mimi ni msindikaji wa nafaka. Ngano hii kiwanda kimoja cha Bakhresa peke yake anasindika tani 2,700 *per day* na hizi tani 2,700 anazosindika kwa siku zinatoka nje *a hundred percent,* Tanzania tumelala. Leo hii tunakuja tunasema kwamba tunataka kuimarisha viwanda, hapo napo sijapaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nirejee kwenye takwimu, hizi takwimu za Mheshimiwa Mpango bado hazijanishawishi. Kwa sababu kwenye akiba ya fedha, pesa za kigeni, tunasema tunayo akiba ya pesa kuendesha miezi 4.1, hapohapo mwisho kabisa anasema kwamba hii ni zaidi ya lengo la chini kabisa ambalo ni la miezi minne. Huko kuongeza tu kwa pointi moja tayari ni sifa kwetu kuona kwamba tumepiga hatua, lakini je, hizi takwimu zinalingana na takwimu za ongezeko letu Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana unaweza kujisifu kwamba wewe ni mtu wa kwanza darasani kwa kupata asilimia 30, ndiyo hiki ninachokiona hapa, lakini kama kweli tuna nia nzuri ya kuwatendea haki Watanzania, naomba kabla hatujafika kwenye mpango huu turejee kwanza kwenye sensa ya watu waetu ili huu mpango na haya maendeleo tunayojisifu kwamba uchumi wetu unaimarika, unalingana na idadi ya watu tulionao unaowahudumia huu mpango? Ndiyo maana leo hii Serikali inasema uchumi umeimarika, lakini kwa

watu tunaokaa nao wanaona hakuna kitu kinachofanyika, ni kwa sababu ule uchumi unaowahudumia ni wengi kuliko hivyo mnavyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka nijielekeze kwenye kufungamanisha maendeleo ya watu na uchumi, hapa napo mmetuacha mbali sana. Leo hii tunaposema hivi, tumeacha vijana wanahangaika, kilimo ambacho kinaajiri watu wengi bado ni kilimo chetu kilimo cha mkono. Zipo taasisi zinakopesha matrekta kwa ajili ya kilimo, lakini hizi taasisi sharti la kwanza uwe na hatimiliki ya shamba. Leo hii nani mkulima wa kijijini anaweza ku-*access* kupata hatimiliki ya shamba, tunawaacha wapi hawa vijana, na hii tunaposema tunafungamisha maendeleo ya uchumi na watu wetu tumewaacha wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, turejee kwenye sekta binafsi, sekta binafsi sasa hivi ndiyo imechukua ajira kubwa sana, lakini hivi asubuhi hapa nimeuliza swali, ni asilimia ngapi ya Watanzania wana hudumu kwenye hivyo viwanda. Lile swali nimeuliza asubuhi hapa sasa nina *messages* zaidi ya 100 kwenye simu yangu, watu wanasema kweli wanateseka. Nimepigiwa simu kutoka Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, watu wanalalamika, hivi viwanda wanahudumiwa na watu wa nje tu, hakuna Mtanzania anakwenda pale akapata ajira, lakini Watanzania bado tunasema tunahimiza uwekezaji. Lakini je, tunapohimiza uwekezaji tupo tayari kufuatilia hawa wawekezaji kwamba wanakidhi masharti ya nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kwa upande wa umiliki wa ardhi. Kumiliki ardhi hapa kwetu tatizo ni kubwa sana na hakuna mtu ambaye anaweza ku-*access,* mtu wa kijijini akaweza kupata hakimiliki. Upimaji sasa hivi wanasema kwamba eka moja ni shilingi 300,000, kitu kama hicho. Sasa hivi mtu wa kijijini ili aweze kupata shamba la eka 10, 20 atahitaji pesa kiasi gani na atazipata wapi? Kwa hiyo, naona huu mpango, pamoja na kwamba nia ni nzuri, lakini utekelezaji wake na upangaji wake haufanani na hali halisi ya watu wetu wanavyoishi huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa upande wa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tusaidie huo mchango mwingine kwa maandishi. Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa sababu ya muda kuwa mfupi nitachangia kama mambo mawili au matatu kwa ajili ya kuisaidia Serikali kwenye huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ninalokwenda moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba ukipitia hotuba yake, hususan maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/2018 utagundua hapa kuna maeneo mengi kweli kweli, hii miradi ya kielelezo ipo karibu kumi na kitu, ukienda kwenye kila sekta wameweka miradi mingi sana. Ninalisema hili kwa sababu unajua *standard* za *priority* unazifahamu, ukitaka kuweka vipaumbele maana yake unatakiwa uchague viwili, vitatu, *maximum* vitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishakuja na vipaumbele zaidi ya kumi na huu unakuwa ni uwongo, ni jambo ambalo halitekelezeki. Kwa hiyo, jambo ambalo nataka kuishauri Serikali, ili waondoe ugomvi na Wabunge, dunia hii ilivyo hata ufanye nini watu hatuwezi kuridhika lakini namna ambavyo unaandika unataka uridhishe, huku na huko tunapeleka mradi, kwa fedha gani? Kwa hiyo, *at the end of the day,* mwisho wa mwaka ni kwamba tutawalaumu tena mwakani kwa sababu haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi wewe mwenyewe unajua, miradi sisi tangu tunasoma shule ya msingi, mfano makaa ya mawe Mchuchuma na Liganga, yaani ipo tu kila mwaka hai-*mature, every year* hai-*mature,* unaweka miradi ya kielelezo, mwakani tutazungumza yale yale, miradi kama hii wewe unaondoa unapeleka kwenye Wizara husika itekeleze katika ile miradi ya miendelezo ya kila siku. Unaweka mradi unaandika kwa mfano, uanzishaji wa Kituo cha Kibiashara cha Kurasini, wawekezaji hawapo, wale Wachina walishaondoka, sasa ukishaweka kielelezo maana yake *what are you doing?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unakuta ni miradi ambayo tunajua kabisa ikifika mwakani tutamweka kwenye 18 Mheshimiwa Mpango atalalamika tena, jamani mimi mgeni kwenye Wizara mnanionea, mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu kwenu Wizara nendeni mkachague miradi mitatu, minne, unajua hata ukitekeleza hapa kwa asilimia 100, 98, watu tutakupongeza, huo ndiyo utaratibu wa kuongoza nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo nililiona kwa sababu nikaona kabisa kwamba sasa tuache kuwapiga tuwape *solution.* Sasa changamoto ni

kwamba mkiamua kuyapuuza *up to you,* lakini hiki ninachokwambia, leta mitatu, minne, nina uhakika mnaweza kutekeleza kwa kiwango cha pesa ambacho kinakusanywa, hilo linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, utekelezaji wa mpango umekuwa ukikutwa na changamoto nyingi sana, na changamoto kubwa ya utekelezaji wa mpango ni fedha. Asilimia kubwa ya mambo ambayo tumekuwa tukikutana nayo hizi fedha mara nyingi zinahusu wahisani, sasa wahisani ndio hao, leo wanaweza wakasema mwakani tutailetea Serikali dola milioni 900 na ikifika mwakani mmekwaruzana kwa sababu fulani wanasitisha ile misaada, na ukija Bungeni sisi kama Wabunge tunakwenda kuwaambia wananchi kwamba Serikali ilitenga kiasi hiki kwa ajili ya mradi huu, wahisani wamejiondoa, anayebeba lawama baada ya hapo ni Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii miradi ya msingi ambayo tunataka kupeleka kwenye utekelezaji lazima kwanza Serikali iwe na uhakika imepata fedha kwanza, halafu ndiyo inaleta kwamba huu mradi tunakwenda kuutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachoshauri ni kwamba mnaweza mkakopa huko, mkishakopa ndiyo unakuja hapa. Nazungumza kama Waziri wa Viwanda na Biashara, kiwanda hiki kitaanza kujengwa kufikia mwezi wa kumi, hela ipo kwenye akaunti, usizungumze kwamba jambo litafanyika wakati hela haipo huo tunaita ni uongo na ni jambo ambalo halitekelezeki. Huu ni ushauri ambao naipa Serikali leo, ikiyafuata haya mambo mwakani hamtalaumiwa, lakini msipoyafuata haya mambo mtaendelea kulaumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nataka nizungumzie *TRA,* kwenye ukusanyaji wa mapato *TRA* wamekuwa wakilalamikiwa sana. Leo ukisikia kila kona ya nchi *TRA* wanakamata, sibishani na watu wanaokwepa kodi, nataka *TRA* wakusanye kodi, lakini kinachofanyika kule nje, wanaenda kwa mtu, ana biashara yake wakimkuta mtu kwa mfano hajalipa kodi wanamkamata, wanafunga biashara yake, sasa matokeo yake nini? Unapomfungia mtu biashara yake na unamdai kodi, maana yake yeye mwenyewe hapati kipato, Serikali inakosa fedha kwa kumfungia yule mtu biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu wamekopa mabenki wanashindwa kurudisha mikopo, kwa hiyo, hapo *TRA* kumfungia mfanya biashara ni kukomoa Watanzania, ni mambo ya kawaida ni madogo madogo sana yanaweza kutekelezeka humu ndani. Serikali inachotakiwa kifanye wale wote wanaodaiwa kodi watengeneze utaratibu waweke kama malipo benki, benki ukishindwa kulipa fedha zako zikiwa nyingi wanakuambia tunakupunguzia ama tunakuongezea muda wa kulipa, utakuwa unalipa kiasi hiki *in installment*. Sasa *TRA* wanataka wao ….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E.SILINDE:** Haya ahsante.

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi.

**MHE. DAVID E.SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo nilikuwa nashauri kwa sababu mmepigwa sana na ukiona watu wanasema sana ujue kuna tatizo sio kwamba watu wanawaonea.

Kwa hiyo, ushauri wangu naomba hayo mambo matatu myafanyie kazi mwakani hatutawalaumu, mkiendelea kutaka kufanya yote kuridhisha kila mtu hamtafanikiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Silinde. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuataiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Edward Mwalongo ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia.

Kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo imeendelea kushughulikia tatizo la tetemeko katika Mkoa wa Kagera, tunaipongeza sana Serikali yetu kwa jitihada zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo imeshughulikia suala la ukame ambalo limeupata Mkoa wetu, tayari Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali sikivu imeshaleta chakula kuonyesha jinsi gani inavyowajali wana Kagera na wana Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali lakini ombi langu niendelee kuiomba Serikali sisi Mkoa wa Kagera hatujawahi kupata njaa kiasi hiki, Serikali iendelee kuliangalia na ione ni namna gani ya kusaidia. Chakula kilicholetwa Kyerwa kilisaidia asilimia ifike hata asilimia kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali bado tunahitaji chakula cha gharama nafuu. Lakini kuhusiana na suala la tetemeko niombe Serikali kuna wananchi ambao wanauwezo wa kuweza kujenga nyumba zao, lakini wananchi wengi hawana uwezo na ukilinganisha hali halisi ambayo tumeipata ya ukame.

Mimi niiombe Serikali bado tunahitaji wananchi wasaidiwe wale ambao hawana uwezo Serikali ione namna gani ambavyo inaweza kuwasaidia hasa hasa wale ambao hawajiwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mpango niipongeze Serikali, mpango huu ni mzuri, una mambo ambayo ni mazuri. Lakini kuna mambo ambayo nataka nishauri, tunaposema tunataka kuingia Tanzania iwe ni ya viwanda kuna mambo ambayo tunabidi tuyaangalie; kwa mfano, suala la wakulima, sijaona kama limepewa nafasi kubwa nchi hii asilimia kubwa tunategemea kilimo, lakini hiki kilimo bado hatujawa na kilimo ambacho ni cha kisasa. Asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo cha kutumia jembe ya mkono, lakini mazingira yenyewe haya ya kilimo wananchi bado sio mazuri, mwananchi anapolima bado hana soko la uhakika. Niiombe Serikali katika mpango wake iweke mazingira ambayo ni mazuri, mwananchi anapolima apate mahala pakuuza mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sasa hivi nchi yetu wametangaza maeneo mengi tutakumbwa na ukame. Tanzania tuna vyanzo vingi vya maji hata ukija kwetu kule Kagera, niombe Serikali iwekeze nguvu kubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji, tutapata chakula kingi lakini tutaweza kupata chakula hata cha kuuza. Ninaamini tukiwekeza kwenye kilimo tutapata pesa nyingi ambayo itainua uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye upande wa ardhi niombe Serikali kama ambavyo imekuwa ikiendelea kushughulikia matatizo ya migogoro ya ardhi, Serikali ili iweze kufanikiwa katika mpango wake lazima tupambane na hizi kero ambazo ziko kwa wananchi wetu, tuainishe yale maeneo ambayo tayari yalishatengwa na Serikali kwa ajili ya wakulima yajulikane na yale ambayo yalishatengwa kwa ajili ya wafugaji yajulikane. Kwa mfano kama kule kwetu Kyerwa kuna mgogoro mkubwa wa ardhi, kuna ardhi ambayo ilishatengwa kwa ajili ya wafugaji. Ardhi hii imeporwa na wezi, wameingia humo tayari Serikali ilishatangaza kuwa hili eneo ni la wafugaji, lakini wameingia watu wamejiwekea fensi humo, wananchi hawana maeneo ya kufugia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini haya maeneo yatakapotengwa wafugaji wakapata maeneo ya kufugia tutapata maziwa, tutaweza kuanzisha viwanda. Niiombe sana Serikali tunaposema tunaingia kwenye Serikali ya viwanda tuhakikishe hii migogoro inaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ili tuweze kufanikiwa lazima wananchi wetu wawe na afya nzuri. Kwa upande wa afya bado tuseme ukweli tatizo bado lipo, wananchi hawana dawa, lakini wananchi hao hao ambao hakuna dawa za kutosha kwenye zahanati, hatuna maji ya uhakika. Hawa

wananchi hawana maji safi na salama, hawana dawa za kutosha hospitalini wanapoumwa watapelekwa wapi? Niiombe Serikali tuwekeze nguvu kubwa kwenye zahanati zetu, kwenye maji ili maisha ya wananchi yaweze kuwa mazuri. Tunaposema tunaingia kwenye... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate muda wako umekwisha.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** ...vizuri wananchi wetu wakawa na afya bora, tuboreshe…

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Rashid Chuachua ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia mapendekezo ya Mpango na Mwongozo wa Bajeti.

Kwanza nianze kumpongeza Waziri na timu yake kwa mapendekezo mazuri sana ambayo yanaelekeza ni namna gani kwa mwaka unaokuja tutatekeleza maendeleo ya nchi yetu. Pia nampongeza kwa jinsi alivyojaribu kuangalia *review* kwa kipindi kilichopita na kutulinganisha na sisi na nchi zetu ambazo zinatuzunguka tuna-*perform* namna gani? Nafikiri huo ni muendelezo mzuri kwa sababu katika nchi yoyote katika dunia ya leo ya ushindani, nchi kama ya kwetu lazima tuangalie ni namna gani tunashindana na majirani zetu, ni namna gani tunashindana vilevile na mashirika mengine ambayo yanatuzunguka. Kwa hiyo, hilo nakupongeza sana Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nina mapendekezo machache la mapato, unapoongelea matumizi ni lazima kuwe na mapato ya uhakika. Nchi yetu imejaaliwa neema kubwa mno, naona mapendekezo kwa kiasi kikubwa yanajilenga mno kwenye mapato ya ndani *(tax revenue)*. Nilikuwa naomba sana Waziri jaribu kuangalia ni namna gani tukuze mapato ya *non revenue* hasa kutokana na *investment* tulizoziweka kwenye mashirika yetu. Hali ilivyo sasa haya mashirika yanahitaji msukumo ili yaweze kuzalisha mapato ya kutosha na yaongeze Pato la Taifa ili tuwe na hela nyingi, tuwe na vyanzo vingi ambavyo vina uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ambalo linatakiwa lisimamiwe ni lile la kuangalia kwamba mashirika yetu yanatekeleza yale majukumu yake ya msingi na yasifanye vitu ambavyo haviko katika msingi wa shughuli ambazo tulikuwa tunazitegemea. Kwa mifano, mashirika yetu ya *pension funds* mengi yalienda kujiingiza kwenye kuwekeza kwenye majengo. Shirika letu la *National*

*Health (NHIF)* nalo kwa kiasi kikubwa badala ya kuangalia kuboresha afya nalo likajiingiza kwenye *real estate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapoangalia ni namna gani tunaweza ku-*finance* zahanati, vituo vya afya nafikiri tungeitumia *NHIF* tusingepata shida sana hapa, tungetimiza lengo letu la kujenga zahanati kwa kila kijiji, vituo vya afya kwa kutumia hela ya *NHIF*. Kwa sababu Halmashauri zinauwezo wa kulipa hilo deni kutokana na mapato ya hizo zahanati na vituo vya afya. Kwa hiyo, naomba jaribu kuliangalia hilo tutoke kule tulikozoea tuende kwenye njia mpya ambazo zinaweza ku-*finance* bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wenzangu wameliongelea sana suala la kilimo. Viwanda na kilimo vinaenda pamoja, unapoongelea viwanda tuongelee ni namna gani tutaboresha kilimo chetu. Kwa mfano, kwa Jimbo langu la Mbeya Vijijini mkituwezesha kulima pareto na kahawa ili tuweze kushindana na Kenya, Rwanda, Ethiopia tuna uwezo wa kuleta pato kubwa sana kwa nchi hii tena la *forex*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Njeza. Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Rashid Chuachua ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii iliyopo hapa mbele yetu. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wataalam wote walioshiriki katika kuandaa mpango huu ili na sisi tupate fursa ya kuuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwanza kabisa kwenye viwanda, tunapozungumzia viwanda ni lazima tuwe na viwanda mama na wengi sana wamezungumzia habari ya Mchuchuma na Liganga. Hadithi ya Mchuchuma na Liganga sasa inafikia mahala itabidi hata watoto wetu tuwabatize majina hayo, kwa sababu hadithi hii ni ya miaka mingi sana. Mchuchuma na Liganga lakini ukweli wa mambo ni kwamba wengi tunaongelea Mchuchuma na Liganga tunafikiri Mchuchuma na Liganga viko mahala pamoja. Kutoka Liganga mpaka Mchuchuma kuna umbali wa takribani kilometa 80 au zaidi na Mchuchuma ni mahala ambapo makaa ya mawe yanapatikana. Na Liganga ni mahali ambapo chuma kipo sasa ukiangalia utaona kwamba tumeiweka hii miradi pamoja tukiamini kwamba ni mradi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuona kwamba Serikali sasa ione itenganishe miradi hii, makaa ya mawe yaliyoko mchuchuma yaanze kutoka,

kwa sababu utoaji wa makaa ya mawe hauitaji mitambo ya ajabu, hauhitaji vitu vikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji katika Mkoa wa Njombe tunahitaji barabara ile itengenezwe, tumeambiwa habari ya barabara miaka ilani ya uchaguzi iliyopita ilisema barabara ya Itoni - Manda, ilani hii kuna Itoni - Manda. Kumetengwa kilometa 50 barabara ina zaidi ya kilometa 150, lakini zimewekwa kilometa 50, hasa unaweza ukaona kwamba ni kiasi gani tuko *serious*. *(Makofi)*

Sasa tunahitaji nani muwekezaji aje awekeze kuchimba chuma kwa sababu pale tumekuwa tukisimulia mpaka hadithi za ajabu ajabu, kwamba chumba kile kikianza kuchimbwa malori 600 yatapita kila siku kwenye Mji wa Njombe kusafirisha chuma. Hasa barabara ya vumbi malori 600 hiyo itakuwa ni barabara kweli, hebu tuone *are we serious* kweli kuhakikisha kwamba kile chuma kinataka kutoka, *are we serious* kwamba tunataka yale makaa yatoke? Kwa hiyo, niombe sasa Serikali ione itenganishe miradi hii makaa yaanze kutoka kwa sababu makaa hayaitaji utaalamu sana. Lakini vilevile barabara hii ya Itoni - Manda itengenezwe ili kusudi sasa iweze kufanya kazi ya kupeleka maendeleo upande ule na mali zile ziweze kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ningependa kuliongelea leo ni suala la elimu, nimekuwa nikipitia katika kitabu cha mpango hiki ukurasa wa 53, unaeleza mpango kabambe wa elimu msingi. Ndugu zangu elimu msingi ni kitu kigumu sana kama nchi hii hatujawahi kupata maanguko makubwa tunakwenda kupata maanguko sasa kwenye elimu msingi, kwa sababu elimu msingi inaonyesha kwamba watoto walioko darasa la pili sasa wataishia darasa la sita. Ina maana kwamba mwaka 2011 watoto hawa watakuwa *form one,* lakini wakati huo huo wale walioko darasa la tatu na wao watakuwa *form one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ina maana shule za sekondari tulizonazo zitakuwa na mikondo miwili, na mkondo mkubwa ni huo wa watoto ambao wataishia darasa la sita kwa sababu hawa darasa zima litakuwa linaenda sekondari. Sasa tujiulize leo hii tuna suasua na shule zetu za kata hazijakamilika, kwanza watoto hawa watakuwa na umri mdogo sana kumtoa darasa la sita kumpeleka *form one*, je, atamudu masomo ya sekondari na atamudu umbali? Watoto wengine tumewapangishia mtaani, watoto wengine wanatembea umbali mrefu sana kwenda shule. Tuone sasa kama Serikali tunajipangaje kuhakikisha kwamba hii elimu msingi inatekelezwa, vinginevyo tutaenda kutesa watoto, tutaenda kuharibu elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo elimu kwa uma haipo, nani anajua leo hii kama mtoto aliepo darasa la pili ataishia darasa la sita na ataanza *form one*. Niwaombe sana Serikali hebu jaribuni kuona sasa pamoja na kueleza kwamba kuna mpango kabambe toeni elimu kwa umma ili kusudi

umma ujue kwamba watoto walioko darasa la pili hawa wataishia darasa la sita na wataanza *form one*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie suala la sekta binafsi, sekta binafsi ni tamu sana kuitamka katika midomo ya Serikali na wadau mbalimbali. Lakini ukija ukweli wake unakuja kuona kwamba kuna ugumu mkubwa sana wa sekta binafsi inakabiliwa nao. Kwanza kabisa sekta binafsi imekuwa kama yatima, haipati msaada wa aina yoyote zaidi ya maneneo lakini wamezungumzia kwamba bajeti ya kodi. Suala la kodi naomba liangaliwe sana sasa hivi karibu kila mtu anadaiwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante**.** *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Chuachua atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex ajiandae.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kusema kwa kifupi ili nitoe mchango wangu kwenye mapendekezo ya mpango. Kwanza kabisa tuipongeze Serikali kwa sababu kilicholetwa hapa ni mapendekezo na kama tukitoa mapendekezo mazuri yatafanya mpango wetu uwe bora zaidi kwa ajili ya bajeti ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza katika maeneo mawili; kwanza nitazungumzia suala la kilimo, katika kuzungumzia suala la kilimo nitajikita kwenye miradi ya kimkakati. Katika ukurasa wa 43 tumeelezwa kwamba mradi namba saba utakuwa ni kuimarisha kilimo cha mazao ya chakula na malighafi nakadhalika. Mimi ninaomba niishauri Serikali eneo hili lisomeke kuimarisha ushirika na kilimo, tusiache ushirika, nikiangalia mpango huu sioni namna unavyozungumzia kwa kina suala la ushirika. Katika kipindi kifupi na uzoefu tulioupata wa kuwatetea wananchi katika majimbo yetu tunaona kwa kiwango kikubwa kabisa wakulima wanategemea ushirika, lakini ushirika lazima uimarishwe na usimamiwe vizuri ili kusudi wakulima wetu waweze kupata tija ya mazao wanayolima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kusimamia vema suala la kilimo, mauzo na manunuzi ya zao la korosho kwa msimu wa mwaka huu, hili ni jambo kubwa kwa sababu bei ya korosho imepanda lakini bado kuna changamoto za hapa na pale ambazo kimsingi tunapenda Serikali iziangalie

kwa kina. Nitazisema kwa kifupi, jambo la kwanza katika msimu wa korosho uliopita wananchi wa Mikoa ya Kusini wamepata shida kubwa baada ya vyama vya msingi kukata fedha kwa wakulima wetu. Fedha hizi ni nyingi na tunaomba Serikali ichukue hatua ya haraka ili wakulima walipwe fedha zao ambazo zilikuwa zimekatwa katika msimu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti iliyoandaliwa na TAKUKURU inaonyesha kwamba takribani shilingi bilioni 30 hazijulikani zilipokwenda, lakini bodi ya korosho imeeleza takribani shilingi bilioni 11 hazijulikani zilipokwenda katika Mikoa ya Kusini. Cha kushangaza bado wale wale waliohusika na wizi wa namna hii wanaendelea tena kusimamia mfumo wa mwaka huu. Wakulima wanaendelea kuuza korosho zao, lakini jicho lao lipo kwa Serikali ni namna gani watu hawa watachukuliwa hatua ili fedha zao zirudishwe na hatua zichukuliwe kwa ajili ya ubadhilifu mkubwa uliofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine la msingi ambalo linapaswa kuangaliwa katika ushirika, katika msimu wa mwaka huu mazao mchanganyiko yameuzwa kwa bei holela mno. Tunaiomba sasa Serikali ije na mpango madhubuti wa kuona namna gani mazao mchanganyiko kama vile mbaazi, ufuta, choroko zitauzwa kwa bei inayofaa na kwa utaratibu unaoeleweka ili wakulima wetu waweze kupata manufaa makubwa, tunaiomba Serikali ilisimamie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi ninapochangia katika eneo la elimu nimekuwa nikisema jambo ambalo na leo nitalisema, nina imani Serikali yangu sikivu italisikia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoiangalia elimu tunapaswa kuiangalia elimu kwa jicho pana sana tusiiangalie elimu kwa mtazamo wa elimu rasmi peke yake. Nimekuwa nikilisema hili mara nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utaratibu wenyewe wote wa kuendesha elimu rasmi uliowekwa katika mpango wetu unaonesha wazi kabisa kuna kundi kubwa la watu tunaowaacha, ambao kwa msingi huo hawatapata elimu kwa muda mrefu sana na baadaye tutakuwa na kundi kubwa la watu ambao hawajaelimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia sensa ya watu ya mwaka 2012 tunaona kwamba takribani watu wazima milioni 5.5 hawawezi kusoma na kuandika. Lakini pamoja na hilo tukiangalia tena idadi ya watu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chuachua muda wako umekwisha.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Richard Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Alex na tutamalizia na Mheshimiwa Abdallah Ulega. Mheshimiwa Ikupa Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018.

Awali ya yote napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya ulinzi na mambo mengi ambayo anatujali sisi Waheshimiwa hapa ndani, na hasa mpaka tukafika kipindi hiki kuweza kuchangia mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niipongeze sana Serikali kwa sababu mimi ni Mbunge ambaye nipo katika kundi la vijana, katika mpango huu Serikali imeonesha ni jinsi gani ambavyo vijana wanaweza wakapunguziwa ugumu ama ukali wa maisha. Ukiangalia katika ukurasa wa 55 limeongelewa suala zima la ajira pamoja na mambo ya biashara, lakini pia yameongelewa na mambo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sababu mimi ni mlemavu ninaomba niongelee masuala ambayo yanahusiana na watu wenye ulemavu katika mpango huu. Mpango huu ni mzuri na jukumu letu sisi Wabunge ni kuangalia ni mambo gani ambayo yanakosekana ili tuweze kuyaboresha ama tuweze kuyaongezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu mtu mwenye ulemavu ninamuona sehemu moja katika ukurasa wa 55, naomba ni nukuu, kuna hiki kipengele kimeandikwa kazi, vijana, ajira na wenye ulemavu. Kifungu (d) kinasema kwamba; "Kutenga maeneo maalum ya biashara ili kuwezesha vijana na wenye ulemavu kujiajiri." Ni hapa tu ambapo ninamwona mtu mwenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishauri ama niiombe serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwamba masuala ya ulemavu ni mtambuka, kwa hiyo ninapendekeza yafuatayo, nitaenda *page wise* nikianzia na huu ukurasa wa 55 hapa ambapo inaelezea kwamba; "kuendelea kutekeleza programu ya kukuza ajira kwa vijana."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba isomeke kwamba; kuendelea kutekeleza programu ya kukuza ajira kwa vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la kuimarisha Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Sheria Namba 9 ya mwaka 2010 inaelezea jinsi ya kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu. Mfuko huu ulianzishwa kisheria. Ukiangalia katika hii sheria kifungu namba 57 (1) kinaelezea unazishwaji wake na kifungu kidogo cha (2) kinaelezea vyanzo vya mapato. Katika hivi vyanzo vya mapato fedha inayoidhinishwa na bunge hili ni fedha ambayo ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha mapato, kwa hiyo mimi niiombe Serikali kuutengea mfuko huu fedha

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tatu kinaelezea kazi za mfuko huu. Mfuko huu unakazi nyingi, na iwapo Serikali itautengea fedha kama ambavyo imefanya kwa Mfuko wa Vijana, mfuko huu utasaidia mambo mengi sana ya watu wenye ulemavu zikiwemo tafiti mbalimbali, mambo ya elimu lakini pia uwezeshwaji wa vyama vya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa hivi ni zaidi ya miaka mitatu ama miaka minne hivi vyama vya walemavu havipatiwi hata ruzuku, hivyo uwepo wa mfuko huu utasaidia mambo mengi sana kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakimbia kwaajili ya muda ninaomba niende ukurasa wa 56, niongelee suala la kilimo. Hapa naomba ninukuu, inasema; "kuongeza ushirika wa vijana katika kilimo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba iseme kwamba; kuongeza ushiriki wa vijana na watu wenyeulemavu katika kilimo. Kwa nini ninasema hivi? Ninasema hivi kwa sababu katika maeneo mengi ambayo nimefanya ziara ama nimetembelea watu wenye ulemavu nikakuta ni wakulima, wanalima, kwa hiyo ni vizuri wakajumuishwa katika hili kundi. Watu wenye ulemavu wanalima si kwa kutumia matrekta,  wanalima kwa nguvu zao. utakuta ni mtu mwenye ulemavu amekaa chini kabisa lakini analima pale pale chini alipo kaa, mimi nimeshuhudia kwa macho yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo niombe watu wenye ulemavu wajumuishwe katika hiki kipengele ili waweze kupewa elimu ya kilimo pamoja na biashara ili kuweza kuwaondolea ugumu wa maisha, lakini pia kuendelea kupunguza wimbi la omba omba la wenye ulemavu na tegemezi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niongelee suala la afya. Kwenye suala zima la afya mtu mwenye ulemavu pia anaingia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba umalizie hiyo ya afya Mheshimiwa, kwa kifupi tafadhali.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la afya pia ni muhimu sana kwa hili kundi la watu wenye ulemavu kwa sababu hata wakati naendelea na hizi ziara zangu afya ni moja ya vitu ambavyo watu wenye ulemavu waliviongelea na waliiomba sana Serikali iwasaidie kwenye suala la afya. Na pia niliulizwa maswali mengi ikiwemo bima ya afya, kuna watu wenye ulemavu ambao hawajiwezi kabisa.

Kwa hiyo, niiombe Serikali katika mpango huu iingize ama itenge fungu maalumu ambalo litawawezesha watu wenye ulemavu kupatiwa bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ikupa Alex, tutamalizia na Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yoyote na mimi nianze kwa kuipongeza Serikali na kuunga mkono hoja hii. Lakini kutokana na ufinyu wa muda naomba nizungumze mambo makubwa matatu halafu nitajielekeza katika ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yenyewe ni kama ifuatavyo, na ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji wayachukue mambo haya

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kariakoo ni sehemu yetu ya biashara tunayoweza kuiita ni sehemu ya biashara ya kimataifa. Hivi sasa Kariakoo inahudumia zaidi ya nchi tano za Kiafika ikiwa na sisi wenyewe wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tulikuwa na tatizo bandarini, lakini hapa karibuni kwa takribani wiki mbili, tatu, mwezi tatizo la upatikanaji wa mizigo kwa ajili ya soko letu hili la Kariakoo, kwa maana eneo la Kariakoo limejitokeza kutokana na agizo lile la kwako Mheshimiwa Waziri la *TBS*. Nomba nikueleze kuwa jambo hili siyo baya, lakini nataka hili jambo la *TBS* uweze kuliweka vizuri na elimu kwa wafanyabiashara wale iende sawasawa.

Mheshimiwa Waziri, wafanyabiashara wa Kariakoo wengine ni wafanyabiashara wadogo wadogo ambao ni wanakusanya mitaji yao wanaunganisha katika kontena moja. Mmoja tu anapokosa kukutana na *SGS,* wakala wetu shida kubwa inatokea pale bandarini. Nataka nikuambia *storage* ya wafanyabiashara wale wa Kariakoo hivi sasa imekuwa kubwa sana na mitaji yao inakatika.

Nakuomba sana jambo hili uliingilie uone ni namna gani ya kuweza kuwasaidia ili waweze kuendesha maisha yao na hatimaye biashara iendelee kuweza ku-*propel* katika eneo hili la biashara la Kariakoo.

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba nizungumzie *BRT,* nimeiona katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka huu wa 2017/2018. Naomba nisisitize ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Mkuranga, alisema kwamba *BRT* itakwenda mpaka Mkuranga, itavuka pale maeneo ya Mbagala. Naomba iende kwa sababu tunalo eneo zuri la Serikali, linaweza kutusaidia kwa kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana yuko msemaji mmoja hapa alisema hakuna viwanda vipya. Nikuombe Mheshimiwa Waziri uwachukue baadhi ya Wabunge walete kule Mkuranga wakione kiwanda cha *Good Will Ceramics* kipya ambacho zaidi ya shilingi bilioni 200 zimewekwa pale na tunategemea zaidi ya wafanyakazi 4,500; watu wa Mtwara, Lindi wanajua kiwanda kile cha kilometa moja kinachojengwa pale Mkuranga, naomba jitihada hizo zifanyike zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba pia ulitangaze eneo la Mkiu kuwa ni eneo rasmi la viwanda. Tunazo ekari nyingi pale hazihitaji *compensation,* walete. Na naomba uwabadilishe *mindset* Waheshimiwa Wabunge hawa, mambo ya kuwaza kiwanda kikubwa sana kama kile cha Mkiu Mkuranga waachane nayo. Viwanda vidogo vidogo vya dola 5,000, 10,000, ardhi tunayo pale, waje wawekeze katika kubangua korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na maneno yafuatayo ya ahadi ya Mheshimiwa Rais. Wakati Mheshimiwa Rais anachukua nchi hii mwezi Novemba, 2015 aliahidi kupambana na rushwa, aliahidi kufanya kazi kubwa ya kuzuia matumizi yasiyokuwa mazuri ya pesa za umma pamoja na kushughulika na watu wasiokwepa kodi. Mheshimiwa Rais alipokuja Mkuranga alieleza wazi hana tatizo na wafanyabiashara akitumia uwanja ule wa Bakhresa. Watu leo humu ndani wanazungumza kwamba Serikali hii haina urafiki na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Rais aliwaeleza wazi mfanyabiashara anayelipa kodi huyo atakuwa ni rafiki yake, lakini mfanyabiashara asiyelipa kodi hana urafiki naye. Nataka niwaambieni *IMF* wametoa ripoti Jumatatu, timu ile inaongozwa na mtaalam mmoja anayeitwa Mauricio Villafuerte. Huyu bwana ameeleza wazi, ameeleza namna nzuri ambayo tunakwenda nayo, lakini wametushauri pia juu ya kujaribu kurahisisha kidogo juu ya mzunguko wetu wa fedha na mengineyo, lakini wametupongeza na wamefikia hatua nzuri ya kuwaambia Watanzania kwamba hata madeni ya nje na mengineyo sasa tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka nimalizie na maneno ya Mwenyezi Mungu katika kitabu kitakatifu cha Qurani. Mwenyezi Mungu subhana wa ta'ala anasema katika Qurani tukufu kama ifuatavyo; "Na wale wanaojitahidi kwa ajili yetu tutawaongoza njia zetu. Nasema fanyeni kazi basi ataona Mwenyezi Mungu vitendo vyenu na Mtume wake na waumini wataviona vitendo vyenu. Enyi wanangu wala msikate tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu, hawakati tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu waliokosa imani."

Mheshimiwa Mwenyekiti wale watu waliokosa imani wote wamepotea. Leo mkubwa mmoja amekuja humu ndani anahangaika, anaweweseka, nazungumzia shilingi milioni 10, kama anazitaka zile shilingi milioni 10 aje timu kubwa huku CCM asikate tamaa wamebanwa. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *time!*

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wamebanwa hawa hawana pa kupumulia.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *time!*

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukura sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Oyaa! Oyaa!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kumbe mlipewa *ten*?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Ulega, tutaanza kuwasikia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri sasa wakichangia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kukiri mmehongwa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Halima njoo tukupe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhanga Mpina.

**MHE: HALIMA J. MDEE:** Kumbe mna bei rahisi sana.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Njoo uchukue ishirini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tusikilizane.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuja na mpango huu mzuri wa maendeleo, yapo maeneo ambayo Serikali imefanya vizuri sana:-

(1) Elimu bure licha ya changamoto inayojitokeza. Elimu ya juu hususani mikopo naiomba Serikali itatue changamoto hiyo.

(2) Afya ya mama na mtoto mpango huu umewekwa vizuri sana.

(3) Tulipitisha bajeti ya sh. 50,000,000 kila Kijiji naomba isomeke kila Kijiji na kila Mtaa.

(4) Ongezeko la bajeti ya maendeleo toka trilioni 11.5 mpaka trilioni 13.1 hali hii itatusaidia kuharakisha maendeleo.

(5) Mkakati wa ukusanyaji mapato ikiwa ni pamoja na udhibiti wa upotevu wa mapato.

Naiomba Serikali ipunguze utitiri wa tozo na kero kwa wananchi itawapa unafuu wa kufanya biashara na kuinua pato la Taifa. Serikali iboreshe huduma za maji, afya, umeme, barabara pia na reli.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri Serikali kwenye Mpango wa mwaka 2017/2018 kama ifuatavyo:-

(i) Kilimo; kuongeza nguvu kubwa ya kuwasaidia wakulima kwa kuongeza pembejeo za kilimo na mbegu yenye ruzuku, kwa mikoa inayozalisha mazao mengi ya chakula na biashara.

(ii) Mifugo; ni muhimu kupunguza ama kuondoa kabisa migogoro ya wafugaji na wakulima, kwa kuwatengea maeneo maalum kwa ajili ya malisho ya mifugo yao.

(iii) Elimu; ni muhimu kwa Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuanza *mean test* mapema kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu wanaoomba mikopo, ili kupunguza matatizo yanayotokana na kukopeshwa kwa wahitaji hao. Elimu ya shule zetu iwe ni kwa vitendo zaidi kuliko nadharia.

(iv) Afya; ni muhimu kupanga bajeti ya afya ambayo itakuwa inalenga kujitegemea kama nchi kuliko kutegemea wafadhili. Mfano, magonjwa kama ya UKIMWI, dawa zake zinategemea zaidi *Global*

*fund* na *President's Emergency Plan for Aids and relief from America* (*PEPFAR*) ambapo Serikali bajeti yake ni kidogo sana na hivyo inaweza kupelekea maafa makubwa kama wafadhili hawa watajitoa na ukizingatia kuwa sera za nchi zao zinabadilika.

(v) *Telemedicine;* ni muhimu Wizara ya Afya kufanya matibabu kwa njia za mtandao yaani *telemedicine*.

(vi) Barabara (Miundombinu); kuna umuhimu mkubwa wa kujenga barabara ya kutoka Katumba-Lwangwa –Mbambo-Tukuyu iliyopo Mkoani Mbeya Wilayani Rungwe. Barabara hii inatakiwa kujengwa kwa kiwango cha lami ili wananchi wa Majimbo yote matatu yaani; Busokelo, Kyela na Rungwe wanufaike kwa kuweza kusafirisha mazao mbalimbali kama ndizi, mpunga, kokoa, viazi mviringo, chai, mbao, mahindi na mazao mengine mengi, lakini pia usafirishaji wa gesi asilia aina ya *carbondioxide* ($Co_2$).

(vii) *Geothermal* (Nishati ya Umeme); ni muhimu kama nchi kuweza kuanza kuwekeza kwenye umeme wa joto-ardhi ambao unapatikana Jimbo la Busokelo, Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya eneo la Kata ya Ntaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea mapendekezo yangu yatapewa kipaumbele.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maendeleo uweke kipaumbele suala la maji na miundombinu katika Mkoa wa Lindi. Mkoa wa Lindi unakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa maji safi, takribani asilimia 85 ya wananchi wa Mkoa wa Lindi hawapati maji safi kupelekea kunywa na kutumia maji ya mito na mabwawa pamoja na wanyama. Kitu cha kusikitisha zaidi hospitali ya Mkoa wa Lindi nayo ina tatizo la uhaba wa maji safi kupelekea wagonjwa kuletewa maji ya vidumu kutoka majumbani.

Hii ni hali mbaya inayopelekea wagonjwa kuwa hatarini kupata magonjwa ya mlipuko, nilitegemea mpango wa maendeleo ungekuwa na mipango ya miradi mbalimbali ya maji katika Mkoa wa Lindi na maeneo yote nchini ambako kunakabiliwa na tatizo la maji.

Miundombinu ilipaswa ionekane kwa mapana katika mpango wa maendeleo kati ya mwaka 2012 - 2015 shilingi bilioni 6.4 zilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara yenye urefu wa kilomita 230 inayotoka Nangurukuru kuelekea Liwale. Hali ni hiyo hiyo katika barabara ya Nachingwea – Liwale. Serikali iweke mpango wa kuzijenga hizi barabara katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu; Serikali haijaainisha ina mpango gani juu ya wanafunzi waliofaulu kwenda Vyuo Vikuu, mpaka dakika hii hakuna kinachoeleweka juu ya wengi na hawa wanafunzi waliofaulu vizuri na kukosa mikopo. Serikali itambue kwamba elimu inaelekea kuanguka kama haitoandaa mpango wa kueleweka juu ya mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu afya; nchi nzima inakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa dawa katika hospitali, vifaa tiba na chanjo. Hii imejikita katika Wilaya zote za Mkoa wa Lindi na maeneo mbalimbali nchini. Huu mpango ulipaswa uoneshe maboresho katika sekta ya afya, akinamama na watoto wanaendelea kupoteza maisha yao wakati wa kujifungua kwa kukosa vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kilimo; mpango wa maendeleo umekosa shirikisho la soko la mazao kwa wakulima wa mazao mbalimbali kama ufuta, mbaazi na kadhalika. Ni vema Serikali ingepanua wigo kwa wakulima kwa kuwatafutia masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano; mpango wa maendeleo uzingatie suala la kuhakikisha hata maeneo yote nchini yanapata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uchumi; uchumi unaendelea kuanguka na matumizi kuongezeka hata baada ya wafanyakazi hewa kutambulika. Watumishi wengi wamesimamishwa kupeleka kila mwezi wanaendelea kupokea mishahara. Halmashauri zifikishiwe pesa kwa wakati kwa kutekeleza maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi elimu bure kwa wanafunzi, lakini hii haijaainishwa katika mpango wa maendeleo, kwani elimu bure haina maana yoyote kama wazazi bado wanaendelea kutoa michango. Pia kumekuwa na ucheleweshaji wa pembejeo, mpango huu ungeainisha ni kwa kiwango gani Serikali itahakikisha wakulima wanafikishiwa pembejeo kwa wakati.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Naomba nichangie kwa maandishi katika Mpango wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mizigo kupungua Bandari ya Dar es Salaam; mizigo imepungua kutokana na urasimu au wizi wa mizigo ya wafanyabiashara na kodi kubwa kuliko thamani ya mizigo tofauti na bandari ya Mombasa - Kenya; Beira Port - Mozambique; Durban Cape town na Port Elizabeth za Afrika ya Kusini. Bandari nne za Tanzania ni sawa na mapato ya bandari ya Mombasa, Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri; Mamlaka ya Bandari (*TPA)* isifanye kazi kimazoea *(business as usual)* ifanye kazi kiushindani, iondoe urasimu katika utoaji mizigo; mizigo iweze kutolewa katika muda mfupi *(min – 24 hours – max 72 hours)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili bandari zote za Tanzania zifanye kazi kwa viwango vinavyokusudiwa, mizigo ifanyiwe *classification*. Aina ya mizigo ya Mikoa; Kanda ya Kaskazini- Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Mara, Mwanza na Kagera, mizigo ishushe katika bandari ya Tanga. Mizigo ya Mikoa ya Kanda ya Kati- Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Tabora, Singida, Shinyanga na Kigoma, mizigo ishushwe katika Bandari ya Dar es Salaam; meli nyingi zinatumia muda mrefu katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mizigo ya Mikoa ya Kanda ya Kusini *(Southern Regions)* Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Rukwa, na Katavi, mizigo ishushwe katika bandari ya Mtwara. Hii iangalie pia shehena ya mizigo ya Kimataifa na izingatie hali ya kijiografia *(Geographical Conditions)*. Mfano, mizigo ya Burundi, Rwanda, Uganda na Sudan Kusini ishushwe bandari ya Tanga na mizigo ya Malawi, Zambia na Congo, ishushwe bandari ya Mtwara na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia huzuni kuona au kusikia kuwa katika *Bank Economic and Investment Report* kuwa, katika nchi 140, Tanzania inashika nafasi ya 120 huku tukiwa na rasilimali na malighafi nyingi tofauti na nchi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* na Mapato; pamoja na taarifa ya ukusanyaji mkubwa wa mapato unaofanywa na *TRA*, lakini wafanyabiashara wanakamuliwa sana, wanafanyiwa makisio *(assessment)* makubwa kuliko faida inayopatikana katika biashara zao. Matokeo yake, wafanyabiashara wengi wanafunga biashara zao au viwanda vyao. Wengine wanadiriki kuhamia nchi jirani za Burundi, Rwanda, Mozambique, Uganda, Kenya na Sudan Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati *TRA* inaongeza mapato ya Serikali, lakini inaua biashara na kuzorotesha uchumi wa nchi yetu. *TRA* inakamua ngo'mbe maziwa hadi anatoa damu bado *TRA* inakamua tu! Nashauri *TRA* ifanye utafiti na uchambuzi ili ijue kwa nini wafanyabiashara wanailalamikia *TRA* na ikibidi itumie *Demand Law System.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Third Law of Demand; in the high price low demand and in the low price high demands.* Maana yake, kodi ikiwa kubwa walipaji watakuwa kidogo na kodi ikiwa ndogo walipaji watakuwa wengi. Wahindi wanasema, 'dododogo bili shinda kubwa moja'.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupeleka *property tax* kukusanywa na *TRA* ni kuzuia Halmashauri zetu nchini. Je, Mheshimiwa Waziri Mpango, Serikali imeamua kuziua Halmashauri kwa kuwa vyanzo vyake vikuu vyote vinatwaliwa na *TRA?* Tanga *City Council* imenyang'anywa hadi nyumba za kupangisha! Naomba Serikali irudishe *property tax* itwaliwe na Halmashauri zetu. Tanga *City Council* irudishiwe nyumba zake na kupangisha. Zipo Serikali za aina mbili, *Central Government and Local Government* hivyo, tusizinyong'onyeze *Local Government.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya Viwanda; viwanda vinahitaji umeme wa uhakika, vingi vimekufa au kuuzwa na Serikali. Ushauri; Serikali ifufue viwanda vilivyokufa kwa kuweka mitambo mipya. Mfano, *Steel Rolling Mills, Sikh Saw Mill*, Kamba Ngomeni na kadhalika katika Mkoa wa Tanga; *General Tyres* - Arusha; na Kiwanda cha Nyuzi, Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo, Mifugo, Michezo na Uvuvi vyote vinahitaji kuboreshwa na kutekelezwa kwa vitendo.

**MHE. KIBERA J. KISHIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri pole sana kwa misukosuko unayopitia. Uchumi ni soko gumu sana hasa uchumi wa dunia ya tatu na nchi maskini kama Tanzania na hasa kuwatoa kwenye maisha waliyozoea kwa miaka 25 ni kama kumwachisha mtoto ziwa, lazima kuwe na mgogoro mkubwa, vuta subira!

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu, kwanza ni maoni kuhusu Serikali kuruhusu madini yetu na ya nje ambayo yanazalishwa na wachimbaji wadogo yawe asilimia *zero* wakati wa kuingia, kutoka iwe asilimia moja, itatusaidia sana kama nilivyochangia kwenye mchango wa bajeti mwezi wa Saba ulio kwenye *Hansard* ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wa Kariakoo ni wachangiaji wazuri wa uchumi kwenye *importation,* lakini tatizo lao kubwa liko kwenye vitu viwili: Suala la *TBS* kwa *product* ambazo siyo chakula. Mfano, Redio ya sh. 5,000 wanataka iwe na ubora, lakini wananchi wananunua na wanasikiliza habari au muziki; wanawasumbua na ukizingatia mali nyingi inanunuliwa na watu wa Malawi, Mozambique, Zambia, Congo na majirani wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *tariff* kwa bidhaa kwa mfano, *Colgate gram* 100 inauzwa sh. 2,000, *Colgate herbal* 100 inauzwa sh. 8,000. Kwenye *tariff* zinaitwa *(Toothpaste) TRA* anavyothamini ni sh. 8,000, muagizaji kaagiza kwa sh. 2,000, hapo ndipo mzozo unazuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikiria upya suala la *license* kwenda kwenye mafuta ili kukusanya fedha kwenye ma- *grader*, *tractor, generator* na mashine nyingi, zitapunguza pia rushwa za barabarani.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono jitihada zinazofanyika katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa 2016/2017 hadi 2020/2021, mkakati ni mzuri uelekeo unatoa picha kubwa ya matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, Utekelezaji wa Miradi ya Kipaumbele kama Taifa; Ushauri, miradi ya kielelezo itekelezwe kwa umakini kama Taifa, *we need action and not words.* Miradi ya Reli ya Kati, Kanda Maalum za Kiuchumi, Bagamoyo, Kigoma, Mtwara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Kidahwe-Nyakanazi na Manyovu, Kasulu; miradi hii ni muhimu sana itekelezwe hata kama ni kukopa fedha kutoka nje au ndani, imepangwa vizuri itekelezwe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, ukurasa wa 28; Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Kikosi Kazi cha Maboresho ya Kodi kiangalie vyanzo vipya vya mapato *(New Tax Revenues)* mfano, angalieni *Economic* za Uvuvi wa Bahari Kuu, tunaambiwa ni eneo lenye kuweza kuchangia pato kubwa la Taifa hili. Uzoefu wa nchi za Singapore, Thailand na Austria unatoa rejea sahihi kabisa. Tuwekeze huko, tununue meli ya uvuvi na tuboreshe gati namba Sita, ambayo imetolewa na Mamlaka ya Bandari *(TPA),* kama bandari yetu kituo cha kupokea mavuno hayo ya Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Umma ambazo Serikali inamiliki hisa zake ukurasa wa 43 hadi 44 wa hotuba ya Waziri; taasisi za *Tipper, PUMA Energy,* Kilombero *Sugar* ni taasisi ambazo Serikali yetu ina hisa, lazima tuwekeze huko. Taasisi za *Tipper* na *PUMA Energy* ambako Serikali ina asilimia 50 ni maeneo ambayo yakisimamiwa vema na Serikali kuweka nguvu yanaweza kuongeza pato la Taifa letu. Kampuni hizo zipewe *support* ili zizalishe mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa sekta binafsi kupitia *PPP;* Mheshimiwa Waziri, dhana hii inafahamika vizuri Serikalini? Ipo wapi miradi ya *PPP* mfano, ujenzi wa barabara ya Chalinze- Dar es Salaam wako wapi sekta binafsi? Ushiriki mdogo wa sekta binafsi kutokana na Mazingira yasiyowezeshi ya uwekezaji, angalieni upya vikwazo vinavyokwamisha ushiriki wa *private sector,* tatizo lazima libainishwe na lipatiwe dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 40 kupitia upya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na maendeleo na ustawi wa jamii. Kikosi kazi kiangalie

tozo kwenye pamba, kahawa, tumbaku, mkonge, chai na kadhalika ili mazao haya yalimwe kwa tija bora zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali ili kuongeza ufanisi. Wabunge kwa nyakati mbalimbali wanashauri, ni vizuri Serikali ikawa sikivu na kuchukua ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge la Bajeti, Wabunge walipigia sana kelele masuala ya *VAT* kwenye utalii; *VAT on transit, single customs territory* kuunganisha *RAHCO* na *TRL* na kadhalika. Nchi imeendelea kupoteza mapato ya mabilioni ya fedha na hakuna hatua zinachukuliwa, kama nchi sasa tumekuwa mawakala wa kukusanya kodi kwa nchi ya *DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania, uwekezaji kwenye sekta ya kilimo haukwepeki ikiwa kweli tumeamua kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati. Mpango utoe kipaumbele kwa *agro-processing industries.* Watanzania asilimia 80 wasiwe watazamaji tu katika mpango huu bali wawe ni sehemu muhimu ya mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo chetu kimekuwa tegemezi kwa mvua ambazo hazitoshelezi. Ni muhimu sana tufanye mapinduzi katika kilimo ili kilimo cha umwagiliaji wa kutumia mabwawa na visima virefu kipewe kipaumbele. Pia, masoko ya mazao hayana uhakika, msimu wa 2015/2016 kilogramu moja ya Mbaazi ilikuwa sh. 3,000 na msimu huu wa 2016/2017 bei ya kilogramu moja ni sh. 800. Wakulima wa Mbaazi wamekata tamaa kabisa, ruzuku ya kilimo haipatikani kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Benki ya Kilimo ambayo iko Dar es Salaam, benki hii iongezewe mtaji na ikopeshe wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya huduma za afya nchini ni mbaya sana, hakuna dawa kwenye vituo vya afya, hakuna vifaatiba na pia watalaam hawatoshi, ni vema mpango huu uhakikishe hospitali za Wilaya, vituo vya afya na *dispensary* vinatoa huduma stahiki kwa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuleta mageuzi ya uchumi wa viwanda nchini.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; awali ya yote napenda kunukuu katika kitabu Kitakatifu cha Biblia, Mithali, Sura ya 11, mstari wa 14; mstari huo unasema: "Pasipo mashauri Taifa hupotea, bali kwa wingi wa washauri huja wokovu."

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya afya nchini; ni dhahiri hali ya uchumi wa nchi unayumba. Kuyumba huku kwa uchumi ni hatari sana katika sekta nzima ya afya. Kumekuwepo na malalamiko makubwa katika sekta ya afya kwa muda mrefu sasa na hayajatatuliwa. Takwimu zinaonesha huduma za afya na ustawi wa jamii zilikua kwa asilimia 8.1 mwaka 2014, lakini kwa mwaka 2015 ni asilimia 4.7 pekee. Hii ina maana kwamba, utoaji huduma za afya na ustawi wa jamii umepungua kwa asilimia 3.4. Hivi karibuni nilifanya ziara katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Musoma, Mara ni kilio kwa kweli! Vitanda havitoshi, madawa hakuna, kiasi kwamba wanaokwenda hospitali wakiwa wanaugua malaria wanatoka na *typhoid* au kifua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kauli tata sana na za aibu kwenye sekta hii ya afya. Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amekiri kuwepo kwa ukosefu wa dawa nchini, ndani ya Bunge hili, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu wake wanasema kuna dawa za kutosha katika Bohari ya Dawa Nchini *(MSD)*. Wananchi nao wanalalamika kwa kukosa dawa mahospitalini. Huduma za tiba zinadorora kwa kuwa hakuna vifaatiba katika mahospitali mengi. Pamba na *gloves* zimeadimika, wagonjwa wanalazimika kwenda na pamba na *gloves;* akinamama na watoto wamekuwa wahanga wakubwa katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kuna siku hapa Mheshimiwa Mbunge mmoja aliuliza swali kuhusu Mpango wa Serikali kupambana na ugonjwa wa *fibroid* kwa wanawake. Ni ajabu sana Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwa kubeza kuwa, *fibroid* siyo ugonjwa tishio kwa kiasi hicho. Lakini sisi akinamama tunajua ni kwa namna gani akinamama wenzetu wanasumbuliwa na ugonjwa huo. *Fibroid* kwa akinamama ni tishio na ni tishio kubwa sana maana sasa linawakumba mpaka mabinti wadogo. Hili suala siyo la kuchukulia kimzaha tu! Tunapoteza nguvukazi ya Taifa ha hatuoni mpango madhubuti wa Serikali katika kukabiliana na tatizo hili kama walivyofanya kwa ugonjwa wa malaria kwa akinamama wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko yangu kuona Serikali ikinunua ndege ambazo zinawanufaisha tabaka la watu wachache tu huku hakuna uwekezaji wa kutosha katika sekta ya afya ambayo inamgusa kila mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema, pasipo mashauri, Tanzania itapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la utawala bora; hakuna maendeleo kama hakuna utawala bora. Ndani ya Serikali hii, washauri mbalimbali na watalaam wamekuwa wazito katika kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Tatizo kubwa linaloitafuna Serikali hii ya Awamu ya Tano ni kutokuzingatia misingi

ya utawala bora, kufuata sheria, Kanuni pamoja na kuruhusu mawazo huru kwa kila Mtanzania. Utawala bora ni pamoja na kukaribisha mawazo kutoka katika maeneo mbalimbali bila kujali itikadi za vyama. Ni pamoja na kuwa na kifua cha kupokea changamoto ikiwa ni pamoja na kukosoa na kukosolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko yangu pale ninapoona Vyama vya Upinzani ambavyo ni jicho la pili la Serikali, ni jicho linaloweza kuona pale Serikali isipoweza kuona, ni mdomo wa kuwasemea wadau mbalimbali ikiwemo ninyi Wabunge wa Chama Tawala na Mawaziri pale ambapo mna mambo ambayo hamuwezi kuyasema waziwazi kwa Serikali kwa sababu ya hofu za nafasi au maslahi binafsi. Upinzani ni msaada kwa kuwa, ndiyo Serikali mbadala *(Alternative Government)*. Tunapoona Mawaziri au Wabunge wakichukia Upinzani au kuwa na mawazo potofu kuwa, upinzani ni kupinga inashangaza sana!

Ni vema Waheshimiwa Wabunge wakapewa elimu ili kujua upinzani ni kitu gani ili linapokuja suala la kujadili mambo ya msingi ya kimaendeleo kwa faida ya nchi yetu waweze kuwa-*change* kwa kupokea, kuyachambua yale yanayofaa hasa katika kujadili Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maendeleo inakwama kutokana na sanaa katika mambo ya msingi. Mfano, Mkurugenzi anatumbuliwa tena kwa barua kutoka Ikulu halafu anapelekwa nje ya nchi kuwa Balozi; tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi imekuwa na msururu wa kodi kwa wafanyabiashara wazawa tena wale wenye mitaji midogo. Maliasili kuna kilio kikubwa cha kodi hizo mfano, kodi ya kulipia magari, leseni, mageti na kadhalika. Hii ikiwa ni jumla ya kodi 32 katika biashara ya sekta ya utalii. Yaani inaweza kuchukuwa takribani miezi miwili mpaka mitatu katika kulipia kodi. Hii ni aibu kubwa kwa Serikali, ambayo inashindwa kuleta tija katika kuwasaidia watu wake ambao tayari wengi wao wanapambana na ukuta mkubwa wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, kuna baadhi ya viongozi wanabeza na kusema, eti Watanzania ni wavivu! Kwa wingi huu wa kodi ambao unawafanya wafanyabiashara kushindwa kuendelea kumudu biashara zao, Serikali haioni kuwa tunazalisha wimbi la majambazi na vibaka tena kwa bidii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu kuwa, Serikali iangalie upya namna ya kukusanya kodi. Iangalie ni aina gani za biashara za kukusanya kodi na kwa kiasi gani ili kupunguza mzigo mkubwa uliowaelemea wafanyabiashara wadogo au wachuuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Watendaji wa Serikali na wanasiasa wakaheshimu kazi kubwa inayofanywa na upinzani. Mheshimiwa Rais aheshimu Sheria na Katiba ya nchi ambayo kimsingi inawaruhusu wanasiasa kufanya mikutano yao kwa uhuru na amani. Rais awe ni mfano wa kusimamia Sheria na Katiba ya nchi. Kila Kiongozi ataweza kutekeleza shughuli za maendeleo na kuleta tija katika Taifa endapo kuna uhuru na haki katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho; niombe Waziri wa Fedha aweze kupitia tena vipaumbele hivi vya mpango na kuangalia ni namna gani sekta ya utalii inaweza kuchangia zaidi. Kwa kuwa, awali sekta hii ndiyo ilikuwa inachangia pato kubwa la Taifa takirbani asilimia 27.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuandaa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na mwongozo wa kutayarisha mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada nzuri zinazochukuliwa na Serikali katika kuongeza pato la Taifa kwa kiasi kikubwa tegemeo kubwa ni mapato ya ndani *(tax revenue)* kuliko kuangalia vyanzo vingine vya mapato *(non tax revenue)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikajielekeza katika vyanzo vingine vya mapato *(non tax revenue)*. Serikali ijiimarishe katika usimamizi wa taasisi zake zilizo chini ya Msajili wa Hazina ili zijiendeshe kibiashara na kurudisha mapato Serikalini kupitia gawio *(dividend)* na hata mapato mengine nje ya gawio. Serikali ichukue hatua za kurekebisha Mashirika yanayolegalega na hata kuyafunga yale ambayo hayana tija. Katika kufufua Mashirika na viwanda ambavyo havifanyi kazi, Serikali ichukue tahadhari kubwa hasa pale inapopelekea ubinafsishaji kwa wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na lengo zuri la kufufua viwanda ambavyo kwa muda mrefu havifanyi kazi, lengo liwe kuanzisha kitu kipya katika mazingira ya sasa. Kwa mfano, Kiwanda cha Tanganyika *Packers* cha Mbeya, kwa sasa yaliyolengwa kuwa mashamba ya malisho *(holding ground)* kwa sasa yapo katikati ya mji na sheria za mipango miji zina ukomo wa shughuli za kilimo kwa mijini. Hivyo ni bora kuangalia kupata eneo mbadala jipya nje kidogo ya mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kujikita katika kuimarisha uchumi kupitia sekta ya viwanda. Pamoja na mkakati wa kuimarisha

uchumi kupitia viwanda, Serikali iweke mkakati wa kuimarisha kilimo cha mazao yote. Nchi yetu kwa asilimia zaidi ya 70 wananchi wake wanategemea kilimo hivyo viwanda vilenge kutumia malighafi inayozalishwa Tanzania ili ukuaji wa uchumi uwaguse Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imejaaliwa kuwa na ardhi kubwa na nzuri ambayo inaweza kuzalisha mazao mbalimbali yenye soko zuri la ndani na nje. Zao kama pareto limeachwa yatima licha ya mahitaji makubwa katika soko la dunia. Kuna haja ya kuongeza uzalishaji wa pareto na pia kuwepo na viwanda vya pareto maeneo yanayolima pareto. Kwa sasa soko la pareto hapa Tanzania linayumba kutokana na kukosa ushindani katika manunuzi toka kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie utekelezaji wa miradi iliyomo katika mipango iliyopita. Pamoja na mahitaji ya miradi mipya, mikakati iwepo ya kutekeleza miradi ya nyuma kama vile miradi ya maji, zahanati na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika kama *NHIF* yajikite katika malengo yake ya msingi na yakisimamiwa vizuri wanaweza kuwekeza katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na uwekezaji huo una uhakika wa kuilipa *NHIF* kutokana na mapato ya hizo zahanati na vituo vya afya. Kwa sasa *NHIF* wamejiingiza katika kuwekeza kwenye *real estate* badala ya kuboresha afya za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Serikali kwa kutenga shilingi milioni 50 kwa kila kijiji na mtaa. Ili kutimiza lengo hilo, napendekeza Serikali itenge angalau shilingi bilioni 300 kila mwaka kuanzia 2017/2018 ili kukamilisha upelekaji wa fedha hizo kwenye maeneo yote kabla ya 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya milioni 50 kwa kila kijiji inahitaji kuandaa utaratibu mzuri kushirikisha *SACCOSS* na pia napendekeza kuitumia Benki ya kilimo *TADB*. Kwa kuitumia *TADB* Serikali itatimiza malengo ya kuinua uchumi, wakulima pia kuiwezesha *TADB* kupata mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge,* Serikali iweke mkakati wa kuboresha utendaji wa *TAZARA* ikiwemo kujenga matawi ya reli kuunganisha Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke mkakati wa kuboresha miundombinu ya Baraza la vijijini kuwezesha usafirishaji wa mazao na kurahisisha masoko ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

(1) Mdororo wa uchumi umesababishwa na sera za uchumi wetu. Wakati Serikali imetumia sera zote mbili za *fiscal policy* kubana matumizi na kuongeza kodi katika bidhaa na huduma mbalimbali. Benki Kuu imekaa kimya kabisa bila kuchukua hatua zozote katika kupunguza riba za mabenki na kusimamia mzunguko wa fedha nchini. Hali hii ndiyo iliyosababisha mabenki kuporomoka na kushuka kwa uchumi. Fedha zimepungua kwenye mzunguko.

(2) Kupungua kwa uzalishaji bidhaa na kushuka kwa ajira nchini. Hivi sasa viwanda na makampuni mengi yameanza kupunguza wafanyakazi kama kwenye sekta ya utalii, hoteli na taasisi za elimu.

(3) Lazima Serikali ianze kurasimisha Sekta binafsi na kuziunga mkono ili zichangie katika pato la Taifa.

(4) Kuhamasisha kilimo kikubwa cha mazao ya chakula na biashara kwa kutoa *support* inayohitajika pamoja na masoko ya bidhaa.

(5) Kuendelea kuhakikisha kuwa Serikali inahamasisha na kusimamia sera ya elimu ikiwa ni pamoja na kuanzisha mitaala yetu ili iendane na mahitaji ya soko na kuongeza udahili ili nchi iwe ya wasomi wengi.

(6) Kuangalia vipaumbele ambavyo vina *competitive advantages* kufuatana na mazingira na jiografia ya nchi yetu. Lazima uchambuzi wa kina ufanyike. Kwa mfano; Bahari, Bandari, Mlima Kilimanjaro, Mbuga za Wanyama, Madini, Olduvai Gorge na kadhalika.

(7) Kuimarisha matumizi ya reli ya *TAZARA* ili kupunguza gharama za uzalishaji na uharibifu wa barabara katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwa ni pamoja na kupambana na rushwa, ubabaishaji na kadhalika.

**MHE. ALI HASSAN KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *definition* (maelezo), *recognition* na *money measurement* kwa *item* ambayo imo katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Definition* Maelezo *(Broad or Narrow definition),* naishauri Serikali kuwa maelezo au *definition* ya *item* ambayo imo ndani ya mpango wa maendeleo wa Taifa iwe inahusiana na sehemu ya jambo ambalo litatekelezwa kwa kipindi hicho kuliko kueleza mradi wote ambao unatekelezwa

kwa muda wa miaka mingi ijayo. Mfano, mradi wa Mchuchuma na Liganga, katika miradi hii imeelezwa kwamba itaanza na kumalizika ndani ya muda huo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *recognition,* napendekeza kuwa *item* ambayo itaingizwa humu kama ni mpango iwe imetimiza kigezo ambacho hatua za utekelezaji zitakuwa karibu na utekelezaji ikiwemo mikataba na muda wa dhamira ya kutekeleza ndani ya muda uliowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, m*easurement,* fedha zitakazotajwa kutekeleza jambo hilo ziwe zimezingatia muda wa utekelezaji shughuli zilizoainishwa kutekelezwa na kadhalika. Kwa mfano, miradi ya Mchuchuma na Liganga imepangwa kutumia kwa jumla ya dola za Kimarekani bilioni mbili nukta tisa ambazo takribani ni shilingi trilioni sita za Kitanzania wakati katika kugharamia mpango sekta binafsi inakadiriwa kuchangia kwa shilingi trilioni saba nukta nne za Kitanzania. Miradi ya Mchuchuma na Liganga ni mfano tu lakini kwa maeneo mengi kama vile uanzishwaji wa kituo cha biashara Kurasini, ujenzi wa reli ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wingi wa fedha za maendeleo na ukuaji wa mapato ya ndani. Fedha za maendeleo kwa mwaka 2015/2016 zilikuwa trilioni nne nukta tatu, fedha za maendeleo kwa mwaka 2016/2017 zilikuwa trilioni 11.820 lakini ongezeko la makusanyo ya ndani yanakuwa kidogo. Tumeongeza fedha za maendeleo ili tuongeze uwezo wa mapato ya ndani ili tupunguze kukopa, lakini mikopo nayo inaongezeka badala ya kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuangalia kuwa fedha za maendeleo kwanza zilenge kwenye miradi itakayotoa majibu kwa haraka ili ichangie katika kukuza mapato ya ndani.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mapato, kutokana na ongezeko la mapato shilingi trilioni tatu nukta nne kuna haja ya Serikali kuangalia maeneo mengi zaidi ili kuongeza mapato kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia upya tozo mbalimbali zisizo za kodi katika Serikali na Taasisi zake ambazo hazijapandishwa kwa muda mrefu.

(ii) Kushawisha Kampuni nyingi kuandaa mahesabu badala ya kuwa katika mlipa kodi asiyeandaa hesabu.

(iii) Kufuatilia aina zote za kodi kuwa zinatumika ipasavyo. Mfano *stamp duty on contracts.* Kodi hii kampuni nyingi hazilipi.

(iv) Ripoti ya kuboresha mapato *"CHENGE ONE AND TWO"* itumike ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; Serikali itoe kipaumbele zaidi katika kilimo kwani mchango wake ni mdogo wa asilimia 2.9 wakati lengo ni asilimia sita hivyo suala la pembejeo lipewe kipaumbele hususani ruzuku ili kilimo cha jembe la mkono kiondoke kama ilivyoahidi Serikali. Tumbaku bado tuna tozo nyingi na mkulima ananyonywa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo katika mafuta sh. 50, tunaomba Serikali iweke sh. 50 kwa lita ili kukidhi mahitaji ya wananchi juu ya maji vijijini na zahanati kwa kuwa uwezo wa halmashauri nyingi ni mdogo hivyo bajeti ya 2017/2018 Serikali ikubali ombi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Bunge, kutokana na changamoto za utendaji 2016/2017 tunahitaji Waziri ahakikishe kuwa bajeti ya shughuli za Bunge iongezwe kwa kiasi kikubwa kukidhi shughuli za Bunge kwa mujibu wa katiba angalau 130 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi inayoendelea, Serikali ihakikishe miradi hii inakamilika ili kupunguza gharama. Tunaomba barabara ya Sumbawanga-Mpanda, Manyoni-Itigi-Tabora na Sitalime-Mpanda zikamilike 2017/2018. Pia Shirika la Reli lipewe pesa kuboresha mabehewa na ofisi ili usafiri utumike mwaka mzima hata masika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya msamaha; tunaunga mkono hoja ya kupitia upya mikataba hii ya msamaha wa kodi na kuwezesha Serikali kuongeza mapato pia kusaidia zaidi wakulima kufanya kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mweyekiti, ubia katika uwekezaji; zoezi la uwekezaji katika ubia lipewe muda maalum ili kuharakisha maendeleo kwa wananchi hususani wawekezaji wa ndani wenye uwezo wapewe kipaumbele.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu haujaonesha baadhi ya sekta katika kukuza pato la Taifa:-

(i) Sekta ya madini
(ii) Sekta ya Maliasili na Utalii
(iii) Bandari
(iv) Gesi

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu sekta ya madini itachangia kiasi gani? Hisa za Serikali katika miradi ya uchimbaji madini kwenye migodi ya Geita, Mwadui, Buzwagi, *Tanzanite One* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu, uchimbaji wa gesi umeanza lakini katika mpango huu haujaonyesha ni kwa namna gani sekta hii itaongeza pato la Taifa. Pia ningependa kujua ununuzi wa vitalu mpaka sasa ni vitalu vingapi viko mikononi mwa wawekezaji na vinaingiza shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu haujaonyesha sekta ya maliasili ina malengo kiasi gani. Napenda kujua mchango wa Serikali katika mpango huu wa 2017/2018. Kwenye upande wa Bandari pia uko kimya ni kwamba Bandari ndiyo inakufa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufike kwenye Tanzania ya viwanda ni lazima tuwekeze kwenye kilimo na siyo kilimo tu. Tunahitaji kilimo cha kisasa ili tuwe na malighafi kwa ajili ya viwanda. Pia kwenye mpango huu kilimo alichokitaja Mheshimiwa Waziri upande wa mazao ni mazao ya chakula tu. Ushauri wangu, tuongeze mazao ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afya; ndani ya nchi sasa madawa yamekuwa tatizo, tusipoongeza fedha upande wa afya ni dhahiri kuwa katika viwanda tunavyotarajia kuvijenga tutaendelea kuajiri watu toka nje, hivyo tuna kila sababu ya kuboresha hospitali zetu ili tuwe na jamii yenye afya bora.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na mchango wangu kwa kuangalia vipaumbele vya mpango wenyewe kuelekea Tanzania ya Viwanda. Nilitegemea kuona kilimo kikipewa kipaumbele katika mpango huu, lakini imekuwa kinyume chake sijaona mahali popote pakitajwa kama kipaumbele kwa kilimo cha mazao kama korosho, pamba, katani, ufuta na kadhalika ilikuwa malighafi katika viwanda hivyo. Hata hivyo, sijaona zao la ngano likitajwa popote wakati sasa ulaji wa watu nchini sasa umebadilika kwani sasa ngano huliwa zaidi kuliko mchele, mahindi na mazao mengine ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano katika hili kama ifuatavyo:-

Kampuni ya Bakhresa peke yake kwa siku wanasindika tani 2700 za ngano ambazo zote zinatoka nje ya nchi. Katika miradi iliyotekelezwa hakuna mradi wa kilimo zaidi ya kuona mradi wa kuendeleza Kijiji cha Kilimo Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda sijaona kiwanda chochote kilichotajwa katika viwanda vinavyotarajiwa kukuza uchumi zaidi ya *General Tyre* na makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga. Katika fungamanisha maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya watu hakuna uhalisia kwani hatujawaandaa vijana nchini kushiriki katika uchumi wa kilimo wala viwanda. Wakulima wetu wanashindwa kuondokana na jembe la mkono kwa kuwa hawakopesheki katika taasisi za fedha. Kwani gharama za kupata hati ya

kumiliki mashamba bado ziko juu sana kwani hilo nalo sharti kuu kwa taasisi zinazokopesha vifaa ya kilimo kama *tractor,* hivyo kuwafanya wakulima kushindwa kulima kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilwa sasa imeanza kutoa madini ya *gypsum* ambayo sasa yanatumiwa na viwanda vyote vya *cement* nchini. Hata kusafirishwa kwenye nchi za Zambia, Malawi na Afrika Kusini, lakini sijaona mahali ilipotajwa katika mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Waziri wa Fedha kwa robo ya kwanza, sekta yenye ukuaji mdogo ni sekta ya usambazaji wa maji safi na udhibiti wa maji taka, pamoja na chakula na malazi, hivyo basi kutarajia kupata maendeleo toka kwa jamii yenye huduma hafifu kiafya ni sawa na kukamua ng'ombe bila malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yetu bado ni ya kutegemea ajira kutoka Serikalini au sekta binafsi kwani wahitimu wetu wameshindwa kupata stadi za maisha kulingana na elimu wanayoipata. Vilevile kama hatutakuwa tayari kuboresha maisha ya Walimu na badala yake kuendelea kuwadhalilisha Walimu kwa kuwapa adhabu mbalimbali kama vile kuwapiga viboko mbele ya wanafunzi hakuinui ari ya Walimu hawa ya kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda; mlundikano wa viwanda katika Mji wa Dar es Salaam hasa kwa viwanda vinavyotegemea malighafi toka nje ungeweza kupunguzwa na kusambaza viwanda hivyo mikoa mingine ya nchi yetu. Ikiwa wawekezaji wangeondolewa kodi kwa wale watakaowekeza nje ya Dar es Salaam ili gharama zilingane na yule aliyewekeza Dar es Salaam. Kwa kiwanda kinachofanana kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia kupanua ajira kwa vijana wa mikoa mingine kwa upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sensa ya watu ni muhimu sana kwa sasa kwani takwimu tunazoletewa leo hazina uhalisia ukilinganisha na idadi ya watu. Hayo maendeleo ya kukua kwa uchumi tunayapima kwa kigezo gani wakati hatuna takwimu halisi ya idadi ya watu wetu. Ndio maana matamko mengi ya Serikali kuhusu huduma za jamii yanakosa uhalisia kwa wananchi wa hali ya kawaida. Haingii akilini mtu kuambiwa uchumi unakua wakati kipato cha mtu mmoja mmoja kinashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshauri Waziri mwenye dhamana ni bora akazingatia ushauri wa Wabunge ukizingatia ndiyo wawakilishi wa wananchi. Tunashauri kwa niaba yao kulingana na hali halisi ya maisha ya Mtanzania wa hali ya chini wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuja na mpango ambao unatekeleza ule mpango wa miaka mitano, Mpango wa Maendeleo endelevu na ilani ya CCM. Nipongeze mambo yafuatayo ambayo ni makusanyo yameongezeka na udhibiti wa matumizi umeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie kwa makini changamoto zifuatazo:-

Ukusanyaji wa kodi wenye ufanisi na matatizo ya ukusanyaji kwa maofisa na walipa kodi. Uwekezaji sekta binafsi kumudu ushindani wa bidhaa nje unaotokana na "*application* ya *VAT*; *cash flow management,* mzunguko wa fedha (*money supply),* ukuaji wa uchumi na hali halisi ya maisha, kupeleka fedha za bajeti zilizotengwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, Serikali iendelee kupanua wigo wa ukusanyaji, mkazo uwe pia kwenye makato yasiyo na kodi (*non-tax revenue)* hususan taasisi zilizo chini ya *TRA*. Tuangalie namna kodi *(VAT)* itakavyowalinda sekta binafsi, tuangalie mnyororo wa huduma, mfano tuwezeshe kilimo chenye tija, kilimo kitoe malighafi za viwanda tujenge viwanda ambavyo ni soko la viwanda vyetu. Kilimo na viwanda vitainua uchumi na kuleta ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie vizuri utekelezaji *accounting framework* ya "*accrual basis of accounting* ili tuweze kuwa na *cash* ya kutosha mwanzoni mwa mwaka miradi isisimame mwanzoni mwa mwaka. Uwepo uhakiki wa *data "data integrity"* ili *consumer price index*" ijengwe kwa kuzingatia mtawanyiko wa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itawasaidia menejimenti ya *real economy* na *Nominal economy* ili kuondoa dhana ya ukuaji uchumi na hali halisi. *Program based on budgeting* inayolenga kuanza na Wizara nane itayarishwe kwa makini kwani inahitaji taarifa nyingi, inataja kuwa na "*activity*" nyingi, ngumu sana kuainisha shughuli (*activity)* na matokeo lengwa/malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mpango huu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili mapendekezo ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2017/2018 huku Serikali ikiwa haijatoa fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi kwenye halmashauri na wilaya kwa sehemu kubwa na hivyo kusababisha miradi kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri wa Fedha inaonesha wastani wa pato la kila Mtanzania ilikuwa sh. 1,918,928/= sawa na USD 96.5 mwaka 2015.

Hizi takwimu haziendi na hali halisi ya wananchi wengi zaidi ya 809 wanaoishi vijiji ambao hawana uwezo wa kupata hata 100,000 kwa mwezi. Wengi wanapata mlo mmoja tu kwa siku. Serikali itueleze ni maeneo gani ya nchi yetu ambapo takwimu hizi zinatolewa/zinachukuliwa ambapo hazitoi hali halisi za maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la watu ndani ya nchi yetu ni kubwa sana haliendani na uwezo wa Serikali kutoa huduma muhimu na za uhakika. Ikiwa sensa ya mwaka 2012 tulikuwa watu milioni 45 mwaka 2016 tunakadiriwa watu milioni 50.1 na mwaka 2025 tutakuwa milioni 63 hii ni hatari kwa ustawi wa watu wa Taifa letu. Kwa mikakati gani ya Serikali kudhibiti ongezeko na kasi kubwa ya ongezeko la watu kwa nini Serikali inanyamaza kimya wakati inaona hatari iliyoko mbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ihakikishe kipengele cha kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu kinatekelezwa kikamilifu; mpango wa elimu bure umesaidia kupunguza machungu kwa wazazi na watoto wengi kuandikishwa mashuleni, bado fedha inayotolewa ni kidogo haitoshelezi mahitaji ya watoto na shule zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mpango ujao lazima Serikali iongeze fedha ya *capitation* zinazopelekwa mashuleni baada ya kufanya tathmini na kutambua mahitaji ya wanafunzi ili wapate elimu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwenye mpango ujao ilete mpango kamili wa kujenga vyuo vya mafunzo ya ufundi *(VETA)* kwenye Wilaya zote hapa nchini ambazo hazina mahitaji ya vyuo vya *VETA,* ni muhimu sana kwa ajili ya kujenga stadi za kazi kwa watoto wanaofeli wanaokosa nafasi ya kujiunga na vyuo vikuu na vyuo vingine vya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka mpango ujao uoneshe mikakati ya kujenga zahanati kila kijiji na vituo vya afya kila kata ili kuokoa maisha ya watu yanayopotea kwa sababu ya huduma za afya kuwa mbali na watu. Njia pekee ya kupunguza vifo vya watoto na wanawake, wazee na makundi mengine ni kutotekeleza mpango wa kupeleka huduma hizi jirani na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji safi na salama; tatizo la ukosefu wa maji ni kubwa sana linazidi kukua kutokana na ongezeko kubwa la watu. Mpango wa mwaka 2017/2018 lazima Serikali ioneshe mkakati wa kuondoa tatizo la maji, miradi mikubwa ya maji, Mkoa wa Tabora kutoa maji Ziwa Victoria, mradi wa maji kutoka Malagarasi kwenda Kaliua na Urambo na miradi yote ya kimkakati katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya elimu ya juu; mpango ujao kwanza tathmini ya uhakika ifanyike kuanzia mashuleni na vyuoni ili kubaini mahitaji halisi/wanafunzi wanaohitaji kunufaika na mikopo hiyo ili kutenga fedha za mikopo ya elimu ya juu kuendana na mahitaji na kuwezesha watoto wa maskini kupata elimu mpaka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa mapato yote ya Serikali kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kufuta utaratibu wa *retention* uangaliwe kwa mapana. Lisipoangaliwa vizuri kuna taasisi na mashirika ya Serikali yataathirika sana – mashirika yanayojiendesha yenyewe bila ruzuku ya Serikali na yanalipa kodi zote stahiki na asilimia zilizoelezwa na Serikali mfano mashirika ya uhifadhi mfano *TANAPA, Ngorongoro, TAWA, TFS*, *NHC*.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla sijachangia mpango huu wa Serikali naunga mkono hoja. Nimpongeze Waziri wa Fedha na Naibu wake pamoja na watumishi wote wa Wizara ya fedha walioshiriki katika kuandaa mpango huu ambao unalenga katika kuinua uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia mpango huu mambo mengi yaliyomo ndani mpango huu yana nia ya kuinua uchumi wa nchi yote kwa leo. Nitajikita kwenye maeneo machache ambayo yanahitaji usimamizi na mkakati wa hali ya juu. Maeneo hayo ni Sekta ya Kilimo cha Umwagiliaji, Sekta ya Utalii pamoja na kutazama upya aina ya kodi mbalimbali zinazotozwa na Mamlaka ya Mapato (*TRA*) hususan kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo ni muhimu sana ikisimamiwa kwa karibu na kwa njia za kisasa ni eneo ambalo kwa kiasi kikubwa itachangia pato la Taifa letu. Eneo ninalosisitiza hapa ni kilimo cha umwagiliaji, nchi yetu imebahatika kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba, pia na mabonde mengi. Je, Serikali haioni umefika muda badala ya kutegemea kilimo tulichozoea cha kutegemea mvua, tutumie fursa za mabonde yetu kuzalisha mazao mbalimbali ya chakula na biashara. Aidha, kupitia mpango huu tunaweza kuchimba mabwawa makubwa pamoja na visima virefu ili kilimo chetu kisitegemee mvua tu. Ni muhimu sana kwani ni Mataifa mengi yameweza kupiga hatua, aidha tatizo la vifaa la kila wakati litatuliwa

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa Waziri wa Fedha alitazame katika kuinua pato la nchi yetu ni Sekta ya Utalii. Nchi yetu ina maeneo mengi ya utalii kwa maana mbuga mbalimbali za utalii, lakini bado sekta hii inachangia kiasi kidogo si kwa kiwango ambacho kama Wizara husika ingekuwa na mkakati na mpango thabiti, Taifa lingefaidika sana. Bado naamini hatujaweza kutangaza sekta hii ipasavyo, aidha, gharama au tozo tulizoweka

katika utalii zimepunguza ujio wa watalii ni vema tukubaliane wenzetu wa nchi jirani nao wana fursa kama yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbuga zetu zina wanyama wengi, hivyo tuweke mkazo katika eneo hili, niipongeze Serikali kwa kununua ndege mpya nikiamini zitasaidia ujio wa watalii ambao awali walikuwa wakifikia nchi jirani. Niiombe Serikali yetu pia iboreshe huduma katika mahoteli ambapo watalii wanafikia, pia kodi kwa watalii ipunguzwe kwani imepunguza idadi ya watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kutoa mchango juu ya kodi mbalimbali zinatozwa na Mamlaka ya Mapato *(TRA)*, nchi yoyote duniani haiwezi kusonga mbele bila ya kodi; mipango yote ya maendeleo inategemea kodi hata nchi yetu bila ya kodi haiwezi kusonga mbele. Naunga mkono suala la kodi ila nina mawazo tofauti juu ya utitiri wa kodi na juu ya ukadiriaji wa kodi, eneo hili lina matatizo kwani ukadiriaji huu hauna uhalisia, aidha watumishi wote wa *TRA* wanakosa njia iliyo sahihi ya ukadiriaji kwani wananchi wengi wamekuwa wakilalamika sana kukadiriwa kiwango kikubwa ambacho hakilingani na uhalisia wa biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ione njia nzuri ya kupitia *TRA* ili ipunguze malalamiko haya. Wananchi wengi wana nia ya kulipa kodi, tusiwakatishe tamaa wananchi wote nikiamini kabisa bila kodi hakuna uhai. Ni imani yangu Mheshimiwa Waziri na Serikali watayapokea maoni haya.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Waziri wa Fedha ambaye anajua vizuri uchumi wa nchi; nampongeza Naibu Waziri kwa utendaji mzuri, napongeza juhudi za Serikali kwa kutuletea Mpango mzuri wa Maendeleo 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango nitachangia ukurasa 13, Ujenzi wa Barabara ya Mwendokasi katika Jiji la Dar es Salaam. Naomba Serikali iboreshe mpango wake wa kuendesha mabasi yaendayo kasi kwani usafiri huo ni bora sana na ni msaada mkubwa sana kwa wananchi wetu. Sasa mradi wa mabasi yaendayo kasi yaelekee *phase II* kutoka Kariakoo kwenda Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini. Kituo hiki ni muhimu sana na Serikali sasa imekamilisha malipo ya fidia na kuanza utaratibu wa ujenzi wa ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kituo hicho kikaendelea kuwepo na kifanye kazi kwa maslahi ya Watanzania na wale wengine wageni wanaotoka nchi za jirani kuja kununua bidhaa zao Kurasini, lakini pia, Kurasini kutakuwa ni mji mzuri wenye maendeleo na mvuto mkubwa wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *flyover TAZARA*- Serikali iendelee na mpango wake wa ujenzi wa barabara za juu kwa eneo la *TAZARA* ni jambo la maana sana. Katika kupunguza msongamano katika barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze mtaji Benki ya *TIB* ili iongezee uwezo wa kukopesha wafanyabirashara, wajasiriamali kwa kuanzisha miradi mbalimbali ikiwemo viwanda badala ya kutumia Mifuko yetu ya Pensheni katika maeneo mengi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo, Mpango uelekeze kwenye kukiendeleza kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Pembejeo za kilimo ziwafikie wakulima kwa wakati. Wananchi waweze kuboresha kilimo na kupata mazao mengi ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge;* ni vyema reli iwepo kwa kuwa itatusaidia sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanda ni vyema kabla hatujajenga vipya kwanza tuangalie vile viwanda vya zamani. Tuangalie ni nini kilitufanya tuanguke na tuvifufue angalau vichache, pia viwanda vipya vianzishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Waziri kaza buti, Hapa Kazi Tu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, *single customer territory* imeanza utekelezaji wake mwaka 2014 Januari, kwa nchi za Kenya na Uganda na kwa Tanzania imeanza rasmi Julai, 2014. Changamoto mpaka sasa kwenye himaya hii ya forodha ya pamoja ni kwamba kati ya nchi zote tano za Afrika Mashariki ni Tanzania na Rwanda pekee ambazo zinatekeleza makubaliano haya kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uganda na Kenya bado wanakusanya kwenye baadhi ya bidhaa tu, huku Burundi ikiwa haijawahi kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana hii ya *SCT* ni njema sana kama itakuwa inatekelezwa na nchi zote wanachama. Ndio maana nchi ya Congo DRC imeomba iingizwe katika utaratibu huo. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa nchi zote zilizoridhia *SCT* zinatekeleza ili kudhibiti unyonyaji wa mapato kutoka kwa baadhi ya nchi ambazo hazitekelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali yetu iwasiliane na Serikali ya Jamhuri ya *Mozambique* ili kupitia bandari ya Beira pia utaratibu huu uweze

kutumika. Hii itasaidia kuwadhibiti wale wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za *SCT*; kudhibiti ukwepaji kodi kupitia mizigo ya *transit*, hapo awali kabla ya utaratibu huu mizigo mingine ilikuwa inashushwa ndani ya nchi yetu, hivyo kuwepo na ukwepaji kodi na kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindani hafifu wa kibiashara, kwa sababu wafanyabiashara hasa wakubwa walikuwa *favored* na utaratibu huo, kuliko wajasiriamali wadogo. Wasafirishaji wa mizigo kwenda Congo wamekuwa wakifanya *trip* nyingi zaidi baada ya utaratibu huu wa *SCT* kwa kuwa hakuna usumbufu, tofauti na ilivyokuwa huko nyuma; ilikuwa inawagharimu wasafirishaji zaidi ya miezi miwili hadi minne kusafirisha na ku-*clear* mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; ufufuaji wa zao la Mkonge katika Mikoa ya Tanga, Morogoro na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani, zao la mkonge limepanda thamani sana duniani na kati ya mashamba 56 yaliyopo nchini mashamba 37 yapo Mkoa wa Tanga na mengi yamekuwa mapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari, Bandari ya Tanga ifufuliwe na kupanuliwa ili iende sambamba na ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda–Ziwa *Albert* hadi katika Bandari ya Tanga. Hii itasaidia pia usafirishaji wa mizigo kutoka Tanga Tanzania hadi Uganda na nchi jirani ya Sudani Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda, Kiwanda cha *Afritex* kilichokuwa kina uwezo wa kuajiri wafanyakazi 2000, kimefungwa na kipo Mkoani Tanga kikitengeneza aina mbalimbali za bidhaa za nguo. Serikali inakosa mapato, lakini pia ajira inapungua kwa kiasi kikubwa. Ahsante.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya maskini – Mpango ueleze namna ambavyo wilaya maskini zitasaidiwa kutoka kwenye lindi la umaskini kama ilivyotangazwa kwenye Bunge la Bajeti 2016. Wilaya ya kwanza ni Kakonko ikifuatiwa na Biharamulo. Wilaya hizi zisaidiwe kwenye kilimo (pembejeo za bei nafuu kwa wananchi wote), ufugaji, mabwawa ya samaki, viwanda, vidogo vidogo vya kuchakata mihogo, ujasiriliamali na elimu yake. Wilaya hizi zisipopata *boost* ya kiuchumi zitaendelea kurudisha nyuma uchumi wa nchi *(overall)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara; zipo barabara za Kidahwe hadi Nyakanazi zitengewe fedha za kutosha. Aidha, ikumbukwe Manyovu-Kasulu hadi Nyakanazi, pia barabara ya Sumbawanga-Mpanda-Nyakanazi, kwa nini zisitajwe hivi:-

(i) Manyovu-Kasulu-Kibondo-Kabingo (mpya)
(ii) Sumbawanga-Mpanda-Uvinza-Kasulu (mpya)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyakanazi-Kabingo inaendelea, bajeti iwepo, Kidahwe-Kasulu-Nyakanazi iendelee kutengewa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pato la Taifa; hali ya pato la Taifa kukua litafsiriwe kwenye hali nzima ya maisha ya Watanzania. Haiwezekani pato la Taifa limekua, wananchi wanabakia maskini, karibu Watanzania milioni 20 ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tozo na Kodi; kumekuwa na tozo nyingi kwa wajasiriamali na shughuli zao. Mfano tozo za mazao kama korosho, kahawa na kadhalika wajasiriamali wadogo kama bodaboda wametozwa ushuru wa *parking; parking fee*. Kodi mbalimbali za bandarini zipunguzwe ili zivutie wawekezaji wengi kuja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wamezuiliwa kukata leseni za biashara za halmashauri na kuamriwa wakalipe mapato *TRA* jambo ambalo limewafanya washindwe kufanya biashara hivyo kupotea kwa mapato ya halmashauri/Serikali Kuu. Mfano mfanyabiashara mwenye mtaji wa laki mbili anataka kufungua biashara ndogo anaenda *TRA* anatakiwa alipe kodi ya laki moja nukta tano kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru juu ya mapato kuongezeka; mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na wafanyabiashara. Hali ya kisasa iwe nzuri isiyodhibiti demokrasia nchini. Utulivu wa kutosha usioleta shaka/hofu kwa wawekezaji. Mfano, Serikali ya CCM na kuwakataza wapinzani kufanya mikutano ya hadhara na hivyo nguvu kubwa kutumika kudai demokrasia hiyo. Hili linawaweka wawekezaji katika hofu na wasiwasi, kuleta mitaji inaleta mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira rafiki kibiashara zipunguzwe zinazoleta urasimu wa kusajili biashara na kufanya biashara. Mfano, Mfanyabiashara haruhusiwi kufanyabiashara kwa muda hata wa miezi mitatu ndipo aanze kulipa kodi/ushuru. Vivutio vizuri vitawezesha wafanyabiashara wengi kuingia na hivyo Serikali kupata mapato makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari; ni kosa kubwa kuwa na bandari tatu kubwa nchini halafu nchi inakuwa maskini. Bandari ya Dar es Salaam isiwekwe kodi nyingi zisizo na tija kwa wafanyabiashara na zinazosumbua wananchi. Bandari ifanye *operations* zake *electronically* ili kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini kama vile malipo *all financial transactions* na zionekane kila upande *TRA*- Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi, Sekta iimarishwe ili kuuza samaki wengi ili kuweza kuuzwa nje na ndani ya nchi. Mfano, zinunuliwe meli za uvuvi wa baharini na maziwa kama vile Victoria na Tanganyika, meli zivue samaki wanaoshindikana kuvuliwa kwa sababu ya *poor fishing gears*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; mazao ya biashara na chakula yalimwe kitaalam kwa kutumia mbolea na mbegu bora. Kilimo cha umwagiliaji kisisitizwe ili kuepuka njaa kwa sababu ya ukame. Iteuliwe mikoa/wilaya za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi; nchi yoyote yenye gesi asilia haitakiwi kuwa maskini, tuuze gesi kwa wananchi kwa bei nzuri *affordable* ili kuokoa misitu yetu itakayotuletea mvua. Tuuze gesi nje ya nchi kupata fedha za kigeni tuuze umeme unaotokana na gesi kwa nchi jirani.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Pamoja na kuleta Mpango wa Maendeleo wa 2017/2018 napenda kujua ni kwa kiasi gani mpango wa 2016 uliweza kutekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uchumi kwa maelezo ya Waziri inaimarika, lakini kwa uhalisia hali ni mbaya katika sekta nyingi. Mfano benki nyingi za biashara mikopo imeshuka na riba ni kubwa hata vyombo vya habari vimenukuliwa vikisema hayo. Baadhi ya benki mfano *CRDB* imepata hasara ya shilingi bilioni mbili na zaidi. Wafanyabiashara wanashindwa kurudisha mikopo na wengi wao hawaagizi tena bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Serikali yenyewe kwa mwaka 2016 akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola milioni 3,870.3 na hizi zinaweza kuagiza bidhaa nje kwa miezi minne. Je, baada ya miezi minne Serikali imejipangaje? Thamani ya *Tanzanian shilling* inazidi kushuka na deni la Taifa linazidi kukua, hii ni hatari sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda; Serikali imekuwa ikiimba wimbo wa nchi itakuwa ya viwanda, je, kuanzia wakati wa kampeni hadi sasa ni viwanda vingapi vimeongezeka? Bila kuwa na umeme wa uhakika na kilimo cha kibiashara ili wazalishe, viwanda hivyo vitakuwa ni vya nini? Tulikuwa na kiwanda cha *General Tyre* Arusha kilichobinafsishwa na Serikali ikakichukua na imekuwa ikitoa ahadi zaidi ya miaka kumi kiwanda kitaanza kazi lakini mpaka leo hakuna uelekeo. Ikumbukwe kiwanda kile kilikuwa kinazalisha matairi bora na kutoa ajira nyingi na Serikali kupata mapato. Nilitegemea Serikali ingetueleza ina mpango gani na kiwanda kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii; hii ni kati ya sekta inayochangia katika pato la Taifa kwa zaidi ya 17%, lakini kwa sasa Serikali inaelekea kwenda kuua kabisa utalii katika nchi yetu. Kitendo cha Serikali kuongeza *VAT* katika

utalii ukizingatia tayari sekta hii ina zaidi ya kodi/leseni 31 zinazolipwa, utalii wetu umekuwa ni ghali sana. Sipingi kulipa kodi lakini tupandishe kwa taratibu. Baadhi ya nchi za Ulaya sheria zao huwezi kupandisha bei zaidi ya 10%. Hivi hawa tembo, simba, twiga na kadhalika kutoka Tanzania tumewaongezea thamani gani wawe na bei kubwa kuwaona kuliko wale waliopo nchi jirani ya Kenya ambao hawalipiwi kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetaka kujua hivi Wizara ya Fedha inapoandaa Mpango ni kwa kiasi gani wanashirikiana katika mawazo ya kupanga hii mipango na Wizara nyingine? Hivi inapoanzisha viwanda ni kwa kiasi gani wameandaa wataalam, malighafi na kadhalika?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, malengo makuu *(objectives)* ni matatu badala ya manne. Lengo la nne lililotajwa kama ufuatiliaji si sawa, hii ni 4001 ya kufuatilia utendaji kazi ili kufuatilia malengo tajwa, *page one*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/2018 kunakosekana *the main priorities, page* 18-22 ya hotuba ya Waziri. Maeneo tajwa ni 39, ni mengi mno kuweza kufanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *the concept* (dhima) ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Hali halisi ya kiuchumi, je, tumefanikisha kwa kiasi gani dhana ya kilimo ni uti wa mgongo? *Focus* ya uchumi wa viwanda ni ipi? Ni rasilimali gani zinalengwa kwa aina gani ya viwanda? Kuna rasilimali watu inayolengwa maalum kwa aina gani za viwanda? Je, ni masoko gani yanayolengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango unatakiwa kuainisha *main strategies* zitakazowezesha kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi. Mfano, ni maeneo gani makuu matatu Serikali inatakiwa ku-*focus into* ili kusukuma maendeleo katika sekta nyingine?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, ukurasa wa 52, 6.3(e), nashauri iongezeke mafuta ya mawese. Tanzania inaagiza mawese tani 600,000 kwa mwaka inayogharimu dola milioni 450 ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma unaweza kuzalisha zaidi ya kiwango hiki iwapo wananchi watahamasishwa kulima michikichi na kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vya mazao ya mawese. Manispaa ya Kigoma inahamasisha mfumo wa *one family, 1hc* ili kuzalisha tani 80,000 za *CPO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho, *page* 52 ya mapendekezo, barabara hii inapaswa kuitwa Manyovu-Kasulu-Kibondo-Kabondo na siyo kama ilivyoandikwa. Nashauri muwasiliane na Wizara ya Uchukuzi maana kuna mabadiliko kwenye jina la mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi, *page* ya 18, tafsiri ya Reli ya Kati imetolewa vizuri. Ni sawa sasa, hii ndiyo tafsiri sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 43, kilimo cha mpunga. Katika Mkoa wa Kigoma, Manispaa ya Kigoma-Ujiji kuna mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika *delta* ya Mto Lwiche. Mradi huu unatarajiwa kufadhiliwa na Mfuko wa Falme ya Kuwait *(Kuwait Fund*) kwa gharama ya dola milioni 15. Hata hivyo, Serikali ya Tanzania inapaswa kutoa fedha za *feasibility study* na *detailed design*. Naomba mradi huu mkubwa sana wa hekta 3,000 uingizwe kwenye orodha ya ukurasa wa 43. Pia naomba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umalizike ili tuweze kupata mradi huu ndani ya 2017/2018.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya hatukuweza kuona *performance report* ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha tulionao. Endapo ningepata fursa ya kuona ripoti hiyo, kungekuwa na fursa ya kusema yafuatayo kwa takwimu zaidi. Kuna dalili nzuri kwenye viashiria vya uchumi mkubwa *(macro economic indicators),* lakini kuna kila dalili kuwa tunaporomoka kwenye *micro economic indicators.*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwamba mpango wa 2017/2018 pia hauonekani kuzingatia upungufu huu. Mfano, tungeweka nguvu kubwa kwenye viwanda vya kiwango *(size)* ya kati badala ya vikubwa ingekuwa rahisi kuweka kichocheo kwa sekta ya kilimo kwenye mikoa tofauti tofauti kwa kuzingatia zao la kilimo linalopatikana eneo husika. Tuwe na mtiririko *(sequence)* sahihi wa nini cha kufanya. Kilimo kifunganishwe na upatikanaji wa umeme na maji, soko la ndani ya Tanzania na soko la Afrika Mashariki litatosha kwa awamu hiyo ya kwanza. Hii pia itaongeza wigo wa walipa kodi, miundombinu (ndege, meli, reli) ili kutanua soko nje ya Tanzania na Afrika Mashariki.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kimepungua hadi 2.7% wakati malengo yalikuwa kikue kwa 6%. Hii inaleta wasiwasi hasa kwa wanawake ambao ni wengi katika sekta hii. Sekta hii ni muhimu sana kwani wanawake ni wadau wakubwa sana na mpango huu umejikita kwenye viwanda, hivyo kilimo kiwekewe kipaumbele cha 100% ili kiakisi na viwanda na wakati huo kitaleta tija kwa viwanda vyetu. Maskini wengi wako vijijini ambapo wengi ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei; mwaka 2011 mfumuko wa bei ulikua kwa 19.8%, mwaka 2015 ulishuka kufikia 5.6%, hii ilikuwa sawa lakini kwa sasa imefikia tena 19% na kuleta mkanganyiko kwa jamii maskini. Mfumuko wa bei una madhara mengi kwa jamii hasa wanawake. Nashauri mfumuko ubaki kwenye tarakimu moja kwa kadri inavyowezekana na ikibidi wanawake wakingwe kwa gharama yoyote. Iwepo mipango mahsusi ya kupeleka maendeleo kwa wanawake kwenye vikundi vyao mbalimbali ili kuweza kuzalisha mali kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu kazi ya utaalam; kuna upungufu mkubwa wa takwimu zilizochambuliwa kwa mtazamo wa kijinsia. Maeneo ya miradi mikubwa ya kiuchumi kama miradi ya Mchuchuma na Liganga ingepewa watu mahsusi na kuzingatia jinsia kutoa wataalam.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri wa Fedha na timu yake kwa kutuletea mapendekezo mazuri ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018. Naomba kuchangia suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu. Naomba niishauri Serikali yangu Tukufu tufungue viwanda vidogo vidogo ambavyo malighafi zake zinapatikana hapahapa nchini hasa kwa wakulima wetu. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeongeza mnyororo wa thamani katika mazao yetu pamoja na kuongeza ajira kwa wananchi wetu. Pia pembejeo zifike kwa wakati kwa wakulima wetu na pia wakulima wa mbogamboga na matunda nao wapewe pembejeo za ruzuku kwani wakulima hawa wanachangia sana Halmashauri zetu kwa kulipa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali yangu Tukufu kuwe na mkakati maalum kuhusu suala zima la maji. Suala la maji lingefanywa kama suala la madawati lilivyofanywa tungemaliza tatizo la maji kabisa hapa nchini na kusahau kabisa tatizo hili la maji. Hili ni tatizo kubwa sana hapa nchini na kila Mbunge aliahidi kutatua tatizo hili. Naamini kabisa kama tatizo hili halijatatuliwa, Wabunge wengine tutashindwa hata kurudi majimboni kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana katika suala zima la huduma ya afya upande wa dawa pamoja na kutokuwa na vituo vya afya na zahanati hasa wananchi wanaoishi vijijini wana hali mbaya sana. Sisi kama Wabunge tumehamasisha suala la *CHF* na wanaelewa na kuchangia, lakini wanapofika hospitali wanakuta hakuna dawa zaidi ya kuambiwa wakanunue dawa katika maduka binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili na utalii, naomba niishauri Serikali yangu Tukufu kuhusu suala zima la misitu yetu kuchomwa moto kila siku hali

ambayo husababisha uoto wa asili kutoweka na maeneo ya misitu kubaki vichaka. Nashauri Serikali inunue ndege kwa ajili ya kuzima moto katika misitu yetu inayopata majanga ya moto hasa ikizingatiwa jiografia ya misitu mingi kuna maporomoko makubwa ambayo watu hawawezi kuzima moto unapotokea. Pia maeneo yote yaliyoungua Serikali ipande miti ili kurudisha mandhari ya msitu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na unyanyasaji mkubwa sana hasa kwa mama ntilie, bodaboda, akinamama wanaouza mbogamboga na matunda pamoja na watu wenye ulemavu. Halmashauri zetu hasa Wakurugenzi wanawatoza ushuru watu hawa bila huruma pamoja na kuwatolea maneno yasiyofaa, kubwa zaidi kuwaongezea ushuru kila uchao. Niiombe Serikali yangu Tukufu iwaonye Wakurugenzi hawa ili wasiendelee kuwanyanyasa wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, sisi Wabunge tunapowaambia Wakurugenzi hawa wanatudharau na kutuita wanasiasa hatuna lolote. Kwa hiyo, niishauri Serikali yangu sisi Wabunge tunapoleta matatizo ya Wakurugenzi, tunaomba yafanyiwe kazi haraka na ikiwezekana mhusika achukuliwe hatua, zaidi ya hapo, majimbo yetu yatakuwa hatarini kuyakosa. Kibaya zaidi Wakurugenzi wengi ni wanasiasa pamoja na hayo wanarubuniwa na baadhi ya wanasiasa walioshindwa ili amharibie Mbunge ambaye yupo madarakani ashindwe au aonekane hafai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mazao ya biashara kama pamba, kahawa, korosho, tumbaku pamoja na katani. Mazao haya yamesahaulika wakati ndiyo yanatoa pato kubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali yangu Tukufu kuhusu *TRA*. Mzigo unapoingia kutoka nje huwa unatozwa ushuru/kodi, ukitoka bandarini ukifika sehemu kama Kariakoo, *TRA* tena wanachukua kodi, ukipakiwa kwenda mikoani *TRA* wanachukua kodi, mwisho wa siku biashara hii inamfikia mtumiaji kwa bei ya juu. Kwa hiyo, niishauri Serikali ipunguze mzigo huu wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la *motor vehicle licence,* huwa inakatwa au inalipiwa kila mwaka lakini kuna watu wana magari ambayo yameharibika kwa muda mrefu mpaka limefikia kuchakaa mtu anaamua kuliuza kama skrepa. Cha ajabu mtu huyu anapofika *TRA* kwa ajili ya kuripoti ili arudishe kadi ya gari anaambiwa unadaiwa lazima ulipe, hii inasumbua sana watu wengi na ukizingatia walio wengi hawana uwezo tena. Kwa hiyo, niishauri Serikali iliangalie suala hili upya ili wananchi wetu ambao hawana uwezo wasije wakachukua maamuzi ambayo hawajayapanga na kama kuna uwezekano ifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimtakie Waziri afya njema pamoja na timu yake kwa ujumla.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018. Pili, napenda kutoa mapendekezo au ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo liangaliwe kwa upana zaidi ili kumsaidia mkulima kupitia vyama vya ushirika waweze kusaidiwa kwa urahisi zaidi kwani takribani asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Hivyo, ili kuwahudumia vizuri inapaswa kuangalia chombo chao kinachowaunganisha kupitia vyama vyao vya ushirika vya mazao ili aweze kupata huduma kwa urahisi zaidi wakiwa pamoja kama elimu ya kilimo biashara, matumizi bora ya mbegu za mazao yao, kupata mikopo kupitia mabenki kwa kutumia vyama vya ushirika na mashamba yao kama dhamana ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pembejeo za kilimo zipatikane kwa urahisi na kwa wakati ili wakulima waweze kuendana na msimu wa kilimo ulivyo katika maeneo mbalimbali. Vilevile aina ya pembejeo kwa kila eneo izingatiwe zaidi kulingana na udongo wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa maghala bora ya kuhifadhia mazao ni muhimu katika maeneo ya vijijini na Hifadhi ya Taifa ya Chakula kwa kuwa baada ya kuvuna vyakula hivyo ni vyema vikahifadhiwa vizuri kwa matumizi ya kipindi kijacho ambapo uzalishaji hamna. Ni vyema basi Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2017/2018 ukazingatia ujenzi wa maghala haya kwani kwa mfano maghala ya Hifadhi ya Taifa ya Songea mahindi mengi yapo nje ambapo yana hatari ya kuharibika katika kipindi cha mvua, asilimia 50 ya mahindi yamehifadhiwa nje maghala yamejaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha ushirika na mazao ni vyema basi Mpango wa Maendeleo wa Taifa ukatilia mkazo wa kuimarisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kuiwezesha kifedha. Ni vyema Tume hii ikaimarishwa kiutaalam katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Halmashauri za Wilaya kwa kuongeza watumishi wenye uwezo wa kusimamia ushirika na kurudisha imani ya wakulima kuamini vyama vyao vya ushirika. Ni vyema Makamishna wa Tume ya Ushirika wakateuliwa ili kuipa nguvu Tume hii kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuimarisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ni vyema kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO)* kwa kukiongezea uwezo kifedha na watumishi ili wapate muda wa kukagua vyama vya ushirika kila mwaka kwa maendeleo ya ushirika na

wakulima wetu. Karibu wakulima wote wa Tanzania kwa njia moja au nyingine wanahudumiwa na ushirika wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko la mazao yetu, ni vyema Serikali ikasisitiza kuuza mazao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kama inavyofanyika katika mikoa inayolima korosho ambapo mafanikio makubwa yanaonekana kwa wakulima wa Mkoa wa Lindi na Mtwara na imehakikishia Halmashauri zetu kuwa na uhakika wa kupata ushuru wa mazao kupitia mfumo huu. Mkulima anakuwa na uhakika wa kupata malipo yake ya mazao kupitia mfumo rasmi wa kiuchumi. Naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa mazao yote ya biashara na chakula kuingia katika mfumo huu kwani unaruhusu wanunuzi kushindana katika bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu *Annual Motor Vehicle License*. Nashauri Serikali katika Mpango wake iangalie namna ya kurekebisha sheria hii ili isiwaumize wanaomiliki vyombo vya moto na wale wanaouza vyombo vya moto. Aidha, Serikali iweke katika Mpango wake namna ya kusamehe malimbikizo ya kodi hiyo kwa watu waliouza vyombo vya moto kama pikipiki halafu waliouziwa hawakubadilisha umiliki.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilikutana na wadau mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara wakubwa wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ambapo walieleza kwamba mizigo imepungua kwa kiasi cha asilimia 42 na mingi ni ile inayopita kwenda nje ya nchi hususan Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo ya wadau kupungua kwa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kumesababishwa na kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa huduma zinazotolewa katika mizigo au bidhaa inayopitia bandari hiyo kwenda nchi jirani *(VAT on auxiliary services on transit goods)* za Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda na Uganda. Kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika tozo mbalimbali za bandari kunaongeza gharama ya huduma na biashara katika Bandari ya Dar es Salaam na kupunguza ushindani na bandari nyingine kama zile za Nacala, Beira, Mombasa na Durban. Hivyo basi, ili tuweze kufikia uchumi wa kati, ifikapo mwaka 2025 ni lazima tuiangalie bandari yetu na pia tupunguze ushuru ili tuweze kuzalisha mapato mengi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018, pamoja na kutofahamishwa rasmi mafanikio na upungufu wa utekelezaji wa mwaka 2016/2017 hadi sasa ili kutupa picha kwa mapendekezo ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka asilimia 40 ya bajeti kwa maendeleo lakini hadi sasa fedha hizo hazijafika kwenye Halmashauri zetu na kupelekea kuzorota kwa utekelezaji wa maendeleo kwenye huduma za jamii kama afya, maji na umeme. Nashauri katika kipindi hiki, kabla ya kufika mwaka 2017/2018, kuboresha mwenendo wa usambazaji wa fedha za maendeleo kwa angalau asilimia 75 kwa miradi ya maji, afya na umeme kwani huduma hizi zinawagusa wananchi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kusonga mbele na kuendelea kuweka mazingira ya malalamiko kwa baadhi ya viongozi na wananchi kwa maendeleo yao kiuchumi, nashauri Serikali kujikita zaidi kujenga mikakati ya kufufua mazingira bora ya kilimo, biashara na fursa za ajira binafsi kwa vijana wetu. Pia kuwepo na uratibu wa malalamiko na kuyapanga kwa utekelezaji ili kuepusha malalamiko kujirejea ndani ya mipango yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mapendekezo haya ya Mpango wa mwaka 2017/2018.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua katika mwelekeo wa Mpango huu, juu ya hoja ambayo tulijadili sana mwaka jana wakati wa Mpango wa Serikali 2016/2017, nayo ni kuhusu Mahakama ya Mafisadi. Suala hili limekuwa kimya nashangaa kwa nini wakati mafisadi wapo, wengine wamestaafu, ni kwa nini kwenye mwelekeo wa Mpango huu wa 2017 suala hili la Mahakama ya Mafisadi halipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kujua juu ya mwelekeo wa Mpango huu kuhusu ujenzi na ukarabati wa Mahakama Tanzania na hasa katika Jimbo langu la Mtwara Mjini Mahakama ni chakavu sana na hazikidhi haja. Je, ni lini suala hili litatatuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya korosho ni muhimu sana katika kuinua uchumi wa nchi hii hasa Mikoa ya Kusini. Naomba kujua ni lini Serikali itafufua Viwanda vya Korosho, Mikoa ya Kusini ili kuinua uchumi kwa kuongeza thamani ya korosho na bei?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya gesi na mafuta ni muhimu sana kuletwa Bungeni ili ijadiliwe kabla ya kuingia kwenye mikataba hii. Kwa muda mrefu mikataba imekuwa haina tija kwa Taifa hili na mapendekezo ya Mpango huu suala hili halipo, naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi ni muhimu sana maana kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi hapa nchini. Kwa mfano, kumekuwa na utaratibu wa Serikali kuchukua ardhi kwa wananchi na kukaa muda mrefu bila kulipa fidia kwa mfano Mtwara Mjini tangu mwaka 2012 mpaka leo *UTT* ilipima viwanja Mji Mwema ambako ni mashamba ya wananchi hawajalipwa. Hili ni jambo la hatari sana, naomba majibu tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia elimu ndiyo msingi wa maendeleo wa nchi yoyote ile duniani. Sera ya Elimu bure iangaliwe upya ili shule ziweze kujiendesha. Shule zinapata *OC* ya Sh. 27,000/= tu kwa mwezi itaweza kuendesha ofisi na shule kweli? Ni jambo la ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya elimu ya juu iangaliwe upya ili kila Mtanzania mwenye sifa ya kusoma elimu ya juu apate mkopo kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi. Kunyima mikopo watoto maskini kama ilivyo kwa mwaka huu ni jambo hatari sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana miundombinu ya barabara kama vile reli kutoka Mtwara Mjini hadi Mchuchuma na Liganga kwenye chuma na makaa ya mawe iwekwe kwenye Mpango wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, utanuzi wa Bandari ya Mtwara ufanyike kwa haraka ili kuinua uchumi wa nchi yetu. Bandari hii haihitaji gharama sana kwa kuwa ni *natural harbour*, Serikali itenge fedha haraka kwa ajili ya utanuzi wa bandari hii. Sijaona suala hili kwenye mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo barabara ya Mtwara - Newala imetengewa fedha lakini mpaka sasa hata robo kilomita haijatengenezwa, ni jambo la ajabu sana. Naomba barabara hii ianze kujengwa tafadhali.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kuunga mkono hoja kwa kuipongeza Serikali ya CCM chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Magufuli, kwa kazi kubwa wanayofanya ya kurejesha nidhamu na uwajibikaji katika nchi yetu. Japokuwa hali hii kwa kuwa ni ngeni kwa wengine na kinyume cha matazamio yao wameitafsiri katika namna hasi. Ombi langu, tuendelee hivi hivi huku tukibaki katika lengo letu la kumkomboa Mtanzania kutoka kwenye lindi la umaskini, ujinga na maradhi na kuwapeleka kwenye nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijikite kwenye hoja yangu. Bila kusahau naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni mdau wa elimu wa shule binafsi. Naomba nielekeze mchango wangu kwenye ushirikiano kati ya Umma na Binafsi *(PPP)* katika uwekezaji kwenye sekta zote muhimu nchini ikiwemo elimu, afya, viwanda, miundombinu na kadhalika. Nafahamu kuwa Serikali yetu sikivu ya CCM ina nia njema sana katika hili hivyo naomba nitoe ushauri ufuatao:-

(i) Kubainisha wazi na bayana majukumu ya kila upande katika utekelezaji wa sera ya *PPP* katika sekta ya elimu (utungaji wa sera, sheria, miongozo, uchangiaji wa gharama za elimu, usimamizi wa taasisi za elimu, upimaji na udhibiti ubora);

(ii) Kuwa na mifumo imara na endelevu ya mawasiliano *(dialogue structure)* baina ya pande zote mbili ili kupeana taarifa za mara kwa mara na uzoefu mbalimbali wenye tija kwa maendeleo ya nchi; na

(iii) Kuwe na mifumo imara yenye kujengeana uwezo baina ya pande zote mbili kwa vile kila upande unacho cha kujifunza kutoka kwa mwenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Serikali itakapofungua milango katika *PPP* ni hakika tutaona mafanikio na mabadiliko makubwa ya kiuchumi ndani ya muda mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri pia Serikali kuweka vipaumbele vinavyotekelezeka. Mpango huu ni mzuri lakini umekuja na vipaumbele vingi sana. Tukiendelea hivi tutabaki kupapasa tu na hatutafika tuendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo yetu ya kodi si rafiki hali inayopelekea kutishia kuongezeka hali ya rushwa hasa katika chombo chetu cha kodi (*TRA)*. Kuwe na mazingira rafiki na *dialogue structure* baina ya *TRA* na mlipa kodi badala ya vitisho na kuuza kwa mnada mali za wafanyabiashara kwani kwa kufanya hivyo Serikali inakosa pesa na wale wafanyabiashara wanakuwa wamefilisika na mwisho tunaishia kuumia kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu ina mpango wa kutupelekea kwenye Tanzania ya viwanda, basi niishauri Serikali iweke nguvu kubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji ili viwanda vyetu viweze kufanya kazi kwa kipindi chote cha mwaka. Endapo hatutawekeza kwenye kilimo cha kisasa ambapo asilimia 80 ya Watanzania ndiyo wahusika wakuu katika hili, ni bayana hatutaweza kumwondoa huyu Mtanzania maskini kwenye lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe ushauri wangu kwa Wizara ya Afya. Ni dhahiri kwamba ni pale tu watu wetu watakapokuwa na afya njema ndipo tutakapoweza kufanikiwa katika mambo yote. Mtu mgonjwa asiyeweza kutibiwa kwa wakati hawezi kamwe kufanya uzalishaji wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie suala la ukosefu wa dawa *MSD*. Suala hili linaipeleka Serikali yetu pabaya sana. Naomba hili suala la dawa lifanyiwe kazi kwa gharama yoyote ile ili kulinusuru Taifa na vifo vya watoto na kizazi kijacho kwa kukosa chanjo za muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya ya Mpango bado hayajaweka bayana ni jinsi gani huduma ya maji zitafika vijijini ili kumtua ndoo mama wa Kitanzania. Asilimia zaidi ya 80 ya muda wa wanawake hawa wazalishaji inapotea kwenye kusaka maji usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tena kupongeza juhudi za Serikali kwa jinsi pia inavyoshughulikia suala zima la mikopo ya elimu ya juu inayotishia amani ya wapiga kura wetu. Busara ya hali ya juu itumike ili kumaliza tatizo hili na kila mhusika abaki akiwa ameridhika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niunge mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Waziri aangalie upya ongezeko la kodi eneo la mapato ya ndani. Kila mwaka tunapoongeza *budget projection* ya nchi matokeo yake kila biashara inaongezewa kodi. Kuongezeka kwa kodi katika biashara ileile, mtaji uleule na mauzo yaleyale au yaliyopungua kwa zaidi ya asilimia 50, kunasababisha wafanyabiashara wengi kushindwa kulipa kodi, kufilisika na kufukuza wafanyakazi. Serikali iangalie vyanzo vipya kama kuanzisha malipo au tozo kwenye pikipiki zote kwa kuwa wanaoziendesha siyo wamiliki wake. Kuruhusu biashara hiyo kuwa bure maana yake wapo matajiri wengi hawalipi kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali iongeze uwekezaji katika kilimo cha mazao ya biashara na chakula. Kwa kuwa kama wananchi watawezeshwa vizuri katika kilimo tatizo la fedha litapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke mpango mahsusi kuhusu maji. Mpango huo uhusishe ongezeko la Sh.50 kwenye lita ya mafuta ambayo yanaingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ulipaji wa *Road Licence* uwe tofauti na sasa na nashauri kodi hiyo iunganishwe kwenye bei ya mafuta

ambapo kila lita moja iwekewe ushuru maalum wa mafuta kulipia kodi hii. Mfano gari moja linatumia lita 20 kila siku zidisha kwa mwaka mmoja (20x360=7,200 lita). Ukichukua lita 7,200x50% tu ambayo itaongezwa kwa gari ndogo (*tax*) italipa ushuru wa Sh.360,000. Ushauri wangu hapa ni kwamba *Road Licence fixed* ikiondolewa na kuwekwa kwenye mafuta Serikali itapata pesa nyingi zaidi.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ni ya viwanda, napenda kushauri katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018, sekta ya kilimo ipewe kipaumbele cha kwanza ili kuwezesha pembejeo za kilimo kupatikana kwa wakati na itengwe bajeti ya kutosha. Kwa kufanya hivyo, wananchi watalima mashamba ya mazao ya biashara na chakula na kuwezesha viwanda vyetu kukua kwa kasi na kuinua uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo ili iweze kwenda na wakati ni lazima fedha za miradi zinazopitishwa na Bunge lako Tukufu zipelekwe kipindi husika. Angalia bajeti mwaka 2016/2017 hadi robo ya mwaka hata senti tano ya miradi ya maendeleo hazijapelekwa kwenye Majiji, Manispaa, Halmashauri na Miji Midogo.

**MHE. ANATROPIA L. THEOPIST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuondoa Milolongo ya Vikwazo Katika Uwekezaji; mlolongo wa utaratibu wa kumiliki ardhi ni gharama kubwa ya upimaji na umiliki wake. Wingi wa Tozo mbalimbali, kodi na ushuru katika biashara na huduma ziwe *harmonized* na zipunguzwe ili kuvutia zaidi uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuandaliwe vipaumbele vichache vyenye kuandaa mazingira ya uchumi wa viwanda na kuhakikisha vinatekelezwa. Kwa mfano mpango ujao uhakikishe fidia zinalipwa kwa ajili ya *EPZA* kwa angalau asilimia 60 na Miradi ya Chuma na Umeme tu, tofauti na mpango unaoonesha vipaumbele zaidi ya 16, katika nchi yenye uchumi mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele kingine kuelekezwa iwe katika kilimo ambayo ndiyo sekta inayoajiri watu wengi. Hii iende sambamba na uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya kuhudumia au kuongeza thamani katika mazao yao. Hii iende sambamba na kuongeza pesa katika taasisi zinazounda viwanda hivi kama *TEMDO*, *COSTECH*, *TIRDO* etc.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza ushirikishaji wa sekta binafsi kati maandalizi ya sera, kodi na tozo mbalimbali. Kwa mfano, kuanza kutoza asilimia 18 kwenye *auxiliary services* za bandari na katika sekta ya utalii imepelekea anguko kubwa la kibiashara kwani wahusika hawakuwa

wamejiandaa kwa mabadiliko husika, hali kadhalika wasafirishaji, *TATOA*, *TAFFA* na wadau wengine wanaohusika na upandishaji wa tozo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubunifu Katika Kuibua Vyanzo Vipya vya Mapato. Kumekuwepo na changamoto ya kodi mpaka kuwa kero. Ubambikaji wa kodi toka kwa maafisa wa *TRA* kwa lengo la kuongeza pato la ndani, ikienda sambamba na *focus* kwa makosa ya barabarani ni mzigo unaobebwa na watu wachache tu. Wizara na Serikali iwaze vyanzo vipya vya kodi ili kodi isambae na isiwe mzigo kwa watu wachache kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na mpango wa kuoanisha elimu na uchumi wa viwanda tunaouendea, kuandaa wanafunzi sambamba na tunakotaka kwenda, tofauti na ilivyo sasa ambapo wanafunzi hata wakimaliza vyuo hawana ujuzi wa kile kinachohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kusambaza Uchumi; Mipango ioneshe dhahiri yale maeneo yaliyosahaulika kama vile Mikoa ya Kagera, Mwanza, Kusini na mengineyo inayosadikiwa kuwa maskini ili ipewe kipaumbele katika miradi ya maendeleo. Hatutarajii kuona mchanga unaongezwa kwenye kichuguu, *Priority has to be to less developing regions*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na mkakati thabiti wa kutekeleza bajeti ambazo tumekuwa tukiziandaa kila mara. Kwa mfano, bajeti zimekuwa zikiletwa Bungeni lakini mpaka mwisho wa mwaka pesa zinakuwa hazijapelekwa. Tunatarajia kuona namna ambayo pesa zitapatikana na si tozo na kodi kero tunazoziona kwa sasa.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2017/2018 ni uhuishwaji wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda haviwezi kuwa endelevu kama hakutakuwa na malighafi ambazo kimsingi zinatokana na kilimo. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba bila kuwa na mapinduzi ya kilimo ndoto ya Tanzania ya viwanda haitafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu kilimo chetu bado ni duni sana kuweza kuzalisha malighafi za kulisha viwanda hivyo vinavyokusudiwa. Hivi karibuni nimetembelea Mkoa wa Songwe, wakulima wanapata shida sana kutokana na ukosefu wa pembejeo za kilimo na zile chache zinazotolewa kwa mfumo wa vocha na mawakala zinakuwa za urasimu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kwa mapendekezo ya Mpango huu wa 2017/2018 iweke bajeti ya kufanya tathmini ya idadi ya wakulima ili pembejeo zinazotolewa ziendane na idadi ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya mazao ya wakulima hayaeleweki, naomba Waziri atuambie kwa mpango huu wa 2017/2018 Serikali imejipangaje kufungua masoko ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika. Kumekuwa na changamoto nyingi sana kwenye suala la afya nchini, kwa mfano Hospitali ya Wilaya ya Vwawa inayotegemewa na Mkoa mzima wa Songwe ina upungufu mkubwa wa madawa, Madaktari na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara kuangalia huduma ya mama na mtoto, wanawake 14,695, sawa na wanawake 15 – 20 kwa siku wanajifungulia hapo. Wagonjwa 150 – 200 wanahudumiwa kama *outpatient* kila siku katika hospitali ya Wilaya. Huku idadi ya Madaktari wakiwa watatu na uhitaji ni Madaktari 23. Sambamba na watumishi 507 na uhitaji ni watumishi 1,112. Watoto wa umri wa miaka 0 – 28 wanafariki kwa siku na kupelekea idadi yao kuwa 180 kwa takwimu za 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri anahitimisha aniambie kwa mpango huu wa 2017/2018 wana mkakati gani wa kupandisha hadhi hospitali ya Wilaya ya Vwawa kuwa hospitali ya mkoa ili kuwa na bajeti ya kutosha kukabiliana na changamoto katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako majengo yaliyoachwa na wakandarasi waliojenga barabara ya Sumbawanga – Tunduma ambayo yapo kilomita tatu kutoka Tunduma Mjini eneo la Chipaka na Serikali ilitoa *commitment* ya kufanya majengo yale kuwa hospitali ya Wilaya naomba *commitment* hiyo iwekwe kwenye mpango ili kusaidia kupunguza tatizo la huduma za afya, ukizingatia kwamba Tunduma ni mpakani na watu wanaohitaji huduma ya afya ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *Black market*. Soko hili lipo ndani ya mpaka wa Zambia na wafanyabiashara wengi, zaidi ya 1000, wa upande wa Tanzania wanafanya biashara zao katika mpaka huo; hii inasababisha ukosefu wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu je, katika mpango huu wa 2017/2018, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwarudisha wafanyakazi katika eneo la Tanzania ili kuongeza mapato katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma?

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Umaskini na Athari Zake; kukithiri kwa umaskini kunazalisha uhalifu na ndio unaoondoa amani katika Taifa. Hivyo basi nashauri hatua za kuondoa umaskini zifanye jitihada za haraka ili kunusuru nchi na majanga ya uvunjifu wa amani kunakopelekea magereza kujaa wahalifu na kupelekea Taifa kubeba mzigo mkubwa wa kuwatunza wafungwa badala ya kuelekeza fedha hizo kwenye maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ongezeko la Watu. Ifikapo 2020/2026 idadi ya watu itafikia milioni 63 ambayo kama utekelezaji wa mpango wa miaka mitano hauwiani na ongezeko hilo italeta shida kwenye huduma za jamii wakati huo, hivyo ndoa za utotoni zithibitiwe kupunguza ongezeko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu. Bila elimu yenye tija Taifa haliwezi kufika kwenye uchumi wa kati. Elimu yetu haisaidii kijana kujiajiri, ni vyema kila Mkoa kukawa na *scheme for irrigation* ili kumeza ombwe kubwa la vijana wanaomaliza shule ili kuwafanya wasigeuke kuwa wahalifu katika Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya ukosefu wa ajira kwa vijana kunasababisha uhalifu kuongezeka hivyo kusababisha ongezeko la ajira za Polisi na Magereza na hivyo kuongezeka kwa matumizi kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosa ajira kunasababisha utumiaji madawa ya kulevya hivyo kuligharimu Taifa kuwatibu kwa gharama kubwa na pia kutokana na hali ngumu ya maisha na utumiaji madawa ya kulevya, UKIMWI umeanza kushika kasi sehemu nyingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tuangalie nguvukazi ya Tanzania ambayo iko asilimia 60 ya wananchi wa Tanzania kuwa mzigo kwa nchi, hivyo Taifa lijipange kunusuru tatizo hili ambalo miaka ijayo Taifa halitaweza kulimudu, hilo ni kundi la vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo, naomba iainishwe vijana wametengewa ekari ngapi ili waweze kujiajiri, pia njia ambazo Taifa litawawezesha.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchuchuma na Liganga. Suala la mradi wa madini ya Mchuchuma na Liganga limechukua muda mrefu, naiomba Serikali sasa ichukue hatua haraka ya kutatua tatizo la kulipa fidia kwa wananchi

wanaozunguka maeneo ya madini ambapo waliahidiwa kulipwa mwezi Juni, 2016, kiasi cha Shilingi bilioni 14. Pia Serikali ikamilishe mazungumzo kuhusu bei za umeme ambayo inasuasua. Wananchi wamehamasishwa kulima matunda na nafaka kwa kutegemea kupata soko la uhakika kwenye machimbo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora. Wafanyakazi/watumishi wengi wa umma wanafanya kazi kwa hofu na woga na kupoteza ubunifu kutokana na utumbuaji wa majipu ambao haufuati utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo wamekata tamaa sana kutokana na kodi zisizo na utaratibu, *TRA* inawakamua sana wafanyabiashara hao. Wafanyabishara wadogo wananyanyaswa sana kwa kutozwa kodi nyingi na hata kuua mitaji ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miundombinu. Tunapoongelea suala la Liganga na Mchuchuma lazima suala la barabara lipewe umuhimu sana. Barabara ya Njombe Mjini – Ludewa ni ya vumbi na kipindi cha mvua inaharibika sana. Naomba barabara hii iingie kwenye mpango wa 2017/2018 kwa ajili ya maandalizi ya uchimbaji wa madini ya Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji; gharama za maji zinawatesa wananchi, naomba suala la maji na gharama za maji ziangaliwe, wananchi wanaletewa bili kubwa za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine naleta mapendekezo ya masuala kadhaa yakiwemo na ya kwenye Mpango wa Serikali wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uanzishwaji wa Mkoa Mpya wa Ulanga kama RCC ya Mkoa wa Morogoro ilivyoridhia kuanzishwa kwa Mkoa wa Ulanga wenye Wilaya tatu, Kilombero, Ulanga, Malinyi. Pia napendekeza mpango uweze kupendekeza kuanzishwa Wilaya ya Mlimba ambapo utakapotangazwa Mkoa wa Ulanga uwe na Wilaya nne; Ulanga, Malinyi, Kilombero na Mlimba ili kusogeza huduma kwa wananchi. Pia mpango uoneshe kuwepo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ambapo mchakato wa upatikanaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba umeshakubaliwa na Baraza la Madiwani la Kilombero na hatua zinaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza mpango ueleze ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya Ifakara hadi Mlimba kilomita 153, pia Mlimba – Madeke – Njombe kuunganisha mikoa hiyo miwili. Umuhimu wa barabara hiyo unatokana na kupatikana kwa kilimo cha mpunga na shamba la uwekezaji la

*KPL* Mngeta. Pia mradi mkubwa wa umwagiliaji wa Njage, kilimo cha miwa Ruipa na ujenzi wa kiwanda cha sukari, upatikanaji wa mazao ya biashara kama *cocoa*, ufuta, ndizi, matikiti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia umuhimu wa barabara hiyo ni kumrahisishia mwananchi kusafirisha mazao, kwenda kufuata huduma za matibabu hasa kwa mama mjamzito na mtoto kwani hospitali ya Wilaya iko umbali wa kilomita 263 hivi na barabara haipitiki kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango uingize upatikanaji wa maji katika Mji wa Mlimba ambapo Serikali ione umuhimu wa kusambaza maji yanayopatikana kwenye mito mikubwa iliyoko Mlimba kama vile Mto Mpanga na Mnyela baada ya kuchimba visima ambavyo vingi havina maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango uweke ujenzi wa vituo vya afya kila Kata na hospitali ya Wilaya Mlimba. Pia ujenzi wa kituo cha Polisi Mlimba na Mahakama za Mwanzo katika Kata 16 za Jimbo la Mlimba. Vile vile Mpango uzingatie ajira za Walimu, watumishi wa afya hasa vijijini. Ahsante.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru kuwa nimepata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza kuhusu hoja hii jana tarehe 2 Novemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kuwa na mpango wenye malengo mapana yasiyopimika limejitokeza tena katika Mpango wa 2017/2018 kama ilivyokuwa kwa mpango wa 2016/2017. Inasikitisha sana kuona kuwa Serikali inadhani inajua kila kitu na kwamba inachokisema na inachoandaa ni sahihi. Tunapochangia hoja za Serikali, nia huwa ni kuboresha hoja husika kwa maslahi ya nchi yetu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tatizo la kukosekana utengamano (*integration*) wa Wizara mbalimbali linaonekana tena katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018, kama ulivyokuwa kwa ule uliotangulia. Hili ni tatizo kubwa kwani ndicho chanzo cha kuwa na mipango isiyotekelezeka na bajeti isiyowezeshwa. Vipaumbele vinakuwa vingi mno kutekelezeka katika mwaka mmoja na hata kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Mpango unarudia kusema kuwa miongoni mwa misingi inayoisimamia na kuendelea kuidumisha ni amani, usalama, utulivu na utengamano wa ndani wakati ukweli ni kuwa yote hayo hayapo. Serikali ya Awamu ya Tano inatumia mabavu na vitisho kukandamiza mfumo wa Vyama Vingi na demokrasia iliyojengeka nchini kwa miongo miwili sasa. Vyama vya Upinzani viko katika mazingira magumu sana na mara nyingi inatokea misuguano isiyo na lazima na vyombo vya dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa Serikali haioneshi kuwa na utashi wa kujenga utengamano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Tatizo la kuvurugwa kwa Uchaguzi Mkuu wa 2015 na kesi ya Mashehe wa Zanzibar walioko mahabusu ya Tanzania Bara ni vielelezo tosha vya hali hiyo. Kilichojitokeza kwa suala la Mashehe ni kuwa Tanzania Bara inatumika kama *Guantanamo* ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiongozi Mwandamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alisikika akisema hadharani kuwa wataoleta fujo Zanzibar watapelekwa bara kama wenzao akina Farid waka…

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hii, huwezi kusema nchi ina amani, amani ni neno pana na halina maana ya kutokuwepo vita tu. (*Peace is not absence of war*) mifumo ya kuleta amani na utulivu inavunjwa na kuharibiwa na Serikali zote mbili zilizo madarakani. Naamini Wazanzibari wengi hawafurahishwi na hali hii, kinachotisha zaidi wamekaa kimya. Serikali inajiaminisha kuwa ukimya huu unaashiria amani, mimi siamini hivyo kwa sababu hiyo. Naishauri Serikali kujenga amani ya kweli nchini ili kujenga mazingira mazuri (wezeshi) kwa utekelezaji wa masuala muhimu mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii nchini ukiwemo Mpango wa Maendeleo unaopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wamezungumzia suala la mdororo wa uchumi, na mimi naunga mkono. Nashauri Serikali isijivunie takuwimu za kupanda uchumi bila ya kuangalia ni vipi takwimu hizo zinajionesha katika maisha ya wananchi. Ni lazima mabadiliko au hali ya uchumi mkubwa (*Macro-economy*) ihusiane na uchumi mdogo (*micro-economy*) ambao unagusa hali ya maisha ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli alilizungumzia suala hilo wakati alipokutana na watendaji wa Benki Kuu, kwa kweli ni jambo lenye mantiki. Haiwezekani Serikali ijivunie kuimarika hali ya uchumi wa nchi wakati hali ya maisha ya wananchi walio wengi inadidimia au haiendani na hali hiyo ya nchi/Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namsihi Mheshimiwa Waziri husika na Serikali kwa ujumla kuzingatia mapendekezo mbalimbali yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambayo kama nilivyosema awali yanatolewa kwa nia njema na kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja na badala yake namshauri Waziri Mpango, aisome kwa umakini taarifa ya maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mpango wa Maendeleo ni wa muhimu katika maandalizi ya kutayarisha bajeti ya Taifa, nampongeza sana Waziri wa Fedha, Naibu Waziri pamoja na Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ya kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushauri; katika ukusanyaji wa Mapato Serikali iongeze juhudi ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili kuelewa kuwa kulipa kodi si adhabu ni wajibu wa kila mfanyabiashara. Ili kufikia lengo la kukusanya mapato ya Shilingi trilioni 32.946, Serikali inatakiwa kuhakikisha mikakati ya ukusanyaji kodi kutoka vyanzo mbalimbali kuwa wazi kwa kila mtu na kujua Serikali ina malengo makubwa ya kuboresha huduma za jamiii kama vile kuboresha miundombinu ya maji, barabara, afya, nishati na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matumizi ya bajeti kwa mwaka 2017/2018 lazima pawepo na uwazi wa matumizi ya bajeti kwa wananchi wetu ili kuepuka malalamiko yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* watoe elimu kwa Watanzania juu ya utaratibu unaotumika katika ukusanyaji wa kodi, pia kujua aina ya kodi ambazo mfanyabiashara anatakiwa kulipa. Fedha ya maendeleo katika Halmashauri zetu zipelekwe kwa wakati bila kuchelewa ili kukamilisha miradi ambayo imepangwa. Pia Serikali iwe makini sana na miradi ambayo ipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambazo ni ahadi za Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea mwaka 2017/2018 Miradi ya maji, barabara, afya, itaendelea kutekelezwa kwa kufuata Bajeti ya Taifa na miradi ya kipaumbele ni ile ya ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaamini kwamba mtengamano wa kisiasa ni nguzo moja muhimu katika kujenga nchi yenye maendeleo makubwa na ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtengamano wa kisiasa unajumuisha siasa safi za kiustaarabu na zenye kuheshimu mawazo ya kila mmoja ili kukidhi katika kufikia demokrasia ya ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi washirika, ambayo ni wadau wakuu wa kusukuma maendeleo katika nchi yetu tayari wameanza kurudi nyuma kwa

kukosekana sifa nilizozielezea hapa juu hasa baada ya Serikali ya CCM kuendeleza ubabe wake kwa kutoheshimu maamuzi ya Wazanzibari waliyoyafanya kwenye uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa miujiza gani Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaweza kufanikisha mipango yake ya kuimarisha uchumi wa nchi hasa baada ya kukosekana mtangamano wa kisiasa hapa nchini kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya maamuzi ya kuhamishia Makao Makuu ya Serikali katika Mkoa wa Dodoma, kwa kile kinachoaminika kama ni katikati ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma ni katikati kwa Tanzania Bara na sio kwa Tanzania nzima. Kwa kupunguza usumbufu kwa Wazanzibari wa kufuatilia matatizo yao Dodoma, naishauri Serikali kwamba Wizara zote za Muungano zibakie kule kule Dar es Salaam na zile zisizo za Muungano ndizo zihamishiwe Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2015/2016, Serikali imetoa mafunzo katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi tofauti ndani na nje ya nchi kwa wanafunzi 159. Naomba Mheshimiwa Waziri afafanue kati ya wanafunzi hao, wamo wanafunzi Wazanzibar wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa wanafunzi 35 wanaogharamiwa na washirika wa maendeleo ni wangapi wanatoka Zanzibar?

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hoja hii ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam. Ni bandari ambayo inaipatia pato Serikali yetu kwa kiasi kikubwa, lakini leo hii tunakosa mapato makubwa kutokana na kodi kubwa kuongezeka na wafanyabiashara kukimbia bandari yetu kwa kuogopa kula hasara. Wafanyabiashara wa Congo, Zambia, Malawi, wote hao wamekimbia na kuifanya Bandari kuwa kavu. Kuna upungufu wa makontena, magari ya mizigo hayaingii, wengi wamekosa ajira na uchumi kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge kazi yetu ni kuelekeza Serikali na kuishauri na kuikosoa pale inapofanya vibaya na kuisifu pale inapofanya vizuri. Sasa umefika wakati wa Mawaziri kusema ukweli, wasimdanganye Mheshimiwa Rais kwa kuogopa kutumbuliwa, hii ni nchi yetu sote, Watanzania wanatutegemea, tunakokwenda siko. Uchumi unaporomoka kutokana na

mipango mibovu kuanzia matajiri mpaka mama ntilie. Mheshimiwa Waziri tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano, kipaumbele chake inajipanga kufufua viwanda na kujenga viwanda, lakini haiwezi kufanikiwa ikiwa miundombinu ya umeme na maji ni mibovu, ni lazima kwanza ijipange. Serikali kwa kusimamia kupatikana kwa umeme wa uhakika ili wanapokuja wawekezaji kuingia nao mkataba waweze kufanya kazi na kuipatia nchi uchumi na vijana wetu kupata ajira na kupatikana maendeleo. Porojo za kwenye makaratasi hazitoshi tufanye maamuzi ya kiutekelezaji ndiyo dira ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya umeme wa uhakika inaweza kuendesha viwanda na kukidhi matumizi mengine ya wananchi wa kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo bado hakijapewa kipaumbele kwani benki hazitoi mikopo ili miradi ya kilimo iendelee; ni usumbufu mkubwa. Pembejeo hakuna, vitendea kazi kama vile matrekta, mbegu bora hakuna za kutosha, hivyo wakulima wapate mbolea mapema na bei zipunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo maji vya vingi vimekauka kutokana na uharibifu wa mazingira na ukataji wa miti hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Waziri atatuambia nini kuhusu upatikanaji wa mikopo ya fedha kutoka benki ili wakulima waweze kufaidika kwa kupata mahitaji yao ili kukuza uzalishaji na kupunguza umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema huu mpango haukidhi viwango ambavyo tulivitarajia, wala haukutosheleza matakwa ya Kitaifa na maendeleo tunayoyataka. Kwanza, haujatupa tathmini; tumefikia wapi? Tumekwama wapi? Tuanzie wapi baada ya kupitisha bajeti ndani ya mwaka huu? Huu ni mpango gani usioonesha dira na hali halisi ya mambo yalivyo katika kila sekta?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni mkanganyiko au mgongano wa wazi kati ya kanuni za Bunge na Sheria ya Bajeti kuhusu uwasilishwaji wa mpango na makisio ya bajeti katika mwaka wa fedha unaofuata. Kikawaida, pale panapotokea mgongano kati ya kanuni na sheria, basi, sheria ndiyo husimama, lakini Bunge letu, huipa kanuni kipaumbele. Tukizingatia Kifungu 21(2) cha Sheria ya Bajeti, mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa yalikuwa yawasilishwe katika Bunge la Januari – Februari. Hii ni kwa ajili ya kufanya

tathmini ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoendelea na makisio ya hali ya uchumi kwa miaka mitatu ya fedha inayofuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kutoa mchango kuhusu mapendekezo ya Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa, tunashuhudia hali ya kiuchumi ikiyumba sana ndani ya nchi hii. Hii ni kutokana na sababu tofauti tofauti.

(i) Sekta ya Kilimo imeathirika hasa kutokana na mabenki kuzuia kutoa mikopo kwa wakulima kama ilivyokuwa hapo awali; Benki kujitokeza na kutoa mikopo kwa wakulima ili kuendeleza kilimo bora chenye tija;

(ii) Pia uchumi umedorora kupitia Sekta ya Utalii na kukaribia kufa. Hii ni kutokana na Serikali kuongeza kodi ya ongezeko la thamani, hivyo Serikali imesababisha kupungua kwa watalii kuja Tanzania na hivyo kukosa pato la Taifa;

(iii) Serikali kukamata bidhaa na mali za wafanyabiashara wakubwa, hali iliyosababisha wafanyabiashara kufunga biashara zao nchini kwa kuhofia mali zao kuchukuliwa na Serikali, jambo ambalo linazorotesha uchumi, hivyo Sheria ichukue hatua ya kuwawajibisha wahujumu uchumi wa nchi hii jambo ambalo linasababisha uchumi unakuwa tete;

(iv) Serikali imetengeneza watumishi hewa na kusitisha ajira kwa sababu ya kuwa inafanya uhakiki wa watumishi wake. Jambo hili limepelekea kuyumba kwa uchumi na pesa nyingine kulipwa watumishi kama sehemu ya usumbufu wakati kumewafanya wasomi wa taaluma mbalimbali kuishi kama ombaomba ndani ya nchi yao na kudhalilika kutokana na elimu waliyopata. Wananchi wamekuwa wakimbizi kwenye nchi yao hali inatisha. Serikali izingatie hali ya wananchi na raia wake. Serikali bora ni yenye kujali raia wake na kuweza kuwajibika;

(v) Sekta ya Afya ndiyo iko hoi na kuzorota zaidi. Tumeshuhudia kukosekana dawa, chanjo na vifaa tiba katika hospitali zetu nchini, huku maelfu ya wananchi wakipoteza maisha huku tukishuhudia Waziri wa Sekta hii na Makamu kulumbana, mmoja anasema ziko, Mkuu wake akisema hakuna dawa, chanjo na vifaa tiba na hali ni tete. Hivyo Serikali itafakari kauli hizi na kuwapatia wananchi wao huduma nzuri ya afya ili kunusuru janga hili nchini;

(vi) Sekta ya Elimu pia ni changamoto. Elimu imekuwa bure lakini ni bora ilivyokuwa ya kuchangia kwani Serikali ilikuwa haikujipanga kuhusiana na hilo. Wanafunzi wa Elimu ya Juu wanakosa mikopo hali inayowakatisha tamaa wanafunzi hawa kumaliza masomo yao. Walisomeshwa na wazee kwa hali na mali ili waje kuikwamua jamii na yeye binafsi kutokana na hali duni waliyokuwa nayo. Pia Serikali inashawishi watu wajiajiri wenyewe; hali inajulikana kwamba elimu yetu haifanyi mtu aweze kujiajiri. Hivyo, Serikali ijipange kuwa na mfumo wa elimu hii na ndiyo washawishi watu wajiajiri. Tunatakiwa kujiandaa hivyo, ndiyo tutoe hamasa;

(vii) Tulishuhudia na kuahidiwa viwanda, lakini mpaka sasa hakuna kiwanda hata kimoja, jambo ambalo halikutengenezewa *plan* nzuri, bali Serikali ilikurupuka bila kujiandaa vya kutosha na kusababisha hali ya uchumi kudorora;

(viii) Suala la Bandari; mizigo imepungua hali inayosababisha uchumi kuzorota na mapato kupungua. Kiukweli Serikali imefilisika japokuwa Serikali haikubali, lakini kuwepo viashiria hivyo ni wazi kuwa imeshindwa. Ila naishauri Serikali kuwa makini na kufanya tafiti mbalimbali ili kuinasua nchi hii ya Tanzania katika giza hili nene; na

(ix) Halikadhalika, tunaishauri Serikali irudishe mamlaka ya kuwa Halmashauri kuchukua kodi za nyumba na vyanzo vingine ili zitumike kwenye Halmashauri kuimarisha na kuanzisha miradi kuliko kupewa *TRA* hali ambayo inaonesha imeshindwa kutekeleza hilo kipindi cha kwanza na hiki cha pili mpaka sasa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kwenye maeneo ya maliasili na utalii, elimu, kilimo, viwanda, afya na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa masikitiko makubwa kuona mpango huu haujaweka Sekta ya Maliasili na Utalii kama moja ya maeneo ya vipaumbele licha ya kwamba sekta hii huchangia zaidi kwenye kuingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutolewa kwa maliasili na utalii katika vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ni fedheha na masikitiko makubwa kuwa sekta hii haipo katika Mpango wa mwaka 2017/2018. Tunaomba Serikali itoe sababu za msingi, ni kwa nini Sekta ya Maliasili haipo ilhali ndiyo sekta iliyokuwa ikichangia kukuza uchumi wa ndani kwa miaka yote na ndiyo inayotoa ajira kwa vijana na haihitaji gharama kubwa sana za uendeshaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa watalii wanaoingia nchini na hali mbaya ya Sekta ya Utalii; mfano watalii wamepungua kwa 8% kutoka watalii 1,140,156 mwaka 2014 mpaka watalii 1,048,944 mwaka 2015 na bado hali inazidi kuwa mbaya kwani watalii wanazidi kupungua kila siku hasa baada ya uwepo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za Maliasili na Utalii. Pia kumekuwepo na upungufu wa idadi ya watalii wa hotelini 1,005,058 mwaka 2014 mpaka 969,986.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa mapato ya utalii kutoka dola milioni 1,982 mpaka 1,906; na hizi ni kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2014/2015. Vile vile kwa wastani wa siku za kukaa watalii, zimepungua kutoka siku 12 mpaka kumi na kwa sasa hali imezidi kuwa mbaya zaidi baada ya kuwepo kwa *VAT,* maana Sekta ya Utalii imekuwa na mlundikano wa kodi nyingi sana takriban 32. Hizi zote zinaongeza gharama na kusababisha watalii kuona ni ghali sana kuja kupumzika na kujionea utalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kumekuwepo na matatizo makubwa kwenye Sekta ya Utalii yanayochangia kushuka kwa mapato yatokanayo na utalii. Mfano tu, ninavyoongea sasa, Mamlaka ya Ngorongoro imekataza wamiliki na magari binafsi yanayotoa huduma za kitalii kwa kutumia magari binafsi ambayo kimsingi yamesajiliwa kibiashara na yamekidhi vigezo vyote vya magari ya utalii ila tu siyo magari ya Kampuni, yawe ndiyo kama masharti ya leseni ya utalii inavyotaka. Kama barua yenye Kumbukumbu Namba *NCAA/D/584/Vol.XIII/20*, pamoja na barua *TNP/HQ/L.10/22* iliyohusu zoezi la uhakiki wa leseni kwa makampuni yanayofanya shughuli za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa takriban magari 300 yamezuiwa kufanya kazi za kupeleka wageni ndani ya hifadhi. Makampuni yaliyokuwa yanafanya biashara kupitia magari haya tayari yalikuwa yana wageni ambao wanapaswa kwenda hifadhini, hivyo watalii wengi wanataabika ilhali tayari wameshatoa pesa zao na wanahitaji huduma. Hii ina athari ya moja kwa moja katika soko zima la utalii nchini ambalo mpaka sasa linakumbwa na changamoto lukuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua hitaji la kisheria katika kupata leseni ya utalii, lakini tujiulize, tunawasaidia vipi Watanzania hawa ambao wamejichanga na kupata fedha kidogo kwa ajili ya mtaji wa kuanzisha biashara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kuishukuru Wizara kwa kuwa Waziri Profesa Maghembe na Watendaji wake waliweza kuona ni fursa nzuri za kuendelea kuwaajiri watu kwenye Sekta ya Utalii ya Usafirishaji kwa kulifanyia kazi pendekezo letu tulilolitoa wakati wa bajeti, ambapo tulipendekeza Serikali angalau iweke sharti la magari kuwa matano

badala yake yamekuwa mawili au matatu. Kwa taarifa nilizonazo, ni kuwa magari matatu ndiyo hitajio. Hii ni hatua tatuzi kwa vijana maskini wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu ni kwamba, kufuatia barua ya Ngorongoro ni kuwa, Serikali ipate uhakika wa uwepo wa magari matatu katika kuanzisha biashara, iwe ni magari matatu bila kuwa na kigezo cha umiliki, bali ieleze kuwa kampuni ni lazima iwe na magari matatu, iwe ni magari ya kukodi au ya kibiashara lakini ni lazima kampuni ioneshe uwezo na uhakika wa magari hayo; na yabandikwe *sticker*. Msingi wa hoja hii ni kuwa siyo Watanzania wote wana uwezo wa kumiliki magari matatu yenye viwango elekezi, bali wanaweza kukodi magari yenye viwango elekezi na biashara hii ikaendelea na kutoa ajira na kukuza uchumi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwenye sharti la leseni ya biashara *(TALA License)* hiyo kuna hitaji la kampuni kulipa dola 2,000 kwa makampuni ya ndani na dola 5,000 kwa makampuni ya nje, havijalishi idadi ya magari ambayo kampuni hiyo inamiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isihakikishe kuwa linalipa dola 100 kwa mwaka bila kujali idadi ya magari? Serikali itapata fedha nyingi zaidi kwa kuwa yapo makampuni yana magari zaidi ya 300 na yanalipa dola 2,000 na mengine yana magari matano na yanalipa kiasi sawa cha dola 2,000. Endapo kila kampuni italipa dola 100 kwa mwaka, ina maana kwamba kwa makampuni yenye magari 300 kwa mwaka watalipa dola 3,000 badala ya 2,000 kama ilivyo sasa. Hii itasaidia wafanyabiashara wadogo pia kuweza kumiliki magari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri hii Sekta ipewe kipaumbele. Tulishauri kuwa kodi ya ongezeko la thamani ni bomu kwa uchumi wetu na sasa athari imeanza kuonekana. Tuliwaiga Kenya, lakini wenzetu waliondoa hiyo Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* na *nature* ya utalii ya Kenya ni kama kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni juu ya zoezi zima la uhakiki wa wafanyakazi hewa ambalo limechukua muda mwingi, nalo linaendelea kuwaacha Watanzania wengi bila ajira na kwa wale waliokuwa wanasubiri ajira pamoja na wale walioajiriwa mwezi wa Nane, 2015 ambapo walisitishiwa ajira kupisha uhakiki tangu Februari, 2016 hadi leo hawapo kazini na hawalipwi mshahara. Unategemea hawa Watanzania wataishi vipi? Tunataka majibu kwenye hili maana Mheshimiwa Rais alisema akiwa *BoT* kuwa zoezi la uhakiki wa wafanyakazi hewa kuwa ni kati ya miezi miwili au mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoonekana sasa ni dhahiri Serikali hii haina fedha ama inaelekea kufilisika na hivyo kuamua kwa makusudi kujificha chini ya kivuli cha uhakiki ili kuondoa aibu ya kutokuwa na fedha ya ajira mpya. Fedha

za nyongeza kwenye kupandisha madaraja, kuongeza mishahara kwa mujibu wa Sheria na Mikataba, hakuna watumishi kwenda masomoni wakilipiwa na mwajiri wake. Tunaomba majibu katika hili, maana bila Walimu wenye *motivation,* Madaktari, Manesi na kadhalika, hii nchi tunaiweka kwenye *bomb*. Hatua stahiki zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya viwanda bila mikakati ya elimu yenye kutoa elimu na wanafunzi wa kada mbalimbali ili waweze kwenda kwenye viwanda tarajia; bila mikopo kwa kada zote kwenye elimu ya juu ni *bomb.* Bila kuwekeza kwenye motisha za Walimu kama nyumba, ofisi, *Transport Allowance and Hardship Allowance*; pia bila kuwa na uhakika wa maji ni ndoto kuzungumzia Tanzania ya viwanda kama hakuna umeme, miundombinu imara ya barabara, kuwekeza katika kilimo chenye tija ili kiweze kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda tarajiwa, itakuwa ni ndoto ya Abunuwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni juu ya kutokuwekwa asilimia za pato la Taifa kwenye Mpango wa Maendeleo, sababu na Sheria ya utekelezaji ya Mpango wa Maendeleo. Mpango wa mwaka 2011/2012 – 2015/2016 tuliazimia 35% ya pato la Taifa ziende kwenye Mpango wa Maendeleo lakini kwa sasa mpango hausemi chochote. Hii ni hatari sana maana tunaweza kukuta mpango huu ukitegemea wahisani zaidi, kitu ambacho ni hatari kama nchi tusipowekeza kwenye maendeleo yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni juu ya umuhimu wa kuona *review* kwenye mdororo wa kutokuwa na mizigo Bandarini ambayo inatokana na tozo mbalimbali, *wharfrage* tunatoza dola 240 kwa futi 20 lakini wenzetu dola 70 na *VAT on Transit* na kadhalika.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuleta mapendekezo ya Mpango na Mwongozo wa kuandaa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi kwa ufupi naomba nijazie vitu vichache ama niungane na wachangiaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu. Mfuko huu ni halali maana uliundwa kisheria ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya watu wenye ulemavu ikiwemo suala la elimu na kadhalika. Naiomba Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 mfuko huu utengenezwe na kupelekewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ruzuku za vyama vyenye watu wenye ulemavu, naomba vyama hivi vipewe ama vipelekewe ruzuku kama ilivyokuwa zamani ama miaka ya nyuma. Vyama vya watu wenye ulemavu vinashindwa

kujiendesha na vingine vinaelekea kufa kabisa maana vimekosa fedha za kuviendesha. Naomba sana Serikali yangu ya CCM iliangalie tena na tena suala la ruzuku na Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kifungu maalum kupitia Bunge, Sera, Ajira, Kazi na Walemavu; naiomba Serikali iweke kifungu maalum na kifungu hicho kipewe fedha kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu wana mahitaji mengi ikiwemo mafuta maalum kwa watu wenye ualbino, baiskeli za miguu mitatu au miwili, fimbo nyeupe, vifaa vya kuongeza usikivu *(hearing aids)* na kadhalika. Uwepo wa kifungu hicho chenye fedha, utasaidia mahitaji tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ama ukarabati wa shule maalum, vitengo na shule zote za awali, msingi, sekondari na vyuo ili zifae kwa watoto ama wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya kufundishia na kufundishiwa *(teaching and learning aids),* kuna uhaba mkubwa wa vifaa hivi kwa wanafunzi wenye ulemavu. Naiomba Serikali itoe kipaumbee kwa upatikanaji wa vifaa hivi ili WWU (Watu Wenye Ulemavu) waweze kupata elimu ambayo ndiyo mkombozi wa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkalimani wa lugha ni chakula kwa mlemavu; kiziwi, hivyo naiomba Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 itengwe bajeti na waajiriwe wakalimani hawa (kwenye Televisheni ya Taifa, Hospitali za Serikali, Viwanja vya Ndege, Vituo vya Polisi na kadhalika); kwa vyombo binafsi kama televisheni, hospitali na kadhalika. Serikali itoe tamko la kuviamuru vyombo hivi viajiri wakalimani hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kutengeneza Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Mpango huu kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina azma nzuri katika kuelekea katika uchumi wa viwanda. Hili ni jambo jema sana litakaloivusha nchi yetu katika kuelekea kwenye uchumi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 1970 tuliweka viwanda vingi sana ambavyo kwa sasa vimepoteza uwezo wake na vingine vimekufa kabisa. Hivyo, kwanza naishauri Serikali iangalie sababu za kuanguka kwa viwanda hivyo. Sababu hizo ndizo zitakazotuongoza kuelekea kwenye azma hii baada ya kuzifufua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni vyema Serikali ianze kujiandaa kwa kutayarisha rasilimali ambazo zitaweza kukabiliana na suala hili. Miongoni mwa rasilimali hizi ni rasilimali watu *(HR)*. Serikali ianze kuwasomesha watu wetu badala ya kuja kutegemea wataalam kutoka nje ya nchi kama ilivyo katika sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutoa elimu bure toka shule ya msingi mpaka kidato cha nne. Hii imesaidia kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza. Ufaulu wa watahiniwa wa darasa la saba na wale wa kidato cha sita unaendelea kupanda wakati ngazi ya chini, yaani sekondari, umeshuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hapa ni Walimu. Walimu wa masomo ya sayansi ni wachache sana. Kuna baadhi ya shule hazina kabisa Walimu wa masomo ya Hisabati, Fizikia, Biolojia na Kemia. Shule ambazo hazina Walimu wa masomo haya bado ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya kidato cha nne ni mbaya sana. Hivyo, ni muhimu katika mipango ya Serikali tuwekeze vya kutosha katika kuzalisha Walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nyumba za Walimu katika shule nyingi zimekuwa chache sana. Walimu wengi bado wanakaa mbali na shule, kuna baadhi wanatembea umbali wa kilometa tano mpaka saba kwenda shuleni, hasa maeneo ya vijijini; hivyo, hufika shuleni wakiwa wamechoka na wakati mwingine kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kuwasaidia wanafunzi. Serikali iweke utaratibu madhubuti wa kujenga nyumba za Walimu, hasa kwa shule zilizopo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa hatua inayochukua ya kuanzisha Vyuo vya Ufundi *(VETA)* kwenye baadhi ya maeneo. Kwa kuwa, tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda, hasa viwanda vya kati, tuhitaji zaidi mafundi mchundo ambao ndio watafanya kwenye viwanda hivi. Hivyo ni muhimu kuweka utaratibu wa kujenga vyuo hivi kwa kila Wilaya. Kuendelea kuongeza Vyuo Vikuu haitusaidii sana kutatua tatizo la ajira na nguvukazi, kwani wahitimu wa Vyuo Vikuu ni Maafisa ambao wanatarajiwa kwenda kusimamia

kazi katika sekta mbalimbali. Je, ni nani atafanya kazi katika viwanda hivi kama hatuna watu hawa wenye elimu ya kati?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali katika kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu, bado vijana wengi wamekuwa wakikosa mikopo hiyo. Vijana wengi, hususan watoto wa maskini wanaotokea vijijini ndio ambao wamekuwa wakikosa mikopo. Serikali ipitie upya vigezo vinavyotumika katika utoaji wa mikopo. Vigezo hivyo viwe wazi na ikiwezekana Wakuu wa Shule za Sekondari wapewe hayo maelekezo ya jinsi Bodi ya Mikopo inavyotoa tathmini ya kukopesha wanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na utaratibu wa kufanya *projection/forecast* mapema ili kujipanga na kujua mahitaji ya kiasi cha fedha kitakachohitajika kwa mwaka husika ili tuingize kwenye bajeti ya Serikali. Hii inaweza kufanyika kwa kujua ni vijana wangapi watahitimu kidato cha sita kwa mwaka huo wa fedha? Tunatarajia watafaulu wangapi? Hii itatusaidia kupunguza baadhi usumbufu na matatizo yanayowapata kwa kukosa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naipongeza Serikali kwa kuweka mpango wa kuendeleza utafiti katika kilimo kwa mazao mbalimbali. Serikali sasa ijikite kwenye utafiti wa masoko ya mazao haya. Wakulima wetu, hususan vijijini, wamekuwa wakijituma katika kuzalisha mazao mbalimbali. Tatizo kubwa limekuwa ni kupata soko la mazao hayo. Kuna baadhi ya maeneo, mfano, Lupembe; mazao ya matunda kama vile nanasi, maembe, parachichi, yamekuwa yakiozea shambani kwa kukosa soko la uhakika. Pia, barabara mbovu au zisizopitika wakati wa kifuku zimekuwa zikiathiri soko la mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali ikaweka utaratibu wa kutengeneza barabara zinazoenda kwenye maeneo ya uzalishaji ili kuokoa mamilioni ya fedha yanayopotea au hasara wanayopata wakulima kutokana na ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampongeza Waziri wa Fedha na Watendaji waliopo chini ya Wizara hii kwa kuunda mpango huu. Naunga mkono hoja.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo halijapewa kipaumbele, limezungumzwa kidogo sana katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018. Ni vema kilimo kikapewa kipaumbele ili pia kufikia nchi yenye viwanda tunayoiota. Karne ya 18 na 19 mwanzoni, nchi ya Uingereza ilifanya mapinduzi makubwa sana ya kilimo *(Agrarian Revolution)* na ndiyo matokeo ya viwanda vya Uingereza vilivyopo hadi leo. Vivyo hivyo nchi za China na India zote zilifanya mapinduzi ya kilimo *(Agricultural Revolution)* na

hatimaye zikafikia hatua ya kuwa na viwanda ambavyo vipo hadi leo. Hivyo hakuna nchi yoyote duniani inayoweza kufikia mapinduzi ya viwanda bila kuboresha kilimo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitangulize shukrani zangu za dhati kwa Serikali yangu ya CCM. Nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Waziri wa Fedha na Sekretarieti yake kwa kuthubutu kutoa mapendekezo yao kwa Mpango huu wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya ni mazuri kwa sehemu kubwa. Mchango wangu katika mapendekezo yangu upo katika sehemu tatu:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Elimu ya Bure Shule za Msingi na Sekondari. Kwa maoni yangu, fedha hizi zinazotolewa mashuleni na hasa shule za msingi, hazifanyi kazi iliyokusudiwa. Mfano, Shule ya Msingi 'A' kwa mwezi itapata shilingi 230,000/=. Fedha hizi hugawanywa kwa asilimia ishirini ishirini. Kwa maoni yangu, fedha hizi hazitoshi hata kununua mpira.

Kwa mahitaji makubwa ya shule ni chaki, mitihani na utawala. Kwa nini Serikali isifungue akaunti maalum kila Halmashauri na fedha hizi zikawa katika akaunti hii na kila shule ikapewa mahitaji muhimu ya wanafunzi na utawala. Napendekeza *style* iliyokuwa inatumika enzi za Mwalimu, kila mwanafunzi alikuwa anapewa vitabu, madaftari, chaki na vitu vingine muhimu kuliko fungu la fedha hizi ambazo sehemu kubwa hazifanyi kazi. Fanyeni utafiti.

(b) Nashauri Serikali itenge fidia ya wakulima kwa mazao yaliyoharibiwa na wanyama waharibifu (ndovu) Jimboni kwangu. Wakulima wanadai zaidi ya shilingi milioni 400. Serikali ihakikishe fidia kwa wakulima, inalipwa.

(c) Malambo kwa wafugaji. Maeneo mengi ya hifadhi ya Taifa hayana maji kwa mifugo. Serikali iwe na mpango maalum wa kuchimba malambo Jimbo la Bunda.

(d) Vile vile Serikali iwe na mpango maalum wa kujenga vyumba vya madarasa, vyoo na nyumba za Walimu kwa shule za msingi na sekondari. Mfano, Jimbo langu la Bunda lina upungufu wa vyumba vya madarasa 586 vyenye thamani ya shilingi milioni 687. Serikali iwe na mkakati maalum wa kujenga/kutatua kero hii.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nichangie katika Mpango wa Serikali wa Maendeleo 2017/2018 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza sana Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, lakini ni lazima tuseme ukweli, hali ya maisha ya wananchi vijijini ni ngumu zaidi na wanaishi kwa kula mlo mmoja na wengine wanashindwa hata kupata mlo kutokana na mazingira magumu. Zipo taarifa kutoka vyombo mbalimbali yakiwemo magazeti, mitandao kwamba Septemba, 2015 mabenki yalikuwa na faida ya shilingi trilioni 64, lakini Septemba, 2016 faida za mabenki ni shilingi trilioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Waziri anasema uchumi umekua! Hivi kweli uchumi umekua, *difference* ya shilingi trilioni 60 ni *gap* kubwa. Serikali lazima ijitathmini, imekosea wapi? Hivi sasa mabenki yanajiendesha kwa hasara, hayatengenezi faida. Kama hayatengenezi faida, Serikali inakosa kodi na pia, hata wananchi nao wanakosa mikopo katika benki. Benki za Serikali ndiyo zipo hoi zaidi, *TWB, Twiga Bancorp, TIB,* ndiyo zimesinzia kabisa kwa kuwa na mtaji wa *negative*. Tumeshuhudia Serikali kuichukua Twiga na kuipa jukumu *BOT* kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi ya kujiuliza katika Serikali hii wakati kuna hali ngumu za maisha kwa wananchi, lakini Serikali imeshindwa kuzuia matumizi ya hovyo hovyo yanayogharimu fedha na kusababisha hasara kwa Taifa. Mfano halisi ni Benki ya *TIB* ambayo malengo yake ilikuwa ni kuendeleza kilimo, kutoa mikopo, kusaidia katika miradi ya umwagiliaji, kujenga na kuwekeza katika miradi ya kilimo, lakini zilizokuwa idara zake sasa hivi nazo zimekuwa ni benki kamili; ***TIB Cooperate, TIB Commercial, TABB Bank* ya Kilimo**.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki zote hizi ma-*CEO* wao wote wanalipwa zaidi ya shilingi milioni 20 na kama imeshuka ni baada ya Mheshimiwa Rais kutoa tamko la kupunguza mishahara. Pia, katika hili, benki zote hizi zina Wakurugenzi wanaolipwa zaidi ya shilingi milioni 10, lakini hakuna wanachofanya; kuanzia asubuhi hadi jioni wanahudumia watu wawili au watatu tu kwa siku kwa sababu, benki hizi Makao Makuu yake yapo Dar es Salaam badala ya benki hizi kuwa vijijini kuwasaidia wakulima ambao kwa zaidi ya 80% kilimo hicho kinatengeneza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugumu wa maisha unaonekana waziwazi katika uwekezaji wa viwanda; Bakhresa ameripotiwa na vyombo vya habari kuwa, zaidi ya 70% ya biashara zake zime-*freeze* na anatarajia kuhamishia *hub* zake katika nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *TTPL* hivi sasa kilikuwa kinasindika zaidi ya tani 46,000, sasa hivi kiwanda hiki kinasindika tani 16,000 lakini cha kushangaza Serikali haitazami viwanda vya ndani vilivyo ndani, lakini inaangalia kujenga viwanda vipya badala ya kuangalia kwa jicho lingine viwanda hivi. Badala ya Serikali kutegemea kuanzisha viwanda vipya visivyo na tija na kuacha vya zamani vikiendelea kuteketea, lazima Serikali ikubali kuelezwa ukweli, ikae chini na kujipanga na kuweka vipaumbele vya kuendelea kutafuta mbinu za kufufua uchumi na kuwaondolea wananchi mateso ya ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, *priorities* za Serikali kwa wananchi wake hazieleweki. Tatizo la mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu; kama uchumi umekua, kwa nini wasikopeshwe kama tunakusanya shilingi trilioni saba? Kwa nini Mfalme wa Comoro asingesaidia kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya Vyuo Vikuu? *Priority* ni uwanja wa mpira wa kisasa Dodoma au kujengewa Msikiti na siyo kusaidia wahanga wa Kagera ambao hawajui hatima ya maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama takriban zaidi ya mwaka watumishi hawajui hatma ya maisha yao. Hawajui lini zoezi hili litamalizika; hawakopesheki na mabenki, kisa uhakiki. Hii siyo sawa. Serikali ina watumishi wa umma siyo zaidi ya 5,000, uhakiki gani usioisha? Uhakiki gani unazuia watumishi kupanda madaraja na kushindwa kupata haki yao ya msingi ya kupata mikopo?

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza shukrani kwa *Allah (S.W.)* kwa kuniwezesha kuchangia hoja hii ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018. Nikiri kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imefanya vizuri katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kupambana na wafanyakazi hewa, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na Idara zake zote;

(b) Kuendelea na mapambano dhidi ya ufisadi uliokuwa ukifanyika katika nchi yetu; na

(c) Kupambana na kuzuia mfumuko wa bei katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango kuandaliwa vizuri na kitaalam, bado kuna upungufu ufuatao:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza msingi wenyewe wa viwanda ni jambo linalohitaji maandalizi makubwa na mapema. Kwa kweli, dhana ya viwanda inataka fedha za kutosha kama mtaji, rasilimali watu wenye ujuzi na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mawazo yangu, Serikali bado haijawa kwenye wakati mzuri kutoa fedha kwenye viwanda. Badala yake fedha zipelekwe kwenye miundombinu ya kuwezesha viwanda, badala ya kuanzisha viwanda na hasa ukizingatia Watanzania wengi hawana uelewa wa kutosha kwenye sekta hii ya viwanda.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuwa na mahusiano mabaya na wafanyabiashara wakubwa na wadogo, hatuwezi kujenga nchi bila kushirikiana kati ya Serikali na wafanyabiashara.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wafanyakazi wa Serikali ni watu muhimu sana kwa ujenzi wa Taifa letu. Naomba Serikali yetu iwaangalie kwa jicho la huruma.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mkakati wa kubadilisha watendaji wake. Jambo hilo ni zuri, lakini linahitaji umakini na hasa watendaji wawe na weledi wa kutosha na hasa wasiwe wakereketwa wa Chama, bali wawe watu wanaoweza kufanya kazi bila ya kuathiriwa na siasa na upendeleo wa kivyama.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu amejikita katika usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali za kila siku. Kwa mawazo yangu, kazi hii inaweza pia ikafanywa na Waziri Mkuu na hasa baada ya Rais kuonesha nini anataka katika utendaji wa Serikali na Waziri Mkuu ameona nini Rais anataka ili naye aige.

(f) Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia ni dhana kubwa katika maendeleo ya nchi. Mfano Uchaguzi wa Meya, Tanga, Kinondoni na uchaguzi wa Zanzibar. Kama demokrasia ikiheshimiwa itaongeza mahusiano ya ndani, pia itatoa fursa ya kupata fedha za *MCC* za Marekani, mfano Dola milioni 698.1 kwa mwaka.

(g) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kodi ya majengo kukusanywa na *TRA*. Jambo hili lilikuwa linafanywa na Manispaa vizuri sana, hivyo tunaiomba Serikali jambo hili la Kodi ya Majengo lirejeshwe kwa Manispaa na Halmashauri, kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kwa Serikali yetu:-

(a) Kujenga miundombinu ya viwanda na siyo kujenga viwanda na kuendesha mashirika ya ndege;

(b) Pesa ya Sekta ya Kilimo kufikia 10% ya bajeti ya nchi;

(c) Serikali ihakikihe mchango wa madini kwa pato la Taifa mpaka kufikia 10% ya pato la Taifa;

(d) Kuleta utengamano wa kisiasa kwa Zanzibar, Tanga na Kinondoni;

(e) Ajira kwa vijana, hasa tuongeze fedha kwenye mabenki, kilimo, uvuvi na ufugaji; na

(f) Kuondoa *VAT* katika mizigo ya nje na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Ramo Makani, Mheshimiwa William Ole-Nasha ajiandae, dakika tatu kila mmoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Thamani yenu milioni kumi! Mmechoka sana ninyi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nataka niseme tu kwamba mpango huu ambao tunauzungumza wa mwaka 2017/2018 suala la mazingira na mabadilio ya tabia ya nchi limezingatiwa vizuri sana katika kipengele cha 6.6 (a), (b), (c). Kwa hiyo, mkisoma pale Waheshimiwa Wabunge mtaona jinsi ambavyo suala la mazingira limezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mpango huu wa Maendeleo jambo kubwa lilikuwa ni kuanzisha Mfuko wa Mazingira ambao tayari Serikali imekubali na tayari tumeshaanzisha mfuko huo, kwa hiyo tunaamini kabisa kwamba mambo ya mazingira sasa yatakuwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo nilitaka pia kuyaweka sawasawa. Moja ni suala hili la Mawaziri kutokumshauri Rais na kusababisha mambo mengine kutokwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mambo mengi, sasa hivi Serikali tumeweza kuongeza mapato toka tulivyoingia kila mwezi, wastani wa mapato yetu yameenda shilingi bilioni 400; lilikuwa ni jambo la kupongezwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii toka ilivyoiingia madarakani hivi sasa tumeweza kuanzisha kanuni zile ambazo zilikuwa hazijasainiwa muda mrefu, kanuni zinazowalazimisha wamiliki wa madini kusajili katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Sasa hivi kanuni hizo zimeanzishwa na Mawaziri hao hao ambao leo

wanaambiwa kwamba hawana uwezo wa kumshauri Mheshimiwa Rais. Vilevile Mawaziri hawa hawa, leo tumeweza kufuta mashamba sita yenye zaidi ya hekta 89,388 ambapo baadhi ya mashamba haya wamepewa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo baadhi ya Wabunge wanasema Mawaziri hawa tumeshindwa kumshauri Mheshimiwa Rais, leo Wabunge wote wanapongeza jitihanda za Serikali upande wa kilimo, leo wakulima wa pamba wanajivunia bei imeenda mpaka shilingi 1,200 kwa mara ya kwanza, korosho imeenda mpaka zaidi ya shilingi 3,000 kwa mara ya kwanza, Wabunge hawa hawa ambao wanaambiwa kwamba hawana uwezo wa kumshauri Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mambo mengine ya kusema serikali imefilisika, haiwezi kumudu majukumu yake kwa sababu haina pesa na kwamba hata fedha unazokusanya ni za *arrears*, si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tupongezwe na bunge hili tumeweza kukusanya mapato zaidi ya shilingi bilioni 400 kila mwezi, na kwamba mpaka sasa hivi tumeweza kulipa madeni ya wakandarasi na wazabuni zaidi ya shilingi bilioni 878, tumeweza kulipa miradi mipya ya barabara shilingi bilioni 604, tumeweza kulipia miradi ya umeme shilingi bilioni 305, tumeweza kulipa mikopo ya wanafunzi shilingi bilioni 371, tumeweza kununua ndege kwa shilingi bilioni 103, tumeweza kulipa ndege kubwa *advance* kwa shilingi bilioni 21 na pointi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya yote tumeweza kufanya katika muda mfupi, Bunge hili lilikuwa linatakiwa kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii na kwa sababu muda ni wa dakika hizo ulizozitaja ambazo kwa hakika ni muda mfupi sana nichangie tu haya yafuatayo ambayo na amini yatatosha kwa muda huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza tunajadili mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2017/2018. Mpango wenyewe bado haujaja lakini majadiliano haya ndiyo yanatarajiwa sasa yaboreshe mpango huo kabla hata haujaletwa hapa mbele yetu na ambao bado pia tutakuja kuuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni Mpango wa Pili, wa mwaka moja moja kati ya ile mitano; na katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano tumejikita kwenye suala la kuelekea uchumi wa viwanda, na kila mmoja anakumbuka kwamba viwanda tunavyovizungumzia hapa zaidi ni vile

ambavyo moja kwa moja vinahusiano na kilimo, kwa maana ya malighafi lakini pia kwa maana ya kuongeza thamani mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzungumzia kilimo ambayo maana yake ni kwamba huwezi kuzungumzia viwanda kwa mwelekeo tunaouzungumzia bila kuzungumzia hali ya hewa. Hapa nataka kuipongeza Serikali baada ya kuleta mapendekezo haya ambapo kwenye kitabu tulichonacho hapa ni ukurasa wa nane kwenye misingi ya mpango na bajeti kati ya misingi ile saba inayotajwa pale moja wapo ni hali ya hewa. Hapa naipongeza sana serikali kwa kuzingatia hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya hewa kwa upana wake, maana yake ni pamoja na uoto wa asili ambayo ni misitu, lakini pia ni pamoja na suala zima la tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu niwakumbeshe Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu wengi walizungumza pale awali wakitaja changamoto mbalimbali kwenye sekta hii ya mali asili. Mimi nataka niwakumbushe tu kwamba kwa hali hii ilivyo sasa ni mbaya, na hiyo inatokana na ukweli kwamba tumeharibu sana uoto wa asili, kwa maana ya kwamba misitu imeharibika sana. Tumeshatoa takwimu tukisema jumla tuna hekta milioni 48.1 za uoto wa asili, lakini hizo zinapungua kidogo….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramo Makani naomba umalizie sentensi ya mwisho.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sentensi ya mwisho ni kwamba tutakapokuwa tunajadili mpango pale utakapokuja kule mbele ya safari, kama ambavyo mapendekezo haya yalivyopendekeza, tuzingatie hali ya hewa, na kwahiyo tuzingatie sana suala la kuhakikisha tunazilinda mali ya asili na kuzingatia masharti ya maliasili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa William Ole-Nasha, atafatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Angellah Kairuki ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii na mimi nichangie kwa ufupi kwenye pendekezo la mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tumesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge, na kimsingi mingi imekuwa ikitushauri namna ya kuboresha baadaye mpango wakati tunautayarisha, kwa hiyo kazi waliofanya

ni kazi ya kwao kimsingi wanashauri serikali wao kama wawakilishi wa wananchi tumepokea mapendekezo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kuhusu kilimo, mifugo na uvuvi nyingi zimejikita katika kuonesha kwamba mapendekezo ya mpango hayajajikita kwa undani kuhusu kilimo. Tunapokea mapendekezo ambayo yametolewa, lakini tufahamu kwamba hata baadaye tukiwa na mpango bado itabakiwa ni *frame work* haiwezi ikaingia kiundani kila eneo la kilimo, mifugo na uvuvi, baadaye itabidi tujenge mikakati mahususi kuhusiana na eneo moja moja la sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waheshimiwa Wabunge wanachangia hoja, yamezungumzwa mengi kuhusu hali ya uchumi katika kipindi ambacho Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano tuliahidi kuleta mabadiliko, tena mabadiliko makubwa, hatutegemei mabadiliko makubwa yatokee lakini tusihisi au tusione mabadiko yenyewe. Kwa hiyo tofauti ambayo tunaiona sasa ndio ushahidi kwamba kuna mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo hii tukasema kwamba tunashughulikia kuhusu ubadhilifu na matumizi mabaya ya fedha za Umma lakini hapo hapo pale wanaposhughulikiwa wanaofanya hivyo tukalalamika kwamba ni kitu kibaya, haiwezekani. Lakini vilevile haiwezekani kwamba tunategemea Serikali ilete mabadiliko makubwa lakini sisi Waheshmiwa Wabunge hatutaki kuwa sehemu ya mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahatma Gandhi alishawahi kusema *be the change that you wish to see* (kuwa sehemu ya mabadiliko ambayo unataka tuone). Naombeni Waheshimiwa Wabunge tuweni sehemu ya mabadiliko, tukubali kuondoka kwenye *comfort zone* zetu ili tuweze kuisaidia Serikali ya Awamu ya Tano kuleta mabadiliko ambayo tunaka, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Anjela Kairuki, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa ajiandae.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, na mimi nipitie mapendekezo ya Mpango na zaidi nitoe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka kufafanua nilieleze Bunge lako Tukufu na niwaambie Watanzania. Jukumu la ujenzi wa viwanda ni jukumu la sekta binafsi. Soma mpango wa pili wa miaka mitano, soma vision 2020–2025, sikiliza hotuba za Mheshimiwa Rais, ujenzi wa uchumi wa viwanda, kule kujenga viwanda ni jukumu la sekta binafsi. Serikali kazi yetu ni

kutengeneza mazingira wezeshi, tutatengeneza miundombinu, tutatengeneza maji, tutapeleka umeme, sekta binafsi ndio itajenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ilibidi nilizungumze hili. Sekta binafsi ni nani? Ni mimi Mbunge, mwananchi, mfanyabiashara. Niwaeleze ndugu zangu Wabunge muelewe viwanda maana yake ni nini? Mheshimiwa Waziri Mkuu atawasomea hotuba ya taarifa yangu ya Viwanda vilivyojengwa, wengine mtashangaa na wengine mtapatwa kihoro, kazi imefanyika. Kwa tafsiri ya viwanda ya Benki ya Dunia, kuna kiwanda kinaajiri mtu mmoja mpaka watu wanne kinagharimu shilingi milioni nane, kuna kiwanda kinaajiri watu watano mpaka 49 ni cha shilingi milioni tano mpaka 200, hizo ndizo ambazo nasema zinapatikana na benki zipo tayari kutoa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna viwanda vinaajiri watu 50 mpaka 99 vinathamani ya shilingi milioni 200 mpaka milioni 800 hivyo viwanda vinaitwa viwanda vya kati. Nitumie fursa hii kuwaambia Wabunge wote mnaotoka maeneo ya *SAGCOT* ziko pesa dola milioni 70 za Kimarekani, anayetaka kwenda kujenga kiwanda aje aniambie nipo Dodoma siku tatu hizi nikamuonyeshe namna ya kuomba. Waambieni watu wenu pesa zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilolipata katika ujenzi wa viwanda kulingana na taarifa za wataalamu, kama alivyosema ndugu yangu Ulega ni *mindset*, watu wanalala wanasubiri Serikali ije iwajengee viwanda.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kweli hiyo mzee wa *sound?*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Kwa hiyo hivyo ndivyo vitakavyojengwa na kazi inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la *Kurasini Logistic Center*. *Kurasini Logistic Center* Serikali imeshalipa fidia kilichobaki tutamleta *operator*, ambapo viwanda vita-assemble bidhaa pale zinazotoka nje kuja hapa, lakini pia na kukusanya bidhaa kutoka kwa wananchi kuzi-*assemble* kwenda nje kuuzwa, ndio utaratibu huo. Masharti anayopewa *operator* lazima aajiri vijana wa kitanzania ili wapate ujuzi wanaporudi kwao wajue namna ya kutengeneza viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la *TBS*. *TBS* inasimamia viwango na nimewaeleza hata Mawaziri wenzangu hata rafiki zangu sitaandika *memo* kwa mtendaji yeyote wa *TBS* eti ampendelee mtu yeyote, *you follow the principles* unapata huduma, wanaolalamika wana makando kando yao, sitaandika *memo* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi wa wafanyabiashara bwana Minja amenifuata kwa matatizo ya *TBS,* niwaambia wataalam wangu wawashughulikie wale wafanyabiashara wadogo watashughulikiwa. Lakini ngoja niwaambie mkilegeza *TBS* utendaji wake viwanda vyangu vitakufa, ni kama nilivyowaambia jana lazima *TBS* izuie bidhaa dhaifu na isiyolipa kodi isiingie nchini. Vijana wa *TBS* wanafanya kazi nzuri na nitaendelea kuwaongezea nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchuchuma na Liganga. Mchuchuma na Liganga Serikali hakuna tatizo wala hamtaweka pesa zenu kwenye bajeti, muwekezaji yupo ameshapatikana, nimeelekezwa na mamlaka kwamba niandike *cabinet paper* niipeleke hatua zilizobaki ziweze kupata baraka ya *cabinet paper*, ikishindikana zitaletwa kwenye Bunge. Kwa hiyo, msiwe na wasi wasi kamanda Silinde kwamba tumepanga Mchuchuma na Liganga, *Logistic Center,* haiwahusu, ninyi mmeshatoa baraka tunalishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie wepesi wa kufanya biashara *(the easy of doing business)*. Tulikuwa watu wa 139, tumekuwa watu wa 132, sijaridhika. Kwa hiyo, anayesema kwamba sisi tuna mahusiano mabaya na wafanyabiashara aje aniambie wafanyabiashara anayewawakilisha ni nani. Ukiwataka wafanyabiashara njoo uniambaie mimi, kila siku ninakuwa nao wanazungumza vizuri ila wanasema ukikaza ukaze kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Mipango eti ukaze sawia wote mianya uweze kuibana, kwa hiyo, hatuna matatizo, wafanyabiashara wa kweli ni wenzetu. Lakini Waheshimiwa Wabunge mkubali….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage naomba umalize.

Naona Waheshimiwa Wabunge ukitoka tu hapa tutakuja tupange foleni nyuma yako ili utukabidhi hivyo viwanda.

Mheshimiwa Angellah Kairuki atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa niseme tu kwamba na mimi naunga hoja kuhusiana na mpango huu. Lakini pili, nichukue nafasi hii kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwa kufikisha mwaka mmoja tangu alipoingia madarakani. Lakini zaidi pia mwaka mmoja ambao umejaa mafanikio makubwa katika kuiongoza

nchi yetu. Utendaji wake kwa hakika umetukuka, umeiletea sifa kubwa nchi yetu ndani na nje ya mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niweze kujibu hoja chache kwa haraka. Hoja ya kwanza nisuala zima la usitishaji au ucheleweshwaji wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba sababu kubwa ambazo zilipelekea au zimepelekea kutotoa ajira mpaka hivi sasa; ya kwanza ni suala zima la uwepo wa watumishi hewa kama ambavyo tulikuwa tukisema, na idadi imekuwa ikiendelea kupanda, mpaka sasa hivi tumeshaondoa watumishi 19,629 hewa ambao kwa kweli wangeendelea kubaki katika orodha ya malipo wangeendelea kusababisha hasara kubwa takribani shilingi bilioni 19.7 kwa kila mwezi.

Mheshimiwa mwenyekiti, sababu ya pili, baada ya kuwa tunaendelea kuhakiki watumishi hewa tulibaini pia uwepo wa vyeti vingi vya kughushi, tukaona hapana ni lazima tuhakikishe kwamba tunakuwa na ajira mpya baada ya kuwa tumehakikisha kwamba katika mfumo wetu wa ajira basi wale walioko katika ajira ni wale tu wenye sifa zinazostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya tatu ni uwepo wa miundo mkubwa katika Serikali na taasisi zetu. Tulipopunguza Wizara bado katika taasisi mbalimbali miundo ilikuwa haijafanyiwa tathmini, tumeshaanza huo mchakato na mchakato unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa sasa tumeanza kuimarisha mifumo ya utambulisho na ninawapongeza sana *NIDA* pamoja na wote walioshiriki katia zoezi, tumeongeza alama za utambulisho. Mwanzoni ilikuwa tu ni jina na *check number,* lakini hivi sasa walau tunaweza tukapata picha ya mtumishi wa umma, tunaweza tukapata alama za vidole pamoja na namba ya utambulisho wa Taifa katika kuhakikisha kwamba hakuna alama ambayo inaweza ikagushiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana pia na suala la muundo tumekuwa tukiangalia pia kuhakikisha kwamba tunakuwa na muundo wenye tija na muundo ambao unahimilika. Lakini vilevile tutaendelea kuhakikisha tunafanya uhakiki ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na watumishi wale tu ambao wana sifa. Lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaotusikiliza wakati wowote sasa hivi hatua tumefika pazuri tutatangaza ajira muda sio mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kulikuwa kuna hoja ilitolewa na Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba ni nani anasema ukweli kati yangu na Waziri wa Fedha. Nimwambie tu kwamba Serikali ni moja, Waziri wa Fedha anasema

ukweli na mimi pia ninasema ukweli. Kigezo cha kusema kwamba watumishi hewa; naomba tusikilizane ili muweze kuipata hoja vizuri halafu mtakuja kupinga mnavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hewa wameondoka 19,629, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataeleza kwa kina sana. Lakini ipo michakato mingine *wage bill* maana yake ni nini, ni lazima Mheshimiwa Zitto Kabwe afahamu. Bajeti ya mishahara ina *include* vitu vingi sana, kuna masuala mazima ya upandishwaji vyeo, kuna masuala mazima ya upandishwaji wa madaraja, huwezi kuwa kuna mtu anastaafu usimrekebishie mshahara wake akajikuta anaathirika katika malipo ya pensheni.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Zitto Kabwe, mimi na Mheshimiwa Mpango wote tupo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili alisema pia kwamba tumesema tunaokoa shilingi bilioni 17 kila mwezi, hatujasema hivyo, tunachokisema kwamba endapo watumishi hewa 19,000 kwa mfululizo kuanzia mwezi Machi mpaka sasa hivi wasingeondolewa kwa mkupuo *(cummulative),* basi katika mwezi husika wa mshahara wangeisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 19.7. Lakini hakuna popote tuliposema kwamba kila mwezi Serikali inaokoa shilingi bilioni 17. Lakini maelezo ya kina Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataeleza vizuri sana na nini kimefanyika na niliomba rekodi hiyo iweze kuwekwa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Khamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi naunga mkono hoja ya Dkt. Mpango. Mimi nina maeneo matatu nataka nijielekeze, la kwanza ni kutoa ufafanuzi kuhusu *landing fees* kwenye viwanja vyetu vya ndege, la pili nitajielekeza kwenye bandari ya Dar es salaam na tatu nitajielekeza kwenye ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Wabunge wamezungumza kwamba *landing fees* ya viwanja vyetu vya ndege iko juu sana, lakini ukweli wenyewe ni kwamba *landing fees* ya viwanja vya ndege vyetu vya Tanzania iko chini ukilinganisha na ya viwanja vyote katika *region* yetu. Hapa Dar es Salaam sasa hivi au Tanzania *landing fees* inakuwa ni kati ya dola tano mpaka dola tatu kwa ndege yenye uzito wa kilogramu 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kenya hasa kiwanja cha Nairobi, Mombasa na Moi, wao kwa ndege yenye uzito wa kilogramu moja mpaka kilogramu 1,500 wanachaji dola 10. Kwa upande wa *South Africa* hasa kiwanja cha Johannesburg, Capetown na Durban kwa ndege yenye uzito wa kilogramu 1,000 wanachaji dola 7.52. Kwa upande wa Msumbiji viwanja vya Maputo, Bella na Nampula wanachaji dola 11.5. Kwa hiyo, viwanja vyetu hapa *landing fees* ni ya chini kabisa huwezi ukalinganisha na viwanja vyoyote katika nchi zetu za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa ambayo sasa hivi Serikali inafanya ni ujenzi wa viwanja vyetu, sasa hivi tunajenga jengo la *terminal three* pale uwanja wa Dar es Salaam, tunajenga jengo la abiria huko Mbeya, tunajenga uwanja wa Mwanza na wiki inayokuja tutafungua *tender* au tutapata mkandarasi kwa ajili ya kiwanja cha Sumbawanga, Shinyanga, pia tutajenga jengo la abiria kwa ajili ya uwanja wa Kigoma na Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko mbioni sasa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Musoma, Iringa, pamoja na Songea. Tunaamini kazi yote hii tunayoifanya tuna hakika kwamba viwanja vyetu hivi vitachangia sana na nchi yetu itakua *hub* kwa ajili ya ndege kubwa za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bandari. Ni kweli usiopingika kwamba mizigo kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam imepungua lakini siyo bandari ya Dar es Salaam tu. Kwa mfano bandari ya Durban - *South Africa* mizigo imepungua kwa asilimia 10, bandari ya Mombasa imepungua kwa asilimia 1.5 na bandari ya Dar es Salaam kwa ujumla imepungua kwa asilima 5.47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu za msingi ambazo zilisababisha mizigo kwenye bandari ya Dar es Salaam kupungua. Ya kwanza wafanyabiashara wengi zamani walikuwa hawapendi kulipa kodi, sasa tumeendelea kuwabana na kila mtu analipa kodi na hivyo wafanyabiashara wengi sasa wamekimbia. Pili iliyosababisha hivyo ni kudorora kwa bei ya shaba duniani. Hiyo imesababisha mzigo kutoka Zambia kutokupita kwa wingi kwenye bandari ya Dar es Salaam na kusababisha mzigo wa bandari Dar es Salaam kushuka. Pia kuna matatizo kwenye uchumi wa dunia hasa China ambapo mizigo yetu mingi inatoka huko imesababisha mizigo vile vile kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine kuna changamoto kwenye miundombinu ya reli ambayo haiko vizuri na hii imechangia sana katika kupungua mizigo yetu katika bandari ya Dar es Salaam kwani inachukua muda mrefu kusafirisha mizigo kutoka hapa kupeleka nchi za jirani. Pia kuna changamoto nyingine ambayo bandari yetu ya Dar es Salaam inayo.

Miundombinu ya bandari ya Dar es Salaam si mizuri hasa kina cha maji, kuanzia bandari ya namba moja mpaka namba saba sasa hivi ina kina cha maji takribani mita 10 na kwa meli kubwa za kisasa inatakiwa takribani iwe na kina cha maji ambacho ni mita 14. Sasa tuna mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba tunaboresha bandari yetu ya Dar es Salaam kuhakikisha kwamba meli kubwa za kisasa zinaingia na zinaleta mizigo kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya mwisho kuhusu reli, mchakato wa ujenzi wa reli ya kati unaenda, vizuri tumetangaza *tender* kwa *lot* ya kwanza, ambayo inatoka Dar es Salaam mpaka Morogoro, wakandarasi kama 39 mpaka sasa hivi wameomba, tunaamini tutakapofungua *tender* hiyo tarehe 6 Desemba watafikia wakandarasi kama 50 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili tutaanzia Morogoro mpaka Makutopora alafu na *lot* ya tatu itaanzia Makutopora mpaka Tabora, *lot* ya nne itaanzia Tabora mpaka Isaka na *lot* ya tano itaanzia Isaka mpaka Mwanza ambayo kazi za *tender* kwa ajili ya kazi hiyo zitatangazwa wiki inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchangia naomba kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kutoa michango yao kwenye mambo mbalimbali yanayohusu uboreshaji wa huduma za afya nchini. Niwahakikishie tumesikiliza kwa makini na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo; kwamba wakati tunaomba kura mwaka jana sisi wa Chama cha Mapinduzi tulizungumzia sana kuleta mabadiliko ya kweli kwenye nchi yetu, na tulipoweka mkakati huu wa kuzungumzia kuleta mabadiliko ya kweli, siyo tu mabadiliko kama waliyozungumzia wenzetu, tulijua wazi kwamba mabadiliko yanakuja na maumivu, na tulijua wazi kwamba mabadiliko yatakuja tu kama kutakuwa kuna uwajibikaji na watu watafanya kazi ipasavyo. Pia tunatambua kuwa mabadiliko ni lazima yatokee, kwa sababu kama kuna kitu kina uhakika wa kubadilika basi ni mabadiliko yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani, Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, amepata heshima kubwa sana kwenye duru za Kimataifa kwa kuimarisha mifumo ya uwajibikaji kwenye nchi yetu, lakini pia kwa kurejesha nidhamu ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo anaoutoa Mheshimiwa Rais, umetuwezesha sisi wa Wizara ya Afya kuboresha huduma kwa kiasi kikubwa sana kiasi kwamba utafiti wa TWAWEZA ambao uliwasilishwa takribani miezi miwili iliyopita umeonesha kwamba sekta ya afya inatoa huduma bora, na hii ni kwa mujibu wa utafiti wa sauti za wananchi ambapo wananchi wametoa *feedback* hiyo, kwamba huduma za afya zimeboreka kwa sababu ya uwajibikaji wa Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kuchangia ni kuhusu nia njema ya Serikali kwenye eneo la kuongeza upatikanaji wa dawa nchini. Nia hii inajionyesha wazi kwa Serikali kutenga bajeti ya shilingi bilioni 251.5 ambayo imeanza kutekelezwa mwezi julai mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii shilingi bilioni 70 ndani yake zitakwenda moja kwa moja kununua dawa kwa ajili ya kupeleka kwa wananchi, na mpaka sasa Wizara ya Afya imekwisha pokea shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kununua kuanza kupeleka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la dawa Serikali pia inaimarisha upatikanaji wa dawa za *chemotherapy* yaani dawa ya huduma za kansa kwa tiba ya kemikali ambapo mwaka huu tuna shilingi bilioni saba ukilinganisha na shilingi bilioni moja iliyekuwepo mwaka jana. Kwahiyo naomba Waheshimiwa Wabunge watuamini tuna nia njema ya kuboresha huduma za afya nchini, na kufikia mwezi wa 12 tunaahidi tutakuwa tumewezesha upatikanaji wa dawa wa asilimia 85 ukilinganisha na asilimia 63 tuliyonayo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia sote nafasi na tukaweza kukusanyika katika Bunge hili Tukufu na

kuweza kutoa michango yetu katika hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naomba niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mizuri ambayo mmetupatia sisi Wizara ya Fedha na Serikali yetu ya Awamu ya Tano. Ni imani yangu kubwa kwamba, tumeyasikia mengi mliyoyasema na tutayafanyia kazi, na ninaamini tutakapokuja na mpango kamili mpango huo utakuwa ni mpango mahiri na bajeti yetu itakuwa ni bajeti ionayoonesha michango yenu yote Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichukue fursa hii niweze kuchangia hoja chache sana kulingana na muda wetu tulionao ili tuweze kuahirisha Bunge muda utakapofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja moja ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameisema ambayo ningependa kuichambua katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ilikuwa ni kwamba mpango wetu umesahau mambo ya msingi ikiwa ni pamoja na mambo ya kuinua kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Waheshimiwa Wabunge wanakazi nyingi wana mambo mengi, lakini mpango wetu umeeleza vizuri sana kuhusu sekta hii ya kilimo, mifugo na uvuvi. Tukienda katika ukurasa wa 56 mpaka 59 umeongelea vizuri sana katika sekta hii ambayo na sisi tunaamini bila kilimo hakuna viwanda Tanzania, bila kilimo Mheshimiwa Mwijage hawezi kugawa viwanda kama alivyofanya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunathamini sana naomba tusome ndani ya kurasa hizo *section* ya 6.5 na vipengele vyake, 6.51, 6.52 pamoja na 6.53, vyote hivyo vimeelezwa pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hii ya kilimo.

Kwa hiyo naomba tusome pale, na bado tunaendelea kuandaa mpango wetu mtakapokuwa mmesoma kama bado mnahoja tunaomba muendelee kutuletea hoja zetu ili tuweze kuandika mpango wetu vizuri zaidi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili au hoja ya pili ambayo ningependa kuitolea maelezo kwa ufupi ilikuwa ni kwamba maisha ya wananchi yanakuwa duni wakati mapato yanaongezeka.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme kwamba Serikali inakubaliana na hoja hii na hasa iliwasilishwa na Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha tunakubaliana naye kwamba mapato yanakuwa, lakini si kwamba hali ni duni kwa wananchi kule, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarika kwa hali ya maisha ya wananchi naomba tufahamu jambo moja, haitegemei mapato peke yake, bali hutegemea pia kuimarika kwa huduma za jamii ambazo Serikali yetu ya Awamu ya Tano imekuwa ikizipigania na tukiendelea kutekeleza na ambacho ni kipaumbele chetu kikubwa kabisa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Serikali yetu kuwa pamoja na jitihada tunazozichukua kama Serikali tunaomba pia wananchi watumie muda wao mwingi katika shughuli za kiuchumi kwa ajili ya kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna maendeleo yanayokuja wala hakuna mabadiliko yanayokuja kwa kuletewa lazima sisi wenyewe tukubali na sisi kama wawakilishi wa wananchi hawa Waheshimiwa Wabunge tuweze kuwaelekeza wananchi wetu nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimshukuru na nikampongeza ndugu yangu Mheshimiwa Riziki alipotoa aya za Mwenyezi Mungu kutoka katika Kitabu Kitukufu cha Qurani.

Mimi naomba niseme kwa kumjibu katika aya hizo hizo za kitabu cha Qurani kwamba Mwenyezi Mungu anasema hawezi kubadili chochote katika maisha yako mpaka wewe mwenyewe uamue kubadili mwenyewe maisha yako.

Kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi sana hatuwezi kuendelea kulaumu Serikali, kulaumu Waheshimiwa Mawaziri, sisi wenyewe tumefanya nini katika kujiletea maendelea ni jambo la msingi sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ningependa kuitolea ufafanuzi ambayo imesemwa kwa nguvu sana, na namshukuru Mheshimiwa Profesa Mbarawa ameweza kueleza nayo ni kuporomoka kwa mizigo ndani ya bandari yetu ya Dar es Salaam. Kwa upande wa Wizara ya Fedha ziliongelewa hoja tatu; ya kwanza ilikuwa ni *single customs territory,* ya pili ni *VAT* kwenye *transit goods* na ya tatu ilikuwa ni wingi wa *check points.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge watutendee haki, wamtendee haki Mheshimiwa Rais wetu. Alipoingia tu madarakani aliondoa *check points* zote na zimebaki chache sana. Kwa hiyo, katika *check points* hizi tumtendee haki Mheshimiwa Rais, mtutendee haki na sisi tunaomsaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi tumekuwa tukiyafanyia kazi na haya machache yaliyobaki ikiwemo *single customs territory* pamoja na *VAT on transit goods* tunafahamu faida zake. Kutoka katika *ethical point of view* siamini sana

kama wewe unaweza ukafurahia nyumbani kwako uko salama na kwa jirani yako hakuko salama, haiwezekani. Naamini ilikuwa ni lengo jema la Waheshimiwa Rais wawili, Rais wetu mstaafu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Rais wa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo walipokaa na wakajadili pamoja changamoto hizi na tukaja na hii *single customs territory.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa imepigiwa kelele kwa muda mrefu na sisi kama Wizara ya Fedha hatujakaa kimya tayari timu yetu ya utafiti ipo kazini tutakapokamilisha kuifanya tafiti hii tutawaletea hapa na kwa pamoja kwa sababu tuliipitisha hapa Bungeni tutaleta ili tuoni ni nini cha kufanya. Serikali ni sikivu imesikia na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nisemee suala moja, naona kengele imegonga, nayo ni kuhusu *TRA* kwamba, kwa sasa inakusanya madeni na *arrears* na siyo kwamba hatukusanyi kodi tunayoistahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja, katika hili pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tunasema *no research, no right to speak,* kama huna utafiti usiliongelee jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ambazo zipo na sisi tunazo kwa sababu ndiyo watendaji katika Wizara hii, tunafahamu kabisa ukusanyaji wa kodi ni suala endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2016 *TRA* wamekusanya shilingi bilioni 3,463.8 katika hizi ni shilingi bilioni 90 tu ambazo ni *arrears.* Sasa mtutendee haki mnapokuwa mnaleta hoja zenu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka shilingi bilioni 3,000 tuna shilingi bilioni 90 tu ambazo ni *arrears* na *arrears* ni kawaida katika maisha yetu hakuna mtu asiyedaiwa, na sisi tunawapa nafasi ya wafanya biashara wetu wanadaiwa muda umefika wa kulipa wanalipa, kwahiyo tulete tu taarifa ambazo ni sahihi tusiwadanganye wananchi wetu kule walipo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa maneno machache kwamba Serikali yetu ina nia njema kabisa na Taifa letu na maendeleo ya watu wake. Mheshimiwa Rais wetu ana nia sahihi kabisa na njema na sisi wasaidizi wake tuna nia njema kabisa ya kumsaidia kuhakikisha Tanzania ya viwanda inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejiandaa vizuri, tulichokifanya tumebadilisha tu *spending* ya Serikali, wanasema *the government has shifted its spending pattern from non-productive activities to productive activities* ndiyo maana tunapiga kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tulizoea kuona watumishi wakisafiri hata sisi Waheshimiwa Wabunge tukisafiri, na pia namheshimu sana Mheshimiwa Keissy aliyekuwa akisema safari hewa hizi ndizo tulizofuta. Ukifuta hivi vitu lazima tutalalamika, lakini vitu vya msingi, vitu vya kiuchumi, vitu vya kukuza uchumi wetu tunaendelea kuvifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezoea kuona Taifa letu likiendeshwa na kodi za wafanyakazi, tumesema hapana. Taifa litaendeshwa na kodi za wafanyakazi pamoja na kodi za wafanyabiashara katika sekta binafsi. Sekta binafsi imesahaulika muda mrefu, alisema vizuri Mheshimiwa Bashe, kwamba kama yalifanyika makosa hivi sasa ni sahihi tuendelee na makosa hayo? Hatuwezi kufanya hivyo. Ndiyo kile nilichosema kutoka kwenye kitabu kitukufu lazima tuwe tayari kujibadilisha sisi kama tunataka na Mwenyezi Mungu atukubalie tunayotaka kubadilisha, hilo ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika haya mabadiliko ninaamini Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataongea kuhusu mdororo katika sekta ya mabenki. Lakini naomba niwaambie jambo moja mabenki yetu wamekuwa wavivu, benki zote ziko Dar es Salaam, benki zote ziko sehemu zile ambazo kuna taasisi za Serikali, hivi mbona benki hizi haziwafuati wananchi kule walipo? Kule ndiko pesa zilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaambie mabenki haya, Serikali imechukua pesa yake, Serikali ilikuwa ni mteja kama wateja wengine imechukua pesa zake ili i-*invest* katika *productive economic activities* sasa kwa nini tunalalamika? Mdororo uliopo ni ule mabenki yetu yalikuwa mavivu kwamba tunamkopesha mteja wetu hatujui anaenda kufanyia nini pesa tunayomkopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajidanganya pesa za Serikali ndani ya benki zetu, Serikali imechukua kama mteja mmojawapo. Wateja wale kwa kuwa walikuwa hawafuatiliwi na sasa hawalipi ndiyo maana tunaona Waheshimiwa wabunge mnasema *CRDB* ime-*register* hasara, ni kwa sababu sasa zile pesa walizozoea kutumia zimekwenda kwa mwenyewe na zile ambazo wamekopesha hawana uwezo wa kuzikusanya. Hilo ni jambo la msingi tuseme ukweli, tujitendee haki kama wananchi, tujitendee haki kama Watanzaini na tutaifikisha Tanzania hii salama ndani ya nchi hii na uchumi wa kati tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano kwa ufanisi kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitambue michango mizuri iliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua pia mchango wa Waziri Kivuli na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe. Aidha, ninawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mjadala huu ambapo kwa kuzungumza walichangia Wabunge 70 na kwa maandishi wamechangia Wabunge 48 wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mjadala ulikuwa mzuri na baadhi ya maoni yalitolewa kwa hisia kali na mimi ninaamini kwamba, kwa kuzingatia umuhimu wa uchumi katika nchi yetu ni jambo jema tukawa tunachambua, tukabishana na hatimaye turidhiane juu ya vipaumbele, mikakati na hatua stahiki za kukuza uchumi wa Taifa kwa namna ambayo ni endelevu zitakazo wezesha nchi yetu kufikia malengo ya dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa tumepokea michango na hoja nyingi tena sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge naomba niahidi hapa kuwa nitawasilisha Bungeni taarifa ya maandishi inayofafanua hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema yako maoni na ushauri mwingi uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nisiseme kwa kifupi

yale yaliyosemwa ni mengi sana, nilitamani walau niseme hata kumi tu kwa msisitizo ili mjue kwamba tunasikia, lakini kwa ajili ya muda naomba nijielekeze zaidi kufafanua hoja chache hasa zile ambazo nadhani ni muhimu tukaelewana vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni hoja kubwa ambayo toka mwanzo mpaka mwisho imesemwa kwamba uchumi unahali mbaya, uchumi umedorora na kwamba kuna manung'uniko ya wananchi mtaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Taifa unapimwa kwa vigezo vingi, haupimwi kwa kigezo kimoja wala viwili, nitasema baadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, viko vigezo vya ujumla, ukuaji wa Pato la Taifa. Uchumi wa Taifa kwa kipindi cha Januari mpaka Juni, 2016 kwa wastani umekuwa kwa asilimia 6.7 ukilinganisha na asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Asilimia 6.7 ni kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi. Ngoja niwapeni mfano, wastani wa ukuaji wa uchumi kwa *Sub-Saharan Africa* kwa mwaka 2016 ni asilimia 1.4 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya wanakuwa kwa asilimia 6, Uganda asilimia 4.7, Mozambique asilimia 6.5, Tanzania *quarter* hii iliyokwisha asilimia 7.2 jamani tujitendee haki. Sekta zilizokuwa zaidi hapa kwetu ni uchukuzi na uhifadhi wa mizigo, uchimbaji wa madini, mawasiliano, sekta ya fedha na bima, na hizi zimekuwa kati ya asilimia 17.4 mpaka asilimia 15. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei. Januari, 2016 tulikuwa asilimia 6.5, Juni, 2016 asilimia 5.5, Septemba, 2016 asilimia 4.5, hicho ni kigezo kimojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, akiba ya fedha za kigeni, Ni dola za Kimarekani bilioni 4.1 mwezi Septemba, 2016 ambayo inatuwezesha kununua bidhaa na huduma kwa kipindi cha miezi minne. Urari wa biashara *(current accaount deficit),* imepungua kutoka dola milioni 1,207 katika *quarter* ya Julai mpaka Septemba, 2015, imerudi dola milioni 601.8 Julai mpaka Septemba, 2016. Jamani vigezo vyote hivi vinatuonesha tuko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa sekta ya kibenki. Sekta hii imeendelea kukua na ina mitaji na ukwasi wa kutosha. Mitaji ukilinganisha na mali iliyowekezwa, nilisema wakati natoa hoja hapa, *total risk waited assets* na *off balance sheet exposures* ni asilimia 19.08 ukilinganisha na kiwango cha chini ambacho ni asilimia 12 tu. Mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ikilinganishwa na kiwango cha amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi *(liquid assets to demand liabilities)* asilimia 34.18 wakati kiwango cha chini kinachohitajika ni asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli shida kubwa tunayoona pamekuwepo na mikopo chechefu. Septemba, 2015 ilikuwa ni asilimia 6.7 sasa imeongezeka kufikia asilimia 9.1, na ndiyo sababu tumeona mabenki ambayo yamepata hasara; *CRDB* kati ya Julai na Septemba wamepata hasara, *TIB Development Bank* wamepata hasara, na sababu ni hiyo ya mikopo chechefu. *Twiga Bancorp* nayo tumeiweka chini ya uangalizi wa Benki Kuu, lakini siyo kitu cha ajabu. *Crane Bank Limited* ya Uganda nayo imewekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu yao mwezi uliopita. *Imperial Bank* ya Kenya nayo iliwekwa chini ya uangalizi Oktoba, 2015 na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kibenki kwa ujumla ilipata faida, pato kwa rasilimali *(retain on assets 2.53)* na kadhalika, naweza nikaendelea kueleza lakini sisi tunavyotazama vigezo vingi vya uchumi vinatuonesha tuko sawa sawa. Nitakuja huko kwingine kwanini tunasikia maneno mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya ubadilishanaji fedha *(exchange rate)* hatuko pabaya. Ule upungufu, wastani umekua shilingi 2,172 kwa dola moja mwezi Januari, 2016, Julai zikawa shilingi 2,180 na bado mapaka Septemba bado tuko 2,188, kwa hiyo, *stability* ya *exchange rates* siyo mbaya kama watu wanavyosema maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mwenendo wa bajeti, na hizi namba nitakazo sema ni *preliminary.* Mapato ya ndani kwa *quarter* iliyopita, mapato ya ndani ukijumlisha na fedha kutoka *own sources* za Halmashauri tulikuwa na shilingi bilioni 3,948.4 Mapato ya ndani ukitoa yale ya Halmashauri inakuwa ni shilingi bilioni 3,814.4, tulipata *GBS grant* kutoka *EU* shilingi bilioni 36.1 na kwa upande wa matumizi Waheshimiwa Wabunge tumekwenda vizuri. Matumizi ya kwaida katika *quarter* ya kwanza, fedha zilizotolewa kwa robo ya kwanza ni asilimia 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa shilingi trilioni 4.5 wakati bajeti ya matumizi ya kwaida kwa mwaka huu mzima ni trilioni 17.7 lakini pia kwa upande wa matumizi ya maendeleo hapa tuna changamoto, tunazikiri lakini mwaka ndiyo umeanza *quarter* ya kwanza ina changamoto mwezi wa kwanza mapato yanakuwa kidogo, mwezi wa 9 ndipo mapato kidogo yana-*pick up.*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya maendeleo. Tumesha kutoa shilingi bilioni 915 ambayo ni asilimia nane ya lengo ambalo tulikuwa tumekusudia. Kwa upande wa matumizi kutokana na fedha za nje, na hapa ndipo *challenge* ilipo, ni asilimia moja tu ambazo tumeweza kutoa, tulikuwa tumepata shilingi bilioni 45.9

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa madeni ya ndani. Katika kipindi cha Julai mpaka Oktoba, 2016 tumelipa madeni mbalimbali ambayo yamehakikiwa

na Mkaguzi wa Mkuu Ndani wa Serikali, tumelipa jumla ya shilingi bilioni 187.5 na haya yanajumuisha madeni ya wakandarasi wa barabara, maji, umeme, wazabuni mbalimbali na madeni ya watumishi wa umma na tunaendelea kulipa kupitia mafungu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa deni la nje. Kuanzia Novemba, 2015 hadi Oktoba mwaka huu, Serikali imetumia jumla ya shilingi trilioni 1.19 kwa ajili ya kulipia madeni ya nje. Malipo ya mtaji ni shilingi bilioni 709, malipo ya riba shilingi bilioni 487.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi; Serikali itaendelea kulipa kwa wakati mikopo yote iliyoiva kwa mujibu wa mikataba; kwa kuwa kama hatufanyi hivyo tutahatarisha mahusiano yaliyopo baina ya nchi zetu na wahisani na taasisi za fedha za kimataifa na mabenki ya nje. Aidha, nchi isipolipa kwa wakati inaweza kushitakiwa kwenye Mahakama za Kimataifa na kusababishia nchi yetu kupata hasara na pengine hata tukakosa kabisa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutolipa kwa wakati kutaisababishia nchi yetu kulipa gharama kubwa za ziada *(penalty)* kulingana na makubaliano kwa hiyo ni lazima tulipe. Serikali imeweka mikakati mbalimbali kuhakikisha kwamba Deni la Taifa linadhibitiwa na linaendelea kuwa himilivu na linalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya pembejeo. Mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi bilioni 25 zilitengwa kwa ajili ya kununua Pembejeo. Hadi kufikia Oktoba tumekwisha kulipa shilingi bilioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa chakula cha hifadhi. Mwaka huu wa fedha tulitenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kununua chakula cha hifadhi ya Taifa. Mpaka kufikia Oktoba mwaka huu tumekwishakutoa shilingi bilioni 9.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa fedha za Mfuko wa Jimbo. Serikali ilitenga shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya mfuko wa kuchochea maendeleo jimboni. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni tisa ni kwa ajili ya Tanzania Bara na shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Serikali inatarajia kutoa fedha hizo mwezi huu wa Novemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamekuwepo kama nilivyosema manung'uniko mitaani lakini sisi tunavyoyatafsiri ni kwamba yametokana na jitihada na hatua zilizochukuliwa na Serikali kurudisha nchi kwenye utaratibu na nidhamu ya kazi katika utumishi wa umma, kurejesha nidhamu ya matumizi, kuondoa matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima, kupambana na wizi na ubadhirifu wa fedha na mali ya umma, kuhimiza ulipaji kodi na ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali inaamini kuwa hatua hizi ni kwa maslahi mapana ya Taifa letu, na maumivu ni ya kipindi cha mpito wakati tunaweka mambo sawa ili tuweze kurudisha mifumo kwenye utaratibu unaokubalika na ambao ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, naomba nitumie usemi tena wa kiingereza; *there is no gain without pain.* Maendeleo hayatakuja hivi hivi, *we have to sacrifice* ndugu zangu. Lazima tu- *sacrifice* kama kweli tunataka vizazi vijavyo viweze ku-*enjoy* maisha *in the future,* lakini kama tunakula tu leo haiwezekani tutaendelea kubaki maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo utaratibu wa Serikali yenyewe, taasisi binafsi na mashirika ya kimataifa kufanya tathmini huru ya uchumi wa nchi na kutoa maoni juu yake kadri wanavyoona. *IMF* walikuwa hapa wiki moja iliyopita na wamekamilisha tathmini ya mwenendo wa uchumi wetu. Taarifa iko kwenye mtandao, someni. Wamesema wenyewe si maneno yangu wamesema kabisa wameridhika na hali ya uchumi wa Taifa letu lakini hii haina maana kwamba hatuna changamoto, haitawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo kuhusu misingi ya mpango. Niliambiwa hapa kwamba tulivyoiweka hapa inajenga mazingira ya kushindwa tayari. Mimi nafikiri hapa tatizo lilikuwa dogo tu, neno misingi ambalo tulilitumia katika kitabu cha mapendekezo ya mpango kililenga kumaanisha *assumptions.* Hakika Serikali ya Awamu ya Tano tunafahamu vizuri hali halisi ya mazingira wezeshi kwa uwekezaji nchini kama ambavyo imetathminiwa na Benki ya Dunia katika *Doing Business Report*. Tunafahamu utabiri wa hali ya hewa na maoteo ya upungufu wa chakula katika nchi yetu, *we are not naïve* Waheshimiwa Wabunge, *we are not naïve at all.*

Mheshimiwa Naibu Spika, a*ssumptions* huwa tunazifanya na si lazima ziwe halisi, huwa tunazifanya ili kurahisisha uwekaji wa malengo kwa mwaka ujao wa fedha. Wachumi wanafahamu na ni utaratibu wa kwaida kabisa. Kwa mfano; unapotaka kuchambua biashara baina ya nchi mbalimbali ulimwenguni huwa unafanya *assumtions* unasema *assume there only two trading nations,* lakini kila mtu anajua nchi mbili duniani hazi-*trade* peke yake, kwa hiyo, nadhani hili lilikuwa ni suala la lugha tu, tafsiri yetu pengine *assumptions* haikuwa sahihi, lakini maana yetu ilikuwa ni *assumptions* na siyo hicho ambacho kilielezwa humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha kutopelekwa kwenye Halmashauri. Naomba niseme tu kwamba katika kipindi cha Julai mpaka Oktoba fedha zilizotolewa zinajumuisha mishahara shilingi trilioni 1.18 sawa na asilimia 33. Matumizi mengineyo shilingi bilioni 192.8 ambayo ni sawa na asilimia 32.2 na fedha za maendeleo shilingi bilioni 173.3 sawa na asilimia 14.3. Lakini mbali na

fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu na makusanyo ya ndani ya halmashauri, kiasi cha shilingi bilioni 271 zilizotumika kutekeleza miradi ya maji vijijini ni shilingi bilioni 51.1, umeme vijijini shilingi bilioni 132.4, mfuko wa barabara shilingi bilioni 78.1 na utoaji wa pembejeo kwa wakulima shilingi bilioni 10 katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa taasisi za umma kuweka fedha zao kwenye *revenue account* Benki Kuu tulishauriwa hapa kwamba sasa zirejeshwe. Nafikiri limeelezwa vizuri, naomba niseme tu hivi; uamuzi wa Serikali wa kuzitaka taasisi za umma kufungua *account* za mapato Benki Kuu utaendelea kubaki kama ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tumepigwa sana, kwanini tuendelee kupigwa? Utaratibu ambao ulikuwa umejengeka ulizinufaisha benki chache na haukuwa na maslahi mapana kwa Taifa. Benki hizo zimekuwa zikipata faida kwa kutumia mgongo wa maskini na sasa basi. Naibu Waziri amesema hapa waende na vijijini wakafanye kazi huko ili turejeshe ushindani katika sekta ya benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba *TRA* wanatumia vitisho, mabavu na mifumo kandamizi katika kukusanya kodi. Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inaendelea na jitihada za kuhakikisha kila anayestahili kulipa kodi analipa kodi stahili na kwa wakati. *TRA* inatekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi kulingana na taratibu katika sheria na kanuni za kodi. Mlipa kodi anakadiriwa kulipa na kupewa muda wa kuilipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kodi hiyo itakuwa haijalipwa kwa muda uliyooneshwa kwenye taarifa ya madai, *TRA* huchukua jukumu la kumkumbusha mhusika anapewa *reminder notice* na kumtahadharisha hatua zitakazochukuliwa endapo kodi hiyo itaendelea kutolipwa mpaka tarehe iliyoonyeshwa kwenye *reminder notice.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa kwa mlipa kodi anaekaidi ndizo hizo za kukamata mali na kuziuza kwa njia ya mnada na kuiagiza benki ya mlipa kodi kuhamisha fedha kutoka kwenye *account* yake kwenda *TRA* kulipia hilo deni. Hatua hizi zipo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge. Hatua hizi si vitisho wala mabavu, wala mifumo kandamizi kwa wafanyabiashara. Ninawasihi sana ni vizuri walipa kodi wakazingatia sheria za kulipa kodi kwa hiari na kuepuka usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja hapa kwamba Serikali imeokoa fedha kuondoa watumishi hewa lakini wakati huo huo tarifa za Benki Kuu zinaonesha malipo ya mishahara yaliongezeka. Naomba niseme hivi Waheshimiwa Wabunge, Serikali imeendelea kuajiri watumishi kwa mahitaji

muhimu. Kati ya mwezi Machi na Septemba, 2016 wameajiriwa watumishi 8,908 wakiwemo wa vyombo vya ulinzi na usalama, walimu wa vyuo vikuu, watumishi wa kada za afya kwa ajili ya hospitali mpya ya Mloganzila na watumishi wa kada nyingine ambao mishahara yao imeongeza *wage bill* kwa kiasi cha shilingi bilioni 5.08.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi Serikali imeendelea kulipa malimbikizo ya madeni ya watumishi. Kati ya mwezi Machi na Julai, 2016 shilingi bilioni 11.9 zililipwa kwa watumishi 13,544. Lakini pia Serikali iliamua kujumuisha mishahara yote iliyokuwa inalipwa nje ya *pay roll* kupitia bajeti ya matumizi *(OC)* kwenye *wage bill* ya kila mwezi na hivyo kupelekea ongezeko la shilingi bilioni 33.1 kwa mwezi kwenye *wage bill* kuanzia mwezi Februari. Kwa hiyo, kwa kweli hizi takwimu hizi zinahitaji tu maelezo lakini kila kitu kipo. Nimesikia kengele imeshalia na kama ambavyo nimekwisha kuahidi ziko hoja nyingi ambazo ningependa kuzitolea maelezo lakini inatosha tu niseme na nimalizie na mambo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, vipaumbele vingi. Nimemsikia Mheshimiwa Silinde. Nafikiri tutakapoanza hilo zoezi la kupunguza vipaumbele tutaanza kupunguza na kuondoa miradi katika jimbo la Momba ili ibaki mitatu. Waheshimiwa Wabunge, kazi ya kupunguza vipaumbele katika Taifa letu ni ngumu sana kwa sababu moja; lengo ni kuielekeza sekta binafsi kwenye maeneo ya *priority,* kwahiyo si kwamba hizi *priorities* zote ni Serikali iende ikafanye. Lengo letu ni kuielekeza *private sector* iende kwente *priority areas*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile vipaumbele lazima viwe vingi kwasababu fursa katika Taifa letu zinatofautiana sana, kwahiyo ni lazima miradi iwepo ambayo inazingatia fursa za maeneo husika ndiyo maana ni baadhi tu ya sababu kwanini vipengele ni vingi sana. Lakini kimsingi na umaskini wetu jamani niambieni niache nini, niache reli ya kati, niache miradi ya maji, niache Mchuchuma na Liganga, niache zahanati, niache umeme vijijini au niache barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe na napenda kuwashukuru Wabunge wote waliochangia na kutupatia ushauri kuhusu vipaumbele na mambo muhimu ambayo sasa tunakwenda kuzingatia katika kazi inayofuata ya kuandaa mpango ujao wa maendeleo kwa mwaka 2017/2018. Napenda niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itazingatia ushauri tulipokea kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika haitawezekana kuzingatia kila kitu kinachosemwa hapa. Baadhi yataendelea kuzingatiwa katika mipango ya maendeleo itakayofuata. Na ili Bunge lione wazi kwamba Serikali inasikia na inathamini ushauri mzuri walioutoa ninakusudia kuweka bayana katika kitabu

cha mpango wa maendeleo ujao utakapokamilika muhtasari wa ushauri uliozingatiwa na ule ambao tunaona unafaa uzingatiwe katika mipango inayofuata na mambo ambayo bado yanahitaji kuchambuliwa kwa kina kabla ya kuzingatiwa kwenye mipango. Kwa hiyo, ninawaahidi ili msiseme tunapuuza, tunazingatia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kujenga Tanzania mpya ili kuwaondoa Watanzania kwenye lindi la umaskini kwa haraka. Uamuzi huu unahitaji kuachana na mazoea, unahitaji *sacrifice*, unahitaji tufanye kazi kwa bidii, unahitaji nidhamu na uadilifu. Tunataka uchumi ambao Wananchi wengi wananufaika nao. Nirudie tena, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inawajali wafanyabiashara, lakini hatuna budi wafanyabiashara wetu wazingatie sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge naomba mkae. Kwa wakati huu hoja hii itakuja kutolewa hapo baadae mpango utakapokuwa umeletwa, kwa hiyo mtu asije akawa anajiuliza kwa nini Bunge halijahojiwa kwa sababu kilicholetwa sasa hivi ni mapendekezo mpango wenyewe utaletwa baadae mwakani.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza sana kwa michango mingi mno mliyoitoa kwa mapendekezo ya Serikali, kwa sababu Serikali ilichofanya imeleta mapendekezo kwa Bunge ili Bunge lishiriki kwenye kutengeneza mpango huo. Ninaamini kwamba Serikali mmechukua mawazo ya Wabunge kama ambavyo mlileta mapendekezo ili washiriki kwenye kuboresha hayo mapendekezo yenu.

Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba michango mingi ya Wabunge iliyotolewa katika siku hizi tatu itawasaidia kuboresha huo mpango na mtakapouleta mwakani tutaweza kuona mapendekezo yaliyotajwa humu ndani kwa namna ya uzito sana.

Kwa hiyo nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri mliyoitoa. Lakini nichukue pia nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuja na hayo mapendekezo maana ni lazima ilikuwa mje nayo ili sisi tupate pa kuanzia kwahiyo nawapongeza pia.

Na pia nirudi tena kwa Wabunge nawapongeza kwa kukaa muda wote humu Bungeni, kwa sababu mpo idadi kubwa sana wananchi kule lazima wapate huo ujumbe kwamba Wabunge wao wanakaa Bungeni muda mrefu hakuna muda ambao nimeona viti vikiwa vitupu, kwa hiyo hongereni sana Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya kusema hayo, kuna tangazo moja; Katibu wa Wabunge wa CCM Mheshimiwa Jasson Rweikiza anawatangazia kikao cha Wabunge wa CCM leo Alhamisi tarehe 3 Novemba, 2016 saa 2.00 usiku ukumbi wa *White House,* na mnakumbushwa wote kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 4 Novemba, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*